DT 434
.E27 K19

'mau mau' kizuizini

JOSIAH MWANGI KARIUKI

EAPH VITABU VYA SIKU HIZI—3

'Mau Mau' Kizuizini

JOSIAH MWANGI KARIUKI

'Mau Mau' Kizuizini

Kisa cha miaka saba ndani ya Kampi za
Kuhamishwa katika Kenya

Kitabu hiki kimetafsiriwa katika lugha
ya Kiswahili na Joel Maina



EAST AFRICAN PUBLISHING HOUSE

DT 434
.E27 K19

Kitabu hiki kimetolewa katika lugha ya Kiingereza kwanza mwaka wa 1963 na Oxford University Press, Amen House, London.

Kimetolewa katika lugha ya Kiswahili mwaka wa 1965 na East African Publishing House.

Sheria ya haki ya Kunakili © Oxford University Press, 1963.

Kimepigwa chapa na East African Printers Kenya Ltd., Nairobi.

Mwandishi amegeuza majina mengine ndani ya kitabu hiki kwa sababu hana chuki na mtu ye yote.

Yaliyomo

	Shukrani	vii
	Kwa heshima ya	ix
	Kwa Mkato	x
1	Siku Zilizotangulia Wakati wa Hali ya Hatari	1
2	K.C.A., K.A.U. na 'Mau Mau'	13
3	Kiapo Chenyewe	22
4	Kampi ya Vilima Vitatu Vikavu	40
5	Langata na Kufika Manyani Mara ya Kwanza	50
6	Yatta Kusini na Kurudi Manyani mara ya Pili	68
7	Nyororo, Visiwa na Vumbi	85
8	"Mfereji", "Kuokolewa" na Nyumbani	109
9	Chama Kipya cha Siasa Chabuniwa	123
10	Utisa Uliyojaa ("Kenda Muiyuru")	137
	Nyongeza—Kuunganishwa kwa Mashamba	156

Shukrani

KWA HAKIKAsi jambo nzuri kwangu kujaribu kutoa shukrani kwa wachache tu baina ya wale wote ambao walinisaidia katika jitihada za kuandika kitabu hiki. Lakini hata hivyo, ningalipenda kutoa asante maalum kwa wafuatao:—

Jomo Kenyatta kwa mapendeleo na maongozi yake binafsi; "Jaramogi" Oginga Odinga ambaye aliifanya safari yangu ya kwenda London kuwezekana; Othigo Otieno, Burudi Nabwera, Ngumbu Njururi, Karuga Koinange, na Kamiti ya Umoja wa Afrika iliyoniwezesha kuongeza kukaa kwangu katika Uingereza; bibi wangu Doris Nyambura ambaye alinipa moyo katika nyakati ngumu, Robinson Mwangi Wanjagi, Joseph Kirira, Jeremiah Kirumwa, David Oluoch, Kirori Motoku, Kimana Wachuku na Taddeo Mwaura ambao walishirikiana sana nami; Fenner Brockway, M.P. na John Stonehouse, M.P. ambao kwa sababu ya mkazo wao niliweza kuokoka mara kwa mara; na Chama cha Kupigania Uhuru wa Makoloni; Margery Perham, C.B.E., kwa kuweka chumba chake wazi kwa manufaa yangu na majadiliano mle bustanini mwake malidadi; Bi. Catherine Hoskyns na Bw. na Bi. Antony Hoskyns kwa mapendeleo na usaidizi wao kwa kutengeneza kisibao; Clyde Sanger kwa usaidizi wake juu ya 'grammar'; Carl Rosberg wa Chuo Kikuu cha California kwa hamu yake na upendo; na wafanyi kazi wa Oxford University Press kwa unyenyekevu wao usiofifia katika Nairobi na pia London. Shukrani nyingine yamwendea Joel Maina ambaye alisaidia wakati wa kutafsiri kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili.

Kwa Heshima ya

KENYATTA WA MUIGAI, Kiongozi wa Taifa letu, Baba wa Taifa letu, wa mlango wa Mumbui wa Agikuyu, ukoo wa Gikuyu na Mumbi.

Kumkumbuka DEDAN KIMATHI WACHIURI, Kiongozi katika Nyandarua.

WARUHIU ITOTE (General China), Kiongozi katika Kirinyaga.

STANLEY MATHENGE popote alipo.

Wale wote ambao waliuawa ama kufanywa viwete katika misitu yetu yenye rangi ya kijani kibichi, katika risavu, jela na Kampi za kufungiwa kwa ajili ya kutimiza wajibu wetu kwa uaminifu.

Hao ambao waliosalia kujenga taifa baada ya ghasia na masikitiko ya Hali ya Hatari, wakitumainiwa kukamilisha uhuru wa Afrika Mama wetu kwa Jumla.

Wanachuo wa Kenya ambao wanategemewa na mambo mengi.

Kwa Mkato

C.I.D.	Kachero wa Kupeleleza Uhalifu
D.C.	Mkubwa wa Wilaya (Disi)
D.D.O.	Amri ya Kutoa Uwezo Kumhamisha mtu
D.O.	Naibu wa Mkubwa wa Wilaya
G.M.K.	Gikumbo Mount Kenya
K.A.D.U.	Kenya African Democratic Union
K.A.N.U.	Kenya African National Union
K.A.P.E.	Kenya African Preliminary Examination
K.A.R.	King's African Rifles
K.A.U.	Kenya African Union
K.C.A.	Kikuyu Central Association
K.I.S.A.	Kenya Independent Schools Association
K.K.E.A.	Kikuyu Karinga Educational Association
K.K.M.	Kiama Kia Muingi (Chama cha Wananchi)
K.P.R.	Kenya Police Reserve
M.L.C.	Member of the Legislative Council
M.R.A.	Mafunzo ya kutengeneza tabia ya roho
N.D.P.	Nyeri Democratic Party
N.P.C.P.	Nairobi Peoples Convention Party
P.C.	Mkubwa wa Jimbo (Pisi)
R.S.M.	Regimental Sergeant Major
Y.K.A.	Chama cha Wakikuyu Vijana

1 Siku zilizotangulia wakati wa Hali ya Hatari

MIMI NI MKIKUYU ambaye alifungiwa ndani ya kampi kumi na nne za Kenya kati ya mwaka wa 1953 na 1960. Kitabu hiki kinaeleza juu ya maisha yangu katika kampi hizo. Hakikuandikwa kwa moyo wa uchungu wala madharau bali ni kwa sababu bado hakuna ye yote ambaye amesema ukweli juu yake na kwa sababu zimekuwa ni muhimu katika historia ya nchi yangu. 'Manyani', ilikuwa kampi kubwa zaidi ya zote ambamo kulifungiwa watu 30,000 na sasa ni jina ambalo limehusikana sana katika kila lugha ya kila kabila katika Kenya, na hakuna anayetumaini kufahamikiwa na mwenendo wa siasa za Waafrika wa Kenya bila kuelewa maisha ya wafungiwa 80,000 wa miaka hiyo ya wakati wa Hatari. Yawezekana pia kuwa maelezo juu ya vile tulivyojitayarisha wakati wa shida kuu yangewafaa wale ambao wangali katika hali ya aina hiyo leo, katika zile nchi zingine za Afrika ambazo zatawaliwa na wakoloni. Lakini ili kuwawezesha wasomaji kuhukumu thamani ya vile nitakavyosema, labda ingelifaa kama nikitangulia kwa kuwaambieni juu ya maisha yangu kabla ya kufungiwa.

Nilizaliwa mnamo tarehe Machi 21, 1929 katika Kabati-ini, karibu na Bahati Forest katika jimbo la Rift Valley la Kenya. Wazazi wangu walihama kutoka Chinga ndani ya wilaya ya Nyeri mwaka uliotangulia na wakawa maskwota katika shamba la Mzungu aliyeitwa Muturi. Muturi ni mhunzi kwa Kikikuyu, na alipewa jina hilo kwa ajili ya ujuzi wake juu ya kutengeneza vyombo vya shamba. Sikujua jina lake hasa. Maskwota katika mashamba ya Wazungu walipewa kisehemu cha shamba cha kulima na kuweka mifugo ya ng'ombe na mbuzi iliyopimwa. Kwa ajili hiyo, walitazamiwa kuwa tayari, pamoja na jamaa zao, kufanya kazi ya kawaida au ya muda kwa Mzungu. Mishahara ilikuwa ya chini sana na mpango huo ulionyesha kunyimwa kwa mambo ya starehe kwa njia zote.

Hali hiyo haikuwatosha watu wetu wakati walipovumbua haja ya pesa, kwa ajili ya kununua nguo, elimu au baisikeli. Wazazi wangu, wakifanya kama vile wengine wa Kikuyu na wa Nyanza walivyofanya wakati walikuza mazao ya pesa kama kahawa, chai na "pyrethrum"

ambayo yalikuwa yamepigwa marufuku au hayakujulikana katika sehemu za wenyeji (Native Reserves), walishikwa na hamu sana ya utajiri ambao ungetokana na ufugaji wa ng'ombe na mbuzi katika Nyanda za Juu za Weupe (White Highlands), ambako kwa sheria hakuna Mwafrika angaliyetumaini kuwa na ardhi na ambako shamba moja la Mzungu lingeweza kuwa kubwa zaidi kuliko lokesheni nzima ya wenyeji yenye binadamu elfu sitini.

Nilikuwa mtoto wakati baina ya watano, hao wengine wakiwa wasichana. Dada yangu wa tatu, Wangechi, alifariki dunia akiwa wa miaka mitatu, lakini wale dada wengine wangali hai na wote wameolewa. Mama wangu, Mary Wanjiku, alimshawishi baba yake mzee ahame nasi kutoka Chinga. Baba yake alikuwa mwenye urefu wa futi sita na inchi nne na alikuwa shujaa mkuu kabla ya Waingereza kuingia katika nchi yetu, huku wakipigania ng'ombe na wanawake kwa Wamasai na Wakikuyu pia, wakiongozwa na Mugo Wandiga, Jemedari Mkikuyu mashuhuri, aliyetajwa na John Boyes ndani ya kitabu chake *King of the Agikuyu*. Mugo Wabira, kama alivyoitwa babu wangu, wakati huu aliikuwa na kiasi cha kondoo na mbuzi mia nne, na alichukua kama nusu yake katika shamba la Muturi. Kiasi hicho kilikuwa zaidi ya kile kilichokubaliwa na sheria, lakini haikuwa vigumu kuwaficha, kwani tuliwagawanya baina ya marafiki wetu. Mugo alifariki mnamo 1947, na tulihuzunika sana kupotewa na binadamu kama huyo, ambaye alikuwa kama daraja baina ya siku zilizotangulia kabla ya kufika kwa Wazungu.

Sisi tulikuwa wa ukoo wa Mbari ya Mbogo wa Muhiriga wa Mungari, ambao walijulikana kwa bidii yao, walioheshimu ndoa na waliopendelea kula "nduma" sana ("nduma" ni aina ya viazi vinavyokua karibu na maji). Mungari, aliyefanya shina la Muhiriga, alikuwa mvulana wa Wangari, ambaye alikuwa mmojawapo wa wasichana tisa wa Gikuyu na Mumbi, ambao kila mmoja ni shina la Muhiriga wa Kikikuyu. Gikuyu na Mumbi ndio baba na mama wa kabila letu na nyumbani mwao ilikuwa ni Mukurwe-ini wa Gathanga ambako walitumwa na Mwenye Unyoya (Mungu), ambaye waliamini kuwa aliishi kileleni kwenye theluji iliyofungwa ya Mlima Kerinyaga (Kenya). Kama ilivyo kawaida katika kila kabila la Afrika Mashariki, iko hadithi katika Wakikuyu inayosema kuwa wanawake ndio walitutawala hadi wanaume wakaudhika sana hata wakafanya mpango wa siri kuwatia mimba wanawake wote wakati mmoja. Wakati wanawake wengi walipokuwa wazito, wanaume walichukua utawala. Kama jamii wengine Wakikuyu, tulikuwa na damu kidogo ya Kimasai kutokana na hali ya mashambulio ya zamani.

Baba wangu, Kariuki Kigoni, alirudi Chinga mwaka wa 1940 akiwa pamoja na bibi wa pili mpya mdogo, Gathoni. Akamwacha mama wangu

na watoto wake katika Rift Valley. Mama wangu alikwenda kuishi na Zacharia Ndung'u, na akanichukua pamoja naye. Zacharia sasa anaishi kwenye kiwanda cha mbao (Saw Mills) karibu na Njoro. Anaye bibi na wasichana watano. Kutoka wakati huo, nilimwona kama baba wangu na hata sasa ningali namsaidia wakati niwezapo. Sikumwona Kariuki, baba wangu, tena. Alifariki dunia mwaka wa 1943 baada ya kutangatanga kama mwenye wazimu kwa miezi sita. Ilisemekana kwamba alitiwa wazimu na wachawi walioajiriwa na wengineo wa ukoo wetu ambao walimwonea wivu kwa ajili ya mali yake na mashamba. Dada zangu wawili walionitangulia, Nyakio na Njoki, walipanga mazishi yake huko Chinga. Mama yangu alinikataza kwenda kuchungulia hali ya kifo cha baba, kwani aliogopa ningepatwa na hali iliyompata baba na tena nilikuwa kijana sana kuingilia safari ya hatari kama hiyo nikiwa peke yangu.

Mpaka nilipokuwa na umri wa miaka saba, niliishi maisha ya kawaida ya mtoto wa kiume wa siku hizo, yaani kuchunga ng'ombe na mbuzi, kujifunza desturi za Kikikuyu kutoka kwa babu zangu, kuchungulia michezo ya wazee, kuiba miwa na mahindi, huko nikiharibiwa kabisa na dada wangu na marafiki zao. Kile nilichokitamani sana katika vitu vyangu ni vazi langu la ngozi (*gathii*) ambalo lilikuwa limetiwa maridadi ya shanga na babu yangu. Uzuri ulikuwa kwamba ningetoroka kutoka ndani yake kwa udanganyifu nikishikwa nikitenda maovu, huko nikimwacha mshiki wangu kwa kijinga akijishikilia vazi hilo badala ya mimi.

Mnamo mwaka wa 1936, Muturi alimwuliza mama kama angekubali nikafanye kazi ya jikoni katika nyumba hiyo kubwa. Alikuwa amependezwa na vile sikuwaogopa Wazungu nikilinganishwa na watoto wengine wa rika yangu. Mshahara ulikuwa shilingi tatu pamoja na posho, na kila Jumamosi Bi. Muturi alinipa sukari na chumvi kumpelekea mama. Nilikatazwa kuvaa ngozi humo na, badala yake, Muturi alinipa suruali fupi na shati. Kwanza ilikuwa vigumu sana kuzoea suruali na zaidi, wakati wa kwenda chooni, ilikuwa bora zaidi kuiondoa kabisa kwanza kabla ya kitendo chenyewe. Kazi yangu ilikuwa ya kusafisha vyombo vya jikoni, kuwachunga paka na mbwa (watatu wa kila aina) na kuwalisha bata na kuku. Mbwa aliyekuwa mdogo zaidi alikuwa mwenye urafiki na tulimwita *Macha*, yaani madende, kwa ajili ya miguu yake mikubwa, minono na mifupi. Alikuwa mkubwa, alikuwa wa rangi ya madoadoa na wa kuogofya aliitwa *Kirumi*. Iko hadithi ya Kikuyu inayosema kuwa wakati watoto wa chui wangali wachanga, mama yao hujificha kwa muda na bila onyo hurudi kwa ngurumo kali ili kuwaogofya. Wale watoto ambao wanamwogopa na kukimbia huitwa *Irumi* na wale mashujaa wanaobaki huwa chui halisi. Bila shaka *Kirumi* wetu alikuwa na tabia nyinginezo zisizopendekezwa na zile za chui.

Mkubwa wetu alikuwa Benson, mpishi wa Muturi. Sikuweza kamwe kuacha kushangazwa na vile aliweza kumeza chakula chenye moto wa kuchoma, kinywa chake ni lazima kiwe kilikuwa kama ngozi ya viatu. Alikuwa mpishi wa kupendeza na ninakumbuka usiku mmoja wakati wageni wa Muturi waliuliza kama wanaweza kumwona Benson kibinafsi ili wampongeze kwa upishi wake uliowapendeza. Kama wapishi wengine katika Kenya, Benson alionelea kuwa ni halali kuchukua vyakula vya kutosha kutoka kwa tajiri wake. Usiku huo, wakati alikuwa akijifurahisha kwa mguu wa kondoo uliochomwa ndani ya jiko, aliisikia mitindo ya miguu ya Muturi wakati ambao kwa kawaida Muturi angekuwa akinywa kahawa. Mguu wa kondoo ulikuwa hauwezi kufichika na kwa kushtuka kwake, Benson aliuchukua na kuuweka kichwani ndani ya kofia yake kubwa ya upishi. Akiuweka barabara, alimfuata Muturi hadi ndani ya chumba cha kula. Nyama hiyo ilikuwa moto sana na ilikuwa yamchoma kichwani. Alikuwa anapongezwa wakati alikuwa na maumivu kichwani; wakati huo akajisikia akisindikizwa na kuumia, matone ya mafuta yakitiririka pole pole usoni mwake. Mmojawapo wa wageni aliona yaliyokuwa yakitendeka, akachacha kwa Muturi kwa ajili ya jasho lililomtoka mpishi wake mwenye bidii, akachukua kitambaa cha meza akamwendea Benson, akaanza kumpanguza "jasho." Wakati kichwa cha Benson kilipotikizwa na upanguzo wa "jasho", ule mguu ulitikizwa pia na mara ukaanguka chini kwenye mkeka maridadi sakafuni. Kwenye kimya kilichofuata, mpishi aliuokota mguu huo kwa upole akarudi jikoni akiwa na hofu. Muturi alikasirika sana kwa tukio hilo. Siyo kwa sababu Benson alichukua nyama. Kile kilichomkasirisha mno ni ule udanganyifu ambao uliwafanya wageni wake kumfikiria kama mwenye choyo na ambaye hakumpa mpishi wake mashuhuri chakula cha kutosha. Wote walioishi katika shamba hilo walichekelea tukio hilo kwa majuma kadhaa.

Nilimpenda Muturi na bibi yake sana. Walinitendea vyema na wakanipa picha na vitu vya kuchezea. Walimtendea mama na mimi kwa wema mkubwa. Lakini nikiangalia nyuma, nasikitika sana kwamba hawakunambia juu ya kusoma na kuandika na hawakunihimiza nianze masomo yangu.

Siku moja mwaka wa 1938 wakati wa kupanda, Obadiah Kariuki, aliyehusiana na jamaa ya mama na aliyekuwa mwalimu katika skuli ya C.M.S. mjini Nakuru, alitutembelea. Akiwa na umri wa miaka 25, kwa mimi alionekana kama mungu mdogo kwa mavazi na vyatu vyake vya kupendeza, saa yake na baisikeli. Niliipenda sana baiskeli yake na nikakata shauri kwamba hata na mimi nitajipatia moja hata iweje. Alipokuwa akiongea na sisi, niliona kama utajiri wake ulitokana na elimu yake, ujuzi wake wa kusoma na kuandika na ilikuwa muhimu nijipatie siri hiyo.

Mama yangu, ambaye wakati huo alitimiza miaka 40, alikuwa amejiunga na darasa la wasomaji, ambalo liliendeshwa nyakati za jioni na Mkikuyu mmoja aliyeitwa Evanson Ngamau. Mama aliweza kuandika jina lake na kuhesabu hadi kumi, na ingawa hakuendelea zaidi, aliyoyatenda yalionekana kama miujiza kwangu, hata nikamwuliza anifundishe yote aliyoyajua. Alininunulia sileti na kalamu ya mate na baada ya kazi usiku tulipambana na mambo haya mapya. Katika nyumba kubwa, nilifanya bidii sana kujifunza majina ya Kiingereza ya vyombo vya nyumbani.

Baada ya miezi miwili tangu Obadiah atutembelee mama alinishawishi niache kazi niingie skuli ya mchana ya Evanson kama mwanafunzi kamili. Ada ya skuli ilikuwa senti kumi na tano kwa miezi mitatu. Muturi alikuwa ameijenga skuli hiyo kwa pesa zake na ada zilimlipa mwalimu. Niliingia skuli wakati nilikuwa miaka kumi na mmoja na mara nilikuwa shujaa wa chumba chetu. Kwa ajili ya kazi yangu kwa Muturi, nilijua kuvaa suruali na kusafisha kucha zangu, na nilikuwa nimeanza kuandika na kuhesabu na mama. Wenzangu katika darasa walikuwa nyuma zaidi. Walikuwamo wanafunzi kama arobaini na tulifundishwa kuimba, kucheza, kuchora, kuhesabu na dini tukijifunza katekisimu—(Kitabu cha maelezo ya dini ya ki-Kristo). Haikuwa skuli njema lakini uvumbuzi wangu wa miaka mitatu ulikuwa wa maana katika maisha yangu.

Vita Vikuu vya 1939 havikugeuza hali ya maisha ndani ya shamba kwa njia kubwa. Mwaka wa 1940, ulikuwako uvumi kuwa Hitler angekuja kutuua sote na watu wengi wakakimbilia mitoni wakachimba mashimo kingoni ili kujificha kutoka majeshi yake. Lakini Jeshi la Kiingereza halikuwaajiri askari kutoka mashamba; hakukuwako na ukosefu wa chakula na hatukufahamu wala hatukujali yaliyokuwamo. Nilipoacha skuli ya Evanson, nilijaribu skuli nyinginezo katika Kenya lakini sikuweza kulipa ada ya juu. Mama alipendelea sana nipate elimu, akatumia pesa zote alizokuwa nazo, hata wakati mwingine hakupata chakula cha kutosha na hata dada zangu hawakupata nguo za kutosha. Ilikuwapo misanduku ya jamaa wa mama na wakati mwingine nilikata na kuuza magamba yake. Miti hii huota milimani katika risavu ya Wakikuyu na magamba yake hutumiwa kwa kutengeneza dawa ya ngozi ya viatu.

Mwaka wa 1941, niliingia skuli katika Bahati Forest. Mwalimu mkuu alikuwa James Giteni, mwalimu mwenye ujuzi aliyefundishwa katika misheni karibu na Kiambu. Skuli hiyo ilitawaliwa na Kikuyu Independent Schools Association (K.I.S.A.) ambayo ilianzishwa na viongozi Wakikuyu, baada ya kuachana na Dr. Arthur wa Church of Scotland Mission mnamo mwaka 1929 juu ya tohara ya wanawake. Pamoja na K.I.S.A., kikundi kingine kilianzishwa kwa jina la Kikuyu Karing'a Educational Association (K.K.E.A.) na vikundi hivyo viwili ndivyo tu vya Waafrika vilivyoongoza

mambo ya elimu wakati huo. Kabla ya kupigwa marufuku wakati wa Hali ya Hatari, skuli hizo ziliwapatia nafasi wale wanafunzi ambao wangalikosa kuendelea na masomo kama tulitegemea misheni au serikali, na baina ya wanasiasa washupavu ni mazao ya K.I.S.A. na K.K.E.A. James Gateni alichukua kazi hiyo kwa kuwa ilikuwa na mshahara mwema kuliko kazi nyingine angaliyopewa na wamisheni.

Katika Kenya skuli zilianzishwa na misheni na dini na elimu zimekuwa zimefunganika wakati wote. Skuli hiyo ya K.I.S.A. katika Bahati Forest ilihusiana na udini wa African Independent Pentecostal Church, ambayo ilianzishwa na Johanna Kunyiha, aliyekuwa mwanachama mashuhuri na mzee wa chama katika wilaya ya Nyeri, na ambaye alipewa nishani ya M.B.E. mwaka wa 1961. Aliyewakilisha kanisa lake katika Rift Valley alikuwa ni Petro Muchangariba ambaye alituhutubia wakati mwingine. Alikuwa msemaji wa nguvu aliyesema wazi juu ya maovu ya ubaguzi wa rangi na kuibiwa kwa vichaka vyetu na Wazungu; alifungiwa wakati wa Hali ya Hatari. Lakini siasa hazikujulikana kwa mtu wa kawaida katika sehemu hiyo wakati huo, ingawa tulizungumza juu ya taabu na wasiwasi kwa ardhi yetu ndani ya vyumba vyetu, kwenye moshi wakati wa usiku.

Ujuzi wa kutengeneza pombe halisi (kama vile *wareji*, *kang'arikia* au "nubian gin") haukujulikana hapa kwetu mbele ya Mzungu kufika hapa. Lakini wale askari wa Kisudani ambao walikuja nao walieneza njia kote nchini. Bila shaka ni njia rahisi ya kulewa sana na ilianza kuharibu tabia za watu wetu kwani hapo mbeleni ni wazee tu waliotumia pombe ya kienyeji ambayo haikuwa na ulevi kama huo. Mama alikuwa fundi katika kutengeneza pombe hilo la kinubi, hata akasifika kwa maili nyingi kuzungukia, na ilikuwa kiini cha maana cha pesa kwa ajili ya elimu yangu. Wakati wa kwanza wa vita, askari walitoka Lanet na Nakuru kuja kunywa pombe hiyo ndani ya chumba chetu. Kati yao walikuwamo Wazungu, Waafrika na Makaburu pamoja. Wakati mwengine walilewa sana hata wakapigana na kutukanana. Kaburu mmoja aliumizwa vibaya sana hata ikatulazimu kumficha msituni uliyokuwa karibu ambapo alilala siku tatu bila kujiweza. Tulikuwa na kinanda cha gramafoni na vitu vingine kutokana na pesa tulizopata kwa njia hii. Msaada mwingine uliotokana na vitendo vya ulevi kama kutapika na kelele ya kila aina ulinijia bila kujua kwani vitendo hivyo vilinifanya niape kuwa sitagusa pombe na sijagusa. Lakini mtu mmoja aliyeitwa Abraham aliona wivu kwa ajili ya kufaulu kwetu, na kwa kile kinanda chetu na yeye alituhaini kwa kachero wa polisi. Mama alikamatwa mwezi wa Septemba 1942 na akafungwa miaka miwili. Ingawa Gathoni, bibi wa pili wa baba, alinitunza, nilikosa furaha sana na punde si punde nikawa mnyonge na

mgonjwa. Siku moja nilimtembelea mama katika jela ya Nakuru. Hakuwa na ubaya lakini nililia kwa uchungu wakati nilipomwona na hizo kanzu nyeupe za jela. Nilimpa bibi askari wa jela hiyo aliyekuwa Msudani, kiasi cha shilingi 120/- ili amnunulie cho chote cha kumfurahisha hata chakula ikiwezekana. Hii ilikuwa ni kawaida, lakini wakuu wa jela hawakuwa na habari.

Mnamo 1944, Muturi aliondoka Kenya na tulihamia shamba lingine la Tyron maili mbili zaidi. Alipewa jina la *Karimiramithi* (Mkulima wa Mti mwenye Miiba) kwani alikataza kukatwa kwa miti yenye miiba, alisema ilikuwa mizuri. Tuliona hilo kuwa jambo geni. Tyron alikuwa na mahabusu wawili Waitaliano waliomfanyia kazi, mmoja Starino na mwingine Giuseppi. Walikuwa marafiki na wenye akili—walikuwa wajenzi mashuhuri. Starino alikuwa na kifimbo kilichokuwa na ramani ya dunia ndani yake. Nilitumia saa nyingi nikikiangalia. Walitengeneza firimbi za mikebe ambazo niliwauzia vijana wengine huko nikajipatia bashishi. Wakati mwengine wa jioni walituchekesha kwa miujiza ya uendeshaji wa baiskeli na kuimba nyimbo. Walikuwa na uhuru na waenda ovyo, na hivyo walipendwa na wasichana na hawakuwaepuka kama wale Wazungu wengine. Giuseppi alikuwa rafiki yangu hata alipokwenda kwao alinipa saa yake.

Tangu mama alipotiwa jelani, mambo yalikuwa magumu kwangu na dada zangu wawili. Matumaini yetu yalikuwa kuajiriwa kwa shilingi tatu kila wiki kwa kuokota maua ya "pyrethrum" kutoka asubuhi hadi jioni. Lakini hiyo ilikuwa si kazi ya mwezi, na nikamwuliza Tyron anipe kazi ya mwezi. Alipozisoma barua nilizopewa na Muturi, alinipa kazi ya karani yenye mshahara wa shilingi thelathini kila mwezi. Masikitiko ni kwamba hii kazi ilinilazimu kuwacha masomo katika skuli ya K.I.S.A. ambayo ilinitendea maajabu katika maisha yangu.

Kazi yangu mpya ilikuwa ya kuhesabu galani za maziwa na magunia ya mahindi na kuwazuia wafanyi kazi wa shamba wasiibe. Katika fikira zangu, hiyo ilikuwa ni kazi ngumu kwani watu wangu hawangeweza kujipatia mavuno ya kutosha katika vijishamba vyao na mara nyingi wao na jamaa wao walikuwa na njaa. Lakini sisi Wakikuyu tunayo methali inayosema *murimi ndaunagwo guoko* ambayo ikitafsiriwa ni kusema kuwa *anayefanya kazi shambani hulishwa humo*. Kwa hivyo niliwashauri wasichukue zaidi ya mahitaji yao. Mkamaji aliyeitwa Warui Wanjeri alipomaliza kumkama ng'ombe wake aliinama kwenye ndoo na kwa haraka akayanyonya hayo maziwa yakiwa bado moto moto. Kwa bahati mbaya, Tyron alimwona na baadaye akamwita na kumshtaki kwa kunywa maziwa. Warui alikana, na hapo Tyron akamwongoza kwenye kioo, akayashika masharubu ya Warui na kuyafinya na hapo Tyron akamwuliza kwa nini

yalimdondoka maziwa kama hakuwa amekunywa maziwa. Warui, ambaye alikuwa amesahau masharubu yake, aliyapanguza kwa aibu. Lakini hakufukuzwa; aliambiwa akiwa na haja sana atumie kikombe. Tyron alimweleza pia kuwa ng'ombe huyo hakuwa mali ya Warui.

Wakati nilishikwa na haja sana sana, nilizidisha mshahara wangu kwa kuuza nusu ya maziwa yaliyokamuliwa, ambayo yalikuwa ni ya kupewa nguruwe, senti tano kwa kila chupa kwa watu wa shamba. Wakati wa Krismasi, nilipeana chupa za bure kama zawadi kwa rafiki wangu. Tyron hakugundua michezo hiyo yangu.

Mama aliachiliwa Juni, 1944. Jirani wengi walitembelea chumba chetu kushangilia uhuru wake nami nikamchinjia beberu na tukafurahi sana. Aliniambia kuwa wafungwa wengine wa Kipsigis walimwonea wivu kwa msaada aliyopata kutokana na zile shilingi 120/- na ati walijaribu kumpa sumu. Alisaidiwa na yule askari mwanamke wa Kisudani. Ilionekana kama pesa yangu ilitumika vyema. Alieleza kuwa au si hivyo, jela ya Nakuru haikuwa mahali pabaya na maafisa na askari wa jela walimtendea vyema. Lakini kila wakati aliwakumbuka watoto wake na wakati mwingine alikuwa mgonjwa kwa kufikiri juu yetu.

Baada ya vita vikuu, niliendelea na kazi yangu. Mama alijaribu kunishawishi niendelee na masomo lakini haja yetu ya pesa ilikuwa mno hata nikaona vyema kuendelea kwa muda. Mwishoni wa 1946, nilikwenda kwenye mashindano ya farasi Nakuru. Nilikuwako mashindanoni hayo mara moja tu hapo mbeleni na nilikuwa bado kurudi humo. Nilijichukulia shilingi arobaini kutoka akiba yangu na nikanunua tikiti ya shilingi mbili kwenye mchezo—Nambari 124876. Niliomba na nikaikumbatia sawa kwa muda wa saa moja halafu nikaenda kwenye ubao ulioonyesha nambari zilizoshinda. Nambari 124876 . . . ! Nikatazama tena. Nambari 124876. Nikaketi chini na nikashangaa vile ningeweza kujihakikishia kuwa sikuwa ndotoni. Niligonga kichwa changu kwa mikono kama Mkikuyu na ikaonekana kama si ndoto. Wazungu hujifinya. Nikajifinya na nikasikia uchungu. Bila shaka haikuwa ndoto. Nilienda afisini ambapo afisa alinipa shilingi 1,600/- . . . shilingi elfu moja na mia sita—baiskeli nane . . . zenye taa na kengele . . . .

Niliukimbilia upande wa chooni na nikafikiria hatua nitakayofuata. Dunia yote ilijua nimeshinda na nusu ya dunia ilingoja kuninyang'anya ushindi wangu, ambao kwa ukweli ulikuwa mkubwa. Nilizikunja noti hizo ndani ya kitambaa cha makamasi, nikakifungia kwenye mshipi wangu halafu nikaufunga mshipi ndani ya suruali yangu. Mshipi, kitambaa na pesa hazingeonekana na ni mdanganyi mjanja sana angaliyevumbua pale pesa zilipokuwa. Nilianza kujifikiria kwa furaha lakini sikutosheka mpaka nilipofika nyumbani bila taabu. Nilibakiza shilingi thelathini na mbili

baina ya zile arobaini za kwanza, na hizi nilizitumia kuwanunulia dada zangu mavazi, na nikamnunulia mama shuka, blanketi na chakula. Niliharakisha kupiga mguu hadi nyumbani nikiwa peke yangu—hizo zilikuwa maili nane zenye wasi wasi. Niliwaepuka wote wale wangesafiri nami na nikakataa kubebwa na motokaa. Nilifika nyumbani wakati wa saa kumi na moja na nusu, nikawapa jamaa zawadi zao halafu nikawaambia juu ya bahati yangu. Walifurahi kupindukia usiku huo. Niliwaambia kwa furaha kuwa nitajipatia baisikeli kama ile ya Obadiah. Mama hakusema kitu bali alitwaa shilingi elfu moja na mia nne aweke salama na akanikubali niweke mia mbili. Miaka kadhaa baadaye, aliniarifu kuwa aliweka pesa hizo ndani ya kibeti cha ngozi ambacho alikifungia kiunoni mwake ndani ya nguo. Hatukusherehekea lo lote jioni hiyo kwani alinionya tusionekane kama wenye furaha watu wabaya wasije wakatushuku na kutudanganya.

Siku iliyofuata, mama aliniambia kuwa ni lazima tufanye mipango nirudi skuli na kwamba hakuna baiskeli itakayonunuliwa wakati huo. Tulitiwa nguvu katika shauri hilo wakati kijana mmoja aliyeitwa James Thuku Mangothi, aliyetoka Kihuri katika sehemu ya Othaya ya wilaya ya Nyeri, alikuja kuishi katika shamba hilo na akamsemeza Tyron kwa Kiingereza. Sasa ninafahamu kuwa Kiingereza hicho hakikuwa safi, lakini kwa ujinga wetu, tulifikiria ajabu jambo hilo, na likanifanya nikubaliane na mama. James sasa anafanya kazi Nairobi kama mpishi. Kwa hivyo, mwezi wa Februari, 1946, nilikwenda Nakuru African School na kurudia Standard V pale.

Mwishoni mwa mwaka huo, tulisikia kuwa utakuwako mkutano wa Waafrika wote katika Njoro ambako mtu mmoja aliyeishi Uingereza kwa miaka mingi atahutubu. Ilikuwa siku ya Jumapili, wakati wafanyi kazi katika Rift Valley walikwenda sokoni. Ingawa watu wa sehemu hiyo walihusiana kidogo tu na siasa, kila mtu alikuwa na hamu kumwona mtu mkubwa huyo aliyetoka London na kusikia maneno yake, ingawa wengi walifikiria kuwa hangeweza kusema kwa Kikuyu au Kiswahili baada ya kuishi nje ya nchi yake kwa miaka kumi na mitano. Wengi wa skuli walitaka kwenda na kwa hivyo komiti ya skuli ikakodi lori kutupeleka arobaini wetu huko Njoro. Tulipokaribia, tulikutana na malori mengine yote yakielekea kwenye mahali pa mkutano na wengine wengi wakienda kwa mguu. Wakati mkutano ulipoanza, lazima walikuwamo watu elfu nne au tano pamoja na watoto.

Watu wawili walihutubu ili kumjulisha Kenyatta. Hawakuwa wachangamfu kwani hawakuwa wamezoea kusema mbele ya watu na umati ulianza kutuonyesha hamu. Basi ni wakati huo Jomo Kenyatta mwenyewe alisimama mbele yao. Alikuwa na mkwaju uliopanwa alioushika ovyo mkononi na alivaa kile kizibao chake cha ngozi ya rangi ya ardhi. Alianza

kutusalimia kwa maneno ya heshima ambayo hutumiwa na kila rika. Matokeo ya sauti yake na binafsi ya kiwili chake yalichukua hatua mara moja kwa kuuvuta umati hata watoto wale wachanga kabisa wakanyamaza wakati Kenyatta alipotueleza juu ya aliyoyafanya Uingereza na juu ya hali ya nyumbani ya nchi yetu. Alichanganya Kikuyu na Kiswahili kwa njia ya ajabu na waliokuwa na wasi wasi walifahamu kwamba alijua misemo ya Kikuyu ya zamani zaidi ya vile walivyosikia hapo mbeleni.

Alisema kuwa hakupendelea Wazungu waondoke nchini lakini ulikuwa wakati waanze kujihadhari kama wageni wetu ndani ya nyumba yetu. Walitujia kama wageni, tukawapatia nafasi ndani ya nyumba yetu na sasa walidai kuwa nyumba yetu ni yao. Wakati wa zamani tuliwabeba bibi wao mabegani na kuwavuta kwa gari za mkono kutoka Mombasa hadi Nairobi ili miguu yao isichoke kwa kutembea kwenye nyika na misitu ya miiba. Wasisahau kuwa nchi wanayokanyaga ni yetu. Chini ya utawala wa serikali ya Mwafrika, Wazungu hawangekuwa na cha kuogopa, kama vile yeye, Kenyatta, Mwafrika, hakuogopa alipokuwa Ulaya chini ya serikali ya Mzungu. Wakati wa vita vilivyopita, tuliwapeleka vijana wetu waliotoa maisha yao kusaidia Waingereza kumshinda Mjerumani. Maafisa weupe walishukuriwa kwa kupewa tuzo za mashamba humu kwetu na wakapewa pesa za kuwasaidia kuyafanyia kazi. Askari Waafrika walipewa zawadi ya ubaguzi, ukosefu wa kazi na kipande. Haukuwako ubaguzi kutuzuilia tusife kwa ajili ya Waingereza wakati wa vita.

Wakati huo Kenyatta alituuliza sote tujiunge na tusahau ukabila. Ilitufaa tufanye kazi kwa bidii na tujaribu kuwaelimisha watoto wetu vizuri na kwa haraka kama iwezekanavyo ili waweze kuichukua serikali ya nchi. Wakati alipoketi chini, mabibi walimfanyia *ngemi* tano ambazo hupigiwa mtoto wa kiume akizaliwa na hupigiwa wale wasemaji wa kukumbukwa milele. Mkutano ulitawanyika pole pole, watu wakibaki huko na huku kwa vikundi vidogo wakibishana na kuzungumza juu ya mambo ya ajabu aliyoyasema na kuzungumza juu ya maisha ya nyumani ambayo angewaletea. Huu ndio mwaka ambao Kenyatta alianza kuwafundisha wananchi namna ya kupenda nchi yao. Wale ambao walikuwa wamekwama katika shida zao walianza kutumainia furaha. Kwa muda wa saa nyingi za usiku, watu waliendelea kuzungumza juu ya kiongozi wao mpya aliyetoka London, na matumaini mapya aliyowaletea, kote katika Rift Valley.

Mimi mwenyewe niligeuzwa kabisa na misemo yake na binafsi yake iliyowaka. Niliapa papo hapo kuwa nitamwunga katika kupigania haki na uhuru wa nchi yetu na nikajitoa kumfuata katika jitihada zake katika kuondoa taabu na kuwaletea watu wetu heshima.

Halafu kwa muda ya miaka minne, masomo yangu yalichukua

nguvu zangu zote. Mwishoni wa 1947, nilirudi shambani kwa baba ndani ya risavu ya Nyeri. Hali ya mambo ya huko haikupendeza na watu walionekana kuwa nyuma. Walipanda mimea yao kwa njia ya kuchanganya, tuseme ndizi pamoja na mahindi au maharagwe pamoja na mboga. Wachache sana walifahamu mambo ya siasa. Wale ambao walikuwa wakilima mashamba ya baba wangu hawakunifurahia. Walitumaini kuwa sitajua walivyofanyana na baba na walikuwa na hakika kuwa sitaweza kupata mbuzi au pesa za kuokoa mashamba ambayo baba aliwaachia. Lakini kwa upole, niliweza kuokoa mashamba yote na nikawakubalia wengine waendelee kulima kama "ahoi" (waombaji). Niliendelea na masomo yangu katika Kariko Primary School katika Chinga na katika Karema huko Othaya. Baadaye nilikwenda Kerugoya Intermediate School katika wilaya ya Embu. Skuli hizo zote zilikuwa za Kikatoliki. Mwaka wa 1950, kufuatia mapendekezo ya mwalimu mkuu wa Kerugoya, niliingia Form I katika King's College, Budo, Uganda, ambako nilikaa hadi nikatimiza miaka 21. Skuli hiyo ya "secondary" ilitawaliwa na Church Missionary Society.

Nilifurahia maisha yangu ya Uganda. Ingawa wakati mwingine ni vigumu kuingia ndani ya risavu ya Waganda, niliwahi kufanya urafiki wa kudumu na wengi wao. Wana bidii sana juu ya elimu na wanao vijana mashujaa wengi. Ni jambo la kusikitisha kuwa walipendelea sana hali ya kudumisha ufalme wao ambao kwa muda ulipinga maendeleo yao ya kupata uhuru. Wengi wao wanazo baiskeli na wanazitumia kwa njia za kushtusha: ni jambo la kawaida kuwaona mbuzi walio hai wamefungwa juu ya kiti cha nyuma wakipelekwa sokoni, na baiskeli nyingine hubeba mizigo mikubwa mno. Siku moja nilishangaa sana kwenye kijiji kimoja karibu na Budo wakati mwenye baiskeli aliifunga jiko juu ya kiti cha nyuma; alikuwa anaendesha baiskeli hali alikuwa anamenya viazi, akazipika na kuzila bila kuondoka juu ya baiskeli.

Wakati huo nilipokuwa Uganda nilifikiwa na habari ya kuhuzunisha ya vile watu walivyokuwa wanataabishwa katika mapambano yao na masetla Wazungu. Kutokana na marafiki waliotembelea Uganda na Wakikuyu waliokuwa Kampala, nilisikia juu ya kuongezeka kwa makasiriko na uchungu katika Kenya: nilisikia juu ya ukatili ulioumwa na wananchi kwa ajili ya ubaguzi wa rangi, nilisikia juu ya ukosefu wa ardhi, ukosefu wa nafasi za masomo, ukali wa waliotawala na vile wananchi walinyimwa nafasi kuingia ndani ya Legislative Council. Nilikuwa na shughuli nikijitayarisha kwa mitihani yangu kwa hivyo sikuweza kufanya lo lote kutoka Kampala wakati huo. Kwangu ilinilazimisha kwanza kujitayarisha kwa elimu, nivae silaha za ujuzi na nijipatie nguvu inayotokana na kusoma na kuandika. Lakini ilionekana wazi kwamba mnamo mwaka 1951 na 1952

Serikali ya Mwingereza ingalikubaliana na madai ya Waafrika ama tungalielekea msiba mkuu. Sikushangaa wakati nilipokuwa nangoja matokeo ya mtihani wangu wa School Certificate katika Kenya, kusikia mnamo tarehe 22 Oktoba, 1952, kuwa Kenya ilikuwa imetangazwa kuwa katika Hali ya Hatari siku mbili zilizopita, na yule Gavana mpya, Sir Evelyn Baring.

2 K.C.A., K.A.U., na 'Mau Mau'

KWA MUDA WA miaka kadhaa tangu Waingereza, katika mfano wa akina Lord Lugard na wengine, walipofika nchini mnamo miaka ya 1890, aina nyingi juu ya historia ya Kenya zimeandikwa. Kwa vile ni wachache tu baina ya wananchi walioweza kupata elimu, karibu hizo zote ziliandikwa na Wazungu, wakikusudia kutukuza ushindi na uanzishi wa wengine kama Lord Delamere, huko wakiongeza chumvi juu ya uzuri wa nchi na ujinga wa mwananchi. Wakati mwingine imenichekesha sana kusoma kwa sauti kubwa mengineyo yaliyo uwongo mtupu na yaonyeshao kutofahamikiwa ndani ya vitabu vinginevyo vinavyozungushwa katika nchi hii kwa jina la "historia". Hali hiyo imenihuzunisha kwani ni maongozi ya aina hiyo ambayo yawezekana ndiyo zaidi yalileta mzozo wa 1952.

Nilikuwa nje ya Kenya kwa muda wa miaka minne mbele ya wakati huo, lakini masaa yasiyohesabika niliyoyatumia nikizungumza kwenye moto yaliniwezesha kujua hadithi ya vile watu wangu walikuwa wakipigania uhuru tangu zile siku za uhuru wao wa mbeleni. Hapo kwanza wakati Waingereza walipofika na wamisheni wao, wafanyi biashara na watawala, tulifikiria kuwa walikuwa wanayo mambo ya kutufundisha ambayo yalikuwa mema. Elimu, dawa, ujuzi juu ya ukulima na viwanda—haya yote yalikaribishwa. Wakiwa kama kabila la pekee, Wazungu walikuwa wanazo tabia zinginezo, ambazo labda, hazikupendeza. Walikasirika upesi, si wakarimu, walijitenga na watu, walijivuna na wasiojali; mara nyingine walitenda kama vile Mungu aliiumba Kenya na sisi kwa ajili yao. Walikubali heshima ya binadamu ikiwa yeye alikuwa na ngozi nyeupe. Sasa nitaendelea kuwaelezeni mengineyo ya yale waliacha fikirani mwetu, ingawa kunao wengine wao waliokuwa tofauti.

Labda ni machache tu juu ya haya yangekuwa ya maana kama Serikali ya Uingereza haikulazimishwa na vikundi vingine mapema katika miaka ya 1900 huko Uingereza na Magavana wengine ambao hawakutii kukubali maongozi ya kuchukua vichaka vyetu na kuwapa Wazungu kuvilima. Hicho ndicho kilikuwa kiini cha taabu zote zilizofuata. Wengi wetu hawakuwa na vichaka vya kutosha wakati huo. Katika miaka iliyofuata,

kwa vile watu waliendelea kuzidi, ukosefu wa ardhi ulikuwa kama ugonjwa, na vijana wetu waliokosa ardhi walijiona wakifanya kazi ya mishahara ya kusikitisha katika mashamba makubwa ambayo hapo mbeleni yalikuwa ya baba zao na ambayo sasa iliwaletea wageni (Wazungu) nyumba kubwa na mitokaa ya "Jaguar."

Hatari iliyofuatana na hali hiyo ni yale majaribio ya Wazungu juu ya kutaka kutumia siasa ili kupinga maendeleo ya Mwafrika kwa kila njia. Hawakuwa zaidi ya 60,000 baina ya umati wa 7,000,000 (wa Waafrika) na hakuna hata mmoja baina ya hao 7,000,000 aliyekuwa na kauli katika serikali ya nchi hadi mwaka 1950. Waafrika wa Kenya walitawaliwa na kuongozwa ikikusudiwa watasaidia kuendesha mahitaji ya uchumi wa masetla Wazungu. Sheria za ufanyi kazi, kodi, elimu, kila kitu kilifanywa kulingana na mapendekezo ya Wazungu. Wakati huo huo, wengine wa waheshimiwa Wazungu, hapa Kenya na Uingereza, walijaribu kuondoa maovu mengineyo yaliyokuwa wazi nayo Serikali ya Uingereza, ambayo ilikuwa na bidii kutengeneza mfano wa serikali ya kikoloni, ililazimishwa kutoa elimu. Elimu ilikuwa ni muhimu kwani ndiyo ilitupatia silaha za kupigana kama wale waliotupinga. Viongozi wengine Waafrika walikuwa na uwezo wa kutuongoza na mnamo mwaka wa 1920, hivyo, vita virefu vikaanza; tangazo la Devonshire White Paper la 1923 liliahidi kuwa mahitaji ya walio wengi (Waafrika) yatatangulia; upinzani ulifanywa juu ya kuwako kwa Shirikisho la Afrika Mashariki lililoongozwa na Wazungu katikati ya 1927 na 1932; tena ilikuwako ile Halmashauri ya Ardhi—Carter Land Commission—na matembezi kadhaa ya Jomo Kenyatta huko nchi za Ulaya. Nia yetu hapo kwanza ilikuwa kucheleweshe kwa njia yo yote hatua yo yote ambayo ingewapa Weupe hiyo nguvu ya mwisho ya utawala, na wakati huo tukajijengea kundi la wananchi wenye elimu ambao baadaye wangaliweza kutwaa utawala kama haraka ilivyowezekana.

Baada ya vita vya 1939-45, kwa vile uhuru uliharakishwa penginepo ndani ya Asia na Afrika, Weupe katika Kenya walianza kusindikiza mambo. Kati ya mwaka 1946 na 1951, walitafuta, pengine kwa njia zilizokosa imani, kujenga na kupanua uwezo wao ili usije ukasitizwa kamwe hata milele. Waafrika waliona kuwa hali ya mambo ilifikia wakati ambao labda jitihada za mwisho zitahitajiwa. Jambo muhimu lilikuwa juu ya kuwakilishwa katika Legislative Council, na wakati maombi ya upole yaliyofanywa 1951 yalipopingwa na Serikali ya Uingereza ya Leba, ilionekana mkazo zaidi lazima utiwe ndani ya vyama vya ndani vya Waafrika. Ni katika hali hii, na ikifahamika wazi kule kujitolea kungefanyika ikiwa maonyo yao hayakujaliwa na Serikali ya Uingereza, Waafrika walianza kujitayarisha kutenda la mwisho ambalo lingepinga kuondolewa

kwa nuru ya uhuru kwa mara ya mwisho. Umoja wa idadi ulikuwa silaha yetu iliyokuwa na nguvu zaidi, na ilionekana kama ndio silaha tu tuliobakiza, na mipango ya kuzidisha nguvu umoja huo na kuuhifadhi kwa njia ya kiapo ilianzishwa. Bila shaka ikiwa wakati wo wote Serikali ya Uingereza ilionyesha kuwa ilikusudia kwa ukweli kuipa Kenya uhuru chini ya Serikali ya Mwafrika kwa muda uliofaa, hatua kama hiyo ingelizuilia mengi ya yale yaliyofuata. Hakuna maagano kama hayo, ambayo yangeturudishia imani juu ya urafiki wa Mwingereza, yaliyofanywa. Hayo ndiyo yaliyotangulia kabla ya mimi kurudi Kenya mnamo mwezi wa Oktoba, 1952.

Ni hapo stesheni ya reli ya Eldoret katika safari yangu kutoka Uganda nikielekea Nyeri niliposoma katika *Baraza* kuwa kumetangazwa Wakati wa Hali ya Hatari. Gakeri, rafiki yangu aliyefanya kazi katika reli na aliyefungiwa baadaye, alinipa malazi kwake usiku huo katika Nakuru, na ilinishangaza kwamba wengi wa wale waliokuwako huko walikuwa bado kusikia juu ya Hali ya Hatari. Bila shaka habari ya aina hii ilipaswa kusafiri mbio zaidi kuliko gari la moshi. Asubuhi yake, tuliwakuta wengine waliotoka pande za Nyeri. Walisema kuwa mambo yalikuwa mabaya sana huko, na kwamba risavu ilikuwa mahali pa vijana ambao walikamatwa na kukimbizwa kwa mashitaka yasiyo na maana. Wengi wao walikuwa wamekimbilia misituni kuepukana na hali hiyo. Nilifikiri ni ujinga katika hali hiyo kujaribu kumwona mama huko Nyeri, lakini hata hivyo nilikataa kukaa Nakuru bali nikaenda kwa Wangui, dada ya mama yangu, ambaye aliishi na shemeji wake aliyefanya kazi ya kibarua katika Idara ya Misitu huko Bahati ambako kazi yao ilikuwa ya kukata miti isiyotakikana.

Nilikaa kwa Wangui kwa mwezi mmoja, huko nikijipatia riziki kwa kufanya kibarua mashambani ya wafanyi kazi wa msitu, ambao kila mmoja wao alipewa kishamba kwenye mashamba mapya ya miti ndani ya mipaka ya msitu. Walikusudiwa kulima vishamba hivyo kwa miaka mitatu na kulima kwao kulisaidia miti kuwa na mizizi. Baada ya miaka mitatu walipewa vijishamba vingine katika sehemu nyingine iliyokaribia kupandwa miti mipya, na waliendelea kama hapo kwanza. Waliishi juu na chini ndani ya msitu hapo Bafuni, ambapo palipewa jina hilo kwani palichongoka kutoka kilimani kama ubavu wa mwili. Ilikuwa sehemu nzuri ya Rift Valley, na wakati wa usiku nililala nje huko nikijitazamia ukingoni mwa nchi, macho yangu yakitembelea milimani ya Njoro myeusi, kupitia kwenye wekundu, uzambarau na ubichi wa mwanga ulionimetametea kutoka bondeni chini zaidi.

Nilitembelea Nakuru wakati mwingine na muda si mrefu nilikata shauri kujiunga na tawi la Kenya African Union. Ule moto ulioniwasha tangu nilipomsikia Kenyatta mara ya kwanza huko Njoro mwaka wa 1947

ulikuwa bado haujafifia, na sasa nilikuwa na hakika zaidi ya hapo mwanzoni kwamba ulikuwa wajibu wangu kutoa maisha yangu kwa kupigania uhuru wa watu wangu. Mwenye-kiti wa tawi la Nakuru la K.A.U. alikuwa John Kamonjo, aliyekuwa mfanyi biashara mashuhuri aliyekuwa amejulikana hivi kijuu juu tu na mimi kwa miaka kadhaa. Nilipomwomba aniachilie mimi kujiunga na K.A.U. alicheka kidogo kwa majibu yake na akauliza kwa nini mtu ambaye alikuwa bado ananyonya mama yake afikirie kuingia chama cha siasa. Wakati huo, polisi wa tawi la pekee (special branch) walikuwa wanatumia pesa nyingi wakijaribu kujua yote juu ya chama na kwa hivyo ilimlazimu kujihadhari. Nilimweleza yote niliyoyafikiria juu ya watu wetu. Alitosheka na maelezo yangu kwani nilipolipa ada ya shilingi tano, nilipokea kadi ya chama—No. 745. Nilifanya haraka kurudi nyumbani na nikampa shangazi yangu kadi hiyo aniwekee. Niliogopa isije ikapotea. Alisafisha chupa moja aliyokuwa akiitumia kwa kuwekea chumvi, akaitia kadi ndani, halafu akaizika chupa hiyo mbali shambani mwetu.

Sasa nilianza kuwaingiza wengi katika K.A.U. katika Bahati na kwa muda mfupi nilikuwa nimewaingiza wanaume kumi na sita na wanawake kumi na tisa kuwa wanachama. Baadaye nilijua kuwa wengine wao walikuwa wamekula kiapo cha umoja. Kwa muda wa miaka kumi iliyopita kumekuwako na mazungumzo mengi juu ya uhusiano kamili baina ya Kikuyu Central Association, Kenya African Union na Mau Mau. Misemo mingineyo juu ya uhusiano huo iliongoza vibaya, na hiyo ni pamoja na ile inayoonekana ndani ya *Ripoti ya Corfield.* Bw. Corfield hakusema popote kama alipata ushahidi kutokana na mmojawapo waliokuwa mamemba wa vikundi hivi vitatu. Ningetaka kusema wazi vile hali ilivyokuwa kama nilivyojua.

Kikuyu Central Association ilifuatia nyayoni za Young Kikuyu Association iliyoanzishwa mwaka 1921 na Harry Thuku aliyehamishwa akapelekwa Kismayu mwezi wa Machi, 1922, hatua ambayo ilizusha matata Nairobi. (Baada ya kutoka mahamishoni mwaka wa 1930, Harry Thuku alitajirika kama mwenye shamba, mkulima aliyeongoza na mpole katika siasa. Alikuwa mmojawapo wa "waaminifu" mashuhuri wakati wa Hali ya Hatari). Viongozi wapya, Joseph Kang'ethe, na Jesse Kariuki, walifikiria kuwa jina *Young* Kikuyu Association halikutosha. Hilo *Young* lilifutwa na badala yake likabandikwa Central kwa sababu chama kilifunguliwa kwa wote katika jimbo la Kati hata wale wasiokuwa Wakikuyu kama Wameru na Wakamba. K.C.A. kilikuwa ni chama cha siasa, kilichonuia kurudisha ardhi iliyopotea, uwakili zaidi katika siasa, nafasi zaidi kwa elimu, kupinga udanganyifu kwa wafanyi kazi katika mashamba ya Wazungu na kumaliza kodi ya nyumba. Jomo Kenyatta alifanywa katibu mkuu wa

K.C.A. mwaka wa 1928 na akakiwakilisha mbele ya vyama kadhaa huko Uingereza. Kilifungwa na Serikali mwaka wa 1940 (Mei 30) kwa ajili kilifikiriwa kilifanya uhusiano wa uhaini na waliowakilisha Wa-Italiano na wengi wa viongozi wake walifungiwa Kapenguria.

Wakati mojawapo 1920, kufuatia kiapo kilichotumiwa na Young Kikuyu Association, K.C.A. ilianzisha kiapo rahisi cha kuhimiza uaminifu kwa chama na kuheshimu ardhi yetu. Kiapo hicho kilijulikana kama *muma wa chuba* yaani kiapo cha chupa ambacho kilipewa mtu akiishika Bibilia kwa mkono wa kushoto na udongo katika mkono wa kulia. Kama viapo vinginevyo kote duniani, kiapo hiki kilikuwa cha siri. Mara nyingi tulizungumza juu ya viapo vya Wazungu kama vile "Freemasons" tulipokuwa tumefungiwa, ambavyo pia vilifanywa kwa siri saa za usiku, na tulishangaa kwani vyetu vikafikiriwa viovu zaidi.

Baada ya vita vya 1939-45, wanasiasa kadhaa Waafrika, pamoja na James Gichuru na Eliud Mathu, walianza chama kingine cha siasa chenye shabaha kama zile za K.C.A. Walikata shauri kutofufua K.C.A. kwa sababu mbili: kwanza ingekuwa rahisi kuiuliza Serikali ikubalie chama kipya badala ya kuuliza kufunguliwa kwa K.C.A., ambacho kilikuwa ni kama mbwa mwenye jina baya kulingana na maoni ya Serikali. Pili, wakati ulikuwa umefika wa kuanzisha chama cha nchi yote cha makabila yote hatua ambayo haingewezekana jina la "Kikuyu" likiwamo. K.C.A. kilikuwa tu ndicho kilichowezekana wakati wa giza wa siasa za Kenya, lakini wakati ulikuwa umefika wa kufanya makubwa zaidi. Eliud Mathu alihitaji chama ambacho kingemwambia vile angalivyosema katika Legislative Council ambayo aliingizwa bila uchaguzi mwaka wa 1944. Wakati Jomo Kenyatta aliporudi kutoka Uingereza, alikubaliana na maongozi hayo kamili. Yalikuwako majaribio ya kumkemea Kenyatta kama mwanakabila halisi Mkikuyu. Lakini hakuna mtu mwingine katika Kenya ya leo ambaye anapendelea utoukabila na anayependelea Uafrika zaidi yake. Wakati wa kesi kuu ya Kenyatta, washitaki walifuatia sana juu ya barua moja aliyokuwa nayo wakati aliposhikwa iliyoandikwa mwaka wa 1948 ikiwauliza wanachama wote wa zamani wa K.C.A. wahudhurie mkutano. Katika *Ripoti ya Corfield* anasema: " . . . Mau Mau, mazao halisi ya K.C.A. ambacho ndicho chombo ambacho Jomo Kenyatta na rafiki zake walikusudia kutumia Wakikuyu wafanye kama alivyotaka." Mshitaki wa Serikali katika kesi hiyo na Corfield katika ripoti yake, waligeuza na kutia chumvi cho chote kilichowezesha kupanua maoni kama hayo, kwani ilikuwa ni muhimu watafute njia ya kuficha ujinga wao walipomshika Kenyatta, wakati walipomwondoa mtu mmoja tu ambaye angeweza kuwashauri na kuwapoza wasiowezekana, hapo wakafungua njia ya uhalifu usiyopimika kutoka pande zote mbili uliofuata. Lakini barua hiyo

haikupelekwa, na hata kama ilipelekwa, yale yaliyosemwa juu yake hayakuwa ya ukweli. Mkutano ulikuwa umeitwa ili maongozi hayo mapya yaelezwe viongozi wa zamani wa K.C.A. Katika Nyeri mwezi wa Desemba, 1960, K.A.N.U. iliitisha mkutano wa memba wa Komiti ya K.A.U., viongozi wa K.C.A., waliofungiwa na "waaminifu." Mkutano huo haukufanywa ili kufufua vile vyama vya zamani, bali ulikuwa wa kueleza juu ya chama kipya na kuwaleta wote pamoja. Wala hakuna ushahidi kuunga maoni ya Corfield kuwa "Mau Mau" ilikuwa mazao halisi ya K.C.A. Vile kuwa wengi wale walikuwa maafisa wa K.C.A. walikula kiapo si ushahidi kuwa vyama hivyo vilikuwa sawasawa. Watu wengi zaidi wasiokuwa wa K.C.A. walikula kiapo zaidi ya wale waliokuwa wa K.C.A. Pia kusema kuwa kwa sababu maafisa wengine waliokuwa wa K.C.A. walifanywa maafisa wa K.A.U. vyama hivyo viwili vilikuwa kimoja si ushahidi wa kutosha. Kama ulikuwako ushahidi wo wote ni ule wa kusema kulikuwako na wanasiasa Waafrika wachache sana katika Kenya na maafisa hawa waliendelea kuaminiwa na wananchi.

Kenya African Union iliendeshwa na Gichuru na Mathu kutokana na Kenya African Study Union walioanza mwaka wa 1944. Mwaka wa 1946 walifuta jina "Study" lililoonyesha kama ni chama cha elimu badala ya siasa. K.A.U. kilikuwa ni chama cha nchi yote cha Waafrika kilichofunguliwa makabila yote na chenye mipango ya siasa ya upole. Wanachama wa K.A.U. hawakula kiapo. Miaka iliyofuata kutoka 1947 hadi 1952, K.A.U. ilikuwa na matumaini machache ikifuatia mwendo wake wa siasa za upole. Jomo Kenyatta mwenyewe aliambiwa na Gavana ajizoeze katika siasa za serikali ya kienyeji na asijifikirie kuwa alistahili kiti katika Legislative Council: matusi hayo yalimwalika kuwa mshupavu wa kupita kiasi. Vile miaka ilivyopita bila maendeleo au maagano katika siasa, washupavu ndani na nje ya chama walikuwa wanaendesha mambo, huko wakiwaachilia wengine, kama Kenyatta, ambao walijaribu njia ya katikati. Wale watu wastani walilazimishwa kuchukua hatua kali wakijaribu kuzuia mlipuko mkubwa katika nchi. Ardhi yetu nzuri ilikuwa yatolewa sadaka baina ya pembe mbili zisizokubaliana za Serikali ya Uingereza na ya Kenya—kuwaleta masetla Wazungu waliotumainia haki za pekee kwa mkono mmoja, na ule uwongo wa mdomo juu ya demokrasi na maendeleo ya Mwafrika kwa mkono mwingine.

Sasa yanilazimu nieleze juu ya chama hicho kilichopewa jina la "Mau Mau." Baada ya vita vya 1939-45, mambo yalianza kugeuka. Manung'uniko yetu juu ya mambo ya starehe na uchumi yalikuwa wazi na sasa kulikuwako na Waafrika wengi zaidi walioelimika na waliofahamu kuwa mambo ya starehe hayakulingana. Maelfu walikuwa wamerudi kutoka jeshini kama wana-K.A.R. katika mahali pengi duniani. Kutolewa uhuru kwa India na

Pakistani, jitihadi ya uhuru iliyoendelea Ghana na habari zilizotangazwa ndani ya magazeti juu ya mambo kama hayo na habari kutoka kwa radio, hayo yote yaliendelea kuwaamsha Waafrika wa Kenya juu ya siasa. Mengi ya hayo yalitendeka miongoni mwa kabila langu mwenyewe la Wakikuyu.

Kwa muda mrefu wamekuwa juu ya gari la siasa; waliishi wengi pamoja kwenye risavu zisizoendelea, pengine wakiwa zaidi ya elfu moja kwa maili moja mraba; walikuwa na uchungu mwingi kwa ajili ya ardhi iliyonyakuliwa, na bila hiyo ardhi hawakuwa na usalama wa dini au wa starehe. Wakati Wazungu walipofika nchini kwanza, Wakikuyu walipigana nao wakiongozwa na Waiyaki Hinga, wakilinda ardhi yao. Wengi wao waliuawa na mganga aliyekuwa akiwashauri aliwaambia waache vita au kabila lote litamalizwa. Alitumia methali moja ya Kikikuyu inayosema *Mundu ti mwahu wa irigu oragagwo o umwe o umwe* ambayo ni kusema kuwa binadamu si mkungu wa ndizi wawe wakiuawa mmoja mmoja. Waiyaki, ambaye walifanya undugu wa damu na Lugard, alikufa baadaye katika Kibwezi wakati alipokuwa safarini ya kwenda pwani alikohamishiwa. Haitoshi kusema kuwa Wazungu walikuwa na hati ya ardhi na kwamba walichukua ardhi ambayo haikuwa na watu. Wakikuyu kwa kweli walifikiri kuwa babu zao ambao hawakuwa na elimu hawakufahamu yale waliyolazimishwa kufanya na masetla na watawala, wala hawakuwa na silaha au uwezo wa kukataa maombi yale waliolazimishwa kukubali. Kama Wazungu hawakuingia nchini, Wakikuyu wangeingilia misitu ya Nyanda za Juu za Weupe pole pole. Kama sehemu ilikwisha, wangefikiria la kufanya tena. Lakini kama ilivyokuwa walipigwa mweleka. Wakati huo huo walinyimwa heshima kwa ajili ya ubaguzi wa rangi. Wazungu wengi walikataa kusema Kiingereza kwa Waafrika walioelimika isipokuwa kwa Kiswahili; watu wakubwa waliitwa "boy" (watoto wa kiume) na "nyani"; Waafrika walikatazwa kuingia mahoteli na vilabu vya Wazungu; Waafrika waliokuwa na mashamba karibu na ya Wazungu walikatazwa kukuza kahawa; hapakuwa na heshima ya kibinadamu kwa ye yote aliyekuwa na ngozi nyeusi.

Njia za kawaida za siasa zilizotumiwa na K.A.U. hazikufika po pote. Vijana wa kabila hilo waliona kuwa wakati ulikaribia ambao maumivu mengi yatakuwako ili wapate kile walichoaminia. Ni rahisi kwa ye yote anayejua watu wangu kwamba walikata shauri kwa kauli moja kwamba wajiunge pamoja kwa kula kiapo rahisi. Kutokana na vile nimesikia, kulishwa kwa kiapo kulianza katika wilaya za Kikuyuni, kuanzia Kiambu. Hapakuwako na uongozi kutoka katikati. Kiapo hapo mwanzoni hakikuwa na mengi wala hakikukataliwa kabisa. Kilianza pole pole, bila shaka kwa njia ya kusikitisha, na kilikuwa kiapo cha umoja na undugu katika vita vya kupigania uhuru na ardhi yetu. Kilienea nchini kote miongoni mwa

watu waliokuwa na hamu kudumisha heshima na kupinga kutishwa na Serikali iliyokuwa ya Wazungu. Ingawa hali ya mambo ilikuwa yenye hatari hata Oktoba, 1952, haikuwa ya hatari kuweza kuzuilia mageuko ya mambo kwa kufanya maagano machache ya siasa (ambayo leo, miaka kumi baadaye, yaonekana ya kitoto) na kufahamikiana kidogo. Chama hicho kingalimalizika kwa njia hiyo, lakini Serikali ilichagua kutumia ukatili wa kinyama ambao haujafanyiwa wenyeji penginepo katika Dola ya Kiingereza katika karne ya ishirini, na kwa hivyo chama kikaendelea kwa vitendo vilivyofuatana na vitendo hata ikawa ni vita vya kukataa serikali ambayo ilihusu moyo wa watu wangu.

Ingawa wengi waliokuwa maafisa wa K.C.A. walikula kiapo hicho kipya, hicho hakikuhusiana na K.C.A. au na kile kiapo cha zamani cha K.C.A. Tena ningependa kuhimiza kuwa katika misemo yote iliyofanywa na wafungiwa maelfu juu ya kula kwa kiapo, jina la Kenyatta halikutajwa kamwe kuhusiana na kiapo. 'Mzee' alikuwa angali anajaribu kuifanya Serikali ya Kenya ione ukweli ulipo kwa njia nyinginezo. Nitarudia kwamba hapakuwako na uongozi wa katikati wa chama hicho ambacho kilizuka tu kutoka mizizini ya nyasi. Wakati mambo yalichacha sana kati ya 1952 na 1954, kilifanya kamiti za lokesheni ndogo na malokesheni katika Nairobi, wilaya za Kikuyuni na katika jimbo la Rift Valley, na kamiti hizo ndizo zilisimama kati ya risavu na porini na misituni na kazi yao ilikuwa ni kutafuta vifaa na chakula na kuwapelekea mashujaa misituni au porini. Hapo mwanzoni, hali ya siri na ukosefu wa uongozi kamili wa chama uliwapatia wale mikora wa kawaida nafasi ya kujificha ndani yake ambao ni hatari kwa serikali au watu wo wote. Wakati mwingine, mikora hao walitumia jina la chama hicho ambacho kilianza kama cha umoja baina ya binadamu waliopotewa na tumai. Kama Serikali iliwapa wananchi dalili ya haki, yawezekana Kenyatta na wapiganiaji wengine wa katiba ya uhuru wangepata nafasi ya kuwatuliza Wakikuyu. Lakini kama ilivyotukia, Kenyatta mwenyewe alichukiwa na mikora wengine na kuna ushahidi wa nguvu kuwa ilikusudiwa kumwua katika mkutano uliokuwa Kaloleni Hall na katika maziko ya Senior Chief Waruhiu, aliyeuawa kwa bastola tarehe 7 Oktoba, 1952.

Ni wachache wanaojua chanzo cha "Mau Mau." Kenyatta alisema mara nyingi kuwa hakujua ni nini wala watu wake hawakujua. Ingawa majaribio yamefanywa na Corfield na katika kesi yake kuwa huu ni ujanja wa misemo miwili katika Kikikuyu, Kenyatta hakusema zaidi au chini ya ukweli.

Hiki ndicho chanzo halisi cha jina "Mau Mau." Watoto wa Kikuyu wakati wanapocheza pamoja mara nyingi hucheza na maneno. Wakati nilipokuwa mtoto, niliwaambia wengine: "Ithi, Ithi" badala ya "Thii Thii"

(maana yake "Enda, Enda" ambayo ingesemwa kama "Ndae Ndae" kwa mfano wa kwanza) na "Mau Mau" badala ya "Uma Uma."

Jioni moja, watu walikwenda katika nyumba moja katika sehemu ya Naivasha ambako kiapo kingelishwa. Ilikuwa ni kazi ya mlishaji wa kiapo kuhakikisha kuwa alikuwako mlinzi aliyefaa wa kuangalia nje wakati kiapo kiliendelea. Wakati huo, mlinzi huyo aliambiwa kuwa kama akisikia vishindo vya miguu na ashuku kuwa polisi waja, au adui waja, aseme "Mau Mau" ili wale walio nyumbani watoroke. (*Uma Uma* ikitafsiriwa ni kusema *Ondoka Ondoka*). Ni wale tu waliokuwa nyumbani wangejua na kumfahamu kwani adui hangefahamu maana ya "Mau Mau."

Usiku huo, polisi walikuja kwenye nyumba hiyo na mlinzi akapiga kelele kama alivyoambiwa. Watu waliondoka nyumbani. Walipoingia ndani, polisi walikuta vile vyombo vya kulishia kiapo lakini hapakuwa na mtu. Walipofanya ripoti katika hedikuota, walisema walisikia jina "Mau Mau" walipokaribia nyumba lakini walipofika nyumbani hawakumkuta ye yote isipokuwa hivyo vyombo vya kazi. Tokea wakati huo, kiapo cha umoja kilipewa jina la "Mau Mau". Lakini wanachama hawakukiita chama chao "Mau Mau."

Nimeambiwa kuwa jina la "Mau Mau" lilitumiwa punde kidogo katika Rift Valley na Mkikuyu mmoja aliyeitwa Parmenas aliyekuwa kiongozi wa nguvu wa Protestant aliyetokana na kanisa la Kiamerika la Inland Mission ya Kijabe. Parmenas Kiritu baadaye alikuwa kiongozi wa "Torch Bearers", kikundi cha Waafrika "waaminifu" kilichotungwa na Wazungu katika wilaya ya Naivasha. Wakati Parmenas aliposikia juu ya chama hicho kipya na kiapo kilicholishwa watu, alikifikiria kuwa hakikupendelea Ukristiano. Kwa hivyo alianza kukipinga katika mahubiri yake. Parmenas alijua vile watoto wa Kikuyu walitaja jina "Mau Mau." Alifanya ile kawaida yake ya kufanya madharau juu yake kuwa ni jambo la utoto. Baada ya hayo, wengi ambao hawakujua juu ya chama walianza kutumia jina hilo na likaenea kote nchini.

Yanipasa niseme wazi kuwa chama hicho hakikuwa na jina kamili. Dunia yakijua kwa lile jina kilichopewa na mojawapo waliokipinga sana. Parmenas Kiritu alipewa nisha ya B.E.M. kwa ajili ya kazi yake kwa Serikali. Kulingana na hayo, ni jambo la kuchekesha na kusikitisha kuwa Jomo Kenyatta alifungwa kwa ajili ya kuongoza chama kisichokubaliwa na sheria kilichoitwa "Mau Mau."

3 Kiapo Chenyewe

MIMI MWENYEWE nilikula kiapo mara mbili. Jioni ya Desemba 20, 1953, rafiki yangu aliyeitwa Kanyoi Githenji, ambaye hapo mbeleni alikuwa mwanafunzi mwenzangu katika K.I.S.A. ya Kabati-ini, alinitembelea nyumbani kwa Wangui. Alinialika chai kwake nyumbani. Tulipokuwa twanywa chai, yeye alienda nje mara kadhaa na wakati mmoja nilimsikia akimwuliza mwingine kama aliwahi kuupata "mukuha." "Mukuha" ni aina ya ndoana inayotumiwa kwa kuondoa tekenya au kuunganisha vibuyu vilivyovunjika. Ilipokuwa giza, alitaja kwamba tufanye matembezi mafupi nje. Baada ya kutembea kiasi cha yadi mia tatu hivi, tukipitia kwenye kichorochoro chembamba kilichoelekea mashambani, mara tulivikuta vikundi vya wanaume na wake wakiketi kwenye mahindi kwa upande wa kushoto, na huko upande wa kulia niliziona ndizi mbili zenye urefu wa futi sita au saba hivi, ambazo matawi yake yaliunganishwa huko juu ambako yalifungwa majani ya maharagwe na "mugere."

Nilishangaa sana kuziona hizo ndizi kwani katika ujuzi wangu, hapakuwa na ndizi katika Rift Valley, lakini Kanyoi aliniarifu kuwa zilikatwa kutoka msituni wa Kabati-ini katika shamba la Kaburu Chege ambaye nilimjua na aliyekuwa ameishi msituni huo kwa miaka mingi. Kanyoi alionekana akiiga tabia zisizo za kawaida jioni hiyo, na kwa njia fulani nilidhania mapema yaliyoelekea kutendeka. Niliambiwa niende kwenye wengine watatu ambao niliwajua. Tulikuwa tutakula kiapo pamoja. Hapo tukaamriwa kuondoa viatu, saa na kila kitu kilichokuwa na chuma tulichokuwa nacho. Kanyoi aliwaambia wale wengine kuwa mimi nilikuwa mwanafunzi kutoka shuleni aliyeonyesha dalili za haki za kupendelea kuisaidia nchi na aliyefanya jitihada kuu kuwashawishi wananchi kuingia ndani ya Kenya African Union. Kwa hivyo alisadiki kuwa nilifaa kupewa Kiapo cha Umoja, "*Ndemwa Ithatu*", kwani iliwezekana niweze kusaidia katika chama cha umoja kama vile nilivyosaidia katika K.A.U. Wale wengine watatu walipigwapigwa hivi kidogo, lakini kwa ajili ya maelezo ya Kanyoi juu yangu, wale wengine walisema: "Msimpige mwanafunzi" na hivyo nikaachwa. Tulipitia baina ya ndizi zile mbili mara saba tukiwa laini moja

halafu tukafanya laini moja tukamtazama mtawala wa kiapo, ambaye jina lake lilikuwa Biniathi, aliyengojea kuendesha sehemu iliyofuata ya sherehe ya kiapo.

Biniathi alishika mapafu ya mbuzi kwa mkono wa kulia na akaishika nyama nyingine kwa mkono wa kushoto. Tuliinama chini wakati alipoizungusha ile nyama mara saba kichwani mwetu, huko akihesabu kwa sauti kubwa kwa lugha ya Kikuyu. Baada ya kufanya hivyo, akampa kila mmoja wetu yale mapafu na kutuambia tuyaume. Baadaye akatuamuru turudie yafuatayo nyuma yake kwa upole:

Ninasema haki na ninaapa mbele ya Mungu,
Na mbele ya chama hiki,
Chama cha Umoja,
Umoja ambao umejaribiwa,
Umoja ambao unatolewa mzaha kuwa ni "Mau Mau",
Kuwa nitaenda mbele kupigania ardhi,
Ardhi ya Kirinyaga ambayo tulilima,
Ardhi ambayo ilichukuliwa na Wazungu,
Na nikikosa kufanya hivi,
Kiapo hiki na kiniue,
Na hivi saba viniue,
Nyama hii na iniue.

Nasema ukweli kuwa nitafanya kazi pamoja,
Na majeshi ya Chama cha Umoja,
Na nitasaidia kwa lo lote nitakaloulizwa,
Nitalipa shilingi sitini na mbili na senti hamsini
na ndume kondoo kwa chama,
Kama sina hizo sasa nitalipa baadaye.
Na nikikosa kufanya hivi,
Kiapo hiki na kiniue,
Na hivi saba viniue,
Nyama hii na iniue.

Nilichapwa kofi la masikio kwa kukosa kurudia mojawapo ya maneno hayo sawasawa. Nilipigwa na msaidizi wa yule mganga wa viapo, ambaye alisimama nyuma yake akishika kibuyu kilichojaa damu ya mbuzi iliotumiwa kwa sherehe hiyo. Biniathi alitupaka damu kila mmoja usoni mwake, huku akieleza kuwa alifanya hivyo kutukumbusha kuwa sasa tulikuwa twapigania ardhi yetu na kutuonya kuwa tusifikirie kuuza nchi yetu.

Baada ya hayo, Biniathi alimchanja kila mmoja wetu (kwa ile ndoana) huku akifanya alama tatu katika viwiko vya mikono yetu ya kushoto.

Hii ndiyo iliyokuwa maana ya *Ndemwa Ithatu* (vijeraha vitatu au alama tatu) na pia hii ilieleza haja ya ndoana ambayo Kanyoi alikuwa anatafuta hapo mwanzoni. Hapo akaileta ile nyama na kuigusisha jeraha zetu ili matone ya damu yetu yaingie ndani yake. Halafu alitupa ile nyama ili kila mmoja aiume huko akieleza: "Kitendo hiki cha kula nyama iliyo na damu ya kila mmoja wenu chaonyesha kuwa sasa ninyi mmeunganishwa wenyewe pamoja nasi." Huu ndio ulikuwa mwisho wa sherehe na sisi sote wanne tulienda kuketi pamoja na Kanyoi ambaye aliandika majina yetu na akatuuliza tumlipe shilingi tano zilizokuwa ni ada ya kula kiapo, ambayo sote tulilipa. Halafu tulienda kungojea kama wale wengine ndani ya mahindi, na hapo tukarudishiwa viatu na saa zetu.

Wakati wa sherehe hiyo, fikira zangu zilichanganyikana na hofu na makuu. Huko kwenye mahindi, nilijisikia mwenye roho mpya yenye nguvu na uwezo. Maisha yangu ya hapo mbeleni yalionekana kuwa bure. Hata ile elimu yangu ambayo nilikuwa najivunia ilionekana kama kitu kidogo kulingana na ujasiri huo mpya niliopewa wakati huo. Nilizaliwa mara ya pili na hapo nikayaona mambo kama vile yalikuwa ile siku ya kwanza mama alipoanza kunifundisha kusoma na kuandika. Wale wengine watatu walikuwa kimya na ilikuwa wazi kuwa fikira zao zilifuatia mwenendo huo wa kuwa na moyo mpya kama mimi mwenyewe.

Biniathi alikuwa wa umri wa miaka kama arobaini na alikuwa wa urefu na mwili wa kadiri. Manne ya meno yake hayakuwako. Alivalia koti jeusi na suruali ya kijivu, na shati iliyokuwa ya rangi nyeusi, manjano na ya kijivu lakini hakufunga tai. Hakuna mmoja wa jirani hapo Bahati aliyejua kulisha kiapo na Biniathi alikuwa amefika kutoka pande za Kiambu ili kusaidia. Baada ya kila sherehe, alipewa bakshishi ambayo kiasi chake kilipimwa na komiti ya jirani (*athuri a kirira*) lakini mimi sikuwa mwana-chama wa komiti hiyo. Yeye alikuwa mwenye ujuzi kabisa katika kazi hiyo, na aliwashauri watu juu ya shida zao.

Nilimwuliza Kanyoi kama ilifaa niendelee kuwaandikisha watu kwa K.A.U. Alinieleza kuwa K.A.U. kilikuwa tofauti kabisa kutokana na chama cha umoja na kuwa wengine wa wale waliokuwa kiaponi walikuwa wanachama wa K.A.U. Sikukatazwa kuendelea kusaidia K.A.U. lakini niliambiwa nijihadhari nisiwaambie wana-K.A.U. kuwa mimi nilikuwa mwanachama wa hicho chama kipya kwani hicho kipya ni lazima kibakie siri. Kanyoi, ambaye sasa nilimfikiria kuwa mwalimu wangu, alituonya kuwa tusilale na bibi kwa muda wa siku saba baada ya sherehe. Kama tulitaka kujua kama mtu alikuwa amekula kiapo, tulipaswa kumwuliza: "Wewe ulitahiriwa wapi?" Kama mtu akijibu kama kawaida ilivyo kweli, tulijua kuwa yeye bado kula kiapo. Lakini kama alijibu: "Nilitahiriwa kwa Karimania tukiwa na Karimania" hiyo ilikuwa alama ya kutosha

kuonyesha kuwa alikuwa amekula kiapo. Hapo mbeleni, sikuwa nimelisikia jina la Karimania likitumiwa kama jina. Linaweza kutafsiriwa kusema "kupinduapindua ardhi mara nyingi" kama wakati wa kulima na ndilo jina lililotumiwa kwa ajili hii katika kiapo.

Usiku huo nililala kwa Kanyoi. Sikusema sana kwani kichwa changu kilikuwa kingali chajaa zile ahadi. Asubuhi yake, baada ya kufungua kinywa kwa uji, nilirudi kwa shangazi. Baada ya siku kadhaa, nilimweleza Kanyoi kuwa wakati ulinifikia nirudi Nakuru na hapo akaniuliza nimwone siku ya Jumapili kabla ya kuondoka. Nilimkuta na mtu mwingine aliyejulikana kama Muthee, ambaye baadaye alikwenda kupigana msituni lakini akauawa na askari wa K.A.R. alipokuwa akitafuta chakula. Tulizungumza mengi pole pole na zaidi juu ya siasa na uchungu wetu juu ya ardhi yetu, na hasa juu ya pingamizi iliyowanyima Waafrika haki ya kuwa na ardhi katika Nyanda za Juu za Weupe. Tulighadhabika kama vile mwenye nyumba angekuwa kama akifukuzwa kutoka nyumba yake na mgeni aliyemkaribisha kwa hiyari. Jioni yake, sote tulikwenda kwa jirani mwingine ambako walikuwa wamemchinja mbuzi. Tuliketi chini na Biniathi akatuambia tuondoe mavazi yetu yote isipokuwa suruali zetu, halafu tukasimama kungojea atuite. Nilikuwa wa pili baada ya Kanyoi na hakukuwa na kutotii wakati huu.

Niliondoa suruali yangu nikamtazama Biniathi wakati huo nikipiga magoti yangu. Aliniambia nikishike kifua cha huyo mbuzi aliyechinjwa, nikitie ume wangu kwenye tundu iliokuwa imepenywa ndani yake na nishike mengine yote kwa mkono wa kushoto mbele yangu. Mbele yangu hapo chini palikuwa vijiti viwili ambako kile kifua cha mbuzi kilining'inishwa na kufungiliwa. Kwenye kulia kwangu sakafuni ya nyumba palikuwa na vijiti vingine saba vyenye urefu wa inchi nne hivi. Biniathi aliniambia niokote kimoja kimoja, nikisukume kwenye kile kifua pole pole, na wakati huo nirudie viapo hivi saba, kila kimoja kwa kijiti kimoja. (Baada ya kila ahadi, niliuma ile nyama na kukitupa kijiti kwa upande wangu wa kushoto).

1. Ninasema kweli na ninaapa mbele ya Mungu wetu
   Na kwa kiapo hiki cha "Batuni" cha chama chetu
   Ambacho ni chama cha kupigana
   Kwamba nikiitwa kuua kwa ajili ya ardhi yetu
   Kama nikiitwa kumwaga damu yangu juu yake
   Nitatii na sitajitolea kwa adui
   Na nikikosa kwenda,
      Kiapo hiki kiniue
      Beberu hii iniue

Hivi saba viniue -
Nyama hii iniue.

2. Ninasema kweli na ninaapa mbele ya Mungu wetu
Na mbele ya wananchi wote wa Afrika
Kwamba sitaihaini nchi yetu kamwe
Kwamba sitamhaini mwanachama ye yote wa chama chetu kwa adui
Adui huyo awe Mzungu au Mwafrika
Na kama nikifanya hivyo
Kiapo hiki kiniue, n.k.

3. Ninasema kweli na ninaapa mbele ya Mungu wetu
Kwamba nikiitwa usiku au mchana
Kwenda kuichoma stoo ya Mzungu ambaye ni adui yetu
Nitaenda bila uwoga na sitajitolea kwa adui
Na kama nikikosa kufanya hivyo
Kiapo hiki kiniue, n.k.

4. Ninasema kweli na ninaapa mbele ya Mungu wetu
Kwamba nikiitwa kwenda kupigana na adui
Au kuuwa adui—nitakwenda
Hata adui huyo akiwa ni baba au mama, ndugu au dada
Na kama nikikataa
Kiapo hiki kiniue, n.k.

5. Ninasema kweli na kuapa mbele ya Mungu wetu
Kwamba wanachama wa chama wakinijia mchana au usiku
Na wakiniuliza niwafiche
Nitafanya vile na nitawasaidia
Na nikikosa kufanya hivyo
Kiapo hiki kiniue, n.k.

6. Ninasema kweli na kuapa mbele ya Mungu wetu
Kwamba sitamchukua bibi wa mwengine
Kwamba sitatembea na malaya
Kwamba sitaiba kitu cha mwanachama wa chama hiki
Na sitamdharau mwanachama kwa ajili ya vitendo vyake
Na kama nikifanya cho chote cha hayo
Kiapo hiki kiniue, n.k.

7. Ninasema kweli na kuapa mbele ya Mungu
Na kwa kiapo hiki cha Batuni cha chama

Sitauza nchi yetu kwa pesa au kingine
Kwamba nitaweka ahadi hizi zangu mpaka kifo
Sitatoa siri zetu kwa adui
Wala sitazitoa kwa ye yote ambaye si mwanachama
Na kama nikivunja ahadi yo yote ya zile nilifanya
Nitakubali adhabu yo yote itakayotolewa na chama
Na kama nikikosa kutenda mambo haya
Kiapo hiki kiniue, n.k.

Nilipomaliza kuahidi mambo hayo yote, nilikiondoa hicho kifua na mambo hayo mengineyo, nikavaa suruali yangu halafu nikahamia kwenye sehemu nyingine ya chumba hicho ambapo nilimlipa Kanyoi shilingi sita na sumuni ada ya kiapo hicho. Basi hapo nilikula kiapo cha pili cha Batuni. Jina la kiapo hicho laonekana kama lilitokana na lile la Kiingereza—"Platoon"—na kiapo chenyewe kililiwa na wale ambao wangaliitwa kutenda mambo ya chama.

Kiapo hicho cha pili kilikuwa cha nguvu zaidi kuliko kile cha kwanza na kiliwacha fikira zangu zikiwa na mambo mageni na shuku kuu. Tohara yangu ilikamilika na sasa nikawa Mkikuyu kamili bila wasi wasi wa pale niliposimama katika vita vya kabila langu. Siri kamili ilihimizwa kwani hata wengine ambao walilishana kiapo cha kwanza walikuwa bado kula kiapo cha Batuni. Baada ya sherehe hiyo, nilirudi kulala kwa nyumba ya shangazi yangu. Baada ya siku tatu, nilikwenda Nakuru kukaa na Obadiah Mwaniki, mwungwana ambaye hapo kwanza alifika kwetu nyumbani akiwa na baiskeli miaka kadhaa iliyopita. Angali alikuwa Mkristo wa nguvu na alikuwa Rais wa Korti la Kienyeji la Nakuru, na kwa vile yeye alikuwa ni Mkristo na zile ahadi nilizokuwa nimefanya wakati wa kuapishwa, sikumwambia yale yaliyokuwa yakifanyika. Ingawa sikuapishwa nisihudhurie kanisani au nisikae kama Mkristiano, tangu ile siku ya kwanza niliyopewa kiapo, imani yangu juu ya Mungu wa Kristo ilianza kufifia na sikuhudhuria kanisa bila sababu maalum. Lakini wakati nilipoishi na Obadiah, na kwa vile alikuwa Mkristo jasiri, nilihudhuria kanisa kila Jumapili ili asije akashuku kitu au anikasirikie.

Muma wa Thenge au "Kiapo cha Beberu" ni sherehe ya kawaida katika maisha yetu kwa mambo kama uunganisho katika ndoa, katika uuzaji au ubadilishaji wa ardhi (kabla ya Wazungu kutuingilia, wakati ardhi ilikuwa tele, uuzaji wa ardhi ulikuwa karibu haukujulikana) au katika mambo yaliyohusiana na ng'ombe au mbuzi. Mashujaa pia walikula kiapo kilichoitwa *Muma wa Aanake* ("Kiapo cha Vijana") ambao uliwaunganisha kabla ya kufanya mashambulio. Kusudi la viapo hivi vyote lilikuwa ni kuwapa wale waliokula wawe na heshima, umoja, mapenzi baina ya wao wenyewe na kudumisha urafiki wao, kuondoa fikira mbaya

na kupinga mabishano. Na zaidi ya hayo yote, wale walioungana kwa sherehe ya aina hii hawakuweza kufanyiana uchawi. Watu wetu waliogopa kuuawa na uchawi. Kiapo kiliondoa hofu ya aina hiyo na uhusiano wa aina mpya ukawako baina ya jamaa na ukoo uliohusika. Wivu, chuki au uadui haukuweza kujulikana tena baina yao.

Kiapo cha Umoja (ambacho kilipewa jina la "Mau Mau" na wachochezi wa habari) kilifuatia nyayo hizo pia. Kilikusudiwa kuwaunganisha, siyo Wakikuyu, Waembu na Wameru tu, lakini makabila yote katika Kenya. Makabila haya hayangesherehekea kiapo kwa njia ile ile tu, bali kila kabila katika Kenya lilikuwa na aina ya kiapo cha kuunganisha na kufanyiza mambo kadhaa. Si jambo la kustaajabisha kwamba chama hiki kilianza na Wakikuyu. Wao ndio wa kwanza zaidi ya kabila lingine waliokandamizwa hadi umaskini uliowaumiza, na wao zaidi ya wengine ndio walikuwa karibu na Nairobi ambapo maisha ya mjini na elimu yaliwafahamisha mambo mengi ambayo yaliwakasirisha na wao ndio walishuhudia kila siku vile mashamba walionyang'anywa yalivyozaa utajiri kwa Wazungu.

Bila shaka, wengine walilazimishwa kula kiapo bila kupenda kwao, lakini hawakuwa wengi kama vile wasemaji wengine wa Serikali walivyokusudia tukubali: hawa wa Serikali waliona ni muhimu waifiche dunia zile sababu za kweli zilizoanzisha chama hicho cha siri. Ni kweli kwamba mnamo mwaka wa 1953 na 1954, adhabu kali, hata kifo, zilitolewa na korti za chama hicho kwa wale waliofikiriwa kuwa wasaliti au wahaini kwa chama. Hicho sicho tu chama cha siasa cha kwanza kilicholazimishwa kuwa na korti zake zilizolingana na serikali. Tulikuwa tumekataa utawala wa Serikali ya Kenya. Badala yake, tulijenga Serikali nyingine, iliyokubaliwa na wengi wa wananchi, ambayo wakati ilikuwa changa, ililazimishwa kupigania uhai wake wenyewe, huko ikikabili shida na pingamizi nyingi. Si ajabu kuwa viongozi wetu walihimiza amri ya kijeshi baina ya wafuasi wetu na kutotii wala kutoungana nasi kulifikiriwa ni kukosea Serikali yetu kwa njia kubwa. Hakuna kingine isipokuwa umoja kamili, utii halisi na kuwa na imani haswa juu ya kusudio letu ambacho kingalituwezesha kushindana na bunduki, majeshi, pesa na ule ubongo wa Serikali ya Kenya. Hivyo vilikuwa ni vita juu ya nyumba zetu, ardhi yetu na nchi yetu ambavyo malipo ya kutofaulu yalikuwa ni kifo tu.

Uwongo mwingi umeenezwa kuzunguka dunia juu ya viapo. Yasemekana kuwa kiko kitabu katika chumba cha vitabu cha House of Commons kinachoeleza juu ya mambo mengineyo yasiyoelezeka ati ambayo yalifanywa wakati wa sherehe za kulisha viapo. Inasemekana kuwa watu wengine walilishwa viapo karibu kumi na vinne, kila kimoja kikiwa kiovu zaidi ya kile cha mbele. Vile viapo viwili nilivyoeleza ndivyo tu vilikuwa halali.

Na kwa vile hapakuwa na utawala wa katikati wa chama, zilikuwako tofauti ndogo ndogo juu ya kulishwa kwa viapo kutoka kila wilaya kwani walishaji hawakufuata kanuni moja kila mahali.

Zile hadithi ati penginepo walitumia damu ya mwezi ya bibi, au kwa binadamu kulala na wanyama, au kula mazalisho ya watoto ambao walitolewa matumboni mwa mama zao kabla ya kuzaliwa, hayo yote yalikuwa ni porojo ya wenye wazimu na ikiwa kuna ye yote anayeweza kuthibitisha ukweli wa mambo kama hayo (na hakuna ambaye amenithibitishia nikatosheka) ni lazima mambo kama hayo yawe yalifanywa na wachache tu ambao walipatwa na wazimu kwa ajili ya kukaa msituni peke yao. Lakini kusikia kuwa vitendo kama hivyo vilifanywa na Wakikuyu kwa jumla ni kama kusema kuwa Waingereza wote wanawanajisi wasichana wachanga au wote ni wauaji kwa sababu wachache wao hufanya hivyo kila mwaka.

Katika maisha ya wananchi Wakikuyu, usadaka wa damu ya mwezi ya wanawake huelezwa kwa vijana wote wanaume kwa wake na wachungaji (*atiiri*) wao wakati wa sherehe za tohara. Kukosana na maelezo hayo kulikuwa ni dhambi ambazo zingemfanya bibi kukosa watoto au zilete hasara au taabu kuu kwao ambazo zingeepushwa na sherehe nyingine za kusikitisha mno. Hakuna kiongozi Mkikuyu asiye na wazimu ambaye angefikiria kufanyiza mambo kama hayo katika chama hicho ambayo yangekasirisha roho za babu zetu.

Ushahidi uliohusiana na hadithi hizo ulitungwa kutokana na kuungama kulikofanywa na wengine mara badala ya kuteswa au na wengine wakifahamu kuwa kuteswa kama huko kulikuwa kwawangojea. Hakuna hakika kama kunayo korti katika ulimwengu ambayo ingekubali ushahidi wa aina hiyo. Wakati wote nilipokuwa nimefungiwa sikusema ukweli kama vile ninavyosema sasa, ingawa niliungama uwongo mara sita baada ya kulazimishwa na wale walioniuliza maswali waliandika uwongo huo kwa makini. Iko methali ya Kikuyu isemayo: *Njita murume* ("Niite bwana yako") ambayo ni kusema kuwa baada ya kumpigapiga mtu hata ukimwuliza akuite Mungu, atakuita; lakini ukweli ni kuwa wewe ungali si Mungu.

Mbele ya kutangazwa kwa wakati wa hatari mnamo Oktoba, 1952 hakikuwapo kiapo cha Batuni po pote katika jimbo la Rift Valley. Yawezekana kilikuwako penginepo ndani ya risavu, lakini sijui. Huko kifungoni nilikutana na wengi wale waliokamatwa 1952 wakati wa mwito wa "Jock Scott". Hapakuwa na hata mmoja ambaye alikuwa amekula kiapo cha Batuni na hata wengine walikuwa bado kula kiapo cha kwanza.

Tunayo methali nyingine inayosema: *Mwana angiguikiria ruhiu nawe ndukoe umuikirie* ("Mtoto akikutupia kisu usiokote na kumtupia") maana yake ukiokota na kumtupia, wewe ndio utaonekana mjinga kwani

anaweza kukujeruhi nacho. Siku hizo za kwanza za hali ya hatari, vijana waliokuwa msituni walikuwa na mikuki na vipanga (simi) tu. Badala ya Serikali kufanya masikizano ya siasa, iliwapiga kwa bunduki za "Brengun" na bomu za "grenade" zilizotumiwa na majeshi ya Lancashire Fusiliers, Kenya Regiment na King's African Rifles. Haya majeshi yaliwanyima matumaini yo yote wale waliokuwa msituni wakati huo isipokuwa wapigane au wauawe. Kwa hivyo majeshi ya wananchi yaliyokuwa msituni yalijiunga pamoja kwa kiapo cha Batuni ili wapiganie silaha za kupambana na shurutisho lililowakabili kupindukia. Hapo mwanzoni imani yao juu ya haki na ukweli waliokuwa wakipigania ndizo tu zilikuwa silaha zao za kupambana na majeshi ya ulinzi ya Serikali.

Jambo muhimu la kwanza lilikuwa kupata bunduki na risasi. Malaya waliotembelea kampi za majeshi waliuza miili yao kwa risasi mbili ambazo zilipitishwa kwa siri hadi kuwafikia mashujaa misituni. Wanajeshi wengine wa K.A.R. waliweza kuuza risasi ambazo ziliuzwa kwa usaidizi wa wengine waliofanya kazi ya kiraia katika kampi za majeshi waliowahurumia Wakikuyu. Punde si punde, uwindaji wa silaha uliongozwa kwenye nyumba za Wazungu kwenye mashamba yaliyokuwa peke yao ambako silaha hazikuwa salama. Mauaji mengi ya Wazungu ya siku hizo yalifanywa kwa ajili ya kutafuta silaha. Majeshi ya wananchi yaliyokuwa msituni yalianza kujitengenezea bunduki zao kutoka vyuma vya baiskeli, mifereji, vyuma vya kufunga milango na mipira. Bomu zilitengenezwa kwa chupa na vifaa vya kufyatulia vikaibwa kutoka mastoo ya Serikali na raia wengine ambao hawakuwa msituni lakini ambao hawakupendelea Serikali. Hapo kwanza, silaha hizo za kujitengenezea ziliwaumiza wenyewe.

Hao raia ambao walitayarisha usafirishaji wa vifaa hadi msituni, ambao walikuwa maelfu, walijulikana kwa jina la "Passive Wing" na ndio walipeleka risasi, chakula na dawa kwa mashujaa wetu, vifaa ambavyo viliwawezesha majeshi yetu kuishi msituni. Mnamo mwisho wa 1953, chama hicho cha siri kilikuwa kimefikia mpango ambao haukulingana na mwingine. Hata tulikuwa tunajua mengi juu ya Government House na G.H.Q. na ni machache tu yaliyofanyika katika afisi za ma-District Commissioner au ma-Provincial Commissioner ambayo hatukujua. Nyumba za kuponyeshea wale waliojeruhiwa zilikuwa zimetayarishwa karibu na dispensari za Serikali. Karibu kila kampi ya walinzi wa nyumbani (Home Guards) tulikuwa na watu wetu wengi.

Majeshi yenye nguvu zaidi pamoja na vikundi vya jeshi la Waingereza na eropleni za kutupa bomu zilimiminwa kupambana na mashujaa wetu huko misituni ambao baada ya muda walipotewa na moyo, na ambao roho zao zilijaa chuki ambayo hutokana na hali ya vita vyo vyote. Hawakupewa nafasi yo yote, na wao kadhalika hawakutoa nafasi. Wakishuruti-

shwa na haja kuu, wale wengi ambao hata hawakujua kusoma waliokimbilia misituni, wakiongozwa na majemedari wao wakuu, waligeuka kuwa wapiganaji wakali wa msituni, na walipambana na nguvu kuu za majeshi ya Mwingereza na Serikali ya Kenya kwa muda wa miaka minne. Ni jambo la kusikitisha kufikiria vile hali hii yote ingezuiliwa kwa kufanya masikilizano machache ya siasa. Wakati huo, tangazo lo lote kutoka kwa Serikali ya Uingereza kuwa watamwachilia Jomo Kenyatta na watawapa Waafrika wa Kenya uhuru mnamo mwaka wa 1965 lingalitosha kuwachisha mapigano na kuwaleta vijana kutoka misituni.

Mimi sikuwako msituni mwenyewe lakini ninatumaini kuwa hadithi za vita vikuu vya majeshi yetu huko milimani ya Aberdares na Kenya zitaandikwa hivi karibuni na wale waliokuwamo. Ni jambo la huzuni kuu kuwa Dedan Kimathi alinyongwa na hayuko pamoja nasi kutuhadithia, lakini labda Waruhiu Itote, aliyekuwa General China, siku moja atafanya vile. Sisi hatuwezi kukubaliana na hadithi ya uwongo iliyokuwa ya upande mmoja iliyoandikwa juu ya Dedan Kimathi, yule shujaa wa mashujaa wetu wote, kama vile ilivyoandikwa na Ian Henderson katika kitabu kinachoitwa *The Hunt for Dedan Kimathi* (au "Kuwindwa kwa Dedan Kimathi").

Jambo moja lililowashinda wageni wakati wa Hali ya Hatari ni vile wanawake wa Kikuyu walivyojiweka au walivyofanya. Wakati wa usiku, walionyesha mapenzi yao wakiwalisha na kuwapatia haja nyinginezo wale mashujaa wa msituni lakini asubuhi yake watakataa kabisa kuwa ye yote alikuwa humo msituni kama wakiulizwa na maafisa wa Serikali. Na siku hiyo hiyo baadaye, walikwenda kwa uchangamfu kutii amri za Serikali za kuchimba mitaro mikubwa ambayo ilijazwa na mianzi mikali iliyokusudiwa kufanya ukuta usiopitika baina ya msitu na risavu. Pamoja na hayo walijenga zile kampi za walinzi wa nyumbani ambazo zililindwa sana kwa kuta na seng'enge na mitaro mikubwa ambamo walinzi hao waliishi. Baadaye, kama vile hali ya mambo ilivyoendelea, waliondoka kwa maelfu wakapitia kule misituni huko wakiwafagia wanajeshi wetu waliowakuta humo. Kuna maelezo juu ya vitendo hivyo viwili vilivyopingana vya wanawake wetu?

Kwanza, hakuna wasiwasi kuwa tisaini katika mia ya wanawake wa Kikuyu waliunga vita vya uhuru kwa fikira zao, miili yao na mioyo yao. Ni uwongo kufikiri kuwa kuungwa huko kulikuwa kwa wale waliokuwa na elimu tu. Ya pili, hapo siku za kwanza za Hali ya Hatari, wanawake wengi walisaidia hicho chama ambacho kilidharauliwa kama "Mau Mau". Wakati Jomo Kenyatta alipokamatwa, walifahamu kwamba hatua za amani za kufikia kusudi zao hazikufaulu na hawakuwa na lingine isipokuwa watumie nguvu huko wakifahamu maumivu ambayo hatua hiyo ingewaletea. Wakati huo huo walikuwako wanawake wengine waliounga

Serikali mkono—wengine ingawa si wote, wale waliokuwa bibi wa walinzi wa nyumbani, wanawake Wakristo wengine ambao (na hii ilikuwa kweli kwa wanaume wengine) ambao kwa hakika walimpenda Mungu zaidi ya vile walipenda nchi yao, na wengine ambao walikuwa na mapendekezo yao ya kibinafsi. Kwa vile umoja ulikuwa ndio silaha yetu yenye nguvu zaidi, watu kama hao walikuwa adui wa chama cha siri. Siyo kusema kuwa hatukupenda Ukristo, bali vita vyetu hapa duniani vilikuwa vimefikia hali ambayo Ukristiano haungekubaliwa kujiingiza ndani yake. Zaidi ya hayo, tulikuwa tumejua kuwa adui wetu, kwa njia ya ujanja, walikuwa wanatumia Ukristiano kupinga madai yetu. Tulifikiria kuwa Ukristiano haungeruhusiwa kurudi nyuma namna hiyo.

Sasa wajibu wa kwanza wa walio wengi kwa upande wetu ulikuwa wa kuwasaidia mashujaa wetu katika misitu. Mara nyingi wajibu huo ulitiwa nguvu na mafungamano ya ujamaa kwani wengi wao walikuwa bwana zao, baba zao, kina ndugu na vijana wao katika Majeshi ya Uhuru wa Ardhi, na hakuna uhalifu mkubwa zaidi baina ya Wakikuyu kuliko kuwanyima wajamaa wako chakula. Kwa wakati huo huo iliwalazimu kusaidia Serikali kwani sasa ilikuwa yachukua hatua kali sana katika risavu na kama walikosea amri ya Chifu, waliadhibiwa vikali. Si kweli kusema ati wengi waliogemea chama cha siri; waliogopa Serikali hiyo iliyowakilishwa na Machifu, mahedimeni na walinzi wa nyumbani. Walitii amri zilizotolewa na Serikali lakini kwa moyo mzito: wakati mwengine wakikusudia kusaidia chama cha siri walijionyesha kuwa wenye kupendezwana kazi walioamriwa kufanya, lakini ambayo kusema haki waliichukia, kama vile kufagia kambi au kuchimba mitaro.

Hapo mwanzoni wa Hali ya Hatari, hapakuwako "Waaminifu" ("Loyalists") au walinzi wa nyumbani ("*Home Guards—Humungati*"). Huku na huko walikuwako wachache: machifu, matajiri wa biashara na wenye mali, askari kanga na wengineo ambao walipendelea kuendelea kwa Serikali ya Kiingereza, ambao walipinga chama cha siri. Wengine wengi ambao waliogopa nguvu za majeshi ya Serikali walikaa juu ya "ua" lakini ni wachache sana walioona ni vibaya katika fikira zao au si vizuri kutumia nguvu za aina hiyo kwa kupigania uhuru na waliofikiria kuwa Mwingereza angalipewa muda zaidi kuonyesha imani yake. Serikali ilifahamu kwa haraka kwamba ili iweze kupambana na Majeshi ya Uhuru wa Ardhi katika misitu ni lazima kuwagawanya wana-kabila Wakikuyu. Iliendelea kufanya hivyo ikitumia "propaganda" ya siasa, dini na mambo ya starehe mpaka hali ya hatari ikageukia kuwa ya vita baina ya kabila ambalo lilijaa uadui baina ya wanakabila Wakikuyu. Si ardhi wala mali ya wapigania uhuru vilivyoachiliwa; na wale wa kabila letu wasio mashujaa waliona, kama ilivyo kawaida katika historia, kuwa maisha ya upande wa

majeshi makubwa yalileta zaidi katika hali ya starehe ya mwili ikiwa si kwa starehe ya moyo. Serikali ilitoa "propaganda" kubwa kuwa wale waliokuwa msituni walikusudia kumwua kila mtu mwingine aliyekuwa nje. Wale waliokuwa msituni waliposikia "propaganda" hiyo walizidi kujikaza zaidi na wakakataa kukubaliana na Serikali. Vita vya aina hii vinaweza kumalizika tu wakati majeshi ya upande mmoja yakimalizwa kabisa. Ule mchezo wa kumpiga mtu risasi akionekana uliotumiwa na Majeshi ya Ulinzi unaelezeka vizuri kutokana na idadi za walioumizwa zinazoonekana ndani ya *Ripoti ya Corfield* zinazoonyesha kuwa "magaidi" 11,503 waliuawa wakilinganishwa na wana-Serikali 2,044 waliouawa na mashujaa wetu. Idadi hizi hazionyeshi wale walionyongwa au wale waliokufa katika kampi ya kufungiwa.

Wale walinzi wa nyumbani (*Humungati*) walijulikana kote katika Jimbo la Kati kama *Kamatimu*. Kufuatia desturi za Kikikuyu, zilikuwako daraja mbili za Uzee. Ile daraja ya juu ni ile ya wazee ambao walikuwa wamelipa *mburi ya ihaki* ("mbuzi ya kuhonga") ambayo ilikuwa ni ada ya kuonyesha kuwa umekubaliwa. Ile daraja ya chini ilijulikana kama *kamatimu* na ilikuwa ya wale ambao walikuwa bado kukubaliwa kwa daraja ya juu na kwa hivyo walikuwa bado kulipa mbuzi yao. Mashujaa wetu wa msituni basi waliwapa jina hilo la matusi kuonyesha kuwa walikuwa watu wa chini ambao hawakuweza kupambana na shida za kupigania uhuru bali waliotafuta ulinzi kutoka kwa adui na vile hawakustahili kukubaliwa kwa daraja ya juu. Kwa vile wengi wao walibeba mikuki kama silaha (ingawa baadaye walipewa bunduki nyingi) lile jina la *Kamatimu* linaweza kutafsiriwa kusema 'watu wadogo waliobeba mikuki', na hilo jina lilifaa kwa njia hizo mbili.

Mashtaka makubwa yamefanywa kuwa Mau Mau waliwaua raia wengi katika Nairobi na risavu na kuwatupa ndani ya mashimo ya vyoo. Yale yaliyotokea Lari mnamo mwezi wa Machi 1953 yameelezwa zaidi kama mauaji ya kisasi ya faraghani. Ingawa hakuna anayekanusha kuwa korti za Mau Mau ziliwahukumu wasaliti na adui kufa, hii siyo mara ya kwanza katika historia ya dunia chama cha kuvunja serikali kililazimishwa kufanya hivyo. Nimewasikia wafungiwa wengi wakieleza visa vya wale waliouawa na "waaminifu" kwa ajili ya uadui wa kibinafsi au kwa ajili ya ubishani wa ardhi. Wengine walikuwa mboga za wahalifu wa kawaida. Mauaji yote ya aina hiyo yaliwezekana kusemwa kuwa ni ya Mau Mau na kwa hivyo polisi wa C.I.D. hawakujisumbua kupeleleza. Hata yale yaliyotokea Lari si rahisi kama vile Serikali ilieleza. Inajulikana sasa kwamba mengi hayo yalitokana kutoka amri ya Serikali baada ya Carter Commission kwamba waliwekwa kwa mashamba Lari wengine ambao waliondolewa kutoka mashamba yao kuwapa Wazungu wa Limuru nefasi.

Kwa vile kwa muda wa miaka hiyo wafungiwa wengi waliletwa kutoka ndani ya risavu na wengine mashujaa waliokamatwa misituni, tulijifunza njia moja ambayo hawa Humungati walifanya uzuri. Wale Majoni wa Jeshi la Kiingereza waliona vigumu kutambua baina ya Mau Mau na wale wasiokuwa Mau Mau kwa vile hapakuwako na alama za kutambulisha baina yao. Kwa hivyo Humungati waliandamana na askari hawa na wakawazuia wasiwaue wale raia wa kawaida. Hata hivyo, ajali nyingi zilitukia, na wengi ambao hawakuwa na hatia waliuawa; tulihuzunika sana kusikia kwamba mwenda wazimu mmoja wa Othaya aliyeitwa Karoki aliuawa kwa risasi kwa sababu hakufahamu kwamba amri ya "curfew" haikuwaruhusu raia kutembea usiku karibu na nyumba zao. Lakini tulikata shauri kuwa wakati wa hatari ukiisha, wafungiwa hawataruhusiwa kujilipiza kisasi juu ya Humungati hao kwa vile walikuwa wamejaribu kuwaokoa wengi. Humungati wengine walikuwa wamekula kiapo na walisaidia kwa siri kama vile walivyoweza. Tunayo methali ya Kikuyu inayosema: *Tutikuhe hiti keeri*, ambayo ni kusema "Hatutampa fisi mara mbili". Wakati mtu alipouawa hapo zamani, mwili wake ulipewa fisi. Kumwua yule aliyemwua kwa kulipiza kisasi hakungemsaidia mtu isipokuwa fisi, na kwa hivyo hatukujilipiza kisasi. Kwa ajili ya kukata shauri hivyo kulikofanywa na wote walioumia wakati huo, ndivyo amani ikawarudia Wakikuyu. Viongozi mahsusi wawili wa Humungati walikuwa Senior Chief Muhoya, B.E.M., wa Nyeri, na Senior Chief Njiiri, O.B.E., wa Fort Hall (Murang'a). Vijana wawili wa Muhoya ni waalimu wa viongozi wetu wa mbeleni katika Secondary School; mwanae Njiiri alichaguliwa kuwa mwanachama wa Legislative Council wa wilaya ya Fort Hall, na baadaye akamwondokea Mzee Kenyatta kiti chake mnamo Desemba 1961 ili kumwezesha Mzee kuingia Legco. Hakuna faida ingaliyopatikana kama tukijilipiza kisasi juu ya baba zao, wala hatungefaidika na hiyo roho ya kisasi katika mavuno yetu ya uhuru, ambayo yangevunwa tu kwa njia ya kuvumilia, kujikaza na kushirikiana.

Wakati nilipotembelea Ghana mnamo Agosti 1961, kiongozi mmoja aliuliza ni zawadi gani itakayopewa wale wananchi halisi ambao waliumia sana misituni na katika vifungo. Pia alihimiza vile ni lazima tuwachukie wale "waaminifu" waliokuwa upande wa Wazungu wakati wa vita. Nilimjibu kwa mojawapo ya methali zetu: *Ndurumi irima tiyo ndari kuo*, ambayo ni kusema kuwa 'kile kinachotoboa shimo sicho kinacholala humo'. Ni yule mwaga ambaye huchimba shimo akitafuta mchwa na baada ya kujishibisha na mchwa huliacha shimo kwa matumizi ya wanyama wengine ambao hulala humo. Ni kibinadamu kuwa wale waliopigana zaidi wangetumaini kuvuna mazao ya kwanza ya uhuru, lakini yatakuwako mazao zaidi ya kuwatosha wote na kwa hivyo hakuna haja kupigana tena.

Hatutumaini wala hakuna haja ya kuweko na umwagikaji wa damu tena katika Kenya tukipata uhuru wetu ingawa itatulazimu kujihadhari na hatari za pesa za nje na ubeberu. Yuko mnyama mmoja ambaye baada ya kuzaa, yeye hufanya hivi. Anaukimbilia mti wa *mukuyu* kwa nguvu zake zote na kuupiga kwa kichwa chake. Yale matunda ya mti huanguka na huwa chakula cha mtoto wake, na kule maskini mama huenda akalala bila kujisikia kwa muda mrefu na pengine haamki tena. Hivi ndivyo mashujaa wetu waliopigania uhuru walivyofanya kwa ajili ya watu wetu na vizazi vya baadaye. Labda utakuwako mwito mwingine wa aina hiyo kabla wananchi wote wa Afrika, na zaidi katika Afrika Kusini, kupata uhuru wao.

Baada ya maelezo hayo, yanipasa niendelee na hadithi yangu. Wakati nilipokula kiapo cha pili, nilirudi Nakuru na nikaanza tena kazi yangu ya K.A.U.; mara nyingi nilikodisha baiskeli nikatembelea mashamba na vijiji vilivyokuwa karibu kujaribu kuwaandikisha wanachama wapya. Mwezi wa Januari, 1953, John Kamonjo, aliyekuwa kiongozi wa K.A.U. ya Nakuru, alishikwa karibu na nyumba ya baba yake ambayo ilikuwa inatumiwa kwa kulishia kiapo ambako mmojawao waliokuwako alikataa kula kiapo. Wengine wa vijana waliokuwa askari walimwogofya na wakajaribu kumtia kamba shingoni kama vile walitaka kumnyonga. Wakati kumwogofya huko kulipokosa kumfanya ale kiapo, walimwaachilia naye akaenda moja kwa moja hadi polisi. Ingawa John hakuhusikana na tukio hilo, alishikwa pamoja na wale wengine. Kutokea wakati huo, hakukuwako na mwenye-kiti halisi wa tawi la K.A.U. la Nakuru; karibu lilitoweka. Mwezi wa Juni 8, 1953, Serikali ya Kenya kwa sheria ilifunga K.A.U. na vile ikawaacha wananchi bila njia nyingine isipokuwa kuendelea na vitendo vya kisiri au waishe.

Mimi sikuwa na madaraka yo yote katika chama kile cha siri, lakini Muthee, ambaye tulikula kiapo cha Batuni pamoja, alikuwa amekwenda kupigania msituni na alikuwa ameeneza habari kuwa mimi nilikuwa mtu mwaminifu. Kwa hivyo vikundi kutoka msituni vilinitembelea wakati mwingine. Wakati mmoja, kikundi kimoja kilitoka Nyandarua (Aberdares), kikiongozwa na Mmeru akiwa na mavazi kamili ya inspekita wa polisi, na nilifurahia kuwasaidia kwa pesa, viatu, na malazi ya usiku. Wenye huruma wengine kutoka kwa relwe walinipatia mavazi ya gadi na kwa njia hii sikupata taabu ya kusafiri bila malipo ndani ya gari la gadi kwenda Eldoret na Kisumu. Hatua hii iliniwezesha kuunganisha vikundi vyetu na nikawa kama afisa wa kueneza masikilizano baina ya vikundi katika sehemu hizo.

Mnamo Juni, 1953, nilianza biashara ya mkahawa hapo Nakuru na nikafaulu sana. Wakati huo, Serikali ilikuwa imejenga kampi za kuwahojia

watu—moja ilikuwa Molo, nyingine Kampi ya Simba nje ya Thomson's Falls na nyingine Kwa Nyangwethu karibu na Bahati. Kampi hizi ziliendeshwa na Wazungu wakisaidiwa na wazee Wakikuyu wenye kuwahoji watu ambao walichaguliwa kutokana na Humungati. Mara tulisikia juu ya njia za ukatili walizotumia wakiwahoji watu. Si sehemu ya kitabu hiki kujaribu kupindua hadithi za ukatili katika kampi hizo za kuhojiana: kesi zilizopelekwa mbele ya korti ni ushahidi wa kutosha kueleza yale yaliyofanyika. Lakini kule Kwa Nyangwethu kulikuwa kubaya zaidi, na kulijulikana siyo kwa kupigwa tu bali hata kuhasiwa. Nimeona kwa macho yangu kuwa Kongo Chuma ambaye kwanza nilimkuta Nakuru hapo mbeleni na ambaye anaishi Kiangai katika wilaya ya Embu, amehasiwa. Yeye hakuwa hivyo hapo kwanza kule Nakuru na ni wakati tulipokutana kifungoni huko Athi River alivyonieleza yale aliyotendewa Kwa Nyangwethu. Aliniambia pia kuwa chupa za soda zilifunguliwa na kusindikizwa ndani ya kuma za wanawake ili waungame. Kongo aliniambia kuwa vitendo hivyo vilifanywa na Waafrika lakini Maafisa wale Wazungu walijua yote yaliyokuwa yakifanyika.

Hadithi za kinyama katika kampi hiyo zilikuwa mbovu hivi hata ikanilazimu nione kuwa ulikuwa wajibu wangu kuwaokoa wenzi wetu kama ilivyowezekana wakati nilipokuwa Nakuru wasije wakapelekwa humo. Niliweza kujua wakati ulipokaribia wa kuwashika watu kwani niliambiwa na askari mmoja wa kienyeji aliyeitwa Solomon ambaye tulikuwa masomoni naye huko Kerugoya katika Embu. Kama alijua jina la ye yote aliyeelekea kushikwa, aliniambia, na kama nilimjua huyo mtu, nilikwenda nikamhonga mkuu wa wazee wa kuhoji. Gharama ya kuhongana ilikuwa kutoka shilingi mia nne hadi shilingi mia sita. Wakati mwingine marafiki hao waliweza kunilipa kwa haraka lakini wengine hawakuweza na kwa hivyo nilitumia kama shilingi elfu moja zangu mwenyewe kwa njia hii.

Mwanzoni mwa 1953, masettla Wazungu walikata shauri kuihimiza Serikali ifanye mipango ya kuwarudisha makwao maskwota wote wa Kikuyu waliokuwa maelfu wakiwa na jamii zao kutoka Rift Valley hadi risavu, ambao badala yake kungeletwa watu wa makabila mengine kufanya kazi mashambani. Katika historia ya Kenya, hakuna kitendo kingine kilichofanywa kuwaletea watu msiba mkuu kwa haraka kuliko hiki na vile kwamba kilifanywa ni kuonyesha kuwa hali ya mambo ilifikia hadi ya kuanzisha vita halisi. Kampi moja ilijengwa karibu na Nakuru na nyingine karibu na jela ya Thomson's Falls. Basi hapo Wazungu wakaanza, bila kujali cho chote, kuwaondoa wafanyi kazi kutoka mashambani hadi kwenye kampi hizo, ambako walingojea lori za Serikali zije ziwarudishe makwao katika Nyeri, Kiambu na Fort Hall. Badala ya wengine kungojea

kuona taabu za vitendo hivi, katika kampi, walikodisha malori ya kuwarudisha risavu. Wengi wao walizaliwa humo mashambani ambako walifukuzwa. Walikuwa hawajaona risavu hapo mwanzoni, hawakuwa na ardhi huko, hawakuwa na njia ya kujipatia riziki, iliwalazimu kutafuta pesa za kujijengea nyumba ama si hivyo wasongane kwenye vyumba vilivyosongamana, na wengi hata hawakujua jina la risavu ambako wazazi wao walitoka.

Hawakukubaliwa kuandamana na mifugo yao wala hawakukubaliwa kungojea mavuno ya mahindi waliopanda. Idara ya Kazi ilipewa wajibu wa kuuza mifugo na mavuno halafu mapato yake yapelekwe kwa ma-D.C. wao wapya wawagawanyie baadaye. Ninafikiria kuwa huko kurudishwa kwa Wakikuyu ndiko kuliua ile imani na moyo uliyobaki baina ya wananchi.

Nililetewa malalamiko ya vile mambo yalivyoendelea kila siku na kwa hivyo nikakata shauri kwenda kujionea mwenyewe hapo Leshau, ambako palikuwa ni pa kukusanyia karibu na barabara. Sikujali kuketi kwa muda nisije nikashikwa, lakini niliyaona malori na vibarua wakiweka mizigo juu yake wakisimamiwa na masetla Wazungu. Vibarua hawa walikuwa wakiwatupa watoto wadogo juu ya lori kama vile watoto walikuwa vifungu vya kuni, na pengine walianguka kwa uzito katika mbao za lori. Vilio vya watoto siku hiyo vilisikika kama sauti kutoka ahera na hewa ilinukia chuki tupu. Nilifurahia kurudi Nakuru.

Shangazi yangu, Wangui, na ndugu yangu wa pekee aliyekuwa kipofu, Obadiah Mwangi, walikata shauri kuwa mambo yalielekea kuwa maovu na wangerudi kuishi na mama na Gathoni katika Chinga. Nilikodisha lori kwa gharama ya shilingi 399/- ya kuwapeleka nyumbani na dereva akaniarifu kuwa walifika salama. Nilisikitika kumuaga shangazi yangu ambaye alikuwa amenisaidia sana. Baadaye waliniandikia barua wakaniarifu kwamba watu walitaabishwa sana na kuwa vijana walipigwa ovyo na askari wa Serikali na walikimbilia misituni kwa wingi.

Wakati "kifagio" cha kwanza kililetwa Nakuru mnamo Januar 1953, nilishikwa lakini kwa bahati njema tulipopelekwa mahali pa kuhojiwa nilikutana na askari Mmeru aliyeitwa Baiti aliyekuwa rafiki yangu wa zamani. Alinipeleka hemani kwake nikanywe maji na hapo nikamwuliza anisaidie. Kama wengine waliokuwa katika polisi, aliona huruma juu ya kujikaza kwetu na alijua kuwa sikuwa mtu mbaya. Aliniambia nilale kitandani na akanifunika kwa blanketi. Lile jua, hema na blanketi zilinitoa jasho hasa lakini nilikuwa salama na jioni yake baada ya "ufagiaji" Baiti na mimi tulitembea tukishikana mkono tukapita mlangoni hata nje. Tulikwenda kuona picha pamoja—*Mashimo ya Mfalme Sulemani*—na baada ya hivyo nikamnunulia tembo. Nilijua baadaye kuwa watu wengi

walijiokoa kutoka "kifagio" hicho, wengine kwa kuhonga na wengine kwa kujificha ndani ya choo baada ya kumwaga takataka nje ili polisi wapite haraka wakipitia humo, huko wakishika mapua yao. Siku moja niliwahi kununua bastola kwa thamani ya shilingi 300/- kutoka kwa askari mmoja wa K.A.R. hapo Lanet. Nilimpa Gakeri nikamshauri ampelekee Gathego Thuo na Kimani ambao walielekea msituni kupigana. Kwa bahati mbaya walikamatiwa huko Njoro baadaye na Humungati na wakafungwa miaka kadhaa.

"Kifagio" kingine kilifanywa mwezi wa Juni 1953 lakini kwa bahati njema marafiki zangu katika polisi waliniarifu juu yake. Kwa vile kazi yangu ilikuwa muhimu, nilionelea vizuri nisishikwe na kwa hivyo siku moja mbele ya "kifagio" nilikwenda karibu na kaburi ya Nakuru ambako yule rafiki wa mama, Zacharia Ndung'u, alikuwa na kijumba cha debe kilichokuwa ndani ya kuta zake. Alikuwa yuafanya kazi ya shamba la Mhindi aliyeitwa Farrah Mohamed. Zacharia alikuwa baba wa pili kwangu na hakuweza kunikataza mahali pa kulala. Kama nilivyosikia, polisi hawakufagia kaburini. Baada ya tukio hilo nilirudi Nakuru na nikaambiwa kuwa wengi wa jirani walishikwa; sikuwaona marafiki wengi wangu mpaka tulipojiona pamoja kifungoni.

Mara nilipoanza kufanya biashara ya mkahawa, nilinunua baiskeli mbili ambazo nilikodisha, shilingi moja kwa kila saa au shilingi kumi na mbili kwa mchana mzima. Mtu aliyeongoza kazi hii nilimpa shilingi sitini kila mwezi. Aliwabeba wale ambao hawakuweza kupeleka baiskeli. Mwisho wa mwezi wakati walikuwa wamepokea mishahara, iliwezekana kupata kutoka shilingi kumi na tano hadi shilingi kumi na nane, lakini nilimkubalia kujiwekea cho chote zaidi ya shilingi kumi na mbili.

Saa saba kasorobo mnamo tarehe 28 Oktoba, 1953, Inspekta Mwafrika wa Tawi la Pekee la Kenya Polisi alifika hotelini kwangu. Sasa ilikuwa ni mwaka mmoja baada ya kutangazwa kwa Hali ya Hatari na kukamatwa kwa Jomo Kenyatta. Kama ilivyokuwa kawaida, watu walijaa kwani ni wakati huo walifika kusikiliza habari za gazeti. Usomaji wa gazeti ulifanywa na Ngahu Mara, aliyetoka Fort Hall, aliyekuwa msaidizi wangu katika hoteli. Alikuwa amechukua madaraka ya Gibson Gichuri ambaye aliwasomea watu vizuri lakini ambaye alishikwa na kufungwa miaka mitatu baada ya "kifagio" cha Juni. Ile korti iliyosikiliza kesi yake iliwekwa katika kampi ya kuhojiana karibu na kichinjio na niliambiwa na wengine waliookoka kutoka humo kuwa hukumu zilikuwa za msukosuko. Njia ya kuhukumu kama mhalifu atafungwa miaka mitatu au sita ilikuwa ovyo na hakukubaliwa kujitetea. Gibson alikuwa na hati iliyotiwa sahihi na Kenyatta ambayo ilionyesha kuwa alikuwa amefaulu mtihani wake katika Chuo cha Githunguri, ile skuli ya Kenyatta katika Kiambu. Aliwacha

kuonyesha hati hiyo kwa matajiri wangaliompa kazi. Alikuwa rafiki yangu kamili na alikuwa anakaa hotelini mwangu akitafuta kazi ambayo hakuipata.

Yule Inspekta alikuwa na askari wengine wawili na hapo akaniambia kwa upole kuwa nilitakiwa katika hedikuota ya polisi. Hiyo ilitaja kuwa nitafungiwa. Nilikwenda naye. Wakati polisi walipoonekana, usomaji wa gazeti uliachwa na wasikilizaji walikuwa kimya na wenye huzuni wakati nilipochukuliwa. Niliwaambia wasijisumbue. Katika hedikuota ya polisi ya Nakuru, niliambiwa kuwa nitafungiwa kwa muda usiojulikana kufuatana na sheria za Hali ya Hatari na kuwa ningehamishwa nipelekwe kampini iliyoitwa Kowop mbali kaskazini ya wilaya ya Samburu. Baada ya alama za vidole vyangu kuchukuliwa niliulizwa maswali kadhaa. Nilicheza mpira wa gofu? Nilikunywa tembo au sigara? Nilitembea na malaya? Nilikuwa nimeoa? Nilicheza bahati nasibu katika mashindano ya farasi? Baadaye nikasindikizwa hadi hotelini mwangu kuchukua nguo zangu na vitu vinginevyo vyangu. Pia nilichukua akiba yangu ya Shs. 2,400/- ambayo ilikuwa ni faida yangu ya miezi sita baada ya kuanza biashara ya hoteli, nguo zangu na vitabu kumi hivi vya historia, Kiingereza, jiografia na siasa.

Marafiki wangu wa polisi katika Nakuru waliona kuwa nilikaa starehe wakati nilingojea ndani ya chumba changu nikingojea gari la kunipeleka Kowop. Baada ya siku mbili, safari ilianza na baada ya majuma mawili baada ya kutua katika Thomson's Falls na Maralal katika stesheni ya polisi, tulirushwarushwa hadi Kowop. Wakati lori letu liliposimama katika kampi, tulizungukwa na wafungiwa wengine waliokuwa na hamu kututambua. Kwa furaha kubwa, John Kamonjo, ambaye hapo zamani alikuwa mwenyekiti wa K.A.U. ya Nakuru, aliniamkua. Hapo tena nilikuwa baina ya marafiki. Mahali pageni si kitu ukiwa pamoja na jirani wako wa zamani.

4 Kampi ya Vilima Vitatu Vikavu

KOWOP ILIKUWA ni kambi ya hema iliyojengwa bondeni katikati ya vilima vitatu vyenye majabali. Ilikuwa maili ishirini na tano kaskazini ya Baragoi na kama maili sitini kutoka Ziwa la Rudolf. Karibu na kilima cha Ngiro ziko nyasi nzuri ambako Wasamburu na Waturkana hulisha mifugo yao wakati mwingineo. Wakati mwingine ukitazama kutoka mwinamoni wa vilima waviona vijiji vyao (manyatta) ambako vyumba vyao huonekana kama vyumba vya ndege vilivyoinamishwa, kwani vilikuwa vifupi na vyembamba hivi kwamba haikuwezekana mtu kusimama ndani yake. Ingawa Kowop ilikuwa katika wilaya ya Samburu, Waturkana wengi waliingia huko na makabila hayo mawili yaliishi upande kwa upande kwa urafiki. Tabia ya hewa ilikuwa yenye joto na kavu na tofauti sana kutoka ile ya Kikuyuni au Rift Valley. Hapakuwako na maji isipokuwa katika shimo lililochimbwa na ambayo yakionjwa yalisikika kuwa na aina ya chumvi. Baada ya kuoga ndani ya maji hayo, ngozi ilionekana kama vile ilipakwa chokaa na wafungiwa wengi walihara sana baada ya kunywa. Niliishi kambini humo mpaka tarehe 20 Agosti 1954, wakati ilipofungwa.

Hapo mwanzoni tulikuwa wafungiwa thelathini na sita tu. Tulijivunia kuwa sisi tulikuwa wafungiwa wala hatukuwa mahabusu wa kawaida. Hivyo ni kusema hatukulazimishwa kufanya kazi isipokuwa kusafisha mahali petu; tuliweza kuvaa nguo zetu; tuliweza kuweka pesa zetu na tulikubaliwa kutembeatembea ndani ya kambi saa za jioni. Ilikuwako laini moja tu ya seng'enge iliyotuzunguka na haikushikana sana na hata mbuzi waliweza kuingia na kutoka ikiwa iliinuliwa. Hakuna yeyote aliyejisumbua juu ya kutoroka. Baadaye tulijua sababu yake. Waturkana walisema kuwa waliambiwa na D.C. wa huko kwamba Wakikuyu walikuwa watu waovu ambao desturi yao ilikuwa ya kula matiti ya wanawake na pengine walikula mazaliwa ya watoto wakiwa mimbani ya mama zao. Kwa hivyo, kila Mturkana au Msamburu ambaye angemletea kichwa cha mfungiwa mtoro angepewa zawadi ya posho, sukari na chai. Wakati wananchi wa Gold Coast walipokuwa wakipigania uhuru wao, Muturi na wakulima masetla wengine waliwaambia wafanyi kazi wao kuwa Waghana

walikuwa wala watu na walikula watoto wao. Tuliogopa siku hizo wale *Ngorogothi* (Gold Coast) wasije wakatula. Katika macho ya Wazungu katika Kenya, wale Waafrika waliopigania uhuru waliwala watoto wao. (Linganisha kitabu cha Kenneth Kaunda—*Zambia itakuwa huru*, u.k.109: 'Wa vijiji wameambiwa kuwa watu hawa wa Zambia ni wala watu. Zaidi wanapenda watoto kwa sababu walikuwa na nyama nyororo.') Wasamburu na wengine wa huko walikuwa wenye njaa kila mara kwa vile nchi yao ilivyo, na walivyosikia vile D.C. alivyowaambia, wengi wao walikata shauri kuketi kwenye vilima vile vikavu wakitungojea tutoroke.

Komiti ndogo ilikuwa imetungwa baina ya wale wafungwa wa kwanza ikiongozwa na Gad Kamau Gathumbi, mtu wa Kiambu aliyekuwa na duka Nakuru, na Samuel Kiburi, ambaye alikuwa wa polisi hapo zamani katika wilaya ya Embu. (Gad sasa ni mfanyi biashara katika Limuru na ni kiongozi mshupavu wa KANU katika sehemu hiyo). Masharti kadhaa yalikuwa yametungwa na komiti hiyo na ye yote aliyeyavunja alitozwa faini ya kondoo ndume mmoja ambaye alinunua kutoka kwa Waturkana na ambaye aliliwa na wafungiwa wote. Kupigana katika kambi au kutukanana hakukuruhusiwa. Amri zilizotolewa na komiti juu ya kusafisha kambi lazima zitiwe, na ye yote akiulizwa kusaidia kubeba chakula kutoka stoo ni lazima akubali. Pamoja na hayo, hakuna ye yote aliyekubaliwa kumsumbua Wanjiku, ambaye ndiye tu alikuwa mfungiwa mwanamke katika kambi. Alikuwa katika taabu kwani wale wengi waliompenda walimdanganya kuwa watamwoa wakifunguliwa. Komiti ilifaulu sana katika kumlinda Wanjiku ingawa mmoja aliyeitwa Thuo aliyemwingilia sana alitozwa kondoo dume mmoja. Tulifanya mpango wa kuigawanya mojawapo ya hema kubwa ili asiwe akilala pamoja na wanaume.

Chakula kilikuwa kizuri sana. Tulipewa wakia sita za mchele, ratili moja ya unga wa mahindi, nusu ratili ya mboga, nusu ratili ya maharagwe, wakia kumi za viazi na wakia mbili za sukari kila siku na, kila wiki tulipewa ratili mbili na nusu za nyama na wakia tatu na nusu za chai. Utabibu haukutosha. Mturkana mtabibu aliyekuwa na mafunzo nusu tu ndiye alikuwa katika kampi. Alijua kuchanganya dawa rahisi kama ile ya kutuliza tumbo lakini hakujua lingine. Kwa bahati njema baina yetu wafungiwa palikuwa na mmoja aliyehitimu kama msaidizi wa hospitali, Timothy Mwangi aliyetoka Fort Hall, na kufuatia mashauri yake, tulijinunulia mahitaji yetu ya dawa kutoka Baragoi. Timothy alirudishwa katika kazi yake baada ya kufunguliwa na sasa anafanya kazi kama msaidizi wa hospitali katika wilaya yake.

Kowop ilikuwa kambi iliyonipendeza zaidi baina ya zile nilizofungiwa. Wale wetu tuliokuwa na pesa hatukukosa cho chote tulichotaka, pamoja

na sigara na tumbaku. Mmoja wa askari polisi aliyekuwa humo, Mjaluo aliyeitwa Joram alikuwa rafiki yangu mkubwa katika Nakuru. Alihangaishwa na kushikwa kwangu na kupotewa na biashara yangu, na alipanga niwe nikitumiwa gazeti la *East African Standard* na *Baraza* kwa jina lake. Kazi mojawapo yangu ilikuwa ya kutafsiri magazeti hayo kwa Kikuyu kwa ajili ya wafungiwa hao wengine. Ingawa Serikali haikuweza kutulazimisha kufanya kazi, komiti ilitufanyiza mambo. Pamoja na kufundisha Kiingereza kwa akina Gad na wengine, nilichaguliwa karani wa kuandika barua za malalamiko yetu.

Nilipofika Kowop hapo kwanza, afisa aliyekuwako alikuwa Mzungu wa Kenya Police Reserve aliyekuwa na mguu mbaya na tulimpa jina la Kikikuyu la "Gathua". Alikuwa mtu mwema na mpole ambaye alitumia wakati wake mwingi nyumbani au afisini mwake. Hakupendelea kututembelea kule tulikofungiwa. Hakumwadhibu ye yote wetu wala hakufanya matata na ye yote. Baadaye alipigwa risasi na Mzungu mwingine katika Thomson's Falls kwa ugomvi ya ulevi na tulisikitika sana kusikia kisa hicho. "Gathua" alikuwa na msaidizi Mzungu aliyezaliwa Kenya ambaye hakuwa mtu mwema na aliyezoea kulala na wanawake wa Turkana. Siku moja tulikataa kula nyama zilizonuka na msaidizi huyo aliogopa kutakuwa na matata. Kwa hivyo aliwapasa habari polisi wa Thomson's Falls na asubuhi iliyofuata Assistant Superintendent wa polisi alifika kutuona. Alikuwa mtu mgumu na alitusemesha kwa ukali. Alituambia kuwa tukiendelea kukataa kula nyama hizo tutaona cha mtema kuni na tutamtambua kuwa yeye ni Derby. Hakuogopa ye yote au cho chote na kuwa alikuwa akipigana na kuwaua Mau Mau kwa muda mrefu. Sisi tulikuwa kitu kidogo tu. Halafu alimwita Gad Kamau Gathumbi akamwambia anyoe ndevu zake. Kama Gad alikataa au kufanya matata mengine, angalimwondoa kutoka kampi na kumpiga risasi. Alisema ati tulifuga ndevu kwa sababu kila mmoja alijifikiria kuwa yeye ni Kenyatta mwingine. Kwa hakika Kenyatta na ndevu zake walikuwa wakabana na taabu kubwa katika jela mahali penginepo.

Labda alikuwa akitisha tu lakini wengine wa wafungiwa waliomjua katika Thomson's Falls walifikiria anaweza kumwua Gad kwa risasi. Lakini tulinyamaza kimya na hatukumjibu kwani tulifikiria misemo yake kama ujinga wa mwisho. Kamiti yetu ilikuwa imemchagua Gad kama msemaji wetu na kama akinyamaza sisi wengine sote tunyamaze. Baada ya kuondoka kwa Derby, "Gathua" alirudi kutusemeza. Alieleza kuwa kama Derby akirudi na kutukuta na ndevu zetu, angekuwa katika taabu kubwa. Alitushawishi tunyoe ndevu. Na kwa vile hatukutaka "Gathua" apate taabu, tulikubali kuzinyoa. Tulilea ndefu kwa sababu zinamfanya mtu aonekane kuwa mwanasiasa mwema na zinapanusha nafsi ya mtu

faraghani. Katika Kowop, sote tulijaribu kufuga ndevu na lilikuwa jambo la kuhuzunisha siku ile tulizinyoa, na zaidi, baina ya wale wazee. Mimi nilijichekea binafsi kwani kwa sababu nisizojua, zangu zilikuwa zimekataa kumea.

Siku moja kamiti ilikata shauri kufanya urafiki na Waturkana na Wasamburu. Mara mbili kila wiki, lori ilienda nje kuokota kuni. Vile, tukijaza mifuko yetu na posho, chai na sukari tulimpa vitu hivyo Mturkana au Msamburu ye yote tuliyemkuta. Pole pole walianza kutuamini na kuwa marafiki. Ndiyo punde wakatueleza kwa nini hawakuwa wakisema nasi. Kamiti ilipitisha pendekezo iliyomkataza ye yote kulala na wanawake wa Turkana na wakati Waturkana waliposikia hivyo walianza kutuheshimu. Vilikuwa vigumu kuzungumza siasa nao na ilifaa kusema nao kwa mithali au fumbo. Tulijaribu kuwaonyesha kuwa wakati Waafrika watakapotawala Kenya, yale makabila yaliyo nyuma yatapata msaada zaidi kuliko ule waliopata kutoka kwa Waingereza.

Nilikuwa na rafiki mmoja Mturkana aliyeitwa Ashakala, ambaye alikuwa tajiri na mwerevu ambaye alikuwa vitani wakati mmoja. Kiswahili chake kilikuwa bora kabisa. Alikuwa na bibi na wasichana wake watatu na nilikuwa kama mmoja wa nyumba yao. Wakati wo wote lori lilikwenda nje, palikuwako kitu chao kutoka kwangu, au kitambaa, mchele au sukari. Baadaye nilikata shauri kuwa kwa vile uhusiano wetu ulikuwa wa pekee, niwape majina ya mama na dada zangu kufuatia desturi ya Kikuyu. Kwa hivyo bibi wa Ashakala nilimwita Wanjiku na wasichana wake wakawa Nyakio, Njoki na Wangui. Walifurahiwa kupindukia na wakasema kuwa majina hayo mapya yalikuwa kama rehema kwao. Nilichukua picha zao ambazo nilinyang'anywa nilipokuwa Manyani. Siku ya Krismasi ya 1953, tulicheza michezo ya Kikikuyu katika kambi na Waturkana wengi walihudhuria na kujifurahisha.

Wakati Waturkana walipokuwa na mikutano mikubwa ilinishangaza kuona kwamba hawakuchinja wanyama waliokusudia kula, bali badala ya kukata shingo na mkia, walimweka mnyama juu ya moto pamoja na ngozi yake kama kiazi chenye ngozi yake. Walinieleza kwamba kama wakimchinja mnyama kwanza mafuta yote yangedondoka na kupotea na kwa hivyo hawakumchinja mpaka ameiva. Nikiweka shauri fikirani zangu wakati nilikula nyama, niliwaeleza wengine kuwa hata hivyo mafuta yalipotea. Walionekana kama walifahamu nilivyosema lakini situmaini wanafanya kitu tofauti sasa. Pia niliona kuwa bibi zao walikata nyama kutoka motoni, wakaziweka juu ya nguo zao za ngozi ambazo mabwana walizitumia kama meza walipolia chakula. Wasamburu, ambao hutahiri, wameendelea zaidi ya Waturkana, ambao hawatahiri, na desturi za Wasamburu zinafanana na za Wamasai ambao wana desturi nyingi zinazohusiana

na za Wakikuyu. Waturkana walishangazwa kuona mavazi yetu ya suti na kuona saa zetu zilizometameta na zilizofanya *tiki-tiki*.

Mnamo Desemba 1953 na Januari 1954, wafungiwa wengine mia moja waliletwa Kowop kwa makundi mbali mbali kutoka Nyeri na Embu na mahema ishirini na mbili ya kijani kibichi ikapigwa kama malazi yao. Kati ya mahamisho hayo, "Gathua" na msaidizi yake walipelekwa pengine na maafisa wawili wapya wakaletwa. Yule mkubwa nafikiri aliitwa Sampson. Hapo mbele alikuwa wa polisi ya London na alikuwa mnyenyekevu na mwenye urafiki na hakuwa na chuki yo yote. Kwa vile yeye hakujua Kiswahili, nilikuwa mkalimani wake. Msaidizi wake tena alikuwa Mzungu aliyezaliwa Kenya. Alikuwa mtu mpana aliyeitwa Newbury na alionekana asiye na makuu. Ukosefu wake wa ubongo ulimfanya aitwe "Marebe" (debe tupu). Kati ya Januari wafungiwa wote wapya walikuwa wamefika na siku moja, wakati Sampson hakuwako, Newbury alituambia kuwa lilikuwa kusudi la Serikali kwamba wachimbe mashimo ya vyoo ambayo tulikataa kuchimba kwa sababu hatukuwa mahabusu halisi. Sasa tulikuwa tumetunga komiti nyingine ambayo ilikuwa na mawakili kutoka hao wapya ambayo ilikuwa na Gad Gathumbi, Tiras Muchiri (kutoka Kibutio katika South Tetu, Nyeri, na sasa ni mwalimu na mwanasiasa), Peterson Kariuki (aliyekuwa Chifu wa Lokesheni 15 huko Fort Hall na mfanyi biashara), John Mwangi Gachuhi (ambaye alikuwa mweka-hazina wa A.D.C. ya Fort Hall ambaye sasa ni karani wa kampuni ya biashara Nairobi), John Kamonjo, Samuel Kiburi na wengine sita. Komiti hii ilikata shauri kwa kauli moja kuwa hakuna mtu atakayekubali kuchimba mashimo ya vyoo. Ninafikiri kuwa Newbury alifikiria hatua hii akiwa peke yake kwa sababu Sampson hangekubaliana naye. Tuko na methali ya Kikuyu isemayo: "*Ndiri njega ndiringanaga na muuthi mwega*", ambayo ni kusema kwa mfano: Bwana mwema halingani na bibi mwema, na bila shaka hakuna wakati mmoja tulikuwa na maafisa wawili wema wakati mmoja.

Newbury alikuwa na majembe ya kapekulia, mashoka ya kuchimba chini, na tarimbo na akawaamuru wafungiwa wapya kuanza kazi. Justus Kangethe Gachui, mzee aliyekuwa mwalimu hapo mbele katika Kagumo Secondary School, alikuwa msemaji wao na akasema kuwa hawakukusudia kufanya kazi. Newbury aliwaweka nje juani siku nzima na Sampson aliporudi jioni, alikasirika sana kwa kitendo cha msaidizi wake na akawaamuru Justus na kikundi chake kurudi ndani ya kambi, na hapo akaeleza kuwa haikuwako sheria ya kutulazimisha kufanya kazi. Baadaye aliwaajiri Waturkana kuchimba vyoo. Huo sio tu wakati tuliposhangaa kuona tofauti baina ya Wazungu waliozaliwa Kenya na wale waliozaliwa Ulaya: tulianza kufikiria kuwa wazazi Wazungu wengine katika Kenya waliwa-

fundisha watoto wao kuwadharau Waafrika wote.

Sampson alituruhusu kuwinda wanyama ili tuongeze nyama zetu na lori ilikuwa ikiondoka kwa mawindo huko ikijazwa na askari polisi, Wakikuyu na Waturkana. Ulikuwa mchezo mwema na wakati mmoja tulileta mbogo wawili. Waturkana waliweza kukimbia sana na ndio waliotuongoza. Siku moja tulitembelea nyumbani kwa Ashakala tukaalikwa kunywa pombe, kila mtu—polisi, wafungiwa na Waturkana—sote pamoja, na wakati tuliporudi kambini, wengi walikuwa wamelewa na kukosa adabu. Kwa sababu hii, nilitaja kwa kamiti kwamba unywaji wa pombe upigwe marufuku. Jambo hili lilikubaliwa na wazee na likawa ni kanuni.

Gad aliendelea kuwa kiongozi wetu. Ingawa hakuwa na elimu, alikuwa mwaminifu, aliyesikiliza vizuri na mpenda nchi. Alikuwa amejionyesha kuwa *muthamaki* katika mikutano ya wafungiwa na aliendelea kuwa msemaji wa kupendeza na hakimu aliyekuwa na uwezo katika kuhukumu juu ya mabishano madogo madogo yaliyoletwa mbele yake mara kwa mara. (*Muthamaki* ni jina linalopewa mtu ambaye amejionyesha kuwa kiongozi wa maumbile na mwenye hekima kwa njia ya misemo yake katika majadiliano ya faraghani). Sasa nilikuwa nimepewa madaraka ya kugawanya vyakula na kwa ajili ya kupanua masomo ya wafungiwa, nilikuwa na wakati mdogo tu wa kujifurahisha. Baina ya vitabu kumi nilivyoleta kutoka Nakuru ni kile kinaitwa *Waafrika Kumi* kilichoandikwa na Margery Perham, na nilitafsiri maisha ya walioandikwa ndani yake kwa wafungiwa, na jambo hili lilipendwa sana wakati wetu wa kupumzika. Nilihuzunika sana wakati kitabu hiki kilinyakuliwa na watumishi wa Serikali katika kampi ya Manyani.

Wakati kamiti ilipojua kuwa wawili wa wafungiwa walikuwa bado kula kiapo, ilimwuliza Gitu Ngangu aliyetoka Nakuru kuwalisha. Alikubali na akamchagua msaidizi wake, Ndemi Mukuria, aliyetoka South Tetu, Nyeri, aliyekuwa mwananchi mshupavu na alikuwa wa kikundi cha "Forty." (Hiki kilikuwa ni cha vijana waliotahiri mwaka wa 1940, ambao wengi wao walifanya kazi ya jeshi pamoja katika vita vya 1939-45). Waturkana walituuzia kondoo wa kulishia kiapo kilichokuwa cha kwanza na hakikuhusu uuaji. Kamiti iliona haja ya kujichagulia askari wa kuchunga na kujua ni nani alikuwa anavunja masharti na siku moja tulishangaa kuona makaratasi mengineyo yaliyopatikana ndani ya koti la mmoja wa wale waliopewa kiapo. Yalikuwa nakili za barua nyinginezo alizoandika kwa Tawi la Pekee la Polisi la Thomson's Falls kabla ya kufungiwa, yakieleza vile watu walizidi kupinga Serikali katika sehemu hiyo, na pia palikuwa na barua nyingine ambayo ilikuwa bado kutumwa, iliyoeleza juu ya kiapo katika kampi hiyo. Kamiti ilikata shauri kukamata makaratasi

hayo na kumpiga marufuku kama asiye wa kundi letu. Katika kifungoni, ni adhabu kubwa kama watu wakikataa kusema nawe. Baadaye alirudishwa Thomson's Falls na Serikali. Ni lazima alikuwa ametumwa kupeleleza mambo yetu.

Wanawake Wakikuyu wengine walijiunga na Wanjiku katika Kowop na sasa walikuwa na hema lao wenyewe. Kamiti ilikaza masharti yake lakini wengine walivumbua njia nyingine kama vile kukutana katika chumba cha kuogea, wakati wa usiku. Kwa hivyo tulituma ujumbe kwa Commandant tukamweleza kuwa mipango ya malazi haikufaa na kwamba wanawake wajengewe mahali pao nje ya kampi yetu. Hatua hiyo iliitengeneza mambo kidogo lakini wanaume waliendelea kutafuta njia nyingine za kupatana na mabibi hao mpaka siku moja wanawake wote walihamishwa kutoka Kowop wakapelekwa jela ya Kamiti katika wilaya ya Kiambu karibu na Nairobi, ambako tulisikia baadaye kuwa kiongozi wao, Nyamathira, alifarikia.

Tarehe 14 Februari, wakati Sampson alikuwa nje tena, Newbury alitoa amri kuwa ye yote asitoke nje wakati wa usiku. Ikiwa mtu alitaka kwenda chooni, ni lazima aombe ruhusa. Tangu hapo tulikuwa na uhuru wa kutembeatembea kambini saa za usiku na tuliheshimu uhuru huo na kwa hivyo tulikasirika. Kwa sababu fulani Newbury alienda juu ya mnara wa kuchungulia usiku huo. Mipango hiyo yote ilionekana ya kitoto na kwa hivyo tulipanga kumsumbua kwa kusimama nje ya hema zetu kwa vikundi na kila mtu akipiga kelele: "Bwana, nataka ruhusa". "Kwenda wapi" alijibu. "Kukojoa", "Kwenda Nairobi", "Kwenda Kowop", "Kula tembo" na matusi mengine mengi yasioandikika. Hii yaweza kuonekana kama utoto na upuzi, lakini hata Newbury alikuwa hivyo. Mwishoni alikasirika hata akapiga risasi mara mbili angani na tukarudi mahemani mwetu. Asubuhi yake nilimwambia kuwa alifanya vibaya na nikaandika barua kwa D.C. nikamwuliza aje achungulie jambo hilo.

Kwa mara nyingine Sampson hakupendezwa na vitendo vya Newbury na alituunga mkono wakati D.C. alipofika kuzungumza nasi kufuatia barua yangu. D.C. alionekana kuwa mtu mwenye uchungu na alisema kwa ukali. Lakini wakati alipoona kuwa hatukumwogopa, aligeuka kuwa binadamu na akajibu mengi ya maswali tuliyomwuliza. Baada ya matembezi hayo yake, tulikubaliwa kutembeatembea tena katika kambi. Sampson alikuwa mtu tuliyekuwa na imani ndani yake. Alikuwa akikagua kambi kila Jumamosi na tuliisafisha sawa kwa ajili yake. Wakati tulikuwa kambini, tulimpa mfungiwa wa kumpikia. Alipopelekwa pengine mwezi wa Aprili, tulihuzunika kumwona akituacha. Newbury alikwenda wakati huo huo. Afisa aliyerudi badala yao aliyeitwa Chester alikuwa mkatili na mpumbavu. Alidharau kusema na mfungiwa ye yote

na alituangalia kwa ajabu kama vile tulikuwa wanyama waliowekwa ndani ya seng'enge katika "zoo".

Siku moja aliingia ndani ya kambi akatuambia kuwa atatufanya tufanye kazi. Tulikataa. Ndipo akamvuta mmoja wetu kwa nguvu, Ndung'u Njoroge, hadi nje ya kambi. Ndung'u alikataa kwa nguvu na nikaenda pamoja na wengine kumsaidia. Polisi wote walipiga firimbi na wakaizunguka kambi. Chester aliingia ndani tena akasema nasi. Alikuwa amekasirika sana na alisema kuwa kama hatukufanya kazi vyakula vyetu vingepunguzwa. Tulikataa kabisa na vyakula vyetu vikapunguzwa tokea siku hiyo kwa zaidi ya nusu. Tulianza kumchukia Chester. Punde wengine ishirini wetu walikubali kufanya kazi kwa ajili ya njaa. Hapo kamiti ikafanyiza mkutano na shauri likakatwa kuwa umoja ndio ulikuwa muhimu wakati huo kuliko kusimama kwa maongozi yetu na kwa hivyo tulifanya masikilizano na Commandant tukakubali kufanya kazi juu ya kiwanja cha ndege lakini si pengine. Kiwanja cha ndege kilikuwa na faida kwetu kwa sababu wakati wa mvua barabara zikiharibika mgonjwa wetu angerushwa kwenda hospitali au vyakula vyetu virushwe ndani.

Niliendelea kuandika barua kwa Gavana, Mkuu wa Polisi na Waziri wa Makoloni, huko nikieleza malalamiko yetu. Barua hizo nilizituma kwa mkono wa rafiki yangu Joram, yule askari wa polisi. Nilijihadhari sana Chester asije akaniona nikijipendekeza kwa askari wakati wo wote. Katika barua moja, nilimshitaki Chester kwa ukatili wake na afisa wa polisi alifika kutoka Maralal. Aliita mkutano wa wafungiwa wote. "Wapi Josiah Mwangi?" alipiga kelele. "Ndimi hapa," nilijibu. "Sema Bwana," aliamuru. "Bwana", nilisema. Aliniangalia akiwa kimya kwa muda mrefu akiwa na chuki katika macho yake zaidi ya yote niliyoiona ndani ya mtu yeyote mwingine. Alisema kuwa alijua kuwa nilikuwa ninatuma barua kwa watu wa nje halafu akanikubali nirudi pale wengine walipokuwa.

Pia nilimwandikia barua Chester mwenyewe, na siku moja aliniita nje ya afisi yake na akazirarua zile barua kwa madharau huko akisema maneno maovu sana. Nilikasirika na nikaushika mshipi wake nikamwangusha sakafuni mara tatu. Askari walinitoa nje na baada ya robo saa nikajua yaliyoningojea yaani kusimama juani nikitazama vilima vya Kowop kwa muda wa masaa sita. Miguu yangu ilijikaza na kichwa kiliniuma siku hiyo lakini utumiaji wa nguvu ulisafisha kitu hatari kilichokuwa kimechemka ndani yangu kwa muda.

Ilikuwa ni desturi yetu kuwachinja wale mbuzi tuliopewa kama sehemu ya nyama ya vyakula vyetu. Wakikuyu hufikiria kuwa nyama ile bora zaidi katika mbuzi ni kichwa ambacho hufanyiza mchuzi mtamu sana. Chester aliamuru kwamba tuwape askari vichwa vya

mbuzi, amri ambayo ilitukasirisha sana sote. Nilifikiria njia bora ya kujadiliana na jambo hilo bila matata. Nilikuwa rafiki wa polisi na kwa hivyo niliwaendea nikawauliza kama walifahamu kuwa wakati tuliwapa vichwa hivyo, wafungiwa walivielekeza upande fulani na kusema maovu juu ya ye yote aliyevila. Nilikuwa nimepanga kuwa wafungiwa wawe wakifanya hivyo na wakati askari walipoona hivyo, walishtuka hata wakamtuma sajenti wao akamwambie Chester kuwa hawakutaka vichwa. Pande zote mbili zilipendezwa nami, polisi kwa vile nilivyowaonya juu ya uchawi huo ambao walikisia Wakikuyu wangetumia, na wafungiwa kwa ahadi ya mabakuli mengi ya mchuzi mtamu.

Wakati huo wote tulisikia machache tu ya kweli juu ya mapigano ya misituni. Tulikufa moyo kwa kusikia juu ya "Kifagio Anvil" (Operation Anvil) katika Aprili 1954 kilichofanywa Nairobi, wakati watu 24,000 walishikwa na kupelekwa kambi ya Langata, ili kuhojiwa. Komiti yetu ilijikaza kututia moyo na kuwa wananchi washupavu na wasio vigeugeu. Tulikuwa tumejua ujinga wa kutofahamikiwa na Serikali ambao uliendelea kupanua kutosikilizana, na tulifikiria kuwa kambi za kuwafungia wananchi zitakwisha mwisho wa mwaka huo na kuwa Serikali haikuweza kukosa kusikiliza mapendekezo ya Waafrika na kutupa uhuru mwaka wa 1956.

Agosti 19 lori sita zilifika nje ya kambi yetu na wengi wetu walifikiria wakati ulifika tufunguliwe. Tulipokuwa tukipanda malori, Chester alielekesha kidole chake upande wangu na kumwambia afisa aliyekwenda nasi kuwa mimi ndiye kiongozi wa matata. Afisa huyo alinichapa viboko vitatu. Nilikuwa karibu kujilipiza kisasi lakini nikafikiri aliweza kuniua njiani nikifanya hivyo. Kufika Maralal tulisikia kuwa tulielekea Langata karibu na Nairobi. Kati ya Maralal na Rumuruti tulikwama mahali paitwapo Suguta Marmar wakati wa jioni, na tulisukuma na kuchimbia malori mpaka yakatoka. Tulilala usiku huo bila blanketi, tukijikunja karibu karibu ili kupata joto kama wanyama waliotukiwa na upepo wa nguvu wakiwa nje ya nyumba zao.

Ziko nyimbo nyingi tulizoimba Kowop, lakini huu ndio uliandikiwa pale na Gad Gathumbi, Richard Murugi, aliyekuwa seramala aliyejiita "Yesu" na mimi kufuatia hizi laini mbili zilizoletwa kutoka kwa ndugu zetu waliokuwa wakipigana Thomson's Falls:

Ngai twari ngo twari itimu na ruhiu
Riu ciothe nitwatunyiruo ni ageni.

maana yake

Mungu tulikuwa na ngao tulikuwa na mkuki na kisu
Sasa hizo zote tulinyang'anywa na wageni.

(Ilikuwa ni alama ya uwanaume baina ya Wakikuyu kubeba ngao, mkuki na simi. Serikali ilikuwa imewakataza Waafrika kuzibeba bila ruhusa maalum kufuatia ile sheria inayochunga silaha za Waafrika).

Mararaga matari toro	Walikesha bila kulala usiku kucha
Magiciria uria makahota	Wakifikiria vile watakavyoweza
Kuuraga munene witu Kenyatta	Kumwua kiongozi wetu Kenyatta
Na gutiri undu makahota	Na hakuna watakaloweza
Ngai twari ngo, twari itimu na ruhiu	Mungu tulikuwa na ngao, mkuki na kisu
Riu ciothe nitwatunyiruo ni ageni	Sasa hizo zote tulinyang'anywa na wageni
Haria ciaigiruo wee niui	Zilipowekwa wewe wajua
Ngai cioe umahure nacio	Ziokote uwapige nazo
Aanake a Gikuyu umai	Mashujaa wa Kikuyu ondokeni
Nuu utarona muthuuri naiarakura	Nani haoni mzee anazeeka
Mwakoma igina ithii na ageni	Mwalala wageni waende na mali
Ciana cia mumbi ikagunwo ni ki?	Vizazi vya mumbi vitasaidiwa na nini?
Miaka mirongo itano na iiri mithiru	Miaka hamsini na miwili iliyopita
Nuu utarona uria twikitwo ni ageni	Nani haoni vile tumetendewa na wageni
Nawe kirimu woya mbia	Na mjinga wee wapokea pesa
Wendia ruriri ruaku mbia	Wauza taifa lako pesa
Wee kirimu thii woe ngiri	Wee mjinga nenda upokee elfu
Kai ciathira ukaheo ki?	Kwani zikiisha utapewa nini?
Njoke ngwire atiri wakini	Halafu nikuambie mtu wa rika
Wahitithio njira muthenya	Wakoseshwa njia mchana
Ni mugeni ukuroka guthii	Ni mgeni atakayekwenda kesho
Kiamugeni kiruaga gwaka	Cha mgeni kisijenge
Kiroitiriruo ndia ndiku ni Ngai	Na kitoweke chini ziwani
Wathani wake naguo uthire	Utawala wake nao uishe
Bururi uyu witu wa Kenya	Nchi hii yetu ya Kenya
Twiyathe twi ithuiki andu airu	Tujitawale tukiwa peke yetu sisi weusi

5 Langata na kufika Manyani mara ya kwanza

MSAFARA HUO MREFU wa malori ulifika Langata kukiwa na mvua kidogo kwenye mwendo wa saa mbili za usiku wa Agosti 21, 1954. Langata, nimeambiwa, iko kama maili tatu hivi kutoka kati ya mji wa Nairobi, karibu na National Game Park, lakini tangu nilipofunguliwa sijawahi kupata nafasi kutembelea huko tena na kwa muda wa siku kumi nilizokaa humo mambo ya jiografia hayakujali kitu. Mara hatukuwa na wasiwasi kuwa kukilinganishwa, Kowop ilikuwa kama kambi ya starehe za mapumziko.

Wakati tulikuwa tungali ndani ya malori, askari wa K.P.R. aliyekuwa Mshelisheli alitujia, na akisimama juu ya tairi, aliinama kutuelekea, huku akatushtusha kwa vile alianza kututwanga kwa fimbo yake ndefu. Alipiga kelele: "Ma Ma Mba", "Ma Ma Mba," na alionekana kama mwenye wazimu. Kujilinda binafsi kukiwa muhimu, kila mmoja wetu alianza kujificha nyuma ya mwengine. Wengine walikimbilia kwenye lori dogo lililokuwa upande ule mwingine wa hilo kubwa kujitafutia usalama. Hayo mapigo yalikuwa ovyo na ya bila kujali na damu ilitudondoka kutoka vichwani na mikononi. Alikuwa na uso mbaya wa ukatili na hakuweza kusema Kiingereza au Kiswahili vizuri. Kwa bahati njema, yule Mzungu tuliyetoka naye kutoka Maralal alifika hapo na akatuokoa. Alimwambia huyo Shelisheli kwamba haikumpasa kutupiga bali angalingoja kikosi chake cha wafungiwa ambacho angefanya atakalo nacho. Tuliwaona huruma "hao."

Afisa wetu ambaye alikuwa amewaleta Askari Kanga kama thelathini na Humungati wengine alituamuru tushuke na kukimbia moja kwa moja hadi sehemu yetu iliyokuwa Nambari 21. Tuliharakishwa sana hivi ili tulazimu kuacha mizigo yetu nyuma. Ingawa hivyo, tuliletewa mizigo yetu yote asubuhi yake. Tulipofika katika sehemu yetu kama saa mbili na nusu za usiku, tuliamuriwa kuketi juu ya miguu yetu kwa laini, kila laini ikiwa na watu watano, na tukaambiwa tuwekelee mikono juu ya vichwa vyetu. Huu ndio ulikuwa mpango wa kuwahesabu wafungiwa katika kambi zote. Afisa angetembea kwa haraka baina ya laini hizo za

watu, akihesabu kwa sauti kubwa, huko akimchapa fimbo ye yote kama ilivyompendeza. Laini za katikati zilipendelewa sana kwani waliokuwa humo waliokoka kuchapwa kulikofanyiwa wale waliokuwa mbele au upande kabisa. Hapakuwa na haja ya ushujaa na mimi nilipata laini ya katikati mara kwa mara.

Lakini kuhesabiwa hakukuwa mwisho wa matukio ya usiku huo wa kwanza. Yule Shelisheli mjeuri alisimama mbele yetu akatuambia turudie misemo fulani nyuma yake. Wakati tulipokuwa tukihesabiwa, sehemu yetu ilijazwa na Askari Kanga na Wazungu hata wakaonekana karibu kuwa wengi kama sisi. Yule Shelisheli kwanza alituambia tuseme "Ma Ma Mba": sasa haya yalikuwa maneno yasiyokuwa na maana na tuliyarudia kamili ingawa tulijua kuwa alikuwa akituambia tuseme kwa Kiswahili kuwa *Mau Mau Mbaya.* Humungati mmoja alituambia turudie nyuma yake: "Sisi Wazungu tutatawala nchi hii milele." Kwa vile yeye alikuwa Mkikuyu, sisi tuliona hii ajabu na kurudia kwake hakukupinga maongozi yetu. Wakati huo wote, wale Wazungu na askari kanga walizururazurura baina yetu na kumchapa ye yote ambaye hakusema kwa sauti kubwa. Kwa vile tulikuwa hatujala kitu tangu tulipotoka Kowop, haikuwa ajabu kuwa wengine hawakupendelea kutoa sauti kubwa. Halafu tuliambiwa tusema: "Jomo Kenyatta ni mbwa." Tulinyamaza tukakataa kusema hivyo ingawa tulipigwa sana kwa fimbo. Halafu tuliambiwa tulale chali kwenye matope ya mvua huko ndani ya sehemu yetu. Mmoja wetu alitumia ubongo akavumbua neno la Kikuyu—"mba—yaani *mwumbaji*" na neno likapitishwa tuseme kuwa "Semeni kuwa yeye ni 'mba' wala si *mbwa* (kwa Kiswahili)". "Sema, sema," alisema Askari Kanga huko akiendelea kutuchapa. Tulisema, lakini kwa bahati mbaya Mkikuyu mmoja alifahamu vumbuzi letu na wakawa wakali hao makanga. Walimchagua mmoja wetu aliyetoka South Tetu aliyeitwa Gachahi, wakamsimamisha mbele hapo wakampiga mpaka aliposema yale maneno waliyotaka. Lakini Gachahi alivumilia sana na hakutuaibisha. Baada ya hivyo, tuliambiwa kusema: "Dedan Kimathi na Stanley Mathenge wataishia msituni." Hayo yalikuwa ni majina ya wawili wale viongozi wa Jeshi la Kupigania Ardhi waliokuwa msituni wa Nyandarua, na kwa kweli hatukuweza kububali kusema hivyo. Lakini bahati ni kuwa neno *ishi* linasikika kama *isha,* na kwa hivyo tukisema kwa sauti ya chini tuliwahi kuchanganya maneno hayo mawili. Kufuatia hivyo tuliambiwa kusema kuwa "Dedan Kimathi na Stanley Mathenge ni *mavi*". *Mavi* iliweza kugeuzwa kuwa *maji* kwa urahisi, lakini haikuwa na maana sana. Mwishowe, upuzi huo ulikwisha. Vitendo hivyo vilionekana vya kijinga kwani mtu ye yote mwenye akili angeona kuwa vingeongeza roho zetu nguvu badala ya kupunguza imani yetu na kwa vile wale waliovianzisha

walifanywa kuonekana kama watoto wakati wa vitendo hivyo. Hatukupewa chakula usiku huo na tulipokuwa tukienda kulala tulizungumza yale yaliyotendeka. Tulifikiria vile vilima vitatu vya Kowop tukameza mate. Langata hapakufaa.

Asubuhi yake tuliona kuwa hema zilijaa kote kutuzunguka na kuwa tulikuwa ndani ya laini za seng'enge nyingi kuliko zile tulizokuwa tumeona hapo mbele. Langata ilikuwa kambi ya kuwachagulia wale waliofagiwa na "Operation Anvil." Ufagiaji huo ulianza Aprili 1954 na ulikusudiwa kuvunja komiti za Mau Mau katika Nairobi na kuondoa njia za upelekaji wa dawa na vifaa vya vita ambavyo vilikuwa vingali vinapata njia hadi misituni. Pia ulikusudiwa kuwashikisha wale walaghai kadhaa waliokuwa wakifanya mambo yao mjini. Hii iliwezekana kwa njia ya kuzungukia kila sehemu ya mji na kuwashika wote waliokuwamo wakati huo huo. Wale wote waliokamatwa basi wakaletwa mbele ya wengine walioajiriwa na Tawi la Pekee (Special Branch) la Polisi waliojifunika kwa magunia yenye mashimo ya kuonea ambao walijulikana kama "Tukunia"—yaani *vigunia vidogo*. Vigunia hawa walichanganyikana sana. Wengine wao walikuwa wale mikora wa kawaida ambao waligeuka kuwa wasaliti wenye ujuzi wa kazi ambayo iliwapatia mali imara ambayo hawakuijua hapo mbele: vile hali ya hatari ilivyozidi, ndivyo haja ya watu kama hao ilivyozidi, na hapakuwa na hofu ati watu kama hao watapunguka. Lakini walikuwako wengine tuliowaita "Tai Tai" kwani hao walikuwa wale waliokuwa na elimu ambao walifunga tai. Wengi wa hawa hawakuwa na kazi na waliajiriwa ili wajipatie mali ingawa wengine ni wale waoga ambao waliogopa kushikwa. Hawa wote hapo kwanza walikuwa na ile haja ya uhuru lakini hamu yao ilipunguzwa na mahitaji yao na hofu. Ni wale ambao hawakuwa na elimu ambao walibaki imara wakati wa vita hivyo. Kila mmoja alipitia mbele ya mashetani hao ambao mara wangesema: "Mchukue." Aliyetajwa namna hiyo aliletwa katika kambi yetu ambako alingojea gari la kumsafirisha hadi kifungoni.

Wakati mwingine Vigunia hivyo vilifika Langata yenyewe ambako wangewapa daraja wale waliofungiwa pale. "Nyeusi" ilikuwa daraja ya wale waliokataa kutubu baina ya wana-Mau Mau. "Kijivu" ilikuwa ya wale ambao waliingiliwa sana lakini ambao wangeweza kugeuka baina ya wana-Mau-Mau; "Weupe" ni wale ambao hawakuwa na dhara ya u-Mau Mau au ambao waligeuka. Sikuweza kutambua kama yule kivumbuzi wa daraja hizo alifahamu vile zilikuwa na maana mbili; kwani "Nyeusi" ni rangi ya Mwafrika na "Nyeupe" ni rangi ya Wazungu. Kutoka Langata, mfungiwa alipelekwa katika kambi nyingine kulingana na daraja yake.

Bila shaka Serikali ilishinda katika kusudio lake la wakati huo. Nairobi

ilifagiwa. Lakini iliwashika na kuwafunga wengi ambao hawakuwa na dhara. Ninakumbuka mwenda wazimu mmoja aliyepewa daraja ya "Nyeusi" aliyepelekwa Manyani; hatua hii ilimtia huzuni pamoja na wale waliofungiwa pamoja naye. Ni wazi kuwa hakuna mtu mmoja anayeweza kujua siri za watu hamsini lakini hao Vigunia walijidai kuwajua kwa mamia. Iliwalazimu kuonyesha ujuzi ili wapate riziki yao; pia wangekuwa si binadamu kamili kama hawakuwa wenye chuki wakati mwingine. "Operation Anvil" ilizidisha wafungiwa mara mbili wakati huo na hatua hiyo iliumiza Serikali kichwa na shida ambazo hata sasa hazijaondolewa. Tulipofika Langata, palikuwamo na wafungiwa kama elfu nne na walihamishwa hadi Manyani wakiwa vikundi vya elfu moja mara mbili kila wiki.

Baada ya siku mbili bila chakula wala maji, tulikuwa na njaa sana na koo zetu zilikauka vile ati hata hatukuweza kumeza mate. Tukishauriwa na Timothy Mwangi, tulikunywa maji ya moto yakiwa na chumvi kwa mara ya kwanza. Shauri hilo lilisaidia au tulifikiria lilisaidia. Mwishowe wakati tulipoona chakula tena na tulikuwa twaketi kula ugali, tuliitwa tukahesabiwe. Hii ilionekana amri ambayo haikuwa na haja na tukakataa kwenda. Mambo yalikuwa sawa kwa muda wa dakika chache lakini mara tukayaona mawingu mekundu ya askari kanga waliotutukia na kuanza kutupiga na kutuachisha ugali wetu tuliokula nusu wakatusindikiza hadi kwenye mahali pa kuhesabiwa. Hicho chakula hatukukiona tena. Tukio hilo lilifuatwa na kudungwa masindano ya T.A.B. na inspekisheni. Kama askari kanga alimwona mfungiwa na pesa, alimpiga kofi kali hivi hata akasahau kila kitu kwa muda na wakati fikira zilipomrudia alijiona bila pesa zake. Ilikuwa desturi kwa mfungiwa kuchimbia vitu vya thamani chini baada ya kufika kambini kwani hakuna mfungiwa aliyemwibia mwingine, lakini tukapatwa na hasira kubwa kwani hatukurudishwa Nambari 21 bali tukapelekwa Nambari 10. Kwa vile kuwako na pesa kulikuwa muhimu kwa maisha yetu katika kifungioni, tulighadhibishwa na kitendo hicho, na kwa vile maisha yetu yalikuwa chini ya sheria mbili, yetu na yao, hatukutarajia msaada kutoka kwa ye yote wakati tulivunja sheria zao kwa kutii zetu. Nilikuwa nimeanza kufikiri sana juu ya pesa zangu. Nilikuwa ningali na shilingi elfu mbili, mia mbili na arobaini na ulikuwako uvumi huko Langata kuwa tutapelekwa Manyani ambako hakuna aliyekubaliwa kuwa na pesa. Kwa hivyo nilikata shauri kuzishonea shilingi elfu mbili ndani ya koti kwenye mabegani na kubakia na zile nyingine mia mbili na arobaini mfukoni. Baada ya kazi ya masaa mengi ya ushonaji, hizo elfu mbili zikawa salama. Bila hizo pesa, ingelikuwa shida kufanya mengine niliyofanya baadaye katika Manyani na pengineko.

Maafisa waliokuwa Langata hawakuwa na sehemu za pekee walizo-chunga. Walizunguka kote ndani na nje ya sehemu zote. Alikuwako afisa mmoja mwenye masharubu aliyeonekana mjanja na mwenye akili. Alikuwa akituambia kuwa yeye hakuamini katika kuwapiga watu na baadaye kila mmoja angeungama yote aliyoyatenda. Alikuwa wa kabila la Waskoti na alionekana kama alifahamu vile maisha ya usoni yatakavyokuwa. Tulimjua kwa jina la Maclachlan kwani vyombo vya kupaaza sauti vilikuwa vikimwita kwenda mahali fulani. Yule Mshelisheli alikuwa kinyume cha huyo kabisa kwa tabia zake. Alionekana kama asiyeweza kuhesabu na alitumia wakati wake akipiga kelele na akinguruma. Msemo aliyoupendelea sana ni "Mnawaua watoto, mnawala watu." Wengine wetu walighadhabishwa hata wakamwuliza: "Tumemla mama yako au baba yako?" Alionekana asiyekuwa na furaha na wakati tulipoondoka nilimhurumia.

Wakati nilipokuwa huko watu wawili waliadhibiwa kwa kuwekwa ndani ya *shimo kwa* muda wa masaa ishirini na manne. Hilo lilikuwa ni shimo lenye uchini wa futi kumi, na upana na urefu wa futi nane mraba na lilikuwa na matope ya inchi sita na huko lilifunikwa kwa kifuniko cha chuma. Ilikuwa baridi sana ndani yake na rafiki yangu aliyekuwa katika Namba 9 iliyokuwa jirani alinieleza kuwa halikupendeza kamwe. Hakuna aliyeweza kufikiria chanzo chake kilikuwa nini. Nilipewa Nambari 54505 nilipokuwa Langata na nilibaki nayo wakati nilipelekwa Manyani. Tulilazimishwa kusema "Effendi" wakati wa kuzungumza na Mzungu ye yote. Jina "Effendi" hapo mwanzoni lilikuwa jina la heshima kwa wa-Turki na labda liliingia katika King's African Rifles pande za Uganda kwa ajili ya majeshi ya Wamisri na Wasudani. Leo linatumiwa katika Kenya wakati askari anamjibu mkuu wake. Kwa vile kulisahau kulileta maumivu, tulimjibu ye yote aliyekuwa na uso mweupe, au ni kasisi, mwanachama wa Halmashauri Kuu, daktari au bibi, kwa jina hilo la "Effendi."

Baada ya siku tatu katika Langata, askari wa jela walianza kutuambia kuwa tutakwenda Manyani tarehe Agosti 31. Manyani ilikuwa ni kambi ya "Weusi" daraja ambayo kila mmoja wetu aliyetoka Kowop alipewa. Hatukusumbuliwa na wale wajuzi wa "gunia" na tulimshukuru mwenye uwezo kwa ajili hiyo. Askari walituambia kwa mkazo kuwa katika Manyani kila mmoja wetu angekubaliwa kuweka suti moja tu. Ili kutusaidia, walisema wangeweza kutununulia nguo nyinginezo zaidi ingawa ilitufaa kufahamu kuwa gharama yake ingekuwa ya chini kufuatia vile mambo yalivyokuwa. Kwa hivyo wengi wetu waliuza vitu vyao wakitumaini kuwa wataweza kutunza pesa walizopata.

Tarehe Agosti 31, 1954, wengine wetu waliokuwa 1,200 tulibebwa na

gari la pekee la kusafirisha wafungiwa lililoitwa "Gari la Waya" ambalo madirisha yake yalifungwa na seng'enge. Tulielekea Manyani katika Jimbo la Pwani la Kenya. Tulipoacha gari tena, tuliwaona askari wa jela waliofanya mstari katika kila upande wa barabara pana wakiachana kwa hatua chache tu. Walikuwako maelfu ambao wote walibeba rungu za kiaskari. Kwa vile ulikuwa mwendo wa maili tatu kutoka stesheni kwenda Manyani, maelfu hao wa askari hawakutosha na kwa hivyo walipelekwa kwa malori mbele yetu. Walinyakua kila kitu ambacho hakikufungwa au ambacho hakikuwa katika sanduku. Kama mfungwa alisimama ili kujadiliana, alipigwa ili aendelee. Mwishowe tulifika kambini na huko tukajiona ndani ya Sehemu 26. Afisa aliyeonekana mkali alitulaki na huko akikunja mikono yake kifuani alitoa hotuba ya kutukaribisha kwa maneno haya: "Sasa mmefika Manyani. Hii ndiyo Manyani na punde si punde mtapata kuifahamu. Kama mnavyo vitu kama pesa, barua, saa au visu au kingine cho chote, mvitoeni. Kama ye yote atajaribu kuficha cho chote, ataona kitu kibaya. Baada ya kutoa vitu vyenu mtapelekwa jikoni ambako mtafanyiwa inspekisheni na nguo zenu zilizo zaidi zitawekwa ndani ya stoo. Mtabaki na jozi moja tu la mavazi. Mnafahamu?" Tulijibu kuwa tulifahamu na ingawa tulijifunza yote huko Langata tulianza kuchimbia vitu vyetu vya thamani katika ardhi. Afisa mmoja alichukua pesa na yule mwingine akachukua vitu vinginevyo. Uvumi ulienea kuwa walikuwa wakiandika shilingi 2,000/- kama 200/-, shilingi 200/- kama 20/- na shilingi ishirini zilibaki ishirini. Zile shilingi zangu 242/- nilikuwa bado kuzishonea ndani ya koti langu na sikukusudia kuzipoteza. Kwa hivyo nilizikunja zile noti mbili za mia zikawa nyembamba kama ilivyowezekana halafu nikazishindilia kwenye mafundo ya nywele zangu. Nywele za Kiafrika zinayo faida yake. Nilimpa askari mmoja zile shilingi mbili kwani mtu hakuweza kujua ni wakati gani askari kama huyo angekuwa msaidizi. Nilitoa zile noti mbili za shilingi ishirini pamoja na saa yangu ambazo sikupewa risiti juu yake na sikuzipata tena.

Halafu tulienda karibu na jiko ambako tulifanyiwa inspekisheni. Wafungiwa wengine walificha pesa zao vinywani mwao (ambako kama walizificha sawasawa wangeweza kusema bila kuharibu misemo yao), wengine walizificha kwenye vidole vya miguu, au kwenye mkundu. Tuliamriwa kuondoa mavazi yetu na miili yetu ikachunguliwa sawasawa. Tena tulifanywa kurukaruka kama Wakamba ikikusudiwa kuwa kuruka—ruka huko kutaangusha cho chote kilichokuwa kingali kimefichika. Nguo zangu, chombo cha kupiga picha na vitabu vyangu vilichukuliwa. Vile vitabu vilikuwa hasara kubwa kwangu na usiku huo nilipatwa na huzuni sana. Tulighadhabika kuona kuwa badala ya kurudishwa katika Sehemu

26 tulipelekwa Sehemu 21. Vile vitu tulivyochimbia ardhini vilipotea. Hata vile ilikuwa sawa kwani ni wachache sana wa waliofungiwa katika Manyani waliovipata vile vitu au pesa walizopeana kwa maafisa. Hali hii haikuwa hivyo kwa ajili ya wizi wa askari tu, bali ni kwa vile vitu havikuwekwa vyema ndani ya stoo. Kuviweka sawasawa kungelazimisha mipango kamili na uwezo ambao kwa wakati huo haukuweza kupatikana kutokana na Idara ya Jela.

Asubuhi yake tulionana na "wahoji" kwa mara ya kwanza. Kiongozi wao alikuwa mfungiwa aliyeitwa Henry. Henry alikuwa na desturi ya kumwita mfungiwa mmoja na kumwambia alale chini mbele yake ili aweze kumwekelea mguu wake. Kutokea na hali hiyo ya ukubwa alifaidika kwa nguvu zaidi iliyomwezesha kuita majina yetu. Lakini kwa vile haikuleta kukalia miguu bila kusonga hata kidogo, ilionekana na wengine kuwa afadhali kulala chini na kuwekelewa mguu. Tuliwafikiria wahoji wote kuwa wahaini. Wengi wa wale walioletwa kutoka Rizavu kuwa wahoji walisahau mapenzi ya nchi yao kwa ajili ya pesa. Wale ambao walikuwa wafungwa walipendelea maisha ya raha badala ya kuumia. Ni wachache sana, ambao baina ya vikundi hivyo viwili ambao walifikiria kwa moyo wao kuwa Chama cha Kiapo kilikuwa njia mbaya ya kushindania haja zetu na kuwa Uhuru utaharibika ikiwa kitafaulu. Hawa walikuwa watu waaminifu na wa kweli na tuliwaheshimu ingawa hatukukubaliana na maoni yao. Katika kambi zote nilizofungiwa nilipwajua watatu tu ambao wangebandikwa tabia hiyo. Wahoji wote walihusika sana na ile hali ilivyokuwa ndani ya seng'enge na kwa vile akili zao zilikazwa na kazi yao. Maoni yao hayakuwa imara na mara nyingi walijiona kama wanaishi katika dunia iliyopinduka na huo "ubaya" na "uzuri" uliwachanganyikia, na hawakuweza kutofautisha baina yao. Nikiangalia nyuma, si jambo la kustaajabisha kuwa walijihadhari kwa ukatili namna hiyo. Ilionekana kama iliwalazimu kufanya ugaidi ili kuondoa kujidharau kwao kufuatia vile mioyo yao ilivyopindukapinduka.

Sisi sote tulipewa daraja la "Weusi" na tukawekwa katika Sehemu 9. Tulikuwa kama mia tisa ndani yake na afisa Mzungu aliyetuchunga alionekana kuwa hakuna aliyetupiga. Chakula kiliendelea kupunguka kwani tulipewa wakia nane za unga wa mahindi na maharagwe. Hatukufanyizwa kazi isipokuwa kupika chakula chetu na kupambana na mandoo ya vyoo. Tulipitisha wakati kwa kuzungumza siasa na kucheza dama au "bao". Huo ni mchezo ambao umeenea sana katika Afrika ya Mashariki na zaidi baina ya makabila yanayofuga wanyama ambao hulinganisha kila jiwe na ng'ombe na kila shimo kama boma. Mwisho wa mchezo huu husumbua na unahitaji fikira bila wasiwasi. Mshindi ni yule ambaye humaliza akiwa na mawe zaidi kutoka kwa maboma ya wenzake.

Mambo yalikuwa bado kutulia katika Manyani na ile Sehemu 9 ilitumiwa kama mahali pa kungojea. Kila baada ya siku mbili au tatu, maafisa walikoroga chungu na wafungiwa walihamishwa na kupelekwa sehemu nyinginezo. Hapakuwa na uwezo wa kujifanyia mipango yetu katika hali hiyo lakini kile kikundi kilichotoka Kowop hakikugawika sana. Lakini mnamo tarehe 5 Oktoba, sote tulipelekwa Sehemu 13 na baada ya kungojea humo mwezi mmoja mambo yalielekea kutulia na tukaanza kutayarisha maisha yetu tena. Afisa mkuu wa kambi yote aliuliza kila kikundi kijichagulie kiongozi wa kukiakilisha mbele yake. Katika Sehemu 13 palikuwapo vyumba kumi na saba na kila chumba kilikaliwa na wafungiwa kama sita na nilistaajabu waliponiheshimu kwa kunichagua niwe wakili wao. Labda ni kwa sababu nilikuwa na elimu zaidi ya wengine katika sehemu yetu wakati huo. Wale ambao hawakujua kusoma walikuwa na imani kuu katika wale waliokuwa na elimu ya juu ingawa hatukustahili heshima hiyo, wakati wote.

Niliwauliza wafungiwa wenzangu wachague komiti ya watu sita ambao watanishauri na kunisaidia na nikataja kuwa wajaribu kuchagua mtu kutoka kila wilaya. Waliochaguliwa walikuwa M'Ariunda M'Ikiao (Meru), Grishon Murage (Embu), Zakariah Kibuthu (Kiambu), Tiras Muchiri (Nyeri), Geoffrey Maimba (Embu), and John Waweru (Embu). Hawa wote wamefunguliwa na Grishon ni hedimeni wa Serikali, Kibuthu analo shamba la mpunga katika Mwea-Tebere Rice Irrigation Scheme, Tiras na Geoffrey ni waalimu katika Skuli za kati, na John Waweru ameajiriwa na Serikali kama Afisa mdogo wa maendeleo ya watu wote katika North Tetu, Nyeri. Kwanza tuligawanya kazi kwa njia halali. Kila chumba kilikuwa na mpango wa kugeuza wapishi. Kila chumba kilimchagua mtu wa kupambana na ndoo za vyoo na kila siku walimchagua mtu wa kupeleka habari kama mfanyi kazi wa afisi. Baadaye katika mwezi wa Januari tulipoanza kufanya kazi uwanjani komiti yetu ilihakikisha kuwa hakuna aliyefanyishwa kazi zaidi ya wengine. Tena ilikuwa ni kazi yangu kuchunga suruali mia mbili zenye rangi ya kimanjano tulizoamriwa kuvaa tukiondoka nje ya sehemu yetu. Mnamo mwisho wa Novemba, niliomba kumwona Mkuu wa Kampi (Camp Commandant); niliruhusiwa. Alionekana kama mwenye akili lakini nilifikiri alikuwa na kile tunachoita kwa Kikuyu kama "*kanua monjore*" (kinywa kigumu). Kwanza nilimwambia kuwa sisi tulikuwa kama mahabusu wa vita na kuwa nilijua maongozi ya Geneva Convention. Alionekana kama alishangazwa na maneno yangu. Halafu nikamwuliza atayarishe matembezi ya "Visiting Committee" ili ije Manyani kutuwezesha kutoa maoni yetu kwake. Na sasa ulikuwa wakati wangu wa kushangaa kwani alikubali na akatenda kama nilivyomwuliza.

Katika mwezi huo mambo yaliendelea kuwa mabaya katika kambi hiyo. Wakati huu tulifanya kazi uwanjani na nililetewa malalamiko ya vile wengine walivyotendewa vibaya. Sikufurahi nilipoambiwa kuwa walilazimishwa kukata fimbo ambazo walipigwa nazo wao wenyewe baadaye. Tena wale askari wa jela walisemekana kuwa waliendelea kuwa wakali. Wakati huo hapakuwa na askari Wakikuyu; walikuwako Wanandi, Wakipsigis, Wajaluo waliotoka Kenya na wengine waliotoka Tanganyika. Kwa hivyo tulivyoambiwa kuwa ile Komiti ya Kutembelea (Visiting Committee) itafika huko mwezi wa Januari, nilikata shauri kueleza malalamiko hayo yote. Jimmy Jeremiah na Wilfred Havelock walikuwa wanachama wawili wa komiti hiyo ambao niliwatambua na nikawaeleza juu ya taabu bila kuficha hapo nikawauliza msaada. Walikuwako viongozi wengine kumi kutoka sehemu nyinginezo na wote waliniunga mkono. Bila shaka malalamiko yetu hayakuwapendeza maafisa wa kambi kwani asubuhi yake, nikilala juu ya ubao, bila nguo isipokuwa ile suruali yangu, nilichapwa viboko ishirini na vinne na askari wa jela mbele ya Bwana Marlow, mmoja wa maafisa wa kambi tuliyempa jina la "Mapiga". Hata hivyo kupigwa katika kambi na uwanjani kulipunguka kiasi. Wengi wa viongozi wengine walikata shauri kukaa kimya baada ya kushuhudia niliyotendewa, lakini mmojawao, Rafiki yangu mkuu, Robinson Mwangi, aliniunga mkono mpaka mwisho mbele ya komiti na ya wafungiwa.

Huyo ni mtu ambaye jina lake hunijia kila mara wakati ninapoandika habari ya siku hizo. Alikuwa kiongozi wa Sehemu 16. Robinson ni mwananchi halisi na hata baada ya Kenyatta kushikwa alifanya yote aliyoweza kumsaidia. Alielimishwa hadi Form II. Wakati huo, wengi-wa-vijana walioelimishwa walikuwa wahoji katika kambi: sisi wawili tulichagua kukaa na watu wetu wale ambao hawakujua kusoma, huko tukiwasaidia kwa mipango yao na kuwaandikia barua. Robinson sasa ni kiongozi wa K.A.N.U. Party Organisation katika wilaya ya Fort Hall (Murang'a).

Palikuwako mmisheni wa Protestanti aliyefanya kazi Manyani aliyeitwa S.J. Cole. Tulimwita "Matuini" (Kikuyu kwa Mbinguni) kwani aliwaambia watu juu ya kwenda mbinguni. Alizoea kuzungumza nami juu ya taabu zetu na alileta hali ya wema katika kambi. Alimwuliza Mkuu wa Kambi aniruhusu kusema juu ya Ukristiano katika sehemu nyinginezo, na nilifanya hivyo. Ningewasomea Mlango 13 wa Barua ya Kwanza kwa Wakorintho iliyokuwa na habari nzuri iliyoandikwa na Mtakatifu Paulo juu ya Ukarimu, kwa vile "Unavumilia mambo yote, huamini kila kitu, hutumainia mambo yote na hukubali yote." Halafu niliendelea kuwashauri kwamba wasiwakasirishe maafisa wa kambi bila sababu. Hiyo ingempa Robinson na mimi nguvu zaidi za kupigani

haki zao. Kunayo desturi katika Kikuyuni kuwa wakati kijana anakuwa mwanamume, lazima ampe ndugu wa mama yake mbuzi mwenye masikio yenye rangi ya pekee na tunayo methali isemayo "*Gwita mundu mama tikuo kuruta mburi ya matu*" ambayo ni kusema kuwa "kumwita mtu mjomba siyo kutoa mbuzi wa masikio." Kwa hivyo niliwaeleza wafungiwa kuwa wakitii amri za kambi na kuwaita maafisa "Effendi" siyo kukana maongozi ya Uhuru. Tena niliwahimizia kuwa hatungeweza kuvuka mto kufikia Uhuru bila Umoja, na ni kama vile mchwa unashikana au vile nyani wanaunganisha mikia ili kufanya daraja ya kuvukia mto. Nilisema namna hiyo kwa sababu nilikuwa Mkristiano na hakuna wakati Ukristiano ulipingwa na kiapo. Wafungiwa wengi walihudhuria mikutano ya dini pamoja na wengine waliogeuka katika kambi. Sioni kitu cho chote kinacholeta pingamizi baina ya Ukristiano na Kiapo cha Umoja.

Mnamo mwezi wa Februari ile Komiti ya Kutembelea ilirudi. Mwanachama mmoja wake kasisi aliyeitwa Macpherson aliyekuwa Kiongozi wa Kanisa la Scotland katika Kenya, alisema Kikikuyu *safi* kwa hivyo nilimweleza taabu zetu zote na nikamwambia juu ya kupigwa. Katika Sehemu 26 palikuwa pametoroka wafungiwa kadha na kwa ajili hiyo kikundi cha askari kilichojulikana kama "Special Riot Squad" chenye askari 150 kililetwa kuwafundisha mambo. Kufuatia mambo hayo, wafungiwa sita walikufa ndani ya hospitali ya kambi. Watumishi wa Serikali walieleza kuwa hao walikufa kwa ajili ya kuhara na nilitaka Bwana Macpherson afanyize uchunguzi juu ya vifo hivyo. Pia tuliuliza tuongezewe chakula tofauti tofauti. Wakati tulipokuwa tukiondoka afisini, yule Marlow aliniambia kwa upole kuwa aliona kuwa sikuweza kufunga mdomo wangu. Asubuhi yake nilichapwa viboko kumi na viwili halafu nikafungiwa katika chumba kimoja nikakaa peke yangu bila kutoka kwa muda wa siku saba, wakati ambao nilipewa chakula cha kuadhibu.

Wiki hiyo niliyotumia ndani ya chumba hicho kidogo ndiyo ilikuwa ya hali mbaya zaidi katika maisha yangu. S.J. Cole alinitembelea na alionekana kama mwenye kulia aliponiona. Alionekana mgonjwa na mwenye roho nzito. Aliniuliza kama nilipata maji. Nilipomwambia sikuyapata, alibeba ndoo mwenyewe akaenda kuchota maji mahali ambapo maafisa na askari walimwona. Hawakujaribu kumpinga. Aliporudi, alinipa maji nikanywa halafu tukapiga magoti pamoja tukaomba na akaniambia hadithi ya mtume Paulo na Sila walipofungiwa jela katika Philipi. Aliniachia Agano Jipya. Kwa muda huo wa siku saba sikuenda chooni kwani zikuwa nikila kitu.

Chumba hicho kidogo kilikuwa karibu na sehemu 16 na Robinson Mwangi alipaaza habari zote hadi kwangu. Ingawa nilimsikia, majibu

yangu hayakusikika kwake. Wakati nilipofunguliwa, niliona uchungu sana juu ya Marlow. Kwa hivyo niliandika habari ya malalamiko moja kwa moja hadi Afisi ya Makoloni juu ya yale yaliyofanyika katika kambi hiyo, huko nikiiachilia Serikali ya Kenya kabisa. Nilimhonga askari mmoja ili anipatie karatasi na kalamu na kumtuma akatie barua ndani ya posta, na nilimpa pesa tu baada ya kupokea risiti ya kuonyesha kuwa aliituma barua. Nilituma nakili ya barua hiyo kwa Bi. Barbara Castle, M.P., ambaye baadaye alijaribu kufanyiza uchunguzi wa hali ya mambo humo.

Palikuwako na Mzungu mwingine mwema aliyeitwa Dr. Kirren ambaye alikuwa mwangalizi wa hospitali. Wakati mmojawapo niliwahi kuzungumza naye kwa masaa matatu na alisema kuwa kazi yake ilikuwa kuwaponya wafungiwa waliokuwa na ugonjwa wa kuhara na wala si wale waliokuwa wagonjwa baada ya kupigwa. Alijaribu sana kuleta hali njema katika kambi na kupunguza uwazimu wa maafisa wa kambi. Mtu mwingine aliyekuwa mwema ni Humphrey wa Idara ya Afya, ambaye alijulikana kwa jina la *Kihuga* kwani alikuwa mtu wa vitendo, aliyeokoa maisha ya wengi wetu kwa ajili ya kazi yake ya usafi na maji. Angepigana na ye yote, hata akiwa Mzungu, kama alijaribu kugusa mojawapo wa wafungiwa waliomfanyia kazi. Mwezi wa Februari, wafungiwa wali-pelekwa kufanya kazi katika mashimo ya mawe. Baada ya masaa kadhaa ya jasho katika jua kali, walirudi kambini bila kuoga. Hii yaonekana kama ndiyo sababu ugonjwa wa "pellagra" ulizuka, na ambao ulizidishwa na upungufu wa chakula. Katika matembezi ya Machi ya Kamiti ya Kutembelea, nilihimiza juu ya kuongezwa chakula kwa vile wafungiwa sasa walikuwa wafanya kazi ngumu. Himizo langu lilikubaliwa na pia tukawa tukipewa tembe moja ya kuongeza afya njema kila siku.

Uhusiano wetu na askari wa kambi ulitegemea wingi wa pesa na mali tuliokuwa nayo. Hapo mwanzoni, wengine wao walifikiria kuwa walikuwa na haki kuchukua chakula cho chote walichotaka kutoka kwa kile tulichopewa. Robinson na mimi tulifikiria kupambana nao, na wakati mmoja wakati askari mmoja aliyeitwa Mgogo aliyetokea Tanganyika alichukua wakia sita za nyama kutoka sehemu yetu, nilimkataza mbele ya wafungiwa wengine wote na nikainyakua hiyo nyama kutoka kwake. Nilimwambia kama alihitaji nyama namna hiyo, ingelimfaa awe mfungiwa ili aile pamoja na sisi. Tulikaa kwa hali ya urafiki na askari wa jela ingawa wakati mwingine tuligombana na askari ambao hawakuwa na daraja. Muda mfupi baada ya kumkataza huyo askari nyama, askari mwingine mwenye cheo cha Sajini alikuja kuchukua mafuta ya kupika. Nilimkataza kufanya hivyo. Baada ya dakika chache aliniita nje na akanipeleka chumbani ambamo palikuwa na askari wengine wanane walioketi. Wao walijifanya kama kwa

ya hukumu na hivyo wakaniambia kuwa nilifanya makosa na nitaadhibiwa. Walinipeleka nje mahali ambapo wafungiwa wengine wangeona yale yaliyotendeka, na walinilaza chini na askari Mchaga akanichapa viboko arobaini. Hawakunitoa nguo na vile viboko vilipigwa kwa haraka hivi ati ingawa viliumiza, havikuwa na uchungu kama vinginevyo nilivyopigwa kwa amri ya maafisa. Lakini wafungiwa wengine walighadhabika na mimi sikuwa mtulivu na kwa hivyo nikakata shauri kumwambia Afisa wa Sehemu yetu aliyeitwa R.M. Child. Afisa huyo alikuwa amejeruhiwa kisigino cha mguu mapiganoni huko Kariaini katika msitu wa Aberdare upande wa magharibi wa lokesheni ya Othaya na alikuwa mtu mwema. Aliniambia kuwa haingalifaa kuwashitaki askari hao kwa Mkuu wa kambi lakini aliahidi kujadiliana na askari hao. Alipinga mapigano yo yote katika sehemu yetu na akawaamuru askari hao kutupa fimbo zao mbele yetu. Wale askari wa kupambana na matata (Riot Squad) hawakuitwa katika sehemu yetu na nilijadiliana na shida zote zilizotokea. Katika sehemu nyinginezo, mapigano yaliendelea na nilighadhabika kwamba hakuna cho chote tulichofanywa cha kuachisha hali hiyo.

Kampi ilizungushwa na seng'enge yenye nguvu ya stima, na kwa hivyo, wakuu wa kampi walifikiria seng'enge hiyo iliweza kupinga wafungiwa wasitoroke. Lakini magaidi wawili wa daraja la "general", Mwangi Mambo na Kariuki Chotara, walitoroka kutoka Sehemu 16 kwa njia ya kuwekelea mbao juu ya seng'enge na kutembea juu yake. Ni wachache tu waliokuwa na imani juu ya usalama wake au walikuwa na uwezo wa kusimama imara juu yake lakini tuliuheshimu sana huo ushujaa wao. Baadaye, walikamatwa Nairobi na Mwangi alinyongwa na Kariuki akafungwa maisha. Wakati nilipokuwa Lodwar, Kariuki aliletwa huko na tukakaa naye kabla ya kupelekwa Lokitaung ambako Kenyatta alikuwa atumikia kifungo chake. Sehemu 16 ilipondwa na "Riot Squad" na wafungwa thelathini na watano waliumizwa hata wakawa viwete wa daima. Nilimwandikia Chief Secretary barua juu ya tukio hilo kwa ile njia yangu ya kawaida. Baada ya siku chache nilipoulizwa kama niliiandika hiyo barua nilikubali na afisa akaamuru kwamba nichapwe viboko ishirini na vinne. Nilipewa hiyo adhabu na askari nje machoni wazi mwa Sehemu 11 na 16. Wakati wa kufanyika kwa mambo hayo Robinson alipelekwa Sehemu 6 na Daniel Mbarathi, ambaye alipigania kiti cha National Assembly kama mwana-KANU wa kujitegemea katika wilaya ya Fort Hall bila kufaulu katika uchaguzi wa Februari 1961, alimfuata.

Kwa ajili ya kutoroka kwa wafungwa wale wawili, amri ilitolewa na Mkuu wa kambi kwamba wale waliobeba ndoo za vyoo kuzipeleka kama mwendo wa nusu maili watazibeba kwa kichwa. Ilikuwa kama haikuwezekana wakati wa kawaida na ilikuwa ni shida kabisa wakati wa mvua

kumaliza hiyo safari bila kumwagikiwa kote kichwani na mabegani na mikojo na mavi. Shinda Kikombe, Mkikuyu mchekeshaji anayejulikana sana na aliyefungiwa huko Manyani, anagusa hali hii katika mojawapo ya sahani zake za gramofoni. Robinson na mimi tulilalamika sana kwa Komiti ya Kutembelea katika mwezi wa Aprili na adhabu hiyo ikakomeshwa. Pia tuliuliza turudishiwe vinginevyo vya vitu vyetu ambavyo vilichukuliwa kwa vile nguo tulizokuwa nazo zilianza kuraruka. Tulijibiwa kuwa haikuwezekana kufanya hivyo lakini tungekubaliwa kupokea shati zetu tulizotumiwa na wajamaa. Tuliteta pia juu ya mlio wa kuonya. Ilikuwako amri kwamba ule mlio ukianza, wale wafungiwa waliokuwa wakifanya kazi katika mashimo ya mawe, shambani au kwa matofali lazima walale chini mara moja bila kusonga hata kidogo au si hivyo wangepigwa risasi. Wale waliokuwa karibu na kambi lazima wakimbilie kwenye sehemu zao ili wakahesabiwe. Kama vile mambo yalivyokuwa, mara ule mlio ukianza, ingawa mfungiwa alikimbia kama umeme, wale askari walikuwa karibu walimpiga; wapishi waliacha chakula kikiungua; na kama mlio ulianza wakati wa kula chakula, tulikiacha hicho chakula ili tukahesabiwe. Ilikuwako haja ya usalama katika Manyani kwa upande wa Serikali na ingawa tulifahamu hivyo tuliuliza mioyo yetu ifikiriwe kidogo. Baada ya Komiti ya Aprili, mambo yalionekana kuwa bora kidogo.

Ingawa mvuta sigara aweza kuishi nyuma ya seng'enge bila wanawake, anaweza kuishi kwa muda mfupi tu siku hizi bila "muthogoto"—sigara au tumbaku. Tulipata tumbaku yetu kwa kuinunua kutoka kwa askari na tulipata pesa kwa kuwauzia askari blanketi za kampi. Watu wawili wangekubaliana kuuza moja ya blanketi zao nne kwa shillingi tano, moja wakaitumia kwa kuilalia na kila mmoja akajifunika kwa moja. Wakati afisa alifika kuhesabu blanketi, walifanya haraka na kuirarua blanketi moja ikawa sehemu mbili na kila mmoja akabaki na blanketi moja na nusu. Kwa bahati njema, katika mastoo mengi ya kijeshi na jela, moja na nusu huhesabiwa kama mbili. Wengine waliuza shati walizoletewa na jamii wao.

Ilikuwa muhimu pia kuweza kuwasha sigara na tulikuwa na njia kadhaa za kufanya hivyo. Kwa uangalifu, mti mmoja wa kiberiti uliweza kupasuliwa na kuwa minne. Tena tuliweza kufanya kamba ya kitambaa ambayo ikiwashwa upande mmoja ilichukua muda mrefu na iliweza kuwashwa katika majiko na kupelekwa kwa siri hadi kwenye "vilabu" vyetu (kila chumba au hema iliitwa "kilabu"). Wakati mwingine tulifuata ile njia iliyotumiwa hapo zamani ya kuviringisha kijiti ndani ya shimo la kingine ("githegethi") kwa mikono mpaka kaa likaonekana kutokana na viringisho hilo na hapo moto ukawaka. Kama hayo yote hayakuwezekana iliwezekana kufanya kama kunoa wembe katika sakafu ya simiti kwa nguvu mpaka moto ukatokea. Haja ya sigara ilikuwa kali hivi hata wafu-

ngiwa walikuwa tayari kupeana nyama kwa ajili yake au wavute moshi kutoka majani ya miti yaliyokauka. Mimi mwenyewe sikupatwa na haja hiyo na wakati mwingineo nilishangaa kuona vile rafiki zangu kama kumi na wawili hivi wakifanya mviringo, huko wakipitishania mapato yao ya siku, kila mmoja mpungo mmoja wa moshi na kumpa mwenzake. Wakati mwingineo mtu aliweza kuanguka kwa kuona kizunguzungu kufuatia mpungo mkubwa wa moshi wa sigara.

Wakati mmoja wale askari walianza kuokota mavi ya ng'ombe yaliyokauka, huko wakiyavunja na kuyakunjia karatasini ndogo na kufanya kama sigara na kuyapitishia kwenye seng'enge kwa siri kama vile yalikuwa tumbaku. Wafungiwa waliyaficha katika "vilabu" vyao hadi saa za jioni walipogundua kuwa walipigwa mweleka. Wakati nilipoambiwa habari hiyo, nilikata shauri kuwa tutawafunza jambo. Askari walizoea kununua mafuta ya kupika tuliyoweza kubakiza kwa bei ya shilingi kumi kila debe. Tulipata mikebe midogo ambayo tulijaza nusu yake kwa mavi ya binadamu, tukafunika haya mavi kwa majivu ili yasinuke, hayo majivu tukayafunika kwa mafuta ya tingatinga na ile robo ya mwisho tukaijaza kwa mafuta ya kula ambayo walipenda kununua. Walikasirika sana walipovumbua matusi hayo na nilipoonana na wengine wao niliwaeleza kuwa tulikusudia kuheshimiana katika biashara yetu. Neno lilipitishwa miongoni mwa wafungiwa na hakuna mfungiwa aliyevuta mavi ya ng'ombe tena. Ingawa uvutaji wa sigara ulifungwa katika kambi zote za pekee za kufungiwa watu za Kenya, amri hiyo iliepukwa kwa njia kubwa na wafungiwa. Pamoja na hayo niliagiza magazeti ghali ambayo yalifika kila siku nikiwatumia wale askari.

Litaonekana kuwa jambo geni kwa watu wa nje kuwa baada ya hao askari kutuuzia tumbaku na magazeti siku iliyopita, kesho yake waliingia kupekua vyumba vyetu kufuatia amri za wakubwa wao wakiitafuta hiyo tumbaku na walifurahia kutuvuta nje kuadhibiwa ikiwa waliipata tumbaku baina yetu. Hakuna aliye na haja kuelezwa ilivyofanyika na labda mithali ifuatayo ya Kikikuyu itawasaidia wengine. Tunasema kwamba wakati binadamu anamchukua mbwa kwenda kuwinda mbweha, mbwa hukimbia mbele ambako haonekani na huko huanza kucheza na mbweha katika mahali palipojificha kwani wao ni wa kabila moja. Wakati binadamu anapomkaribia, mara mbwa huanza kuwika kwa nguvu na kuanza kumkimbiza huyo mbweha hadi mahali panapojificha. Hayo hutendeka kwa sababu ni binadamu anayemlisha mbwa na mbwa asipomtii hatapata chakula.

Kwa njia nyingi kilichotufaa sana ni kupata habari kwa njia mbili ambazo tulifanyiza. *Manyani Times* ilikuwa ni habari ya kweli iliyookotwa kutoka magazetini na wale waliokuwa wakifagia kwenye nyumba za

askari au iliyookotwa kutokana na utangazaji ndani ya radio na wale waliofanya kazi karibu na nyumba za maafisa. Tulikuwa wajanja sana kwa kuokota habari bila kujulikana kuwa tulifanya hivyo. *Waya Times* ilikuwa ni habari ya kukisia, uvumi au vichekesho. Wakati wa jioni baada ya chakula, kila "kilabu" kilimtuma wakili kwenye seng'engè ili apokee habari. Tulikuwa na bahati sana katika Sehemu 13 kwani tuliweza kuzungumza na Sehemu tano nyinginezo. Ye yote aliyekuwa na habari mpya angalisimama na kusema "giteo" ambayo ni kusema "heshima" kwa Kikuyu, na mara watu wote walinyamaza. Halafu angeendelea na kusema: "Sasa ninaanza habari yangu ya *Manyani Times* (au ya *Waya Times*) ambayo ni....." Njia hii iliwawezesha wasikilizaji watakayoamini baina yatakayosemwa. Habari ya *Waya Times* wakati mwingine ingekuwa juu ya kufutwa kwa Gavana, tarehe ya Uhuru (ambayo haikuwa nyuma ya 1956), kufutwa kwa sheria nyinginezo na Mkuu wa Jela, kukaribia kwa kufunguliwa kwetu, kuhamishwa kwa afisa ambaye hatukumpenda au ushindi wa uchaguzi na chama cha Leba cha Serikali ya Uingereza. Habari nyingi za *Waya Times* zilionyesha makisio yasiowezekana katika wale waliozitoa. Tena kulikuwako na vichekesho vingine kama vile "Jeremiah (mhojani) alitumana kwa mama yake aletewe shati na mama wake amemtumia cha kubebea mtoto (ngoi) badala ya shati" au "Jonathan (mhojani mwingine) alitumana kwa bibi wake aletewe suruali ya ndani ya kiume lakini badala yake bibi amemtumia suruali yake (ya bibi) ya ndani." Labda bibi huyo hakujua suruali ya kiume ya ndani ilikuwaje lakini tulieneza uvumi wa aina ili kuonyesha kuwa bibi hakukubaliana na yale aliyokuwa akifanya. Vichekesho visivyo vya kawaida lakini vilitufaa katika hali yetu ya siku hizo. Askari hawakupendezwa na mipango yetu ya kueneza habari hata kidogo na kila wakati walipotuona tukisikiliza kwa makini, mmojawao alitupa jiwe ili kututawanya. Ile saa ya jioni ya habari tuliitumia pia kwa kutupania tumbaku baina ya marafiki wa Sehemu tofauti. Wakati mwingine tumbaku ilianguka katika njia iliyopakanisha sehemu mbili na iliyofuata ni taabu ndani ya Sehemu kama hizo mbili.

Mwanzoni wa Aprili, tulitembelewa na watu wengine tuliowabatiza "Ogi a Njata" (au Werevu wa Nyota) kwa ajili ya alama nyekundu ya nyota waliovaa mifukoni ya vifua vyao. Hao walikuwa ni wale walifungwa kwa Amri ya Gavana (Governor's Detention Orders) na ambao waliokubali kuunga Serikali mkono baada ya kuhojiwa katika kambi ya Athi River. Walikuwa wengi. Waliishi pamoja na wale wahojani wengine lakini kila asubuhi walitembelea ile Sehemu mtu alipendelea ili kujaribu kuwashawishi wafungiwa wengine waungame kama vile walivyokuwa wamefanya. Waliwahi kuwageuza wengine hapa na hapo na haikupendeza

kuona ule umoja wetu uliokuwa imara ukisita ingawa kwa njia ndogo. Tuliona kuwa *Waya Times* ilipungukiwa na uvumi wake.

Mwishoni wa Aprili, palikuwako na mgomo wa wafanyi kazi wa meli katika Mombasa. Ilitajwa kuwa wafungiwa 10,000 wapelekwe huko wakauvunje huo mgomo, na mara nyingine, ile akiba yangu iliendelea kupunguka kuniwezesha kutuma barua kwa Waziri wa Makoloni, Gavana na wanachama wengine wa Halmashauri Kuu, huko nikihimiza kuwa hatua hiyo haingelingana na Maagano ya Geneva (Geneva Convention). Pia nililalamika juu ya ukatili tuliotendewa. Yule Marlow (au "Hitler") aliendelea kuwa mtu mbaya zaidi na katika Sehemu 17, alimtupia mfungiwa bakuli ya uji wa moto moto uliomchoma vibaya kote mwilini hata ikamlazimu kutumia wakati mrefu katika hospitali. Siku moja, Marlow huyo alifika Sehemu yetu kufanya speksheni. Alikuwa ametoa amri kuwa akiingia lazima kila mmoja kusimama na kutulia. Kamau Nduyu aliyetoka South Tetu hakuweza kutulia na Marlow akamchapa kofi kali hivi ati pamoja na kumwangusha Kamau, iliifanya kofia ya Marlow kuanguka. Wafungiwa wengine walikimbia kuiokota hiyo kofia wakamwacha Kamau alipolala. Baadaye niliwagombesha kwa dakika kadha huko nikawaeleza tofauti baina ya kofia na binadamu. Lakini niliwasamehe; Marlow alikuwa dude la kuogopewa. Mwishoni, niliwashitaki maafisa wa Manyani kwa vile walivyojaribu kuficha ukatili tuliotendewa huko wakidanganya kwamba watu walikufa kwa ajili ya ugonjwa wa kuhara, hapo nikauliza waonyeshe ushahidi kuwa kulikuwako na askari au afisa aliyekufa kwa ajili ya ugonjwa huo wa kuhara. Kwa sababu moja au nyingine, hatukupelekwa kumaliza mgomo wa Mombasa na ile mikate iliyonunuliwa tukaile huko Mombasa tuliila mle ndani ya kambi.

Wakati ile Kamiti ya Kutembelea ilipofika mwanzoni wa Aprili, nilileta malalamiko hayo yote mbele yake. Komiti ilipoondoka, Marlow aliniita na wakiwa na afisa mwingine na askari Mluhya waliniendesha hadi karibu na chumba kidogo katika hedikuota na hapo wakamwamuru huyo askari anichape viboko sita. Nguo zangu hazikuondolewa, sikupigwa mahali pamoja tu mwilini na nilipigwa upesi upesi na kwa hivyo sikuumia kama ningalivyoumia pengine ingawa matako yangu yalivimba kadiri. Marlow alikuwa binafsi akiwapiga wafungiwa katika sehemu zao ingawa Mkuu wa Kampi labda hakujua.

Asubuhi yake Marlow aliniita nje ya kambi "C" akanipeleka mahali karibu na msitu akaniambia kuwa atanipiga risasi nisipoandika juu ya karatasi kuwa sitapeleka barua nyingine Ulaya, kuwa nitashirikiana na Serikali na kuwa nitasaidia kuchapa barua katika afisi ya kuhojiwa. Ingawa fikira za kifo hazikuvuta, nilikataa. Halafu alitoa ubao wenye urefu wa futi tatu na upana wa futi mbili akaniamuru niuinue juu ya kichwa changu huko

nikiushikilia kwa mikono yangu miwili ikinyoka. Alitembea mwendo wa yadi tano hivi halafu akanionya kuwa ataniua nisipokubali kuandika kama vile alivyopenda. Hata hivyo, ningali nikifikiria alikuwa akicheza tu, nilikataa. Aliinua bunduki yake na akafiatua risasi. Ninakumbuka mgurumo mkubwa na nikafahamu kuwa nimekufa halafu nikajisahau. Kusema kweli alikuwa ameupiga risasi ule ubao na mimi nilianguka pamoja nao. Kutoka kimya kilichofuata, nilisikia "Simama, simama" na kwa vile hali ya mambo ilivyokuwa nilifikiria kuwa hiyo si lugha ya mbinguni au ahera na labda nilikuwa hai. Nikiwa katika hali ya kupumbaa, nilisimama nikamwangalia na akarudia yale aliyoniambia hapo mbeleni. Nilikataa na akafiatua risasi tena; nilianguka tena nikafahamu utupu na nikanusa kifo. Kutoka kama bali nilisikia "Amka, amka", na kwa mara ya pili nilifufuka kutoka kwa wafu. Mwili wangu ulidondoka jasho na fikira zangu hasikufahamu yale yaliyokuwa yakitendeka au nilipokuwa. "Kwa mara ya tatu na ya mwisho", alisema, "utakubali kuandika yale niliyokuambia?" Sasa ilionekana kama ni mchezo katika nyumba za sinema na bila kufahamu kamili vile nilivyokuwa nikisema, nilimjibu "La." Alipiga risasi tena na wakati huo nilisikia moto ukipitia shinani la kidole kikubwa cha mkono wangu wa kulia. Nikifikiria bila shaka kuwa nilijeruhiwa vibaya na nilikaribia kufa, nilianguka chini tena. Wakati nilipoiona damu ambayo ilichanganyika na jasho hivyo nikawa kama mwenye damu kila mahali, nilimkimbilia nikamshika kiunoni nikamwambia: "Tazama damu hii, umeniua, damu iko pote mwili mwangu." Marlow alicheka akasema: "Wewe hadi-koa (mgumu sana) mbaya sana." Halafu akanirudisha katika kampi akanifungia ndani ya kile chumba kidogo ambacho hakihudhuriwi na mwingine. Ninafikiri leo kuwa hakukusudia kuniua na kuwa alitaka kuniogofya tu na bila shaka alifaulu katika kuniogofya.

Mnamo tarehe mosi Juni, nilibebwa kwa motokaa hadi Sehemu ya 13 na Marlow wakiwa na Mkuu wa Kampi. Wafungiwa wengine walifanya nusu mviringo na wale waliokuwa katika Sehemu nyinginezo waliangalia: walikuwako kama elfu sita. Waliniambia niubebe ubao wa kukalia uliokuwa ndani ya motokaa nikaupeleke kati kati ya wafungwa wengine. Wafungiwa wote waliambiwa wasimame na maafisa wengine na askari walifika kuona mambo. Ulikuwa mkutano huo. Yule Mkuu wa Kampi alipaaza sauti kwa Kiswahili akasema: "Hapa yuko kiongozi wenu. Anataka kuwaonyesha kuwa yeye ni Mungu. Mnamfuata kwa sababu anaandika barua kwa Afisi ya Makoloni. Msimfuate tena. Mkimfuata mtakuwa katika taabu kama ile aliyo nayo leo. Mwangi, ondoa nguo zako na ulale juu ya ubao." Hapo nilichapwa viboko kumi na viwili na sajenti-meja Mjaluo. Hakika alijua kuchapa kwani hivyo viboko vilikuwa vikali. Mkuu wa Kampi hapo akaniuliza kama nitaacha kutuma barua. Nilimjibu kwamba nitaacha

baada ya kuhakikishiwa kuwa malalamiko ya haki ya wafungiwa yalijibiwa. Kama mapigano yaliendelea, barua zangu zingeendelea. Sitashirikiana na Serikali wala sitasaidia "Special Branch." Baada ya hayo nilipelekwa Sehemu ya 6 ambapo afisa Mzungu alinichapa viboko vingine ishirini na vinne na wafungiwa wengine wakashuhudia. Mwishoni, nilitupwa ndani ya chumba Nambari 1 katika Sehemu hiyo na nikafungwa kuchanganyika na wengine. Jioni yake, *Manyani Times* ilitoa ripoti juu ya yale yaliyotendeka mchana huo. Baada ya kutendewa vile faraghani, nilitukiwa na uchungu mwingi moyoni ambao haujakuwa rahisi kusahau.

Chumba Nambari Moja kilizungukiwa na seng'enge na ingawa sikuruhusiwa kuonana na ye yote, Robinson Mwangi alitayarisha njia ya kunilisha nilipolala nikiwa mnyonge na mchovu. Kwa uangalifu wake, nilirudiwa na nguvu zangu pole pole. Wakati huo, Sehemu 6 ndiyo ilikuwa mbaya zaidi katika Kampi yote. Wale wafungiwa ambao hawakukubaliana na maafisa walipelekwa humo na walitendewa vikali. Kile kikosi cha askari wa "Riot Squad" kiliingia humo kila mara na kumfanya kila mtu kutoa nguo na kuwapiga kote ndani ya sehemu hiyo, huku vijana na wazee wakiwa pamoja, ambayo ni aibu kwa wananchi. Lakini mimi hawakunisumbua nikiwa katika chumba changu, ingawa nilifikiria kuwa huenda mahali hapo pakawa kama pa wenda wazimu.

Tarehe Juni 16, kikundi kingine miongoni mwetu kilihamishwa hadi Sehemu 8, ambako nilichaguliwa kiongozi tena. Tulikuwa mia nane na wanane ndani yake lakini hatukukaa humo kwa muda mrefu. Tarehe Juni 22, tulitawanywa kwa njia kubwa kote katika nchi, mia tano walipelekwa Mwea, mia moja na ishirini wakapelekwa South Yatta, mia moja na hamsini wakapelekwa Fort Hall na thelathini wakapelekwa Nyeri. Ni wanane tu waliobaki. Tulipokuwa tukiacha Manyani, Marlow alinambia: "Usirudi kamwe katika Manyani." Roho yangu ilikuwa nzito nilipofikiria kuwaacha wengi wetu nyuma katika kambi hiyo ambayo hakuna angefurahi au kuishi maisha ya kawaida, akiwa mfungiwa, askari au afisa Mzungu.

6 Yatta Kusini na kurudi Manyani mara ya pili

KAMPI ZOTE za Wafungiwa katika Kenya zilijengwa katika sehemu zisizo na watu, zenye joto na kavu na kambi ya kufanyia kazi ya South Yatta iliyokuwa kama maili ishirini na tano kutoka Thika ilikuwa mojawapo. Sababu ya kujenga kampi hii ilikuwa kuwezesha kuchimbwa kwa mtaro wa Yatta. Kusudio la mtaro huo ambalo lilibaniwa mwaka wa 1925 lilikuwa kuleta maji kutoka mto wa Athi, mwendo wa maili arobaini kupitia katika nchi ya Wakamba mpaka nyandani kavu za Yatta. Katika kampi ya South Yatta kila mmoja alikusudiwa kufanya kazi, vijana na wenye nguvu wakichimba mtaro, wazee na wasiojiweza wakipambana na ndoo za vyoo, na wale wagonjwa wakifagia kampi na kufanya kazi nyinginezo zisizo za nguvu. Wale waliobaki nyuma katika kampi walifanya kazi nyingi hivi ati wengine wao ingawa wagonjwa wangependelea kufanya kazi katika mtaro. Mpango huo ulipunguza waliojifanya wagonjwa lakini uliwapinga wagonjwa wengi kutibiwa na kuponyeshwa kwa wakati uliofaa. Tulipofika huko kutoka Manyani, mtaro huo ulikuwa umeendelea maili nne na nusu. Katika muda wa miezi miwili huko, tulichimba maili nyingine mbili.

Serikali ya Kenya, mwishoni ikifahamu vile ilivyokuwa vigumu kuwafungia watu 80,000 ndani ya seng'enge milele, ilianzisha mpango wa kuwarudisha wafungwa makwao. Kurudishwa huko kulitegemea mambo mawili ya kuungama na kufanya kazi kwa bidii. Kwanza kila mmoja alihojiwa tena na kupewa daraja za Weusi, Kijivu na Weupe; baadaye, vile maana ya daraja hizo kwa njia nyingine ilipojulikana na Serikali, ziligeuzwa na kuwa Z (weusi wasiookoleka), Z2 (weusi wa kawaida), Y1 (kijivu) na Y2 (weupe). Kampi zenyewe ziligawanywa kuwa Kampi za Pekee (Special Camps) na Kampi za Kazi (Works Camps). Watu wa Z waliwekwa katika Kambi za Pekee pamoja na wachache wa Y1 na wale wa Y2 walipelekwa katika Kampi za Kazi. Kampi za Kazi zilikuwa karibu na mipango ya kazi ambako wafungiwa wangefanyiza dhambi zao kazi na kuokolewa kwa kufanya kazi ngumu. Kwa ajili ya Maagano ya Madola ya Dunia (International Agreement) wangelipwa kwa kazi waliofanya na pesa zile wangepewa zingewekwa ndani ya Posta, na zingepewa mfungiwa

wakati wa kufunguliwa au apewe vitu vingine vya kupendeza katika kampi badala ya pesa. Kampi zote za Kazi zilikuwako kote katika wilaya za Wakikuyu na mfungiwa angeendelea kufanya kazi na kuungama dhambi zake akielekea makwao. Mwishoni angefikia mwisho wa "mfereji"('pipe line') kama vile mpango huo ulivyoitwa, katika kampi iliyojengwa katika sehemu yake ambako angelazimishwa kugeuza nia yake na akina jamaa na wazee na machifu. Halafu ile siku kuu itafika wakati viapo vya 'Mau Mau' na imani ndani yake vitakuwa vimefifia na atakuwa mfano wa wema wote, na hapo ndipo atafika mbele ya komiti ambayo afisa mmoja aliipa jina la "Wafalme na Wakubwa" wake, ambao hatimaye wataamrisha kuachiliwa kwake kama Mkikuyu aliyegeuka na hapo atarudi kwa watu wake. Hata wakati wa mpango huo wa "mfereji" ilifikiriwa kuwa watakuwako wafungiwa 12,000 ambao wangefungiwa daima nje ya nchi ya Wakikuyu, wakifanya kazi katika sehemu nyinginezo za nchi ambako hakungekuwa na watu wengine.

Mpango huo wa "mfereji" ulionyesha wazi vile watumishi wa Serikali walikuwa bado kufahamu 'Mau Mau' iliendelea namna gani. Ule moyo wa Kiafrika wa kitaifa, ambao sisi tulikuwa sehemu yake, si kitu ambacho kiliweza kuondolewa tu na uhojaji. Shinani, moyo huo ni sehemu maalum ya miili yetu, na mnamo miaka ya 1950 hakuna Mwafrika katika Kenya angaliyejiita binadamu bila moyo huo. Baina ya watu wengine, moyo huo ulivunjwa au kuumizwa na kutumiwa kwa nia nyinginezo ambazo haukukusudiwa. Nyakati nyinginezo, Waafrika wachache waliwahi kuishi kwa muda mrefu bila huo moyo lakini hatimaye ulimalizwa na kifo tu. Serikali ya Kenya ilifanya makosa mawili. Wakati mwingine ilifikiriwa ingewezekana zile nia za 'Mau Mau' na mambo yaliyofanya watu kula kiapo zingeondolewa kutoka moyo wa kitaifa wa tawi la Kenya na kuwa kila moja ya hayo ingeweza kujadiliwa kwa njia mbali mbali: Serikali haikuona kuwa kufikia wakati huo, 'Mau Mau' ilikuwa matokeo ya ndani kabisa ya kitaifa ya Kiafrika ambayo yalinyimwa nafasi ya kawaida ya kujionyesha. Pili, Serikali ilitumaini kuwa watu wakiungama kula kiapo, yule mtoto wa utaifa atafagiliwa mbali na maji ya bafu. Serikali ya Makoloni haikutumainiwa kuona mambo kama vile tulivyoyaona. Walifikiri kuwa baada ya kuungama, tulifaidika kwa kitu kingine. Wale wetu ambao tulikataa kuungama mpaka mwisho tulifanya hivyo kwa sababu tulisadiki kuwa tukifanya hivyo tutapoteza kitu muhimu ambacho maisha yetu yalitegemea na bila hicho hatungeweza kuishi. Tulifikiria kuwa wale ambao waliungama halafu wakawa wahojani waliuza roho zao kwa bei ya maisha matamu. Walikuwa wanyonge ambao hawakuweza kupambana na shida na waliweza kusamehewa kwa ajili ya unyonge wao ikiwa si kwa sababu ya mambo mengine. Wengi wa wale ambao waliungama na kuji-

peana sasa wamepata kile walichopoteza kwa muda mfupi. Maafisa wengi waliwacha kambi baada ya kulinganisha nyuso zenye furaha za wale walioungama na za wale kama sisi ambazo zilionekana kama zisizo za binadamu kwa uchungu. Na hata hivyo sisi "hadi-koa" tulikuwa na furaha na amani katika roho zetu kuliko hao waliojipeana ambao walilazimishwa katika hali ya uwongo ya kufanya mambo mawili kule wakijua katika roho zao kuwa sisi "hadi-koa" ndio tulionyoka, wa kweli na haki kwa wananchi wa Afrika.

Wafungiwa walifikiria njia hizo kwa mioyo tofauti kwani zilionekana kama za kurahisisha nafsi ya binadamu. Wachache waliachiliwa kwa kusema ukweli na wengi kwa kusema uwongo. Wengi wetu walikata shauri kukataa kuungama mbele ya wahojaji ili kupigania haki za wananchi kuiangamiza Serikali kwa wingi kama ilivyowezekana. Mpango huo wa "mfereji" haukukusudia kuwapiga watu kwa njia yo yote. Ni watu wachache sana ambao wangesemekana kuwa wanatii yale wanayosema wakiwa maumivuni. Lakini kwa vile mpango huo haukuwa imara ulianza kufifia na ni wakati huo Serikali ilianza kutumia nguvu ambayo mwishowe ilionyesha kuwa kuungama siyo shina la "mfereji." Ni watu wachache ambao wangesemekana kuwa wanatii wasemayo wakati wianaumizwa Ni vigumu kwa mimi kusema ni nani aliyetoa amri hizo lakni ni wazi kuwa Mawaziri wengine wa Serikali na maafisa wakuu wa Serikali walijua yale yaliyokuwa yakitendeka. Tulizoea kuambiana kuwa Serikali ilikuwa na mfereji ambao ilikusudia sisi sote tupitie tukielekea kwetu. Kwa bahati mbaya huo mfereji ulikuwa wa kipimo kimoja hali wengine wetu walikuwa wakubwa zaidi (hadi-koa) zaidi ya wengine na tulikwama ndani yake mara moja. Kwa hivyo waliinua nyundo wakatupondaponda ili tuweze kuingia ndani ya "mfereji" kwa nguvu. Wengine wetu walijua njia bora ya kufikia nyumbani zaidi ya mfereji huo mdogo hivyo lakini hakuna aliyetusikiliza.

Yatta ya Kusini ilikuwa Kampi ya Kazi ya kwanza niliyokuwako. Nambari yangu mpya ilikuwa S.Y.W.C. 1880. Ilikuwa kambi ndogo iliyoweza kufungiwa watu elfu moja na tuliishi ndani ya vyumba vya mabati membamba yaliyojengwa kama hema ambavyo vilikaribiana kuliko vile vya Manyani. Tulijisikia wema wakati tulipoona kwamba hapakuwa na askari wa kutupiga tulipofika. Tulipewa riziki ya wakia kumi na nane za unga wa mahindi, wakia sita za maharagwe na hali ya maisha ilikuwa ya kimaskini. Hapakuwa na msaidizi wa daktari lakini kwa bahati tulikuwa na mfungiwa mmoja aliyefanya kazi hiyo aliyeitwa Muriithi Kihara ambaye alikuwa ameishafanya kazi katika King George VI (Kenyatta National) Hospital, Nairobi, kabla ya kushikwa. Alifanya yote aliyoweza kutusaidia, lakini hakuweza kuzuia tukio la ugonjwa wa "pellagra," ambao ulileta kifo cha

mfungiwa mmoja katika hospitali ya kampi hiyo. Sigara na tumbaku zilikubaliwa katika kambi na tulipeana vitu ili tuzipate.

Mchana ulikuwa mgumu: tuliamshwa saa kumi na moja ya usiku, tukanywa uji na ikifika saa thenashara tulikuwako Mlangoni Mkubwa ili tugawanywe vikundi vya kazi. Halafu tulitembea mwendo wa maili baina ya tano na saba kwenda mtaroni na kurudi saa za jioni. Tulifanya kazi ya kipimo ya kuchimba mtaro uliokuwa na upana wa futi kumi na uchini wa futi kutoka kumi na sita hata kumi na nane. Wazee na hata vijana wengine hawakuweza kumaliza kipimo chao cha urefu wa futi mbili kwenye ardhi yenye mawe magumu, ambayo kwanza ilimlazimu mtu kuitikisha halafu auteke mchanga autupe nje kwa jembe kubwa. Wale walioshindwa kumaliza "futi" yao hawakupewa mshahara kwa hiyo siku mwisho wa mwezi. Wengine hata hawakupata mshahara kwa miezi miwili kabla ya wakati tulipoondoka huko.

Askari wale waliotuchunga tukienda mtaroni walikuwa Wakamba. Walikuwa wema na wanyenyekevu na hawakutupiga kamwe, na wakati mwingine wa kazi, waliwachukua wachache baina ya wafungiwa na kuwapeleka karibu na nyumba za Wakamba raia na huko walipewa chakula na labda uji na Wakamba walioishi huko. Kabla ya kufika huko, hiyo kambi ilitumiwa kwa kuwapokea Wakikuyu waliofukuzwa kutoka Jimbo la Kaskazini la Tanganyika ambako walikuwa wakifanya kazi. Wengi wao walikuwa hawajakula Kiapo cha Umoja: kama walikuwa wamekula kiapo, yafuatayo yaliyotendeka kabla hatujafika huko hayangetendeka. Walipokwenda kuchimba mtaro, walikutana na wasichana Wakamba ambao waliwaingiza ndani ya kambi saa za jioni kwa kuinua seng'enge. Mkuu wa Kampi aliyekuwa huko wakati huo alipendelea usafi wa kambi zaidi ya binadamu waliokuwamo, lakini aliwakubalia wasichana wa Kikamba kuingia katika kambi siku ya Jumapili kuuza chakula kwa wafungiwa. Aliitwa Chichester. Matokeo yake yalikuwa kuwa wale vijana Wakikuyu walifanya maagano na wasichana wengineo wa Kikamba waliokuwa wazuri kubaki ndani ya kambi wakati wa usiku kama rafiki zao. Mambo hayo yaliendelea kwa miezi minne na haikushangaza wakati mmoja wa wasichana hao alipopata mimba. Kufuatia desturi ya Kikamba, na kwa vile aliyemtia mimba hakukusudia kumwoa huyo msichana, yeye au baba yake ilikuwa ni lazima atozwe faini ya mbuzi wawili na kondoo ndume mmoja. Lakini hakuweza kuwapata hao mbuzi na ndume kondoo, na kwa vile ilikuwa ni lazima mmoja wao awapate hao wanyama, wazee walikata shauri kwamba Chichester atakuwa kama baba na awatafute hao wanyama. Hakukataa kufanya kama alivyoambiwa kwani hakupendelea mambo hayo yajulikane kwa wakubwa wake na hao wazee walifurahia sana huo mlo wa nyama waliokula pamoja na askari wa

Kikamba. Huyo msichana Mkamba alitukia kuzaa mapacha. Kutuatia tukio hilo, wasichana hawakukubaliwa tena kufanya soko yao ya Jumapili katika kampi lakini hakuna kilichowakataza kukutana na wafungiwa wakati waliokuwa kazini.

Mambo hayo hayangetendeka baina ya wale waliokula kiapo. Hakuna mmoja baina ya "hadi-koa" aliyekubaliwa kukutana na bibi, kunywa tembo au kutumia "bhangi." Ye yote aliyepatikana akisema mambo ya mapenzi kwa msichana tulimhukumia kama kwamba alitenda haya mambo ya mapenzi. Tulimhukumu kutembea kwa magoti juu ya sakafu ya simiti mara nyingi ndani ya chumba: adhabu hiyo iliweza kuumiza sana. Lakini adhabu iliyokuwa kubwa ni ya kutolewa makende (kuhasiwa) kwa makosa yale mabaya zaidi, na hiyo ilikuwa kama kufa ungali hai. Katika mambo kama hayo tulikuwa tumezoea kujihadhari na tulipofika Yatta Kusini tulikuwa marafiki na tuliwaheshimu Wakamba lakini hakuna aliyesema mambo ya mapenzi kwa wanawake wao; kwa hivyo walituheshimu na kutuamini.

Nilikutana na marafiki wengine wa zamani katika kampi hii na nilifurahiwa sana kumwona tena Gad Kamau Gathumbi, ambaye aliletwa hapa mbele kutoka Manyani. Tuliona kwamba wananchi walitaabika kwa ajili ya chakula kibaya, kazi ya nguvu na ukosefu wa utabibu na kufuatana na mapendekezo yao, niliandika barua kwa wakubwa kama kawaida (yaani kwa Waziri wa Makoloni, wajumbe wa Parliament, Gavana, Mkuu wa Jela na Mkuu wa Jimbo) hapo nikauliza tupewe lori za kutupeleka kazini na tupatiwe utabibu wa kutosha, daktari msaidizi aliyehitimu, mahali pa wagonjwa na nafasi. Pamoja na hayo niliuliza kwamba chakula chetu kitolewe kulingana na masharti, wakia sita za mchele, wakia kumi na mbili za maharagwe, wakia nane za viazi, wakia nane za mboga, wakia ishirini na moja za unga wa mahindi na wakia nane za nyama. Iliwezekana kupata karatasi na stampu ndani ya mkahawa na kwa hivyo nikampa askari mmoja kuipeleka barua katika posta. Gad na mimi tulikasirishwa na wafungiwa wengine waliokuwa na elimu ambao waliogopa matokeo ya kuandika barua kama hiyo, lakini ilikuwa ni ile hadithi ya zamani kuwa walio na elimu walikuwa wanyonge kuliko wale ambao hawakuwa na elimu.

Hiyo barua ilileta maajabu. Baada ya wiki mbili, malalamiko yetu yote yaliondolewa. Chichester alipelekwa pengine na tulipofika katika kambi tarehe Julai 28, 1955, Mkuu wa Kampi mpya aliniita afisini kwake. Nilikubali kuwa niliandika barua na kwa hivyo akanifungia ndani ya kile chumba kisicho na mwengine ambapo nilikaa mwezi mmoja nikipewa chakula cha kuadhibiwa. Kwa mara nyingine, yale maongozi yangu ya kusikizana na askari wa daraja ya chini, yalinifaidi na waliniletea chakula

zaidi. Wakati Mkuu wa Kambi alipovumbua hivyo, chumba changu kiliongezwa seng'enge zaidi. Kwa wakati huu, watumishi wa Serikali walikuwa wamechokezwa na tabia zangu na mnamo tarehe Agosti 30 mimi na wengine 42 wa kikundi cha Z tulipelekwa hadi Manyani, hivyo ilikuwa ni kama kurudishwa nyuma kupitia huo "mfereji."

Manyani ilikuwa kama hapo zamani: mamia ya vyumba vya mabati yaling'ara kote, askari maelfu wakitembea huko na huko wakiwa na nguo zao za khaki na zaidi ya elfu kumi na tano walitawanyika ndani ya seng'enge ya stima, ngozi nyeusi zilizovaliwa nguo nyeupe, wakingojea uhuru. Kulikuwako na mageuko kadhaa. Marlow alikuwa amekwenda, na kwa hivyo nikamshukuru Mungu kwa unyenyekevu; chakula kilikuwa bora na kiliongezwa "njahi", aina ya chakula kinachopendelewa sana na Wakikuyu. Katika nyumbani makwetu, "njahi" zinapewa "athoni" yaani wajamaa kwa ndoa na wazee. Baada ya kufunguliwa, nilichofanya kwanza ni kumpelekea Mzee Kenyatta fungu la "njahi" ili kuonyesha heshima yangu kuu juu yake. Huko Manyani, "njahi" zilikwisha haraka kwa vile tulikuwa wengi na badala yake wakatupa "njugu" ambazo ni aina nyingine ya chakula kinachopendwa na Wakikuyu.

Kabla ya kukubaliwa kuingia ndani ya kambi, tulipelekwa kwenye mnada. Huo mnada ulikuwa kama ile inayojengwa kwa ajili ya ng'ombe na ulikuwa kama futi ishirini urefu, futi sita uchini na futi nne upana. Ulijazwa na maji ambayo yalitiwa kero nyingi. Tuliambiwa ati tutatia miguu yetu ndani ya maji hayo kwani waliotoka nje walifikiriwa kuwa ndio walioleta magonjwa ya kuambukiza. Kwa hivyo tuliendeshwa kwa mstari mmoja hadi tumevaa nguo zetu lakini huku tukibeba mizigo yetu mingine na nguo zetu nyinginezo. Kila kitu kilikuwa ni lazima kipitie ndani ya maji hayo na kila sehemu ya miili yetu ilitumbukizwa ndani ya maji. Maafisa na askari waliokuwa huko pandeni za mnada walitupiga vichwa ili kutulazimisha kutumbukiza vichwa vyetu kabisa. Machozi yalinitiririka kutoka kwa macho yangu yalioniuma wakati nilipotoka mnadani. Sisi sote tulifikiria kuwa kitendo hicho kilikuwa cha kuonyesha madharau juu yetu wala siyo cha kuondoa madhara ya kuambukiza.

Tulipelekwa Sehemu ya 9 na mara nyingine nilichaguliwa kiongozi. Afisa aliyechunga sehemu hiyo alikuwa mkosa-kabila tuliyembatiza "Muru-wa-Chuka" (yaani mtoto wa Wachuka). Wafungiwa wengine walijua kuwa mama yake alikuwa malaya na kwamba baba yake alikuwa Mwingereza. Alikuwa ameelimishwa vibaya na alisema Kiingereza kidogo sana na kwa hivyo aliniuliza nimsaidie kuandika barua alizokusudia kumwandikia Mkuu wa Kambi. Jioni moja wakati wa kufunga aliingia katika Sehemu ya 9 wakati alikuwa amekunywa tembo na hapo akaanza kuwapiga wafungiwa waliokuwa karibu naye bila sababu yoyote. Nili-

ghadhabika na hapo nikampokonya ile fimbo aliyotumia, nikaivunjavunja na kuitupilia mbali. Nilimwonya kuwa akiendelea kufanya vile nitamwonyesha kama ni yeye au ni mimi aliyekuwa na nguvu zaidi. Hayo matusi yangu ya faraghani yalimkasirisha na hivyo akaniita afisini kwake ambamo aliniogofya kuwa atanipiga. Wakati huo nilikuwa mwenye ghadhabu kuu na alishangaa kwani nilimjibu kwa kumkaba shingo na kumfinya hata asiweze kuvuta pumzi. Alikuwa mrefu lakini mnyonge na alionekana kama asiyeweza kunipiga. Baada ya nukta chache, niliwahi kumwangusha chini karibu na miguu yangu na nikamwambia ajihadhari. Pole pole aliinuka halafu akamwita Sajenti Okello, Mjaluo ambaye alikuwa mtu mwema aliyetutendea kama binadamu, akamwambia akanifungie peke yangu katika *gadirumu* humo katika sehemu yetu. Mwezi wa Julai 1961, nilimkuta "Muru-wa-Wachuka" katika Nairobi, na nilipoanza kusema naye, alipinduka na kutoroka kwa haraka akielekea upande mwingine.

Alimchagua George Kibocha kama kiongozi badala yangu (sasa hapakuwa uchaguzi) na aliwaita wahojaji wengine wawili ili waseme na wafungiwa wengine; wa kwanza aliitwa Saul, ambaye baadaye alikuwa mwanasiasa mashuhuri, na mwingine aliitwa Samuel, ambaye alidai kuwa alikuwa wa ukoo wa Mzee Jomo Kenyatta. Wafungiwa waliniambia kuwa walimwachukia watu hao wawili na ati walimwambia Samuel: "Umejaribu kuharibu jina la kiongozi wetu aliye Lokitaung na umeuza roho ya Afrika ili ule uji mnono wa unga mweupe na ukatuacha tukipigana peke yetu tukinywa uji mwembamba wa mawele. Hatuwezi kukusikiliza kwa sababu wewe si mmoja wetu." Lokitaung ilikuwa ni jela ya kuumiza ambako Mzee Kenyatta alifungwa huko pande za Wilaya ya Kaskazini ya Kenya. Wahojaji waliokuwa Manyani walipewa chakula kizuri na walikunywa uji wa unga wa mahindi, hali chakula cha wafungiwa wa daraja ya "hadi-koa" kilikuwa uji mwembamba wa mawele. Samuel sasa ni mfanyi biashara na ingawa hakuvumilia taabu za Manyani, sasa roho yake iko pale panapofaa.

Baada ya kuwa peke yangu kwa muda wa siku tatu, wafungiwa wengine walinitetea na nikafunguliwa. Kutokea wakati huo, "Muruwa" aliniepuka na aliwacha kuwapiga wengine nikiwa karibu, lakini tuliendelea kumchukia. Hakuweza hata kuhesabu bila kutumia vidole kama mtoto wa darasa la pili. Ilionekana ajabu kuwa mtu mjinga kama huyo alipewa madaraka yo yote. Baada ya muda mfupi, wengine wetu walipelekwa Sehemu 13 ambako niliwakuta marafiki wangu ambao tuliwaacha nyuma huko. Yatta ya Kusini na tulilakiwa kwa furaha na wao. Kiongozi wa Sehemu hiyo alitoka Fort Hall na aliitwa Adam aliyesaidiwa na Daniel.

Nilitaja kwamba tuanze kuwasomesha wale ambao hawakujua kusoma kwa vile wakati huo kazi haikuwa nyingi kwa sababu ule uwanja wa

ndege ulikuwa umekwisha. Kwa hivyo tuliwachagua vijana waliojua kusoma na tukaanzisha masomo ya asubuhi. Haikuwezekana kufanya masomo ya jioni kwa vile hatukupewa taa katika kambi tangu mwanzo mpaka mwisho nilipofungiwa huko Manyani. Tuliokota mchanga mwororo na kuuweka kituo kimoja na kuulainisha ukawa kipimo kama cha kibao cha kuandikia. Tulitumia vijiti vilivyochongwa nchani ambavyo vilisaidia vizuri sana ikiwa mchanga ulikuwa mkavu na ikiwa vijiwe vyake vilikuwa vidogo kutosha. Tuliwagawanya wanafunzi wetu katika madarasa zao tofauti na nilifundisha wale waliokuwa wa darasa la juu—sita, saba na nane. Pia nilifundisha mambo ya siasa na mambo yaliyokuwa yakitendeka kwa wale waliopendelea. Bila shaka, mafunzo hayo yalijenga na kudumisha umoja baina yetu na kwa hivyo tuliweza kujikinga majivuno ya wahojaji. Daniel, ambaye baadaye alijiunga na "waliojitolea" aliogopa mambo niliyokuwa nikifanyiza na akapeleka habari kwa maafisa. Kwa hivyo niliondolewa Sehemu 6 na baadaye nilisikia kuwa yale masomo yalifungwa kufuatana na amri za wahojaji.

Sehemu 6 ilikuwa mbaya zaidi ya nyingine zote, siyo tu katika Kenya bali katika dunia nzima kwa wakati huo. Wengine waliokuwamo walikuwa wafungiwa wanane ambao waliletwa kutoka Sehemu 9 kwa ajili ya kula kiapo. Lakini huo ulikuwa uwongo mtupu. Kiongozi aliyechaguliwa badala ya George Kibocha, ambaye jina lake silifahamu, alikuwa mmojawapo wa wale waliotafuta heshima na Serikali ili aachiliwe haraka. Katika Kikuyuni, wazee hutumia mafuta ya nyama kung'arisha ngozi zao, baada ya kuoga, hujipaka mafuta hayo na inafikiriwa kuwa tabia hiyo huwafaidi. Wale ambao wamesoma sayansi huniambia kuwa huwezekana hii ikawa ni kweli. Wafungiwa walikuwa wakiweka akiba ya mafuta ya nyama yalipopatikana katika chakula chetu. Kwa ajili ya ambukizo la ugonjwa wa "pellagra", hatua hiyo ilionekana ya kufaa kwa kujilinda. Kiongozi wa Sehemu aliona visehemu vya mafuta hayo na ndivyo alipeleka habari kwa maafisa ambao walifurahia sana kuhukumu kuwa yalitumiwa kwa kulisha kiapo. Wafungiwa waliokuwa katika Sehemu 9 walikuwa marafiki wangu wa zamani.

Afisa aliyechunga sehemu hiyo alikuwa Mzungu aliyeitwa Wells. Sipendelei kutumia majina makali lakini yeye hakuwa kitu zaidi au chini ya mwenye tabia za kikatili na kinyama. Chini yake alikuwako Sajenti Mwafrika wa kabila la Mnyakyusa kutoka Tanganyika ambaye tulimpa majina mawili—"Wagithundia" na "Wakaranja." Alipoelekea pande ya Sehemu yetu tulikuwa tukisema "Giguthundia" ambayo kwa Kikuyu ni kusema "arejea." Alituuliza kwa nini tulisema hivyo na sisi tulimwambia kuwa lilikuwa jina jema, yaani jina la kumtukuza mtu wa heshima kama yeye. Alinguruma kwa furaha na akatuambia tuwe tukimwita hivyo

daima. Pia tulimwita "Wakaranja" kwa vile Karanja ndilo lililokuwa jina la Mkikuyu wa kwanza aliyemkuta Manyani kwani alifikiria kuwa wakikuyu wote huitwa Karanja. Yeye hakuwa mwenye akili; hata kama afisa aliapa kwa kukasirika mbele yake, yeye alijibu kwa mshindo. "Ahsante, *effendi*." Wakati John O'Washika alipojali kusema Kiingereza kwa afisa badala ya Kiswahili, Wakaranja alimshika na kumwambia: "Kimbelembele chako kirefu kama tereni," huko akimpiga kwa nguvu. John alipigania uchaguzi wa Februari 1961 bila kufaulu lakini sasa ni mwanachama mshupavu wa KANU ya tawi la North Nyanza. Tulikuwa tukizungumza "Wakaranja" saa za jioni na tulihukumu kwamba kama ikiwezekana kujengwe Chuo cha Wapumbavu, bila shaka angekuwa Mkuu wa chuo hicho.

Baada ya siku chache, vikundi vya hadi-koa kutoka Sehemu nyingine vililetwa katika Sehemu 6, na baina ya hao walikuwa Stephen Aloo (aliyekuwa inspekita polisi hapo mbele na sasa anafanya kazi kwa Brooke Bond) na David Oluoch Okello (aliyekuwa mwenyekiti wa K.A.U. katika Central Nyanza ambaye sasa amerudia wana-siasa), ambao hao wote walikuwa wanataifa halisi ambao hawakuwa Wakikuyu. John O'Washika pia alipelekwa humo. Yeye alikuwa Mluhya. Kumekuwako uvumi kuwa hawakuweka watu wa makabila mengineyo wakiwa wafungiwa katika kambi hizi. Ingawa wafungiwa wengi walikuwa Wakikuyu, palikuwako na wengine kutoka makabila ya Wajaluo, Wabaluhya, Kitosh, Wakamba na Wamasai ambao walisimama nasi kwa kupinga maongozi ya Serikali.

Sehemu 6 ilikuwa na mambo ya kipekee. Wells alionekana kama alipewa uhuru kufanya kama alivyotenda na Mkuu wa Kambi, akisaidiwa na Wagithundia na askari Mkamba. Wale askari wa kawaida, ambao tulikuwa na mipango ya kisiri nao hawakuhusiana na yale nitakayoeleza sasa. Asubuhi saa thenashara tuliamshwa tukapelekwa nje ambako tulifanywa tukimbie sana; saa moja na nusu, tulikunywa uji mwembamba. Saa mbili, ile kazi ya siku ndipo ilianza. Wale wenye kuutumiza, Wells, Wagithundia na yule askari Mkamba, walichukua kila mtu muda wake kutuchunga. Mpaka saa saba za mchana, tulifanyizwa kwata ya kutuadhibu. Baina ya yale tuliotendewa yalikuwa kukimbia sana mikono yetu juu ya vichwa vyetu, kurukaruka kama chura magoti yetu tukiyakunja kwa mwendo mrefu na mengineyo ya kuumiza katika jua kali la mchana. Amri zilikuwa kali wakati wa kuenda, lazima kukimbia na cho chote tulichofanya lazima kifanywe kwa haraka. Ye yote aliyefanya upole na hata wengine ambao hawakufanya upole, alipigwa kwa fimbo au kwa mpira wa maji uliobebwa na aliyetuchunga. Waliongeza amri za kurukaruka hata hakuna wetu aliyeweza kutii na tulionekana kama Charlie Chaplin anavyoonekana katika sinema wakati picha yake inapoharakishwa.

Wengi walianguka waliporukaruka kama chura na waliposhindwa na kurukaruka walianguka mbele huko wakaumia uso na meno yao kwa njia mbaya.

Siku moja nilifanya kama kupumzika na askari Mkamba alinijia akanichapa makofi ya kusisimua masikioni yangu. Alipomaliza nilijiona kama kiziwi kwani sikuweza kusikia kitu na kwa muda wa siku mbili nilikaa katika hali hiyo huko nikijaribu kufahamu mambo kwa kuangalia midomo ya waliokuwa wakisema. Halafu nilitia maji katika masikio yangu, nikajaribu kujaza kinywa changu kwa pumzi ili kujaribu kufungua masikio. Hatua hiyo ilifungua sikio moja na wakati huo Wells alimtuma mganga aliyenisafisha sikio hilo lingine kwa dawa. Nilipokuwa Lodwar nilipigwa sindano kumi na sita kwa vile sikio hilo lilikuwa latoka damu na mara nyingi hata leo ninaumia na wakati mwingine mimi ni kama asiyesikia kwa sikio moja. Wale ambao walidharauliwa na Wells walilazimishwa kuondoa hata suruali na kuwapandishana kama nguruwe. Kitendo hiki kilikuwa cha kuaibisha kuliko vingine vyote. Wakati mmoja wakati wa kurukaruka, Wells alifika na ndoo ya maji akamwagia kijana mmoja aliyeitwa Kimani matakoni, huko akicheka kama alifurahia kitendo hicho.

Ilipofika saa saba, tulichezeshwa "Fanya hivi" na "Fanya vile." Wakati huo tuliupendelea na Wagithundia alifurahiwa sana kama aliweza kutukuta tuko nje na tulipendelea kufanya makosa ili kumchekesha na kuongeza muda wa kupumzika. Ilipofika saa kumi na moja, tulirudishwa katika kiwanja chetu na ile taabu ya mchana iliisha. Jioni na usiku zilikuwa kama wakati wa ruhusa. Watu hawafahamu vile maisha ya kawaida yalivyo ya ajabu, au ni furaha gani iliyomo katika kuepukana na kupigwa na seng'enge na kuweza kujifanyia mambo na kuvuta hewa safi na kuwa na uhuru wa kusema na wengine. Katika fikira za pande zote mbili, mambo mageni yalikuwa yakitendeka na nafsi zetu zilikuwa zageuka kwa njia zisizoelezeka.

Siku moja Paul Muchemi, mvulana wa Johanna Kunyiha, M.B.E., wa pande za Nyeri, alipigwa vibaya na yule Mkamba hivi ati damu ilimtoka kichwani. Nilikata shauri kujihatarisha kwa kuandika barua nyingine ingawa kuandika kwangu kwa hapo kwanza hakukunitia moyo sana. Ilikuwa shida kusikilizana na askari ye yote katika Sehemu 6 lakini baada ya kufikiri sana, niliandika barua juu ya karatasi ya choo halafu nikaificha chini ya ndoo ya choo. Hatukukubaliwa kutoka nje ya Sehemu 6 na kwa hivyo choo chetu kilisafishwa na watu wa Sehemu 7. Kamau Githirwa aliiona hiyo barua na akawahi kuipeleka kwa njia ile yetu ya kawaida. Niliituma kwa Chief Secretary na Mkuu wa Jela. Nilikuwa nimeshauri juu yake kuwa ye yote atakayeipata aiandike tena juu ya karatasi nzuri kabla ya kuipeleka, lakini sina habari kama alifanya hivyo.

Baada ya siku chache, Mkuu wa Kampi aliniita mbele yake akaniuliza kama barua hiyo ilikuwa yangu. Sikujua kama alikuwa ameambiwa na wakuu wake achungulie malalamiko yangu. Nilikubali na hapo akaniambia kuwa nitaadhibiwa. Ilikuwako amri kwamba hakuna aliyekubaliwa kupeleka barua nje bila kuipitishia kwa maafisa waisome kwanza. Lakini aina ya barua yangu haingekubaliwa kutoka nje na kwa hivyo haikuwezekana kutii amri hiyo. Wafungiwa wote waliokuwa kama elfu nne walikutanishwa nje ya Sehemu 6, na yule Mkuu wa Kampi aliwaambia: "Huyu ndiye kiongozi wenu, Mwangi. Yeye ni mtu wa kuhatarisha sana na anatumia wakati wake akiandika barua nje ya kampi, kitendo ambacho kinakosea sheria. Tulimpeleka South Yatta kwa njia ya 'mfereji' akielekea nyumbani kwao na akiwa huko aliandika barua nyingine iliyomfanya arudishwe hapa Manyani ambapo ameandika barua nyingine. Sasa atajifunza somo lake mbele yenu na ninawashauri kwamba ninyi msiandike barua." Niliondolewa nguo zangu nikachapwa viboko kumi na viwili na yule sajenti Mkamba. Viboko hivyo viliniumiza zaidi ya vingine nilivyopigwa na damu ilinitoka matakoni mwangu. Wakati wafungiwa wengine walipoona hali ya mwili wangu ambao sasa ulikuwa mwembamba na mwenye majeraha kufuatia vitendo tulivyotendewa katika Sehemu 6, walinguruma kwa uchungu kama fungu la nyuki. Nilivumilia mambo hayo yote kwa vile nilijua kuwa mimi sikuwa na makosa na wafungiwa wengine walijua mimi nilifuatia haki. Nguvu ya aina hiyo haiwezi kumalizwa na viboko hata viwe vingi namna gani. Ni wakati gani watu watafahamu kuwa kupigwa kwa aina hiyo kunazidisha nguvu za yule anayepigwa? Kupigwa kunaweza kumfaa mtu ikiwa anafahamu kuwa amefanya makosa, ingawa mimi sifikirii sana hivyo. Lakini ikiwa mtu anafikiri amefanya haki (awe amefanya au bado) kupigwa kunaongeza nia yake. Mwishoni, vitendo vya maafisa hao vilinijenga kuwa kama mtu mwenye kudhulumiwa tukio ambalo halikuwa nia yao. Hawakutawaliwa tena na fikira zenye sababu bali walitenda vile roho zao zilivyoamuru kama vile mnyama mkubwa anamwonea mnyama mdogo na kumtwanga.

Baada ya hivyo, Mkuu wa Kampi aliniambia nisimame niwaambie wafungiwa wengine kuwa sitaandika barua nyingine kamwe. Lakini hakuchagua muda ulionifaa zaidi kwani nilimwambia wakati watakapoacha kuwapiga na kuwafanyia ukatili watu wangu, nitaacha kuandika barua. Lakini, nilisema kwa uchungu mwingi, hata kama aliniua, watu wangu watajua kuwa nilikufa kwa ajili ya haki zao. Majibu yangu yalimkasirisha zaidi na akaamuru niwekwe peke yangu katika chumba kidogo kwa muda wa siku saba. Lakini kwanza aliniambia niende hospitali kwani damu ilinidondoka matakoni na wale wafungiwa waliotutibu waliniambia nisife moyo kwani kila mfungiwa alikuwa upande wangu na

walifurahia kuwa nilipigania haki zao. Halafu walinipeleka katika kifungoni karibu na Headquarters Company.

Hiyo jela ndogo ilikuwa chumba cha mabati chenye sakafu ya simiti ya kipimo cha urefu wa futi sita na upana wa futi nne. Vilikuwako vyumba kama hivyo thelathini na vitano katika Manyani ambazo zilijengwa kama vikundi vinne. Hawakunipa maji wala chakula lakini kwa bahati njema, mtu mmoja alikuwa amemwaga ndoo ya maji katika chumba ili kukifanya cha kutopendeza, wakati wa kulala. Kwa hivyo kwa muda wa siku tatu kabla kukauka kwa maji niliwahi kuonja maji yaliyobaki kwa kutumia ulimi na wakati huo niliweza kufikiri sawasawa na nilijisemesha kwa sauti kubwa. Ilipofikia siku ya nne na ya tano, jasho baridi lilianza kunitoka mwilini. Bado sikupewa chakula wala maji, hakuna aliyefika kuniona—jasho tu na kimya. Ilipofikia siku ya sita na ya saba, macho yangu yalikuwa kama pembe nzito cha mawe na zile ndoto za kuogofya zilinianza. Wahindi wenye vilemba walipitia pale wakiwa na ndevu nyekundu; nyota zenye rangi rangi zilipitia machoni mwangu; wanawake wazee Wakikuyu walicheza na kila mara palikuwako na watu wakienda huku na huko. Hawakuwa na nyuso nilizojua lakini walionekana kama ni watu niliokuwa nimekutana nao, na ilionekana kama kumbukumbu ya mambo yaliyonitukia hapo mbeleni. Ilipofikia siku ya nane, sikufahamu tena pale nilipokuwako wala huo mwili wangu haukuwa kama sehemu yangu. Nilijisikia kama gurudumu la binadamu lililozungukazunguka na kama mtu aliyekuwa akianguka kutoka umbali wa futi maelfu kutoka juu ya mlima akielekea bondeni kwenye msitu mzito. Kinywa changu hakikufunguka na kilichonibakia ni huo mwanguko mkubwa wa kuelekea kwenye bonde kuu lenye rangi ya buluu ambalo nililiona wazi. Huo ulionekana kuwa mwisho; hakuna nilichoweza kufanya kuzuilia hali hii na bali sehemu nyingine yangu haikuanza kuanguka, kitu kilinizuilia nisianguke huko kwenye amani kwenye bonde la buluu.

Mnamo siku ya sita, ingawa sikufahamu hivyo, Gad Kamau Gathumbi na wengine watatu walifungiwa ndani ya vyumba vidogo karibu na changu kwa sababu walikisiwa kuwa walimpiga Adam, aliyekuwa kiongozi katika Sehemu 13. Gad alijua kuwa nilikuwa pale na alistaajabu aliponikosa wakati wa kuitwa majina asubuhi ya siku ya saba. Alisumbuka katika fikira juu yangu siku hiyo yote na siku ya nane alimhimiza askari yule Mkamba afungue chumba changu. Walinibeba pole pole kutoka chumba changu hadi kwenye jua na walifikiria kuwa nilifariki. Daktari aliitwa akanipiga sindano halafu akanipeleka hospitali. Nilikaa siku moja katika hospitali halafu nikarudishwa katika chumba hicho mara nyingine! Lakini Gad akawa mwuguzi wangu na hapo nikaanza kujiona tena kwa kutumia maziwa na mchuzi. Sina shaka kwamba Gad Kamau Gathumbi aliokoa maisha yangu kwani kama si yeye singeishi tena.

Robinson Mwangi alikuwa kiongozi wa Sehemu 1 wakati huo na alikuwa ameona yale niliyotendewa na hakuwacha kamwe kufanya malalamiko na kutaka tutendewe vyema. Wafungiwa wengine waliokuwa na elimu walitufikiria kuwa wenye wazimu kwa vile tulikataa kuachilia mbali wale wasiokuwa na elimu, kitendo ambacho kingetupatia maisha ya raha ya wale "waliojipeana." Lakini ni wao waliokuwa hitilafuni na hii ndiyo sababu moja iliyomfanya Daniel, aliyetugeukia, asifaulu wakati wa uchaguzi. Watu walifikiria kuwa ingelifaa kumchagua mtu ambaye ingawa hakufungiwa lakini ambaye hakufanya kinyume cha kupigania uhuru badala ya kuongozwa na mtu ambaye alijaribiwa katika moto wa kampi za wafungiwa na kuonekana hatoshi.

Kwa ajili ya kujiingiza katika hali ya starehe yetu, Robinson alihamishwa akapelekwa Sehemu 6, ambako alichaguliwa kuwa kiongozi na ambako nilijiunga naye baada ya kufunguliwa kutoka kichumba changu. Wakati Komiti ya Kutembelea ilipofika, yeye hakusita kuwaambia juu ya ukatili tuliotendewa, na kama kawaida, malalamiko yake yalileta manufaa kwani waliofungiwa katika Sehemu 6 walipelekwa Sehemu 21. Wakati huo, maelfu ya wafungiwa yaliletwa Manyani kutoka Kampi ya Pekee ya Mackinnon Road ambayo iliweza kukaliwa na wafungiwa 6,000 na ambayo ilikuwa yafungwa wakati huo. Wafungwa hao walituambia hadithi nyingi ambazo hatukuwa na sababu za kuzitozisadiki na zilizoonyesha kuwa walitendewa vibaya kama vile sisi tulivyotendewa. Walikuwa wakilala ndani ya mabanda yaliyojengwa wakati wa vita yaliyogawanywa katika vyumba kadhaa. Walikuwamo wafungiwa elfu moja na mia mbili katika kila chumba. Hawakutoka nje kamwe kwenye jua na hawakuweza kujua kama ulikuwa mchana au usiku walipoamshwa. Kwa ajili ya misemo ya watu wengi, ilisikika kama walikuwa katika soko. Walikuwako maafisa kadhaa wakatili, mmojawao akiwa Mjerumani. Wafungiwa hawakupendezwa na hali ya mambo humo.

Robinson na mimi tulijisikia twataka kuandika barua nyingine, na hapo tukaungana kuandika moja kwa Waziri wa Makoloni huko tukaeleza malalamiko yetu juu ya hali ya kambi hata tukaeleza yale yaliyokuwa yakitendeka ndani ya risavu. Wakati huo tulikuwa tumebuni aina ya pekee ya *Waya Times* juu ya hali hii kutokana na General Kibera Gatu, ambaye alikamatwa alipotembelea Othaya kutoka Misitu ya Aberdare. (Sasa yeye ni mwenye mkahawa katika Othaya). Alituambia juu ya unyama wa amri ya "kafiu" ya masaa ishirini na manne na vile watoto walivyokufa kwa njaa katika vijiji. Ingawa hivyo, tulifahamishwa juu ya vile vyama vinginevyo kama International na British Red Cross vilivyokuwa vikipigana na njaa baina ya watoto; pia wamisheni wengine wa Roman Catholic walifanya mambo ya kumaliza njaa na kuleta msaada mwingine kwa

waliokuwa na haja. Wafungiwa walifurahiwa sana na msaada huo ambao kama haukuwako wengi wangekufa bila shaka. Pia tulitaka uchunguzi ufanywe juu ya kifo cha Maina Matawa (aliyetoka Othaya katika Nyeri), ambaye alikuwa ametoroka kutoka Mackinnon Road kwa ajili ya mapigano yaliyokuwamo juu yake na kwa vile alipigwa risasi akafa karibu na Manyani.

Tulipeleka barua hiyo kwa njia ile yetu ya kawaida, lakini kwa bahati mbaya, nakili yake ilipatikana wakati wa uchunguzi ulioanzishwa kutafuta barua zo zote; ilikuwa imefichwa katika mfuko wa kitambaa uliowekwa na Wambugu Mangua na Ngunjiri Githiomo (wote walitoka Nyeri; mmojawao sasa anafanya kazi ya ukarani Nairobi na mwingine ni karani katika Idara ya Kazi katika Nyeri). Wakati maafisa walipouliza ni nani aliyeiandika barua hiyo, niliwaambia kuwa ni mimi niliyeiandika. Nilimlazimisha Robinson kukubali kuwa ni mimi niliyeiandika kwani ilikuwa muhimu kuwazuilia maafisa wasiwachukue sisi wawili na kuwaacha wasiokuwa na elimu kama watoto wasio na wazazi. Mkuu wa Kampuni ya "C", Romney, alinihoji juu ya barua hiyo. Aliujua mwandiko wa Robinson na alikisia nilivyokusudia katika kujitoa mimi peke yangu. Alitaka kutuondoa sote wawili. Aliniuliza kwa nini niliiandika barua hiyo na alikasirishwa na majibu yangu kuwa sababu zake zilikuwako ndani ya barua na zilikuwa wazi. Aliponiuliza vile nilivyowahi kupeleka barua bila kujulikana, nilimjibu kuwa nilimpa ndege mdogo akaipeleka kwa niaba yangu. Sikukusudia kumwambia jina la askari ye yote aliyetusaidia kwani wangekataa kupeleka barua nyingine zetu. Alikasirika zaidi na mara nikahamishiwa kwenye chumba kidogo ambako niliishi kutoka kati ya Machi hadi Juni 8, 1956. Gad Kamau Gathumbi alikuwa angali humo na tuliishi naye wakati huo wote.

Wakati huo tulipewa nusu ya chakula cha kawaida lakini wafungiwa wale wengine waliwahi kutuibia nyama kutoka mastoo ambayo walikunja ndani ya gunia au karatasi na kuisukuma kwa kifagio kupitia kwenye mitaro ya maji wakati walikuwa wakifagia mitaro hiyo kwa maji. Tulikuwa na njaa hivi hata hatukujali uchafu uliokuwa na nyama wakati mwingineo. Wakati huo, ilisemekana kuwa kiapo kilichoitwa "Manyani 25 Thenge" kililiwa katika Sehemu 25 ambayo kiongozi wake alikuwa Daniel Mathenge ambaye mwaka wa 1960 alichaguliwa kuwa mwenye-kiti wa K.A.N.U. katika North Tetu Division ya Nyeri. Hapakuwako na ukweli wo wote juu ya kiapo, na katika ujuzi wangu, kiapo kilicholishwa ni kile kilichopewa wawili katika Kowop. Ili kutafuta ushahidi, maafisa walipata sababu ya kuwaumiza wafungiwa wengine na vile wengine walivyoungama wakati wa "kuokolewa" kuwa walikula kiapo hicho kunaonyesha ubure wa mpango huo wakati huo. Ukatili ulikuwa umegeuza maana ya ukweli na

hivyo ni kusema wengi walisema vile wahojaji walivyotaka kusikia wakitumia uwongo mfupi kama ilivyowezekana.

Wakati huu, mambo mengine katika Manyani yalikuwa mema kidogo. Tulipinga kabisa amri iliyotolewa kuwa tunyolewe sote. Siyo tu kuwa hii ni aibu kufuatana na desturi zetu ambako kunyolewa kunafanywa na wazee waume kwa wake, bali hatua hiyo iliwaumiza sana wale waliofanya kazi bila nywele katika joto la jua moto.

Nilipokuwa katika Sehemu 13, nilikutana na wengine wa wale waliokuwa wamepigana katika misitu na baina yao alikuwako mwingine aliyekuwa mgaidi wa "kuigiza," aliyetoka Lokesheni 12 katika Fort Hall. Magaidi hao wa kujiigiza walifanywa kutokana na wengine waliokuwa katika misitu, lakini ambao kulingana na maelezo ya Serikali, walijitoa mara walipokamatwa na kukubali kurudi msituni kama magaidi ili kuwakamatisha wale waliowacha msituni saa chache mbeleni. Nilitaka kujua kwa nini walijihadhari namna hiyo. Ili kufahamu nia zao, ni haja kuelewa kuwa kulikuwako na vikundi vya aina mbili vilivyohusika katika vita hivi. Cha kwanza kiliitwa *Njamba cia Ita* (yaani Ndume za Vita), mashujaa wa kweli ambao tuliwapa jina la *Ihee* (ambao bado kutahiri). Hao ilikuwa ni kazi yao kupigana na majeshi ya Kiingereza na ya Ulinzi na mwingine ye yote aliyewawinda huko msituni. Hao ndio walikuwa "Jeshi la Uhuru wa Ardhi" na walijipanga vikundi vikundi kama majeshi ya vita vingine vyo vyote. Katika msitu, kambi zao ambazo zilipewa nambari zilijulikana kama "Bush 12" au "Bush 4" na zilipangwa malidadi kama nyinginezo zo zote za kijeshi. Walipojitoa kupigana katika Risavu, walipiga tarumbeta au firimbi wakati walipozungukia kambi ili kuwaalika majeshi ya Ulinzi kwa vita. Haikuwa kazi yao kuwaua raia; walipigana na wale waliowashambulia na ndio walipigana vita vya kujali kama vile mashambulio yaliyofanywa katika stesheni ya polisi ya Naivasha, mashambulio ya kambi za Humungati na hedikuota za Serikali. Inaposemwa kuwa vita vilipiganwa kisafi, wao walipigana vita vyao kwa kisafi.

Mmoja wa watu maalum katika vita hivi alikuwa *Mundu Mugo wa Ita* au "Nabii wa Jeshi", ambaye ndiye aliyewashauri wakati na mahali pa kushambulia. Wangombe Ruga, ambaye alikuwa wa ukoo wa zamani wa manabii (wenye kuota) katika Nyeri, alikuwa na madaraka hayo katika Jeshi la Kimathi huko milimani ya Nyandarua (Aberdare Mauntains) na tulikuwa naye Manyani, Aguthi na katika kambi za maonyesho. Aliniambia kuwa walikuwa na sheria zao kali walipokuwa msituni kama zile tulizokuwa nazo tulikofungiwa. Sheria hizo zilipitishwa katika mikutano ya kila mwaka na *Kenya Parliament* ambayo ilikutanika mara tatu kwenye mashimo makubwa ndani kabisa misituni. Jemedari mwingine aliniambia kuwa Serikali ilipoteza mali nyingi kwa kujaribu kuwapiga na

bomu ndani ya misitu. Ingawa wengine walikufa ilikuwa ni rahisi kuwadanganya waendeshaji wa ndege kwa kuasha moto na kufanya moshi ili kuwavuta, huko wakatupa mabomu kwenye moshi hali mashujaa walikuwa mbali. Kwa njia nyingi, Serikali ilifahamu kidogo juu ya nia na akili za majeshi ya msituni. Eropleni ziliitwa *Nyagikonyo* kwa vile zilivyovimba upande wa chini ambako bomu ziliwekwa.

Aina ya pili ya vikundi vya kupigana kiliitwa *Komerera*. Jina hilo hupewa wale ambao hufikiriwa wamelala na bali wajisikia, na hao walikuwa wakijificha katika Risavu au ukingoni wa misitu na walipigana hata kuwaua jirani wao kwa ajili ya chakula au bunduki. Walipigana na kila mtu hata raia, na hawakuwa na ujuzi wa kujitengenezea silaha wala hawakuweza kupigana vita halisi. Kikundi hicho kilikuwa cha wenye tabia nyonge na ambao hawakuwa na uwezo wa kujiweza, na wala hawakupokea amri kutoka kwa wakuu wengine au kutokana na sheria za *Kenya Parliament* na hawakufuatia mashauri ya *Mundu Mugo* na hawa *Komerera* walifanya kama vile ilivyowapendeza. Ingawa vitendo vya ukatili vilivyofanywa na mashujaa wetu vimeongezwa chumvi na kupanuliwa, hakuna shaka kuwa mambo maovu yalifanywa. Mtu aliyeuawa kwa panga alionekana kuwa picha ya kughadhabisha zaidi ya maiti ya risasi kwani panga haiwezi kuua kwa usafi, lakini hata hivyo kunayo mambo mengine yasiyoelezeka yaliyotendeka. Ningetaka kueleza wazi kuwa mambo kama hayo yalikemewa na *Kenya Parliament* ndani ya misitu na sisi katika vifungoni. Hatukupendezwa tuliposikia bibi Mzungu au mtoto aliuawa katika shamba au kusikia juu ya ng'ombe walioumizwa. Lakini tuliwapongeza na kuwashukuru wale walioonyesha ushujaa na ubongo wa kupigana vita halisi na adui wetu wa kweli, bila woga na kwa heshima wakitoka vituoni vyao huko misituni.

Zilikuwako sababu tatu zilizowafanya magaidi wa "kuiga" kurudi misituni. Sababu ya kwanza ni kuwa hali ya mambo ilikuwa yageuka kila mwaka. Ikifikia mwaka wa 1954, jitihadi iliyoonyeshwa na mashujaa wale waliokwenda misituni mwaka wa 1952 ilikuwa imeilazimisha Serikali kugeuza mambo mengineyo katika hali ya maisha ya Mwafrika. Wakati huo hapakuwako na msemo wa kumaliza ugaidi baada ya miezi sita au mitatu. Baada ya miaka kadhaa ule mlango uliofungiwa wananchi hata wakafanya upinzani na Serikali ulifunguliwa. Wengine wa hao magaidi wa "kuiga" walitaka kuwaambia wenzao hivyo na kuwauliza wajitokeze. Hali ya siasa iliendelea kuwa njema tena. Pili, wengine wa hao magaidi wa "kuiga" walitendewa vibaya hivi ati ili kuokoa maisha yao iliwalazimu kufanya kama walivyoulizwa. Katika hali hiyo, ambayo hailingani na sheria za vita, walilazimishwa kurudi misituni. Tatu, wengi wa hao magaidi walitaka kuwaambia wenzao wa msituni wajue kuwa wakati wa "kupigana

au kufa" ulikuwa umekwisha. Tena ilikuwako njia nyingine—kujitolea na kuishi. Ni wachache waliokuwa misituni walisadiki mambo hayo na hata mnamo mwaka wa 1956, na kulikuwako na maripoti juu ya kupigwa risasi kwa wafungwa ambayo hayakuwa bure kabisa. Wakati mmoja katika Lokesheni ya Chinga, Jeshi la Ulinzi halikuwachukua mateka. Mnamo 1957 wakati ilipotangazwa uchaguzi na uweko kwa Waafrika wanachama waliochaguliwa katika Lejiko vita vilikuwa vimeshindaniwa. Hii ndio sababu kunao wengi ambao walikuwa maje-medari au mashujaa wanaoendelea na kazi zao za biashara au za ukulima kwa amani katika nchi. Tumepata yote na hakuna haja tena ya kufanya matata, kuwa na vyama vya siri au vita na wale wanaofanya mambo kama hayo hawayafanyi kwa jina letu.

Tarehe Juni 8, 205 wa wale viongozi waliopingana na maafisa katika kambi yote waliitwa Sehemu 30 ambako miguu yetu ilifungwa kwa nyororo tukitayarishwa kwa safari ya kuhamishiwa kisiwa cha Saiyusi. Robinson, Gad na mimi tulifurahiwa sana tulipojiona pamoja tena. Tuli-kata shauri kufanya mzaha wa minyororo kwa hivyo tulisema kuwa tutakimbilia hizo nyororo kwa nyuso zenye furaha kutoka kwa maafisa. Hatukutaka wafikiri kuwa walituweza wakati wo wote. Saiyusi ni kisiwa chenye maili tatu mraba katikati ya Ziwa Victoria karibu na Kisumu. Tulifahamu kwamba Serikali ya Kenya ilikiita "Kisiwa cha Kutorudi."

7 Nyororo, Visiwa na Vumbi

SIJUI NI nani anayeunda nyororo, lakini Kenya ni lazima iwe ilinunua schemu yake kubwa katika mwaka 1956. Kwa vile ni wachache wa siku hizi wanaojua kuzivaa, na wengine wengi wafikiria kuwa walikwenda wakiwa na ulizo, labda ingefaa nieleze kidogo juu ya nyororo. Ikiwa umefungiwa nyororo miguuni, yakupasa kutembea pole kwa hatua fupi kwani zimetengenezwa kuzuia mwendo. Ilituchukua muda wa saa nne na nusu, kutoka saa kumi na moja za usiku hadi saa tatu za mchana, kutembea urefu wa maili tatu kutoka kambi kwenda stesheni ya reli. Nyororo kubwa hazizuilii mwendo sana kama zile ndogo, lakini zile ndogo huwezesha mtu kuruka kama kwamba yuko ndani ya mashindano ya gunia. Vijana wengine waliweza kutembea upesi kwa kurukaruka. Lakini hizo chuma huumiza mwili hata ukienda namna gani. Nyororo nyinginezo zinazo vyuma vilivyoachana kuliko vingine. Haiwezekani kutembea kwa kupanua miguu—hali hii huumiza miguu. Kwa hivyo urefu mwingineo wa nyororo hubaki chini, na huko hurusha vumbi ambalo huongezeka huko nyuma. Hali hiyo ilifanya mwenendo kuwa wa upole na tulitumia kamba na kuivuta hiyo nyororo juu tukiifunga kamba kiunoni. Tuliweza kukaza kamba hiyo na kuiinua nyororo kabisa kutoka chini.

Tena ilikuwako taabu ya kugeuza suruali. Kila mmoja alikuwa na suruali moja tu ndefu na mara kwa mara ilikuwa haja kuisafisha. Ilituchukua muda kabla ya kuvumbua njia ya kupambana na hali hii na hata Mzee Kenyatta aliniambia kuwa walipatwa na shida hiyo hapo kwanza walipokuwa Lokitaung. Singetaka mwingine awe katika hali ya shida kama hiyo, na hili ndilo jibu. Siri ni kufanya mguu mmoja kwa wakati mmoja. Shusha suruali, sindikiza mguu mmoja wa suruali kupitishia baina ya nyororo na mguu mpaka uone umetia kubwa kama iwezekanavyo, halafu vuta ile nyororo juu kama uwezavyo na uondoe nyayo zako kutoka kwenye suruali. Sasa mguu mmoja wa suruali uko huru. Fanya vile vile kwa mguu huo mwingine. Sasa vuta suruali juu kuachishana na nyororo, na sasa iko tayari kusafishwa. Kuirudisha ni kufanya kinyume cha maelezo hayo yaliyotangulia.

Tulipofika Nairobi, gari la moshi liliongezwa wafungiwa wengine watatu, mmojawao akiwa General Kahinga, na Nakuru ilipumzika kwa muda wa masaa matatu. Watu wengi walionijua hapo mbeleni walifika kutuona waliposikia tuko pale na wakatuletea chakula na tumbaku ambayo hapo kwanza askari walitukataza kuweka. Wakati wanawake walipoziona hizo nyororo zilizokuwa miguuni ya Gathogo Mwitumi wakati alipojaribu kumwendea askari aliyemwita nje ya gari, walilia machozi ya uchungu. Tuliwaambia wawe wenye furaha kwa sababu tulikuwa tumezoea kuzivaa na hazikutuumiza. Hizo nyororo zilikuwa za kuumiza sana lakini tuliwaambia hao mabibi Wakikuyu ili wajue kuwa tulikuwa tungali na nguvu na bado nyoyo zetu zilikuwa na nguvu na zaidi ya hayo hatukupenda watesi wetu wafikiri kuwa walitufanyia tendo la kuvunja nyoyo zetu. Ndio wakati huo bibi mmoja aliyeitwa Kabura alimwendea afisa wetu kwa ushujaa akamwomba ruhusa awakubali watupe chakula, na huyo afisa akakubali—kinyume cha amri ya askari. Tulipofika Saiyusi, tulitunga wimbo wa kumshukuru bibi huyo na bibi hao wengine.

Tulifika Kisumu Juni 11, 1956 na mara moja tulipelekwa jela ya Odiaga, Kisumu. Asubuhi yake, tuligawanywa vikundi viwili, mia moja wakabaki Odiaga na wale wengine mia moja na wanane wakaelekea Saiyusi. Nilikuwa mmoja wa wale waliopelekwa Saiyusi, hali Robinson Mwangi aliwachwa Odiaga. Ingawa nilisikitika sana kumwacha nyuma, labda mambo yangekuwa mabaya zaidi kama kikundi kimoja kilibaki bila mtu mwenye elimu. Asubuhi ya Juni 12, tungali tukiwa na nyororo zetu, tulipakiwa ndani ya malori na tulipekuliwa, tukiwa thelathini na watano ndani ya kila lori, tulikasirika tulipoona askari wakiweka nyavu juu ya malori kama vile tulikuwa samaki au ndege. Nyavu hizo zilikuwa za kipimo cha zile zinazotumiwa katika vituo vya viwanja vya mipira na zilitengenezewa huko jelani ya Odiaga. Tulifikiria kuwa kitendo hicho kilikuwa kingine zaidi cha kuvunja roho zetu, na kama kawaida kilituongeza nguvu kwa kufahamikiwa kuwa tulikuwa twaelekea kuwa mfano gani. Kama wengine wetu wangejitolea, ingekuwa rahisi kueleza kuwa Mau Mau ilikuwa kitu cha ushenzi ambacho kilikusudiwa kuwarudisha nyuma watu ambao waliongozwa vibaya na kiongozi mjinga. Kutoka ndani ya wavu, vitu vilionekana kama vigeni na askari walionekana kama waliokuwa na mipasuko na hakuna kilichoonekana wazi. Basi tukasafirishwa kutoka Odiaga kupitia Bondo na Sakwa hadi kingoni mwa Ziwa Victoria ambako nyororo zetu ziliondolewa na badala yake tukafungwa pingu. Mitumbwi iliweza kuwabeba watu hamsini kila mara na nilikuwa mmoja wa kwanza kuvuka hadi kisiwani. Huo mwendo wa mtumbwi ulikuwa mgeni kwangu na wengine wetu walitapika.

Nyumba za kambi na za maafisa katika Saiyusi zilijengwa na wafungwa

wa Mau Mau waliopelekwa humo mwaka wa 1954. Mwisho wa 1955, wafungwa hao walikuwa waelekea kukamilisha vifungo vyao na mahali pao palikuwa parudishwa wafungiwa. Wafungiwa kama 800 walikuwa wamepelekwa humo kutoka Manyani tulipofika na nilishangazwa na kuchangamshwa kwa vigelegele walivyofanya kwa kunilaki. Nilishtuka kupindukia waliponibeba kutoka mlangoni hadi ndani ya chumba kimoja ambako walikuwa wametayarisha chakula kizuri cha kutukaribisha ambacho kilikuwa na chai na mkate halisi wenye siagi. Muda wa miaka minne ulikuwa umepita tangu nile mkate wa siagi ambavyo vilikuwa baina ya chakula nilichopenda wakati wa kawaida na ulikuwa mtamu ajabu. Wengi wa wale waliokuwa humo walikuwa nami katika Sehemu 13 ya Manyani na tuliongea kwa masaa mengi pamoja kabla ya kuungana na kundi langu katika chumba kingine, huku nikifurahi zaidi ya vile nilivyofurahi kwa muda wa siku nyingi.

Asubuhi yake, tuliamriwa kwenda nje kufanya kazi kama vile wafungiwa wengine walivyokuwa wakifanya, lakini tulikataa kutii amri hiyo ambayo haikulingana na sheria. Wafungiwa walichagua ujumbe wa kumwona Mkuu wa Kambi, ambao ulikuwa na Harry Kamanda Njoroge (ambaye sasa ni mwuzaji Nairobi), Gathogo Mwitumi (sasa ni mfanyi biashara mwenye-kiti mdogo wa rais wa K.A.N.U. ya Nakuru), Wambugu Kamuiru na mimi. Kwa upole, tulimweleza afisa huyo kuwa hatukukusudia kufanya kazi kwa sababu sisi hatukuwa mahabusu waliofungwa na korti ya hukumu na kuwa kukataa kwetu kulitegemea Kifungu 18B cha "International Convention." Hatukukusudia kupigana au kutumia nguvu au kuwa wasio na sababu lakini hatutafanya kazi. Tulisikilizwa na kukataa kwetu kukakubaliwa na tukaambiwa tukae vyumbani vyetu isipokuwa wakati wa chakula au wa kuoga. Vyumba hivyo vilikuwa vikubwa na kimoja kiliweza kukaliwa na watu mia moja; tuliziita "barracks." Tulitumia wakati wetu tukizungumza siasa na kujifunza. Nilifurahi sana kuona niliweza tena kununua vitabu katika kantini ya kambi na tulipata vitabu vinginevyo vya Kiingereza na Kamusi moja ya Kiingereza iliyoandikwa na Michael West. Mafunzo mengi yalifanywa na John Gakuha ambaye sasa ni mwalimu mkuu wa skuli katika Nyeri. Alikuwa mwalimu wa ajabu na aliwahi kuwafaidi wengi wetu. Nikiwa kiongozi wa kikundi chetu, niliona kuwa sikuwa na nafasi ya kufundisha. Nilikuwa na kazi nyingi ya kuwaandikia barua wale ambao hawakujua kusoma ambazo walizituma kwa jamaa zao nyumbani, kuandika barua za mateta, kutayarisha kuonana na mkuu wa kambi na kutawala mambo ya kila siku katika chumba chetu.

Pia ilikuwa kazi yangu kutayarisha matangazo ya kila siku yaliyokusanywa kama kawaida yaliyojulikana huko Saiyusi kama *Kamongo Times*. "Kamongo" ni jina la Kijaluo lililopewa samaki mkubwa anayepatikana

katika Ziwa Victoria, ambaye pengine huwa mrefu kama futi tano na upana wa futi moja na nusu. Anayo nyama tamu na hufanyiza mchuzi wa kupendeza na wafungiwa walizoea kumkamata wakati wa kufyeka nyasi karibu na ukingo wa kisiwa kwa ajili ya mashamba ya mboga. Hao "Kamongo" hutembea kutoka Ziwani na huchimba ndani ya mchanga na kufanya mtaro wa futi kama kumi na kufanya nafasi ya kupitia maji. Halafu yeye huenda juu kidogo na kufanya ziwa dogo la maji la kuwavuta vidudu na wanyama wengine. Yeye hurudi mtaroni na mara kwa mara hurudi na kuzungusha mkia wake katika ziwa lake ili kuondoa uchafu. Wakati mfungiwa alipoliona hilo ziwa na labda hata huo mkia, aliwaita wale wengine na hapo walikuwa tayari kwa panga zao, mmojawao akisimama mkiani na mwingine alipofikiria kuwa "Kamongo" alificha kichwa. Kufuatia neno moja la amri walisindikiza panga zao pamoja na mara nyingi walimwua "Kamongo." Wakati mwingine tuliachwa na mkia peke yake tu kwani samaki huyo aliponyoka wakati mwingine na kurudi ziwani kuu; wakati mwingineo utumiaji wa nguvu ulihitajikana kabla ya kumshika Alikuwa mzito kwani alibebwa na watu wawili.

Lilikuwa jambo geni kwa sisi Wakikuyu kuamka asubuhi na kujiona tumezungukwa na maji ya rangi ya kijani kibichi yaliyotulia ambayo yalijaa mamba wenye njaa. Hakuna angaliyefikiria kutoroka na wakati mwingine tulianza kupotewa na imani ya kuona tena milima yetu ya buluu, ardhi nyekundu na mabonde yasiyohesabika. Mkuu wa Kampi alikuwa Mkanada aliyeitwa Kendal, ambaye tulimpa jina la "Karimanjaga" (mlima uchi) kwa sababu hakuvaa shati au vesti alipokuwa kisiwani. Hakutupiga lakini hatukuwa na urafiki kwa vile tulikataa kufanya kazi. Kabla ya sisi kufika huko Saiyusi, wafungiwa wengine walikuwa wanafanya kazi katika mashamba makubwa yaliyokuwa kisiwani hicho ambayo yalijaa mapapai, mihogo, mahindi, maharagwe na mboga za aina nyingi, zote ambazo zilikuwa zimechanganyikana. Baada ya muda mfupi, ili kuzuia wasije wakawa kama sisi, wafungiwa wengine wote isipokuwa thelathini ambao pia walijulikana kama "hadi-koa", walihamishwa tena. Nilifurahi nilipojua kuwa rafiki wa zamani kutoka Kihuri pande za Othaya, aliyeitwa James Thuku Mangothi, aliyekuja katika shamba la Tyron miaka mingi iliyopita na alimsemesha Kiingereza akanitia hamu ya elimu, alibaki nyuma.

Mkuu wa Kambi alituambia kuwa kwa vile hatukufanya kazi, chakula chetu kitapunguzwa. Wakati hatua hiyo ilivyochukuliwa, tuligomea chakula na wafungiwa wengine waliniambia nikamwone afisa huyo. Nilimwuliza alitumia sheria gani alipopunguza chakula chetu na nikamwuliza aniarifu kile kifungu cha sheria alichotumia. Hakuweza na alishtuka nilipomwambia kutoka kukumbuka kile kifungu cha sheria

kinachoeleza juu ya chakula cha chini ambacho kingepewa wafungiwa. Nilipokuwa Manyani mara ya pili, nilinunua kitabu juu ya Sheria katika Kambi za Wafungiwa (Detention Camp Regulations) kwa bei ya shilingi ishirini kutoka kwa Mkamba aliyekuwa akifanya kazi ya ukarani kwa askari katika hedikuota. Ingawa kilikuwa gali zaidi ya thamani yake, ilinilazimu niwe nacho na nilikifungia pamoja na pesa zangu katika koti langu. Nilimweleza Kendal kuwa hatukukusudia kufanya matata kwake lakini tulipenda turudishiwe kanuni yetu ya chakula na pia tupatiwe nafasi za utabibu mwema kwa vile kisiwa kilijaa inzi na mbu. Matakwa yetu hayo mawili yalikubaliwa.

Lakini Mkuu wa Jela (Commissioner of Prisons) alimwezesha afisa huyo aniweke katika chumba kidogo kwa muda wa siku 16 huko nikapewa chakula cha kuniadhibisha. Nilifanyiwa hivyo kwa sababu ilionekana kama ni mimi niliyeongoza juu ya kukataa kazi na ule mgomo wa njaa. Lakini kwa wakati huo, maisha yangu yalikuwa ya starehe kidogo kwani wale askari Wajaluo, ambao walitufanyia urafiki na kutuhurumia, walipendezwa kuniletea chakula zaidi baina ya kile walichopewa na wafungiwa waliokuwa wapishi na kwa hakika niliongeza uzito. Taabu yangu ilikuwa kuwa sikuwa na la kufanya wala cha kusoma bali mengi tu ya kufikiria. Wakati nilipokuwa chumbani mwangu, wale mia moja waliobaki huko Odiaga waliletwa na Robinson Mwangi alikuwa mmojawapo. Aliniambia kuwa hali ya mambo huko haikuwa mbaya sana lakini walikuwa wakipewa chakula kama mahabusu badala ya kanuni ya wafungiwa: walikuwa wakitazamia kuungana nasi hapo Saiyusi.

Mkuu wa Kambi alikuwa ametoa amri kwamba tufungiwe nyumba usiku na mchana kwa sababu tulikataa kufanya kazi. Tulipinga hatua hiyo kwa nguvu lakini hatukusikilizwa, na kwa hivyo siku moja baada ya chakula tulikataa kuingia ndani ya nyumba. Askari walituzunguka, wakatupiga na kutusukuma ndani ya nyumba. Tulikuwa tumekubaliana hapo mbeleni kwamba kama tukitendewa vile, tungeshindana nao, na ikiwa kuna haja tupigane nao. Mara tulijiweka tayari kwa sahani na mawe, na tukitumia sahani kama ngao, tuliwashambulia hao askari. Pamoja na hayo tulitumia fito za mbao zilizokuwa upande wa ndani wa seng'enge. Wakati Robinson na wenzake waliposikia vile vita vilikuwa vyaendelea, waliuvunja mlango wa nyumba waliofungiwa wakaja kutusaidia. Utupianaji wa sahani na mawe uliwaumiza wengi pande zote mbili lakini tuliwahi kuwafukuza hao askari kwa vile tulikuwa tumekasirika. Gad Kamau alikuwa mmojawao aliyejeruhiwa lakini alipata nafuu baadaye kidogo. Wakati huo tulisikia milio minne ya bunduki iliyopigwa na Kendal na huko tukamwona aja uwanjani wa vita akiwa peke yake. Kwa upole, alituuliza tuketi chini na akatuhesabu, halafu akatuambia turudi ndani ya

nyumba. Alikubali kuonana na ujumbe wetu asubuhi yake ili kusikiliza mateta yetu lakini hakupendelea mapigano tena.

Nilikwenda kumwona kama vile tulivyoagana na baada ya hivyo tulikubaliwa kutoka nje ya nyumba yetu kwa muda wa masaa fulani kila siku. Sote wawili tulijua kuwa kulazimishwa kukaa ndani ya nyumba hakukulingana na sheria. Baadaye niliandika barua kwa Chief Secretary juu ya tukio hilo, nikapeleka nakili yake kwa E. W. Mathu na W. W. W. Awori, ambao ndio walikuwa wajumbe Waafrika katika Legislative Council waliochaguliwa na Serikali wakati huo. Ingawa urafiki wetu na askari ulipunguka tangu mapigano hayo, walikuwako wengine walioendelea kuwa marafiki na nilipanga njia ya kuzituma barua hizo ambazo zilichukuliwa na bibi wa Mjaluo mmoja aliyekuwa akienda ruhusa (livu). Aliificha katika suruali yake ya ndani na sina shaka kwanza alizituma salama.

Taabu ya aina hii pia ilikuwa yaendelea katika kisiwa cha Mageta na tulipata habari hiyo kutoka kwa askari walioletwa Saiyusi kutoka huko. Hatukushangazwa na habari hiyo kwani kabla ya kuondoka Manyani, tulikuwa tumeagana kuwa tutakataa kufanya kazi po pote tulipopelekwa hata iweji. Kitendo hiki kilionekana kama silaha kali ya kuiaibisha Serikali na ya kusaidia mashujaa waliokuwa bado wakipigana msituni.

Serikali ilikata shauri kuileta timu ya Wazungu wa Special Branch kuchungulia matata haya. Walianza huko Mageta halafu wakaja Saiyusi ambako waliwaita arobaini na wawili baina yetu katika afisi yao. Hapo tuliulizwa mambo huko tukipigwa kisayansi kwa fimbo na makofi. Kwa vile walikuwako watano, hakuna wetu aliyeweza kujilinda ingawa nilijaribu kujilinda kwa nguvu kama nilivyoweza. Watano baina yetu walikubali kuunga Serikali mkono baada ya kutendewa vile lakini thelathini na saba walikataa. Thelathini na watano wa hawa walifungiwa nyumba ya pekee hali Robinson Mwangi nami tulifungiwa katika chumba kidogo pamoja. Shati zetu zilikuwa zimeraruliwa vibaya na miili yetu ilijeruhiwa pia. Huo ulikuwa usiku wa kukumbuka: hatukuwa na blanketi na ilikuwa baridi sana na kwa hivyo tulilala juu ya sakafu ya simiti, tukakaribiana pamoja ili kujaribu kupata joto, huku tukijifunika macho na vitambaa vilivyobaki. Wale mbu walionekana kama wenye kazi nyingi juu ya miili yetu na uchungu wa mwisho ulikuwa wa kujaribu kuzuilia mkojo kwani hatukupewa ndoo katika chumba chetu. Tuliona mwangaza wa jua chini ya mlango kwa furaha.

Siku iliyofuata, tulirudishwa Jela ya Odiaga ambako tuliungana na wengine kutoka kisiwa cha Mageta, tukawa kama mia nne sote. Zile nyororo zilifungiwa miguuni mwetu na wakati wa kwenda kula chakula zilifanya mlio kama wa kengele ya kanisa, kengele za machozi, zikililia kutaabishwa

kwa watu wetu. Katika Odiaga nilikutana na Joseph Kirira Karechu kwa mara ya kwanza ambaye tangu siku hiyo tumekuwa tukifanyizana kazi. Anayo akili na uwezo na mtu wa tabia njema. Sasa tulikuwa watatu pamoja na Robinson na tulikata shauri kujitoa kuwasaidia wenzetu waweze kuhifadhi uwananchi na imani yao. Askari walikuwa wasaidifu na tuliandika barua kwa Mkuu wa Jela tukalalamika juu ya ubaya wa chakula—kwani tulipewa nusu ya chakula—na askari aliipeleka barua baada ya kumhonga kwa shilingi tano.

Serikali haikuonekana kama ilijua ingetupeleka wapi wakati huo, lakini siku moja afisa wa Special Branch aliniambia kuwa "Serikali watakupeleka mahali penye joto sana panapoitwa Lodwar ili ukafe huko." Tuliwachekelea na matumaini yao kuwa watavunja roho zetu kwa njia hiyo. Wengine wetu tulijisikia kuwa tumepitia kwenye mambo mengi na kitu kingine kilionekana kidogo tu. Baada ya mwezi mmoja huko Odiaga, tulipelekwa uwanjani wa ndege wa Kisumu mnamo Agosti 11, 1956, tukifunganishwa wawili wawili kwa pingu. Mwenzangu alikuwa Kirori Motoku, mzee wa kupendeza aliyekuwa wa umri wa miaka sitini. Kirori alikuwa kama mwiba katika nyama ya Serikali katika wilaya ya Nyeri kwa miaka mingi: alikuwa mwananchi halisi, mfanyi biashara mashuhuri na kiongozi wa watu wake. Mwaka wa 1961, alifanywa kiongozi wa KANU katika sehemu yao huko Nyeri.

Tulikuwa tutasafiri kwa ndege za East African Airways hadi Lodwar, thelathini na watano wetu katika kila ndege, tukifunganishwa kila wawili kwa pingu isipokuwa mzee mmoja aliyeitwa Gathekya aliyefungwa peke yake. Gathekya alienda safari hiyo yote akijikunja, akilishikilia tumbo lake kwa kujikaza kabisa na alitetemeka kama mwenye ugonjwa. Alituambia baadaye kuwa alipoangalia nje ya dirisha, aliona mafuta yakimiminika kutoka kwa injini. Alijadiliana na moyo wake juu ya vile angefanya na akakata shauri angemwambia mwendeshaji wa ndege lakini kama mwendeshaji alifika kuangalia angewacha gurudumu la kuendesha na ndege ingeanguka. Kwa hivyo alinyamaza, akangojea mfyatuko usiozuilika, na akasali.

Baada ya muda mfupi, rangi nyekundu ilionekana mbele yetu na sauti ikasikika ikisema kwa Kiingereza kwa ngurumo: "Wangwana, twaelekea kuvuka Ziwa Victoria. Mtaziona kanda za kulinda maisha chini ya viti vyenu." Ni wachache tu wetu waliofahamu Kiingereza, na wale tuliojua Kiingereza tulipitisha neno na hao wasafiri waliofungwa pamoja kwa pingu walijaribu kwa wasiwasi mwingi kutafuta hizo kanda za kulinda maisha, kila mmoja akivuta kwa upande mwingine. Gathekya sasa alikunjuka, akiangalia mafuta yake, akiwa amesahau juu ya koti ambalo ingawaje hangeweza kulifikia. Wale wengine wetu tulijiuliza kama kunaye angeweza

kutufungua pingu kama ndege ililazimika kuanguka kwa haraka. Tulinusa vifo kwa safari yetu iliyobaki.

Wale waliokuwa katika ndege yetu walikuwa na bahati njema: tulifika saa za jioni na kwa hivyo tulichelewa kukaribishwa na kikundi kilichotarajiwa kwa wale waliofika mapema. Joseph Kirira aliniambia kuwa walilazimishwa kukimbia wakibeba karai zilizojazwa mawe, bila sababu yo yote, na kuwa walipigwa vibaya na polisi wa Kiturkana hata mfungiwa mmoja aliyeitwa Ngugi Mwarari, alizimia roho akapelekwa dispensari ya kambi. Jioni hiyo hiyo, Robinson, Joseph na mimi, tuliandika barua kwa Mkuu wa Kambi, aliyeitwa Buxton, tukamtaka aje kuzungumza jambo hilo nasi asubuhi iliyofuata. Alifika na akawaita wafungiwa wote pamoja na kuwahutubia kama ifuatavyo kwa Kiswahili:

"Ninyi ni hadi-koa waovu kabisa wa Mau Mau ambao mlitoka Saiyusi na Mageta ambako mlikataa kufanya kazi. Hapa ni lazima kufanya kazi na mkipenda au msipende mtafanya kazi na hii ni amri ambayo ni wajibu wangu kuona kuwa imetiiwa. Kama mkikataa, mtaona yale yatakayofanyika." Halafu aliketi chini naye Gathogo Mwitumi alisimama akamwuliza amwalike D.C. wa wilaya hiyo ili tujadiliane mambo haya pamoja. Buxton aliruka mara moja na akamjibu kwa ukali: "Ninyi watu—ninataka mfahamu kwa mara ya kwanza na ya mwisho kuwa mimi ndiye Afisa wa Kampi na Afisa wa "Wokozi". Mimi ndiye Gavana na D.C. wa Lodwar. Mimi ndiye Mungu wa Lodwar. Mimi niko tayari kabisa kupambana nanyi nyote kwa njia yo yote ninayofikiri yafaa mpaka mtii amri." Gathogo hapo akamwuliza alikuwa anatumia sheria gani ambayo ingetulazimisha kufanya kazi. Buxton alimjibu mara moja akasema: "Sahau sheria zote ambazo mmekuwa mkitumia kama silaha katika Saiyusi na Mageta. Serikali si pumbavu. Neno langu ni Sheria ya Lodwar na ni lazima mfanye kazi. Hayo tu." Mara hiyo aligeuka akaenda zake. Nilimheshimu afisa huyo kwa maneno yake makali na yasiyo ya kusikilizana yaliyokuwa ya mtu aliyenyoka, wa kweli na aliyekuwa akifanya wajibu wake. Tulimpenda mtu wa aina hii, ambaye alisema vile alivyoamini na afanyaye vile asemavyo, na hii ndiyo sababu wanasiasa Waafrika walio wengi hupendelea Briggs na Cavendish-Bentinck kuliko Blundell na Havelock. Labda sababu yake ni kuwa ni rahisi kukata karatasi ngumu kuliko kukata mto wa kulalia.

Tulirudi majumbani mwetu huko tukishangaa kwa nini mtu kama huyo alisema kwa ukali namna hiyo. Wafungiwa wengi walinijia chumbani mwangu Nambari 13, na tukaendelea kujadiliana juu ya hatua ambazo tungechukua. Wakati huo, kulikuwako na wafungiwa wengine ambao walitoka Athi River na walikuwa wakifanya kazi. (Baina ya hawa alikuwa Jeremiah Kirumwa Keiru, ambaye amekuwa akifanya biashara nami tangu alipofunguliwa). Walipendelea kufanya kazi. Wengine wengi

walipendelea kwa nguvu tusifanye kazi isipokuwa ile kazi ya kawaida ya kusafisha kampi. Wakati huo nilikuwa ninafikiri juu ya matamshi ya Mkuu wa Kampi na nikaona kuwa yeye si mtu aliyesema mambo asiyoweza kufanya. Pamoja na hayo nilifikiria kilikuwako kitu kilichotendeka ambacho kilimpa nguvu aina hiyo. Ni desturi baina ya watu wetu kwa viongozi kutoa maoni ya mwisho wakati kama huo na ni juu yao kuzungumza juu ya yote yaliyoletwa na kutoa maoni yao. Kwa hivyo walipomaliza niliwahutubia kama ifuatavyo: "Watu wangu, nimekuwa kiongozi wenu sasa kwa miaka mingi na wakati huo wote nimekuwa nikifanya cho chote kuwaweka nje ya hatari. Sasa tumefikia taabu ya mwisho katika hali hii. Hivi ni vita kamili na tusipotumia akili tutapoteza." Hapo nikawaeleza juu ya hadithi ya Napoleon Bonaparte, ambaye alishinda Ulaya halafu akatuma majeshi yake hadi Urussi, ambako adui alirudi nyuma, huku akamnasa akimtumia "Jemedari Baridi" mpaka wengi wa majeshi yake walikufa kwa njaa, baridi kali na kukosa nyumba. Halafu nikawakumbusha vile Mkuu wa Kambi alivyosema juu ya sisi kutumia sheria kama silaha katika Saiyusi na Mageta na vile alisema kuwa Serikali haikuwa pumbavu. "Hii, katika maoni yangu ni kuwa sheria imegeuzwa katika Kenya au katika Afisi ya Makoloni ili wafungiwa walazimishwe kufanya kazi. Kama mjuavyo, kwa muda uliyopita tumekuwa tukijilinda katika haki zetu ndani ya sheria. Tumejaribu sana kama tuwezavyo kutofanya kisicholingana na sheria na hii ndiyo ilikuwa nguvu yetu. Ni wajibu wangu kuwaambieni kuwa silaha yetu imeondolewa na tutajiumiza kama tukiendelea kukataa kufanya kazi bila silaha. Kwa hivyo sasa sisi sote tukubaliane kufanya kazi na kila mtu atumie ubongo wake kufumbua njia nyingine ambayo tungetumia kupigania haki zetu na Uhuru."

Baada ya mazungumzo mafupi zaidi juu ya maoni yangu, sote tulikubaliana kuanza kazi Jumatatu tarehe 13 Agosti, 1956. Asubuhi sana siku hiyo, bila kujua kama tumekubali kufanya kazi, Mkuu wa Kampi alikuwa na shughuli nyingi akiwapanga askari, akawapa bunduki na fimbo. Tuligundua baadaye kuwa D.O. wa Lodwar alikuwa ameficha kikundi cha askari wa polisi 120 na askari kanga arobaini wa Kiturkana, ambao wote walikuwa tayari kutulazimisha kufanya kazi kama tuliendelea kukataa. Walipotuona tukienda nje bila kulazimishwa wala matata, walifurahi bila kiasi kwani walifikiri walifanya ushindi mkuu. Lakini vile walivyofanya ni kutufanya tugeuze silaha zetu, na fikira zangu zilikuwa zafikiria kutumia miujiza ya "kwenda pole", yaani kutembea pole pole wakati wa kwenda kazini, na miujiza mingineyo katika sheria yetu. Wenzangu walifurahi sana kwa vile walikubaliana na shauri langu.

Lodwar iko kama maili arobaini kutoka Ziwa Rudolf katika nchi kavu yenye miiba na vumbi kaskazini ya jimbo la Kaskazini la Kenya.

Iko maili 200 kutoka Kitale na maili 450 kutoka Nairobi. Kama vile ilivyokuwa Kowop, Lodwar ilizungukwa na vilima vikavu karibu na ukingo wa mto Turkwell ambao hukauka kabisa wakati wa joto lakini ambao huwa mto mkubwa wenye mafuriko wakati wa mvua. Jua huanza kukaanga kila kitu kutokea thenashara asubuhi na usiku hauwezi kupowesha joto la mchana kabisa kabla ya joto jingine kuanza asubuhi yake. Hakuna anayeweza kujifunika kwa blanketi saa za usiku. Wanaoishi huko ni Waturkana, na maisha yao na ya wanyama wao ni magumu kabisa. Wengi wao hutembea uchi na hula nyama na kunywa maziwa ya ng'ombe wao. Wanatumia sana mti unaoitwa "mukoma", ambao hukua kutoka futi kumi na tano hadi ishirini na unaonekana kama mpapai. Waturkana hula matunda yake, ambayo huwa kiasi cha matunda ya kawaida, na ambayo wakati mwingine huyaponda kuwa donge wanazochanganya na damu ya ng'ombe au mbuzi, damu ambayo hukamuliwa kutoka shingoni kwa kuwachoma hao ng'ombe au mbuzi kwa mshale wa kazi hiyo. Pia wanafanya pombe kutokana na matunda haya na hutumia majani ya "mkoma" kwa kutengeneza vikapu, masanduku na mikeka. Tuliyatumia kwa kuezeka nyumba zetu lakini Waturkana hawakufanya vile. Baada ya muda mfupi, niliweza kuvuma vitu hivyo, na nilijiongezea pesa kwa kuviuzia askari kwa bei ya rejareja kutoka shilingi tano hadi shilingi ishirini. Tulitarajia kumtumia Mzee Jomo Kenyatta, Kiongozi mpendwa wetu, sanduku moja na pia nilimtengenezea kofia kubwa ambayo huonekana naye katika picha zake za zamani za wakati huo katika Maralal. Wakati huo alikuwa Lokitaung na tulikuwa tukiandikiana barua tukiwatumia askari waliohamishwa baina ya kambi hizo mbili.

Kambi yenyewe ilikuwa jela ambayo ilijengwa kuwafungia mahabusu wa Mau Mau ambao walipelekwa huko kujenga kiwanja cha ndege. Ilikuwa eneo mlamba lililozungushiwa seng'enge mara mbili na ambalo lilipasuliwa katikati na "*veranda*" ya upana wa futi nne. Kila upande wa "*veranda*" uligawanywa katika vyumba vitatu ambavyo vilizungushwa seng'enge pia. Ndani ya kila chumba ilikuwako nyumba ya mawe iliyoezekwa kwa mabati. Nyumba hizo ziligawanywa mara nne. Tulijigawanya na kama kawaida marafiki walipendelea kukaa pamoja. Nilikuwa katika Nambari 13 na mara nyingi tulikuwa watu kumi na watatu ndani yake. Hapo nje palikuwako majiko na mahali pa kutengenezea nguo zilizoraruka kwa cherehani na ndipo Kirori Motoku aliwashia mataa. Lodwar ndipo tu tulipatiwa taa. Mwendo mfupi kutoka jikoni vilikuwako vyumba vidogo vya kutengwa.

Joseph Kirira na mimi tulilalia kitanda kimoja kwa muda wa miezi kumi na minne tuliyoishi katika Lodwar. Iko methali ya Kiswahili isemayo: "Usimwamini mtu ikiwa hamjamaliza gunia la chumvi pamoja." Mimi

na Joseph tumeanza juu ya gunia la pili kwani yeye ni mwenzangu ninaye-mwamini katika siasa na biashara yetu.

Katika Lodwar, tulifanya mpango wa wafungiwa ambao tulikuwa hatujafanya penginepo tulipofungiwa. Robinson Mwangi alichaguliwa kiongozi wa kambi naye Joseph Kirira akawa mwenye-kiti wa komiti ya kambi.

Kila sehemu ilijichagulia kiongozi wake aliyepokea amri kutoka kwa kiongozi wa kampi kwa kufanyiza yaliyokubaliwa. Komiti ya kambi ilikuwa na wakili kutoka kila sehemu, wanachama wote wakawa ishirini na wawili pamoja na kiongozi wa kambi, msaidizi wake na mimi kama mwanachama wa elimu na mshauri wa siasa. Komiti hiyo ilikutana mara moja kila wiki, lakini wakati mwingine ilifanya mkutano wa haraka kama mwenye-kiti alitaka au katibu wake (Maina Muhiki, kutoka Fort Hall, mmoja wa hao ishirini na wawili, na ambaye sasa anafanya kazi ya karani wa kampuni moja ijulikanayo duniani ya kujenga katika Nairobi), wakisha-uriana na kiongozi wa kambi. Hapakuwa na haja ya sehemu zenyewe kuwa na komiti zao kwa vile walikuwa wachache na vile hawakuweza kufanya mikutano ya kuwachagua wajumbe au wapishi wao. Tuliweka miniti za mikutano ya komiti yetu, na tulichoma kitabu hicho tulipokuwa tukiondoka huko. Kiongozi wa kambi ndiye alikuwa mtawala wa hukumu za komiti na wao ndio walimpa madaraka kufanya kama alivyofanya. Lakini baina ya mikutano ya komiti, alikuwa na uwezo wa mwisho. Wakati huo wote tulipokuwa Lodwar, Robinson hakufanya cho chote kisichoipendeza komiti na alikuwa kiongozi wa kupendwa. Msaidizi wake alikuwa John Giathi wa Kiambu, ambaye sasa anafanya kazi ya ukarani kwa kampuni ya East African Breweries. Kazi yangu ilikuwa ile ya kawaida kuandika barua kwa Serikali na kwa wajumbe wa Parliament wa Labour huko Uingereza na kuwafundisha wenzangu juu ya kusoma na kuandika. Kila sehemu ilitoa mpishi mmoja ambayo ni kazi iliyowapendeza wengi kwa wema iliyowapatia. Lakini hatukumchagua mtu tu kwa kupenda kwake—kila sehemu ilimchagua mpishi kwa kidemokirasi. Nambari 13 ilimchagua Wambugu Wachira ambaye alitutumikia vizuri.

Tulikuwa na mahali pa vitabu katika Lodwar ambavyo vililetwa na Wizara ya Maendeleo. Havikuwa vitabu vya maana kwa vile vilikuwa vimechaguliwa kwa uangalifu mwingi kabla ya kukubaliwa huko na hakuna kilichokubaliwa ikiwa kilihusu siasa. Lakini hata hivyo, ilipendeza kuona maandishi tena na wakati mwingine tulikipata kitabu cha historia juu ya biashara ya utumwa ambacho ni lazima kilipita bila kuonekana. Vitabu hivyo viliwekwa katika sehemu yetu na mwangalizi wake alikuwa Wachira Kariga ambaye alishauri juu ya kile kilichomfaa kusoma aliyetaka kitabu. Kutokuwako na vitabu vya siasa kulitukasirisha lakini kwa vile

tulijua kuwa si kila mmoja ambaye angekuwa mwanasiasa, tulipanga masomo kutoka darasa la kwanza hadi tisa ili kila mtu, hata akiwa hajui kusoma kamwe, aweze kuanza kupata elimu huko. Hatukuwa na walimu waliohitimu ambao wangeweza kuendesha mpango huo kwa hivyo tulipanga kuwa wale waliokuwa wa darasa la 3, 4 na 5 watumie wakati wao wakifundisha wale wa madarasa ya 1 na 2. Wale waliokuwa wa darasa 5 na 7 wawe wakisomesha madarasa 2, 3 na 4. Mimi nilifundisha darasa 8 na 9 ambazo zilikuwa za wale ambao walikuwa wamekamilisha masomo ya shule ya kati. Wanafunzi wetu walifanya kazi kwa bidii na ninajivunia sana kuona leo kuwa baina ya wanafunzi wetu wa siku hizo wako wengine wanaoweza kuweka hesabu za biashara na wengine sasa ni walimu wakiwafundisha viongozi na raia wa kesho. Sitasahau jitihadi iliyoonyeshwa na mzee mmoja aliyeitwa Kimana Wachuku aliyetoka Fort Hall, ambaye alikuwa wa umri wa miaka sabini na mitano, aliyehudhuria Standard I bila kuachisha ili kujifunza kusoma na kuandika. Uwezo wake ulikuwa hivi ati punde alikubaliwa kuingia darasa la 2. Wakati mwingine tulimzunguka na kumsikiliza akituhadithia juu ya historia ya nchi yetu kutokana na ujuzi wake na kwa vile yeye alizaliwa kabla ya Wazungu kuingia hapa, tulijifunza mengi juu ya makosa yaliyofanywa na Serikali kwa miaka iliyopita makosa ambayo yalituingiza katika hali tulivyokuwa nayo. Wafungiwa wengi walitiwa moyo na masomo hayo na hata sasa, baada ya kufunguliwa, wanaendelea kujifunza. Katika Lodwar, tulianzisha skuli ya kwanza ya bure katika Afrika Mashariki.

Komiti ya Kambi ilitengeneza masharti haya, ambayo yaliongoza tabia zetu zaidi ya amri za Serikali:

1. Hakuna mfungiwa angelipigana na mfungiwa mwingine, ndani au nje ya kambi;
2. Hakuna mfungiwa aliyekubaliwa kulala na bibi wa Kiturkana au na bibi wa wafanyi kazi wa kambi;
3. Hakuna aliyeruhusiwa kumtukana au kumwonyesha 'chuki mfungiwa mwingine;
4. Hakuna aliyekubaliwa kutema mate au kukojoa ndani ya kambi au kuiharibu kwa njia nyingine yo yote.
5. Hakuna aliyeruhusiwa kunywa tembo ndani au nje ya kambi. Hakuna aliyekubaliwa kuvuta bhangi nje au ndani ya kambi.
6. Hakuna aliyekubaliwa kumwibia mfungiwa mwingine au askari. Hakuna aliyekubaliwa kuchukua kitabu daima.
7. Hakuna aliyekubaliwa kutotii amri ya kiongozi wa sehemu ya kuondoa ndoo za vyoo, hata ikiwa ni Jumapili au siku nyingine ya ruhusa ya faragha.

8. Hakuna aliyeruhusiwa kujichagulia kazi aliyoifikiria kuwa rahisi na ya kupumzika. Wafungiwa wengine ni lazima wakubaliane.
9. Wakati wafungiwa wengi wanapofanya kazi, hakuna aliyekubaliwa kujifanya mgonjwa.
10. Hakuna aliyeruhusiwa kumtukana mkuu wa kambi, askari au wageni kutoka nje pasipo na sababu ya kutosha au bila ruhusa ya kiongozi wa kambi.
11. Hakuna aliyekubaliwa kuwadanganya wafungiwa wengine.
12. Hakuna aliyeruhusiwa kupita mstari wakati wa kupokea chakula.

Hizo ndizo zilikuwa Sheria Kumi na Mbili za Lodwar na zilithibitishwa na watu wote katika mkutano wa faraghani. Kuvunja mojawapo kulimfanya mfungiwa kuhukumiwa na hakimu wa kambi, ambaye wakati huo alikuwa Wakamore aliyetoka Kiambu. Alisaidiwa na wazee wengine watano, mmoja kutoka kila wilaya za Jimbo la Kati, isipokuwa Kiambu na Meru, pamoja na mjumbe mmoja kutoka Jimbo la Nyanza. Aliyepeleka mashtaka mara nyingi alikuwa Paul Muchemi, ambaye baba yake (Johanna Kunyiha) alikuwa Rais wa mojawapo za Korti za Serikali katika wilaya ya Nyeri, na siwezi kukumbuka kesi moja iliyoletwa ambayo haikufaulu. Komiti ilimchagua Nguru Ndirangu kuwa polisi wa kampi (upande wetu). Ulikuwa wajibu wake kuwa macho na kujulisha kiongozi wa kambi ikiwa fulani alivunja sheria, naye alifanya kazi barabara. Sasa amefunguliwa na ni mkulima na kiongozi wa K.A.N.U. katika sehemu ya kwao. Mpango wetu ulifanya kazi sawasawa na wote waliheshimu sheria yetu na wakaheshimiana wao wenyewe. Korti yetu iliwezeshwa kupitisha hukumu ambazo ziliendeshwa bila kukawia isipokuwa mtu alitaka kufanya rufani. Ilikuwako Korti ya Rufani iliyokuwa ya wazee watano waliochaguliwa kutoka Embu, Fort Hall, Kiambu na Nyeri, na pia kutoka Jimbo la Nyanza. Palikuwako na rufani chache sana. Korti ilizoea kukutana saa za alfajiri katika mojawapo ya vyumba. Korti ilikuwa imefunguliwa kwa wote lakini kwa vile nyumba zilikuwa ndogo na kazi ilikuwa nyingi, ni wachache tu waliohudhuria. Adhabu ya juu kwa kila kosa ilikuwa tofauti nayo ilikuwa namna hii:

Sheria 1 *na* 2. Kubeba ndoo thelathini na tatu za maji za kujaza matangi ya nyumba au kutolewa makende. Hiyo ya mwisho ilifanyiwa mtu mmoja tu, kijana mmoja kutoka Embu ambaye alikutwa akimsemeza na kumchekesha mpenzi wa askari.

(Msomaji aweza kufikiri kuwa kubeba ndoo thelathini na mbili za maji kuwa kitu rahisi, lakini wakati uliowezekana kufanya hivyo ulikuwa baina ya saa kumi na thenashara wakati joto lilipokuwa limepunguka. Tangi la maji lilikuwa nje ya kampi kama hatua mia nne na maji yaliletwa

pale na mfereji kutoka mto Turkwell. Maji yalitoka pole pole, na mtu angekuwa na bahati kuwahi kubeba zaidi ya ndoo nne jioni moja. Ninakumbuka hofu nilioiona usoni wa maskini mmoja ambaye aliteleza akaipindua moja ya ndoo alizobeba na hali hiyo ikaitikisa ile nyingine. Ndoo zilizohesabiwa ni zile tu zilizokuwa ndani ya pipa—zile zilizokuwa "kichakani" hazikuhesabiwa).

Sheria 3. Kujaza mapipa ya jiko kwa maji kwa siku mbili. (Hii ilikuwa adabu kali).

Sheria 4 *na* 7. Kuondoa na kusafisha ndoo za vyoo kwa siku nne.

Sheria 5 *na* 6. Kuchota ndoo ishirini na sita za maji.

Sheria 8. Kuchota ndoo ishirini na nane za maji na kuzunguka nyumba mara nane kwa magoti. (Hii iliumiza sana).

Sheria 9. Kukamilisha mazunguko kumi kwa magoti na kuanza kazi mara moja isipokuwa korti itosheke kuwa mtu alikuwa mgonjwa.

Sheria 10. Kukamilisha mazunguko kumi kwa magoti na kuchota ndoo ishirini na nane za maji au kuondolewa makende.

Sheria 11. Kuchota ndoo kumi na mbili za maji na kukamilisha mazunguko manane kwa magoti.

Sheria 12. Kuhukumiwa na kiongozi wa jikoni kuwa mkosaji angoje mpaka wale wengine walipomaliza kupokea chakula. Korti ambayo iliketi baadaye iliweza kumhukumia kuzunguka mara kumi kwa magoti na kuchota ndoo kumi na nne za maji. Kiongozi wa jikoni alichaguliwa na komiti ya kambi, ambayo yeye hakuwa mwanachama ingawa wakati mwingineo alialikwa kwa sababu maalum.

Hukumu za korti zilitangazwa katika kila chumba. Ili kila mmoja ajue aina ya kosa, aliyekosa na alivyohukumiwa. Palikuwa na kesi chache sana kwani wafungiwa walitii sheria na wakajihadhari vyema sana.

Yasemwa penginepo kuwa wafungiwa walimwomba Shetani kwa njia za kishetani na kishenzi. Sasa ni wakati ukweli utambulishwe na kwa vile ilikuwa kazi yangu kuongoza sala katika Lodwar kila asubuhi katika chumba chetu, nitakuelezeni vile sala zilivyoongozwa. Mara nyingi tuliomba tukiketi chini, ingawa wakati mwingineo (kama vile siku ya ukumbusho wa kukamatwa kwa Jomo Kenyatta, Oktoba 20, au wakati wa kesi ya siasa) tulisimama. Wengine wetu walikuwa Wakristo lakini wengine hawakuwa: tuliomba sote pamoja. Tulielekea upande wa Mlima Kenya na tukatemea mikono yetu. Katika nchi yetu, tunatemea mikono mate kabla ya kuamkuana na mwengine ambaye ni lazima kuamkuliwa kwa heshima. Halafu tuliinua mikono tukaipanua kulingana na vichwa vyetu na mwenye kuongoza sala angeimba:

Ewe Mungu, aliye Mwumbaji na Mvunjaji wa vizazi vya Adam;
Ewe Mungu, uliyetupa hii nchi ya Afrika;

Sisi ambao tumefanya dhambi twaomba mbele yako, kwa unyenyekevu na kwa makini,
Ati usikilize vilio vya watoto wako,
Ambao sasa wanateseka katika jangwa la moto wa jua,
Wale ambao uliwapa nchi hii ya Kirinyaga (Mt. Kenya),
Nchi hii ambayo inateswa na kabila la Watu Weupe.

Ewe Mungu, daima usikubali urithi huu uliotuachia,
Ukamatwe na wageni;
Mungu wetu, tunayo imani kuwa utatuunga mkono.
Kama vile ulimpa Mtu Mweupe nchi ya Ulaya
Kama urithi wake,
Vile vile uliweka maji kama mpaka baina yetu.
Kwa vile hatuoni wivu kwa ajili ya nchi au vitu vyao,
Ewe Mtukufu, ambaye unaishi vileleni vya Kirinyaga,
Wasaidie kufahamu mambo hayo watuachie urithi wetu.
Msaidie Kiongozi wetu, Kenyatta, na uwasaidie viongozi wote wengine wa Afrika,
Ambao wanajikaza kutuokoa kutoka minyororo ya utumwa,
Mashariki na Magharibi, kutoka Kaskazini na Kusini.

Wasaidie wote walio wagonjwa katika hospitali na wale walioumizwa misituni na hawawezi kupata dawa,
Wasaidie watoto wasio na wazazi na bibi waliopotelewa na mabwana zao, wasaidie waliojeruhiwa po pote walipo.
Ewe Mtukufu, harakisha mwisho wa wakati huu wa damu ambayo yamwagika kama mto ndani ya nchi yetu,
Na ulete amani na masikilizano katika nchi yetu.

Ewe Mtukufu, fanya roho zetu zikukumbuke wewe kila wakati,
Fanya moyo wetu ushikamane kama njia ndani ya shimo la panya,
Uwafanye Waafrika waseme kwa sauti moja,
Utuondolee mateso na maumivu yote.

Wageuze, Ewe Mungu, wale wanaotuchukia ili wawe marafiki zetu.
Harakisha Uhuru wa Waafrika.

Tuokoe kutoka utumwani tuliomo
Ewe Mungu, hatukusudii kukuamuru utufanyie mambo hayo,
Lakini twakusihi kwa makini,
Mwenyezi, ajabu kuliko nguvu za ulimwengu,
Ewe Mungu ambaye huwako na huishi daima,
Twakuomba hivyo, tukiwakumbuka wazazi wetu

Gikuyu na Mumbi ambao uliwaweka chini ya mlima Kirinyaga,
Ili wavune matunda ya nchi hii.
Twaweka imani yetu kwako wewe, Ewe Mungu
Ambaye huishi milele na milele.
Mungu na atukuzwe,
Mungu na atukuzwe,
Mungu na atukuzwe.

Kazi tuliyofanya huko ilikuwa ya kuvunja na kubeba mawe ya kujenga hospitali ya Lodwar wakati ambao wengine wetu walienda pamoja na Idara ya Maji kusaidia kufyeka mahali ilipokuwa ikitafuta maji. Ingawa kwanza tuliiona kazi hiyo kuwa ngumu na isiyo na faida, tulifurahi sana tuliposikia kuwa Waturkana wengi na Mzee Jomo Kenyatta walitibiwa katika hospitali yetu. Siku moja, watatu wa wale waliosaidia kufyeka —Cornelius Gathungu, Kibocho na Kibaki, walitaka kutoroka. Kwa kawaida ye yote aliyekusudia kutoroka angeomba ruhusa ya komiti ya kambi ili tujitayarishe kwa yale yangefuata, lakini hawa watatu hawakue fanya vile. Mimi binafsi sikukusudia kamwe juu ya kutoroka kwa vilnilifikiria kuwa mahali pangu ni pa wale wasiojua kusoma katika kambi, ambao walikuwa wakipigania uhuru kwa nguvu kama wale waliokuwa nje.

Katika Manyani, kutoroka kulikuwa alama ya siku kadhaa za kutendewa kinyama kwa wale waliohusika. Lakini tulishangazwa wakati Buxton alifika kutuona katika kambi na huko alikuwa akicheka na kusema "Kunao watatu wenu ambao wametoroka. Mtaona kuwa Serikali inao mkono mrefu. Ninawahakikishieni kuwa hawatavukia wilaya nyingine kabla hawajauawa au kukamatwa na kurudishwa hapa." Nilianza kukisia ukweli —ni ile hadithi ya Kowop tena: unga wa mahindi na chai kutolewa kwa ajili ya kichwa cha mfungiwa. Buxton alisema kweli kwani walikamatwa wote na kurudishwa katika kambi kabla ya saa sita za usiku siku hiyo hiyo. Vichwa vyao ndivyo vingalirudishwa kama chifu mmoja Mturkana hakupinga askari wake na kuwashauri wawarudishe wakiwa hai kwani hiyo ingewaongezea fungu lao la zawadi ya chakula. Zawadi walizopewa zilikatwa kutoka chakula chetu ingawa walipewa mchele pia ambao ulitoka mahali pengine kwa vile sisi hatukupewa mchele. Watoro hao watatu walihukumiwa kufungwa miezi sita kifungo ambacho kulingana na hali wangaliopambana nayo mikononi ya Waturkana kilikuwa cha ukarimu. Tukio hilo liliwatia moyo wale waliokuwa wakifikiria kufanya hivyo. Baadaye, Cornelius alifungwa miaka saba mwaka wa 1961 kwa kuwa mwanachama wa Jeshi la Uhuru wa Ardhi, Kibocho anafanya kazi dukani Nairobi na Kibaki ni mwanasiasa katika Fort Hall.

Tulipokubali kufanya kazi kwa vile tulikisia kuwa sheria ilikuwa imegeuzwa, tulikata shauri kutopokea pesa kwa ajili ya siku tulizofanya

kazi. Hatua hiyo yaweza kuonekana kama ya kijinga lakini ilikuwa muhimu katika hali yetu. Tulikusudia kutii amri za Serikali ilipowezekana. Sheria ilikuwa imegeuzwa na ilitulazimisha kufanya kazi. Sheria hiyo ilisema kuwa tulipwe pesa kwa kazi tuliyofanya. Haikusema ati ni lazima tupokee pesa hizo. Sasa tulikuwa wafungiwa tu na hatukuhukumiwa mbele ya korti yo yote; tulikuwa mahabusu wa siasa. Hatukufikiria kuwa mahabusu wa siasa wangelazimishwa kufanya kazi na Serikali yo yote iliyofanya vile ilikuwa ikifanya kinyume cha Haki za Binadamu, na katika maoni yetu, ilikuwa yatufanya watumwa. Kupokea pesa kungemfanya mtu wa nje afikiri kuwa tunakubaliana na maongozi ya sheria hiyo. Kwa hivyo tulimwambia Mkuu wa kambi kuwa ingawa tutatii sheria hiyo, hatutakubali mshahara. Tutafanya kazi kama watumwa. Hatukutumaini ataweza kufahamu hali yetu na hakufahamu. Barua zilizoonyesha kutofahamikiana huko zilipitia zile njia za kawaida.

Hali yetu ilibahatiwa kwa njia nyingine. Kama tulikataa pesa, Serikali haingetulazimisha kufanya kazi kwa nguvu. Ndipo nikaishauri komiti ya kambi tuandike barua kwa Serikali na Mkuu wa Jela tumweleze maoni yetu na kwamba wale waliopendelea kufanya kazi kama watumwa watie sahihi zao katika barua hiyo. Tulikubaliana na katika wafungiwa mia nne na ishirini na wawili katika kambi hiyo, zaidi ya mia nne walitia sahihi zao. Wachache hawakuweka sahihi lakini sikujua sababu yake, lakini ni watano tu ambao walikuwa wakipokea pesa. Tulituma nakili moja kwa njia ile yetu ya kawaida lakini tukafikiria kupitishia ile ya Serikali kwa Mkuu wa Kambi. Tulingojea matokeo yake, tukafanya kazi pole pole na bila kupigwa na askari. Wakati huo tuliona maongezeko katika chakula chetu. Hali ya utulivu ilitufikia katika kambi na tulijiona kama wenye furaha kidogo.

Mkuu wa Jela, Lewis, alitembelea kambi na akatueleza juu ya sheria hiyo mpya iliyotulazimisha kufanya kazi. Tulimwuliza maswali kadhaa na akatujibu kuwa tukipenda au tusipopenda, tutalipwa pesa hizo wakati wa kufunguliwa. Hata hivyo, tulikaa kama tulivyokata shauri hapo mbeleni. Baada ya muda mfupi, Buxton alienda livu. Aliyekuja badala yake alikuwa mtu wa tabia kinyume chake kabisa. Alisema kuwa kila mmoja ilimlazimu kufanya kazi, hata wagonjwa na viwete, na alizoea kuzunguka katika vyumba vyetu, tendo ambalo Buxton hakutenda, na aliposema na sisi alikuwa na sauti ya kukasirika, na uchungu ulijaza matamshi yake. Tulimdharau hivi ati tulituma barua ya siri kwa wakuu wake, kitu ambacho hatungemfanyia Buxton. Alipovumbua vile tulivyomtendea, alikasirika zaidi na hali ya kambi ikawa isiyo ya kupendeza au ya utulivu mpaka wakati tulipotembelewa na komiti ya International Red Cross kutoka Geneva, iliyoongozwa na Phillipe Junod. Tuliwachagua wajumbe watano

baina ya wana-komiti yetu ili waonane nao. Nilikuwa msemaji wao na nilijisikia mwema baada ya kumwaga ubaya na shida zetu ambazo tulipambana nazo. Junod alikuwa mtu mjanja na mwenye kimya na alisikiliza mateta yetu kwa makini. Tulimpa jina la Kikuyu la "Muthuri wa Itathi". Hilo ni jina la heshima kubwa ambalo hupewa mzee (muthuuri) ambaye huhukumu mambo kwa amani, bila wasiwasi na bila mapendeleo; "Itathi" ni tawi la mti ambalo hutumiwa na wazee kwa kuwafukuza inzi na mti huo hutumiwa kama fimbo za kuchunga mbuzi au ng'ombe. Alikuwa mtu mwema kabisa. Baada ya matembezi yao hali ya mambo ilikuwa njema kwa miezi mitatu iliyofuata. Lilikuwa jambo ligeni vile mambo yalirudi nyuma kama yalivyokuwa baada ya kuwa mazuri kwa muda uliofuata matembezi ya komiti. Labda hatua ingaliyofaa ni ya komiti kukaa humo daima ingawa ninafikiri kwa vile Hali ya Hatari ilivyokuwa katika Kenya, wangeambukizwa kuwa kama Wazungu wengine: uovu huo uliambukiza kwa njia kubwa.

Hali yetu iliharakishwa kuwa baya na kufika kwa msaidizi mpya wa Mkuu wa Kambi aliyeitwa Mansfield ambaye alikuwa mbaya kama mkubwa wake, na basi hapo kukawa wabaya wawili na hali ya mambo ilielekea kuwa chungu. Tulimpa jina la *Kamao* ambalo ni jina la kikombe kidogo cha jela kwa vile alikuwa mfupi mwenye urefu wa futi nne na inchi nane na mwili mpana kama wa ndovu. Alianza kututesa, alitupiga wakati wa kazi na akapunguza chakula chetu kwa nusu. Vile siku moja tulikataa kwenda kazini mpaka arudishe chakula chetu na akubali kuacha kututesa. Alikasirika aliposikia hivyo na akaongeza kuwa alitupa muda wa dakika tano za kuondoka nje: kama tulikataa, angepiga firimbi na askari wangefika kutulazimisha tuondoke. Baada ya dakika tatu alirudi na akasema: "Mbili: (akangojea) zinabaki dakika (akangojea) mbili." Alionekana mjinga hivi hatukukosa kumwonea huruma: si jambo la kupendeza kungojea onyo. Wengi wetu walimwambia: "Hatutaki kungojea hata nukta moja. Endelea."

Alingojea dakika nyingine mbili, mikono yake akiikunja, huko akitutazama kama aliyepumbaa halafu akakimbilia kwenye chombo cha mlio wa onyo, akakizungusha mara moja, akatuangalia tena kwa ukali, akakizungusha tena, akatuangalia tena kama aliyepotewa na imani halafu akakizungusha kwa mara ya mwisho. Askari walikimbia wakielekea katika nyumba zetu na Mansfield aliwaambia waingie watupige tutoke nje. Lakini hawakufanya cho chote—bahati mbaya kwake. R.S.M. wa askari hao, aliyekuwa Mjaluo aliwaonya kuwa wajihadhari kwa vile wafungiwa walielekea kufunguliwa baada ya muda mfupi na wangeweza kukumbuka yale waliotendewa. Lakini hata hivyo, askari waliona kuwa amri hiyo haikuwa na maana kwa vile walikuwa wameishi na sisi kwa amani kwa miaka mingi. Wengi wao walikuwa wanafunzi wangu na nilikuwa nikisa-

hihisha masomo yao na kuwapa majaribio. Pia nilikuwa namsomesha yule R.S.M. wao katika nyumba yake na tulikuwa marafiki wakuu. Nilitaka kumsaidia lakini hata zaidi nilitaka kusikiliza radio yake ili niweze kuwapelekea wale wengine habari za dunia: saa za kumsomesha zililingana na saa za kutangazwa kwa habari. Askari hao walikuwa binadamu kama sisi na mara nyingi walitumia haki. Tulikuwa mbwa na mbweha pamoja.

Mkuu wa Kambi aliitwa kuhukumu hali ya tukio hilo. Hakusema cho chote kwa Mansfield lakini alikubali kuturudishia chakula chetu na tusipigwe tena na tulikubali kufanya kazi. Baada ya mwezi mwingine tulisikia kuwa kazi yetu haikumtosheleza D.C. wa huko. Ilisemekana kuwa alitoa amri kuwa tufanyishwe kazi zaidi tuwe tukiharakishwa kutoka mashimoni ya mawe hadi hospitali ambako tulipeleka mawe ya kujenga. Hawakuonekana kama wana lori yo yote huko. "Mukoma Times", jina lililopewa utangazaji wa habari katika Lodwar, ilitangaza habari kuwa hali yetu ilikuwa kama ile iliyokuwa ya kujenga "Pyramids" na watoto wa Israel walipotawaliwa na Firauni wa Misri. Wakati wafungiwa waliposikia amri hiyo kwa mara ya kwanza, walisema kuwa ni lazima tukatae kufanya kazi kabisa bila kujali yatakayotokea mpaka mmoja wetu afe. Nilizungumza nao. "Haja gani kukataa mpaka mmoja afe halafu kukubali kufanya vile ulivyokataa kufanya hapo kwanza? Tutafaidi nini na kifo cha mtu mmoja? Au sote tukatae mpaka sote tufe au kama tukifikiri kuwa hatuna nguvu za kutosha, ni vizuri kukubali kabla ya kulazimishwa. Lakini yabaki njia ya tatu. Yafaa tukafanye kazi; yafaa tuvae nguo zetu zile nyepesi na tuyabebe haya mawe na kukimbia kutoka hospitali kwa haraka kama iwezekanavyo, halafu tuyabebe haya mawe kwa haraka tena hadi hospitali, na baada ya kufanya hivyo mara kadhaa, mtaona matokeo yake. Mtaona wale askari ambao watakuwa nasi, ambao watakuwa wamevaa viatu vizito, nguo za kipimo za khaki zenye joto, sokisi na patizi na zaidi ya hayo wanabeba fimbo ndefu na bunduki zenye uzito wa ratili tisa—hawataweza kuwa pamoja nasi tukiwa na nguo nyepesi."

Siku hiyo, wafungiwa walifanya kama nilivyowashauri na matokeo yake yalitutosha kabisa. Lodwar ni mahali pa joto sana na ingawa wafungiwa waliona shida wakati wa kupeleka mawe, wakati wa kurudi walikimbia kama sungura. Askari walisumbuka, waliondoa bunduki mabegani mwao, wakazining'inisha nyuma mikononi mwao wakati wa kurudi. Lile jasho katika patizi lilifanya miguu yao kuumia; walifungua nguo zao, walivuta hewa kwa nguvu na kukohoa hata wakatushawishi tuende pole pole. Tulijibu kuwa ilitulazimu kutii amri ya D.C. na tukaendelea tu. Jioni ya siku hiyo, ile barabara ya kwenda hospitali ilichafuliwa na askari walioenda kama viwete kwa kuumia miguu. Asubuhi yake, walimwambia Mkuu wa Kambi kuwa hawangeweza kufanya kazi katika hali hiyo na

yule R.S.M. akatuarifu kuwa tuwe tukifanya kazi kama hapo mbeleni na kama D.C. aliuliza swali, angetuunga mkono. Tunasema kwa Kikuyu: *Ng'enda thi ndiagaga mutegi* na hivyo ni kusema kuwa "Ile inayopitia chini haikosi wa kuinasa." Hata D.C. aweza kupigwa mweleka.

Kazi katika Lodwar ilikwisha saa saba na baada ya kupika na kula chakula chetu, tuliondokea jua hilo la kukaanga na kuingia ndani ya vyumba vyetu ambako tulijifunza tukingojea baridi ya jioni. Baina ya saa kumi na moja na thenashara na nusu jioni, waliokuwa na nguvu walicheza tenikoiti na mpira hali wale wenye akili zaidi walicheza dama na "chess." Mimi nilicheza senta-fowadi na nilikuwa kapiteni wa timu ya mpira ambayo mara nyingi iliwashinda askari wa timu ya Warders XI.

Tulisikitika sana siku moja wakati askari ambaye tulimpa zawadi ampelekee Mzee Kenyatta na wengine katika Lokitaung alirudi na habari kuwa Mzee alikuwa anaumia mguu. Komiti ya kambi iliuliza kila nyumba kumwombea Mzee kila jioni ili apone. Hivyo ilifanywa na tulifurahiwa sana kusikia kuwa alipona, na pia kuwa alikuwa anawaelimisha wenzake huko. Waruhiu Itote, aliyejulikana kama "General China", hajasahau mafunzo aliyopewa na Mzee Kenyatta na tulipokutana na Waruhiu katika Kambi ya Pekee ya Gathigiriri, alimtukuza Mzee kwa ajili ya ukarimu wake na uvumilivu wake kama mwalimu.

Asubuhi moja tulipokuwa tukienda kazini kwa kawaida ya "pole ndio mwendo" tuliitwa nyuma na Mkuu wa Kambi, ambaye alionekana mchangamfu akatuambia: "Shujaa wenu, Field Marshall Sir Dedan Kimathi, alikamatwa na kujeruhiwa jana na askari kanga wa Nyeri. Majemedari wote waliobaki watakamatwa kwa njia hiyo tu. Nafikiri sasa mnaweza kuona wazi kuwa Serikali itashinda. Kwendeni kufanya kazi sasa."

Tulisumbuka sana rohoni mwetu tuliposikia habari hiyo na hapo kwanza wengine wetu hawakusadiki hadithi hiyo. Lakini baadaye, habari hiyo ilithibitishwa katika radio. Hakuna wetu aliyejisikia awezaye kufanya kazi na askari hawakutulazimisha. Wengi wao walionekana wenye huzuni kama sisi na bila shaka tulijua huruma zao zilikuwa wapi. Siku hiyo hatukufanya masomo yo yote, mechi ya mpira ilifutwa na hakuna aliyekula kujipendeza. Korti yetu haikuketi alfajiri hiyo. Wafungiwa wote walilia wakiwa kimya na wale waliowahi kupata kitambaa cheusi kutokana na patizi mzee walikifunga mabegani kuonyesha huzuni zao. Jioni yake, tulisali katika vyumba vyetu na tukaimba wimbo wake. Wimbo huo ulitungiwa ndani ya msitu na unajulikana sana katika nchi yetu.

WIMBO WA KIMATHI

1. Wakati Kimathi alipoupanda
   Mlima akiwa peke yake

Aliuliza apewe nguvu na ushujaa
Wa kuwashinda Weupe.

2. Alisema hatua zangu zote
Ambako mimi nilipitia
Nanyi myafuatie
Na mnywe kutoka vikombe hivyo.

3. Mkinywea vikombe hivyo vya ushujaa
Vile ambavyo nilinywea
Ni vya maumivu na huzuni
Na machozi na kifo.

4. Tunalia kwa sababu sisi watu Weusi
Na sisi si Weupe
Na sisi si wa urithi wao
Mungu wetu yuko mbele.

5. Msishtushwe na kuhamishwa
Au kwa ajili ya kufungiwa kama wanyama
Au kwa ajili ya kunyang'anywa na kuuawa
Mungu wetu yuko mbele.

6. Hata mioyo yetu ikiteswa,
Jomo hatatuacha
Kwa sababu yeye hakuachiliwa huko
Kapenguria ni Mungu.

7. Vaeni kusubiri kwake
Kuteswa au kuuawa
Muwe mkijua kuwa ninyi wa Ufalme
Wa Kikuyu na Mumbi.

8. Twamuomba Mungu atukubalie
Watu Weupe warudi kwao
Kwani mti usio na mazao
Haupandwi shambani.

(Dedan Kimathi alikuwa kiongozi wa majeshi ya msitu wa milima ya Aberdares tangu 1952 mpaka 1957 alipokamatwa).

Dedan Kimathi alikuwa shujaa mpigania uhuru na alikuwa kiongozi mkuu wa watu wake katika msitu. Wakati wa Vita Vikuu vya Pili, alikuwa katika majeshi yaliyopigania Uingereza. Baada ya vita, aliajiriwa na Tetu Dairymen's Association ya Nyeri halafu akaajiriwa na Shell Company huko Thomson's Falls. Niliambiwa na mwanafunzi ambaye alifundishwa na Kimathi kuwa wakati huo alikuwa mwungwana aliyewapenda watu.

Msituni, ushujaa wake haukupimika na wananchi wanafikiria kufanya sanamu yake katika mji wa Nairobi. Wengine hata sasa wanakataa kusadiki kuwa Serikali ya Kenya ilimnyonga: wangali wanafikiri yu hai. Bibi wake, Mukami, na watoto wake, waliteswa sana katika Nyeri baada ya kunyongwa kwake, na nimefanya niwezavyo kuwasaidia, tangu nilipofunguliwa. Serikali lazima iwasaidie jamaa kama hao na wote wengine waliopotelewa na wazazi wao wakati wa vita.

Wakati Ghana ilipopata uhuru wake tarehe 3 Juni, 1957, palikuwako furaha kuu baina ya wafungiwa na tulifanya sherehe ya pekee, hata tukacheza dansi nyinginezo za Kikuyu na "wathi" wa Kikamba. Askari wengi, bibi zao na vipenzi vyao walifika kuona sherehe hiyo na walijiunga nasi walipofahamu kwa nini tulifanya hivyo. Sala mpya zilifanywa ili nchi hiyo ifaulu na ziliongozwa na Kimani Wachuku, aliyekuwa mzee zaidi katika kambi hiyo. Kimani alizoea kutukumbusha kuwa kwa muda huo wa uzee wake wa miaka sabini na mitano alifahamu kuwa kupigania uhuru wa Kenya kulianza miaka mingi iliyopita, na tusichoke kwa ajili ya shida zisizokawia. Wazee walikaribia kuwaachia sisi vijana madaraka hayo na ilitufaa tujielimishe kama tuwezavyo wakati tulipokuwa na nafasi. Joseph Kirira na mimi tulitunga wimbo mwingine kwa ajili ya wakati huo, nao tuliuita Wimbo wa Afrika.

WIMBO WA AFRIKA

1. Mungu aliwapa Watu Weusi
   Hii nchi ya Afrika
   Mshukuruni Mwenyezi
   Kwa sababu ya mapenzi yake.

   Kiitikio

   Tutaishi tukishukuru
   Nchi ya Afrika
   Kutoka jua lianziapo na liishiapo
   Magharibi na Mashariki

2. Baada ya shida nyingi
   Nchi ya Misri
   Iliokolewa kutoka ukomboni
   Ikapata uhuru wake.

3. Wakati Abyssinia ilipoona mwanga
   Uliotoka upande wa kaskazini
   Ilijikaza mno
   Ikaondoka matopeni.

4. Tulifurahi sana
Tuliposikia habari ya Ghana
Ile bendera ya Mwingereza
Wameishusha.

6. Ukiitazama Kenya yote
Yote ni mto wa damu
Kwa sababu nia ni moja tu
Ya kupata uhuru.

7. Sikilizeni kilio
Afrika ya Kusini
Kwani wanateswa
Na watu wale weupe.

8. Tutafurahi sana sana
Watu Weusi tukiwa pamoja
Tufanye ushirika
Ufalme wa Waafrika.

Wakati kambi ilipoonekana kuwa na amani, Serikali iliwapeleka wale wa "kutuokoa" (rehabilitation) ili kuiharibu hiyo amani, na kwa vile tulikuwa tumekata shauri kuungana katika kutokubaliana na Serikali, walimleta afisa Mzungu na wasaidizi wawili Waafrika, James na Walter. Komiti ya Kambi ilipitisha Sheria ya 13 ya Lodwar iliyompinga ye yote kusema na maafisa hao. Baada ya siku chache walipokuwa wakiingia nyumbani mwetu na kujaribu kusema nasi bila kufaulu, waliwacha kutumia njia hiyo kabisa na mnamo Agosti 1957, walituita kwa vikundi vikundi katika chumba cha pekee nje ya kambi. Hapo walituhoji kila mtu binafsi na wakatuwekelea zile daraja zao kama vile walivyofikiria juu ya kila mmoja. Tuliwauliza maswali mengi ambayo hawakuweza kuyajibu kutosha fikira zetu na mara tuliwawekelea cheo cha wasaliti.

Huko Lodwar tulisoma magazeti ambayo tuliletewa na marafiki wetu baina ya askari na kwa hivyo tulikuwa twajua yale yalioendelea katika hali ya siasa katika nchi. Tulimshukuru Oginga Odinga aliyekuwa Mjumbe aliyewakilisha Wilaya ya Nyanza ya Katikati, wakati alipotaja katika Lejiko kuwa Jomo Kenyatta alikuwa Kiongozi wetu na tuliona vile wajumbe wengine walivyojaribu kuepukana na matamshi yake. Wakati alipoulizwa mwezi wa Machi, 1961 vile alivyofikiria hali ya maisha katika Lodwar, Mzee Kenyatta alieleza kuwa yalikuwa ni maisha ya "Uhuru na Vumbi". Maneno yake yalitafsiriwa kwa njia nyingi lakini yeye alikusudia kusema vile alivyosema wala hakuwa akitumia methali. Wakati mwingine katika Lodwar, vumbi hutawala kwani hufunika kila kitu, kila mtu na maisha huenda yakawa yasiopendeza likiongezwa

hilo joto la jua. Ben Gacathi na mfungiwa mwingine walipatwa na wazimu kwa muda mfupi kwa ajili ya joto na hali ya mambo, lakini baada ya kuuguzwa katika hospitali waliturudia salama.

Tukifikia mwisho wa maisha yetu katika Lodwar, tulikuwa tumefanya urafiki na Waturkana wa hapo na wakati huo hawakutufikiria kama vichwa ambavyo wangeuza kwa bei ya unga wa mahindi na sukari. Tulihuzunika kuona hali ya nchi ambapo walijaribu kuishi na tulifikiria kuwa Serikali ilipaswa kuwapa msaada hata ikiwa msaada huo ungepunguza maendeleo katika sehemu zetu za Kikuyu na Nyanza. Tulifahamu maneno mengine yao na tuliwapa chakula. Chakula chetu kilitosha wakati huo lakini kilikuwa cha aina moja kila wakati na kilichosha. Kwa vile uko mwisho wa wingi wa ugali ambao mtu anaweza kutumia, mara nyingi tulijiona tukiwa na mabaki. Komiti ya kambi ilisema kuwa mtu asitupilie mbali cho chote na kilichobaki kiwekwe salama na kupitishwa kwa Waturkana mara nafasi ikipatikana.

Mnamo Desemba 25, 1957, sitini baina yetu waliambiwa kuwa watasindikizwa ndani ya ule "mfereji" na kuwa tutaanza mambo katika kambi ya Athi River ya "kuokolewa." Hadithi ya yale yaliyotendeka huko ilikuwa yajulikana: James na Walter walijaribu kulinganisha yaliyotendewa watu huko na vile ingekuwa rahisi kujipatia usalama tena kwa kuungama tu. Asubuhi sana, tuliingia ndani ya malori, tukawaaga ndugu zetu kwa huzuni, tukaelekea pande za Kitale, huko nyuma tukaliacha joto na vumbi, hospitali mpya na wenzetu pia.

8 "Mfereji", "Kuokolewa" na Nyumbani

MIMI HUPENDA kusafiri na kuona nchi mpya na kwa hivyo nilipendezwa kusafiri kupitia kwenye mchanga, majabali makubwa meusi na miti minyonge yenye miiba tukielekea pande za Kitale. Kuna kilima chenye mwinuko kasi kinachoitwa "Royal" njiani hiyo, na barabara hukizunguka mara kadhaa huko ikifanya kona nyembamba. Iliogofya kuangalia nje kwenye mwinuko na hakuna aliyesema neno mpaka tulipofika kileleni. Tulilala ndani ya Jela ya Kitale usiku huo, halafu tukaanza safari yetu asubuhi yake kwa gari la moshi. Tulifika Athi River baada ya siku mbili, yaani tarehe Oktoba 28, 1957, mwaka wangu wa nne tangu nilipokamatwa na kufungiwa.

Katika Athi River tuliwakuta wenzetu wengine wa zamani, yule Buxton wa Lodwar na Mansfield (tuliyembandika jina la "Kamao"). Buxton alionyesha urafiki na uchangamfu, Mansfield alionekana mwenye hasira kwani alikuwa hajasahau tulivyomtendea mara ya mwisho huko Lodwar. Kambi ilikuwa imegawanywa katika sehemu sita, na kila sehemu iliweza kukaliwa na watu mia tatu, lakini zote hazikujaa kabisa, kwani kila moja ilikaliwa na watu kutoka mia moja na hamsini hadi mia mbili. Kikundi chetu cha watu sitini kiligawanywa mara sita na kutawanywa kote. Nilipelekwa Nambari 6, ambako nilikutana na marafiki wengi wa Manyani, na nilifurahiwa kwa vile nilikuwa nimewaacha Robinson Mwangi, Gad Kamau, Joseph Kirira na David Oluoch Okello huko Lodwar ambao sikuwaona tena mpaka nilipofunguliwa mwaka wa 1960.

Kambi ya Athi River haikuwa imemalizika kujengwa wakati Hali ya Hatari ilipotangazwa lakini ilipokamilika wale wote waliofungiwa kufuatia "Operation Jock Scott" na kufungiwa kwa amri ya Gavana (G.D.O.) walihamishiwa huko kutoka Kajiado katika nchi ya Masai. Wafungiwa hao wa kwanza walikuwa pamoja na wengi walioelimika sana. Amri za kwanza za kufungiwa zilihitaji tu sahihi ya Gavana binafsi. Vile Hali ya Hatari ilivyoendelea na waliokuwa mia wakawa maelfu, nguvu za kuwafungia watu zilipewa ma-P.C. hapo kwanza, halafu ma-D.C. Wengi wetu walifungiwa chini ya amri hizo zilizojulikana kama D.D.O. (Delegated

Detention Orders). Sababu yake ilikuwa kwa vile wafungiwa walikuwa wengi, Gavana hakuweza kuendelea kutosheka kuwa kila amri ilikuwa ya haki hali ma-P.C. na ma-D.C. wangekuwa na nafasi zaidi. Ilivyotendeka ni kuwa hakuna aliyejali kupeleleza sawasawa kabla ya amri kama hizo kutolewa; sahihi ya D.C. ilikuwa rahisi kupata kuliko ya Gavana.

Wakati Serikali ilipoanza "kuwaokoa" wafungiwa, kambi ya Athi River iliachwa mikononi mwa "M.R.A." (Moral Rearmament). Wakati huo, Joseph Kirira alikuwa Athi River na aliniambia kuwa kambi ilitawaliwa vizuri na kuwa maisha yalipendeza kidogo. Lakini mara ule upuzi wa kuungama ukaletwa. Maafisa wa hapo hawakuwapiga watu lakini walitumia njia nyinginezo, nyingine ambazo zilifichika kuliko nyingine. Chakula kilipunguzwa na hatua hiyo iliwafanya wengine kuungama. Joseph aliniambia kuwa malaya walikuwa wanaletwa mbele ya wafungiwa na kuweka miguu yao ovyo ili kuwakumbusha wafungiwa hali ya maisha waliyokuwa wanakosa. Hawakukubaliwa kuonja furaha hizo—walikuwa wanakumbushwa tu kabla ya kuondoka kwa hao malaya. Wawili au watatu "waliokolewa" kwa njia hiyo, lakini hiyo ilikuwa bure kwa mwananchi halisi. Tunasema kuwa mapenzi ya bibi hayawezi kulinganishwa na mapenzi ya nchi ya mtu; tofauti baina yake ni kama ile ya duniani na mbinguni. Kwa vile wafungiwa wengi hawakunaswa na njia hizo, Serikali iliwahamisha hadi-koa wote mpaka Kisiwa cha Manda na Mackinnon Road, na baadaye wakawa wachungaji wa kambi ambayo sasa ilikuwa ya wanyonge, kutoka mikononi ya M.R.A. Wengine katika Manda waliungama na kurudishwa Athi River kuwasaidia wahojaji. Wengi wa wale walioungama walifanya hivyo kwa kufikiria mambo ya nyumbani lakini hata hivyo Serikali iliwaambia kuwa ni lazima wathibitishe uaminifu wao katika Serikali wakiwa Athi River, na ni wazi kuwa kama vile walivyoweza kuwafanya wengi waungame, vile ndivyo uaminifu wao ulivyoongezeka na pia nafasi ya kurudi kwao ikaharakishwa. Wale walioungama lakini wakashindwa kuungamisha wengine walipelekwa Mokowe Settlement Scheme katika Jimbo la Pwani ambapo walipewa nyumba na kazi. Hawa baadaye walirudi makwao wakipitia katika "mfereji".

Mwaka wa 1957, afisa aliyetoka jeshini, Rochester, na bibi wake, ndio waliochunga "uokozi" katika kambi. Kwa wakati huu, Serikali ilikuwa imegeuza maongozi yake. Ilifikiriwa kuwa kila mtu ataungama hatimaye na ikaonekana kuwa wale waliokosa kuungama waligharamisha Serikali kwa kiasi kadiri. Kulazimisha watu kuungama kwa nguvu kulianzishwa ingawa hakuna aliyekuwa mjinga kuandika hivyo katika sheria. Buxton alimwita John Giathi na mimi katika afisi yake siku moja baada ya kufika huko Athi River akatueleza kuwa kama tuliendelea kukaza roho zetu kama tulivyofanya huko Lodwar, hatungeweza kupitia ndani ya "mfereji."

Ilitupasa tuwe weroro ili tuweze kuingia na alikusudia sisi kushirikiana na wakuu wa kambi na wakati wetu ukifika hakuna taabu ingetupata. "O.K.?" "Ndio Bwana", tukamjibu. Alimwambia John Giathi aende ndani ya afisi moja akahesabu pesa za wafungiwa na mimi nikapelekwa uwanjani kufundisha kucheza mpira na michezo mingine. Hakuna aliyenung'unika juu ya michezo kwani ilikuwa sheria yetu katika Lodwar kuwa tutatii amri za kambi, ikiwa amri kama hizo zililingana na sheria na zenye maana.

Baada ya siku mbili, Rochester aliniambia kuwa alinitaka nijiunge na "Atiriri", gazeti la kambi, ambalo liliandikwa na Benjamin, ambaye alirudia kazi yake ya kuchapa alipofunguliwa, na alitoa matangazo yake bure kwa wafungiwa. Kazi yangu ilikuwa ya kutafsiri Kikuyu kiwe Kiingereza. Kabla ya kufanya hivyo, niliwaambia kuwa iliwapasa kufahamu kuwa niliifanya kazi hiyo kama mahabusu anayefanya asiyopenda kwa ajili ya kutii amri. Nilitafsiri yale tu yaliyoandikwa bila kusahihisha, kwani kama niliona kosa kuwa shilingi tano kuongeza nyingine tano huwa ishirini, sikugeuza—niliandika tu hivyo pamoja na makosa yake. Hivyo tulikubaliana. Wengine waliofanya kazi ya kuandika walikuwa Linus M. Mugi, Zakaria Kinja Kibachia na Mathew Kimani.

Benjamin alikuwa mwenye akili na uwezo na alikuwa shujaa katika kuandika vitabu vya Kikikuyu. Alikuwa mwenye masikizano lakini mwerevu. Hakumpiga ye yote na aliwatendea vyema wale wafungiwa wengine. Alitangaza kitabu cha kuungama ambacho sote tulipewa nakili. Alichora picha zilizoonyesha kuwa aliyeungama alikuwa tajiri au alimshinda yule aliyebaki hadi-koa. Askari pamoja na wale weroro walipendelea hivyo sana. Tulizikemea kama Michezo ya "Wamarebe" (michezo ya debe tupu).

Baada ya muda mfupi, Rochester na Buxton walifahamu kuwa sikuweza kuungama kwa kujipendea, na iliyokuwa hatari zaidi ni kuwa fungu lingine lilikuwa lanifuata. Kwa hivyo walikata shauri kutumia silaha yao ya mwisho—kutumia nguvu. Siku moja waliniita wakaniambia niungame. Kama kawaida, nilikataa na pia nikawaambia wazi kuwa waliweza "kumwokoa" mtu ikiwa mtu huyo anataka "kuokolewa" na kuwa kuungama kunakofanywa kwa utumiaji wa nguvu hakukuwa na maana. Niliposema hivyo, Rochester alinichapa kofi la nguvu ambalo liliniangusha.

Pole pole niliinuka halafu nikapelekwa nje karibu na stoo ya chakula ambako watu wengine watatu waliitwa wakaambiwa wanihoji. Walikuwa Jonah na Elijah, wote kutoka Nyeri na karani aliyetoka Kiambu. Wazungu wanne pia walikuwako—Rochester, Buxton na afisa wawili wa jela. Walinionya kuwa hiyo ndiyo ilikuwa nafasi yangu ya mwisho ya kuungama. Niliwajibu kama hapo mbeleni. Pole pole lakini bila wasi wasi walinianza. Wazungu peke yao: Waafrika hawakuhusika na yale yaliyo-

tendeka: watu walisema kuwa Wazungu waliweza kutenda hayo mambo bila kupitisha kiasi na kuwa waliogopa kuwa Waafrika wangepiga kuua. Wafungiwa wengi waliokuwa karibu waliona yale yaliyokuwa yakitendeka na baada ya muda ulioonekana kuwa mrefu nilianguka bila kujisikia, lakini nikawahi kumwona Kiragu Wamugure, rafiki wangu mkuu kutoka Lodwar, ambaye machozi yalimtiririka usoni kwa kuona vile nilivyoumizwa. Uso wangu ulikuwa umepasuliwa, goti langu la kulia lilikuwa limevunjika kwa kupigwa na fimbo na kifua changu kilichomwa na kitu kama fimbo yenye misumari. Niliwahi kuishi lakini alama zinazoonekana usoni mwangu, magoti na kifua zitabaki nami na hata leo ninaumia vikali tumboni na kifuani mwangu. Nilinyolewa kabisa, na damu ilinitoka pia kwa ajili ya kunyolewa. Wale wahojaji waliniongoza, nguo zangu zikiwa damu tupu, wakanipeleka mbele ya wafungiwa wengine kupitia seng'enge iliyozunguka kila sehemu, huko wakawaambia wafungiwa kuja kuona vile kiongozi wao alivyoonekana wakati huo. Nilitupwa ndani ya chumba kidogo na kwa muda wa siku mbili sikupewa chakula; hata kama nililetewa chakula, singeweza kufunua mdomo wangu. Jioni ya siku hiyo niliyopigwa, mfungiwa mwingine alijinyonga katika Sehemu 4. Mwenzake aliyelala naye aliyeitwa Jimmy kutoka Embu aliniambia kuwa aliona vile nilivyotendewa na wakati huo akakata shauri kuwa hakuweza kuvumilia kuishi katika ahera hiyo mara nyingine. Alitumia kamba aliyopewa na Serikali ya kufunga suruali.

Siku ya tatu wafungiwa wengine walinileta uji. Waliniambia kuwa watu katika kambi walisumbuka sana kwani walifikiri nitapigwa mpaka kufa na walitumwa na wengine waniulize nifanye uungamo fulani, lakini nikumbuke kuwa hilo ni la kulazimishwa na linaweza kukanushwa baadaye. Walifikiria pia kuwa hatua hiyo ingenipatia nafasi ya kuandika barua kwa Serikali na kueleza yale yaliyokuwa yakiendelea. Hawakupendelea mimi nife, walitaka mimi niishi nao, hata ikiwa nitakuwa kiwete maisha yangu.

Kwa hivyo niliungama uwongo mtupu, nikauchanganya na ukweli kidogo hapo na hapa, na baadaye nilirudishwa katika Sehemu yangu. Siku iliyofuata, niliandika barua ndefu kwa ye yote aliyeingia kichwa changu. Waziri wa Makoloni, Barbara Castle, John Stonehouse, Tom Mboya, Argwings-Kodhek, Mkuu wa Jela na Attorney-General. Barua hizo nilizituma kwa mikono ya Kaguongo na Nyota Githenji, wafungiwa waliokuwa wakichimba shimo nje ya kambi, na ambao waliwahonga askari wengine wazitie ndani ya posta. Nilikuwa na pesa wakati huo kwani nilikuwa na kiasi cha Shs. 2,400/-, nyingi ambazo nilipata kwa kuuza vikapu na mikeka katika Lodwar.

Halimashauri ya Kuchungulia ilifika kutoka Nairobi kufuatia barua

yangu. Niliulizwa kama ni mimi niliyeandika barua hiyo, nami nikajibu ni mimi, na nikaongeza kuwa sitaandika nyingine tena. Lakini katika moyo wangu sikukusudia kuacha kwani kule kupigwa kulinifanya nisijali kuwaambia ukweli tena.

Athi River ilikuwa kambi ya kuungama. Ingawa palikuwako na kazi nyingine iliyoendelea katika kambi, kazi iliyokuwa ya maana ni ya kuwahoji wafungiwa. Ilikuwa lazima watu waungame kwa hiyari au kwa kulazimishwa kwa nguvu. Wahojaji walikuwa wazee waliotoka ndani ya risavu na ni wakati huo tulipokutana tena na Noah ambaye hapo mbeleni alikuwa akichunga kambi ya Kwa Nyangwethu karibu na Nakuru. Nilimwuliza kwa nini watu walipondwa makende katika Kwa Nyangwethu na alinijambia kuwa zilikuwako sababu mbili. Ya kwanza, walitaka kupambana na wale hadi-koa waliokataa kuungama, na nilibahatiwa kuwa sikuwa mmojawao. Ya pili, walitaka kujua kama binadamu aliyetendewa hivyo angenona kama dume wa ng'ombe ambaye ametendewa hivyo. Mtu huyo alikuwa kama mwenda wazimu—pumbavu wa mwisho.

Wakati wa asubuhi tulihojiwa na kufanyizwa kazi. Wakati wa alfajiri wakuu wa kambi walijaribu kujaza wakati wetu na mambo ya "uokozi" ili tusipate nafasi ya kushirikiana na kuungana. Bila shaka walifaulu kwani hapakuwako na komiti ya waliyofungiwa katika Athi River. Huu ulikuwa mfano wa mambo ya kila alfajiri:

Sehemu 1: Kuhudhuria masomo nyumbani mwao. Masomo haya yalikuwa juu ya historia ya Kenya, himizo kuu likitiwa juu ya vita vya ukabila vilivyokuwako kabla ya kufika kwa Wazungu na vile Wazungu walituokoa kutoka ushenzi, na mwishowe maelezo juu ya faida ambayo Wazungu walileta katika nchi, na zaidi kwa muda wa miaka michache iliyopita. (Lazima niseme kuwa si sote tuliona mambo kwa njia hiyo kama wale waalimu wetu).

Sehemu 2: Kuhudhuria mahubiri kutoka kwa wazee wa kuhojiana. Juu ya kuungama, mambo ya kuungama na juu ya kusaidia Serikali kwa kuiambia vile magaidi waliobaki wangekamatwa.

Sehemu 3 na 4: Mpira, tenikoiti, mpira wa mikono ukichungwa na wazee wa kuhojiana.

Sehemu 5: Michezo ya kienyeji. Mucungwa, Mugoiyo, Muthuu, Kumunda Mburi, Mukuogo, Kamano. Wazee waliketi chini na kucheza "marobo". Tulizoea kuvumbua maneno ya matusi kwa Serikali lakini tulikuwa twachungwa.

Sehemu 6: Kwenda sinema.

Kila sehemu ilifanya jambo tofauti kila siku.

Palikuwako na chombo cha kupasa sauti katika kila nyumba, ambacho kazi yake ilionekana kuwa mara mbili. Kila wakati ilitoa propaganda ya Serikali, ikawatukuza "waaminifu", Waingereza na Magharibi. Mara nyingine ilichosha hivi ati tulilazimishwa kuikaba kwa blanketi mpaka ikawa kitu cha kuchekesha. Mara mmoja wetu alijitolea na kudai vile tunavyofanya uhalifu juu ya paazi na blanketi zikaondolewa. Lakini tulipata muda mfupi wa amani. Matumizi ya pili ya chombo hicho ilikuwa ya kuwaita majina wale ambao watakaohojiwa siku ifuatayo. Wakati tuliposikia ikianza, tulipiga kelele na kusema: "Nyamaza na usikilize ni shingo ya nani itakayozungushiwa kamba kesho." Mara hiyo tulinyamaza kwani kuhojiwa kulikuwa jaribio kali na ilikuwa vigumu kupata usingizi ikiwa jina lako lilitajwa. Nilihuzunishwa sana kuona vile walivyowatendea wazee kama Kirori Motoku, Wambugu Kamuiru (ambaye sasa ni mweka-hazina wa K.A.N.U. ya Nyeri) na mweka-vitabu wetu wa Lodwar, Wachira Karige. Sitasahau kamwe vile Kirori alivyoonyesha nguvu na ushujaa alipoteswa na kuaibishwa na wahojaji hao. Yeye hakusitasita na tulisikiliza mashauri yake kwa makini. Alifahamishwa wakati huo na akiwa kifungoni, Serikali ilikubali ombi la A.D.C. ya Nyeri, iliyokuwa kibaraka cha Serikali cha kukamata kichaka chake cha ekari ishirini na nane na kumlipa pauni 15 (shilingi mia tatu) kwa kila ekari. Kichaka hicho ambacho kilikuwa ukingoni wa mji wa Nyeri ni cha thamani mara kumi ya hiyo.

Baada ya Rochester kuondoka, D.O. aliletwa Athi River. Aliitwa Dennis Lakin na hakunipiga kamwe lakini alisema kama mwenye maana na rafiki. Mpango wake ulikuwa wa kumtuma kila mtu makwao katika ma-Divishoni ambako Machifu wao wangejua la kuwafanyia. Kwa vile tulikuwa wachache sana katika Athi River wakati huo hakupendelea kuwaleta wafungiwa wengine tusije tukawaambukiza. Kwa hivyo alisifu kuwa nipelekwe katika Divishoni yetu ya Othaya ambako ningengojea kuachiliwa.

Mwishoni wa Februari, 1958, siku chache baada ya kuwa katika kampi ya kazi ya Karatina ambayo ilijengwa kwa ajili ya watu wa Divishoni ya Mathira, nilifika Othaya. Sijui bahati mbaya hiyo namna gani kwani Mkuu wa kambi alikuwa yule yule aliyerudi mahali pa Buxton huko Lodwar, na hivyo tulikuwa maadui wa zamani. Baada ya kupekuliwa sote tulinyolewa kwa wembe na tukaambiwa kuwa tutafanyiwa hivyo kila wiki. Halafu tukapewa nguo kuukuu hali kila kitu kingine tulichokuwa nacho kiliwekwa ndani ya stoo, viatu, saa, pesa n.k. Hakuna aliyekubaliwa kuwa hata na kitambaa cha mfuko au sindano. Baada ya hivyo tuliambiwa kukimbia kuzunguka kambi na huko askari alitukimbiza akitupiga kwa kiboko bila kujali. Mwishowe tuliamriwa kwenda katika Sehemu 6 tukiwa na suruali fupi nyeupe na shati nyeupe

Hatukupewa nguo za ndani. Sehemu hiyo iliwekwa kwa watu wapya. Zilikuwako sehemu sita zote, na ilikusudiwa kuwa tutakaa mwezi mmoja katika kila moja ikikusudiwa tutakuwa wapya baada ya miezi sita. Usiku huo nililala vibaya, nikifikiria vile mahali pale palikuwa pa kitoto na pa kuaibisha.

Kulikuwako na watu wengine katika sehemu yetu walioletwa kutoka kambi za pekee huko Mwea, kwenye nchi tambarare za Embu. Walituhadithia juu ya mateso ya huko na zaidi juu ya kuwapokea wafungiwa wapya, mateso ambayo kukubaliwa kwake kulileta msiba mkubwa wa Hola. Wakati wafungiwa wapya walipofika kambi za Mwea, walipewa amri rahisi ambazo kwa kawaida walikataa kutii. Amri hizo zililingana na sheria kabisa lakini hazikuwa amri ambazo mahabusu angetii kwa wakati wa kawaida. Serikali ilikuwa imetoa maelezo kwamba kama mfungiwa akikataa amri yo yote iliyolingana na sheria, nguvu ya "kumlazimisha" ingetumiwa ili atii amri. Jeshi kubwa la askari na maafisa Wazungu walingojea kuwaamkua wageni wapya na hapo ndipo wakatumia hiyo nguvu ya kulazimisha. Maovu yasiyotajika yalifanywa kwa jina la "kulazimisha", maovu ambayo hayawezi kuandikwa ndani ya kitabu kama hiki. Baada ya kuteswa hivyo, wafungiwa walilazimishwa kuungama viapo vyao na kuungama kwao kuliandikwa katika karatasi wakati walikuwa katika hali ya wasiwasi huo. Wataalamu juu ya uhoji walisema kuwa hii ndiyo ilikuwa dawa iliyohitajikana ya kutikisha ubongo mgumu wa "hadi-koa" ambao ulikataa mambo yote. Lakini pale ubongo wetu ulipokuwa ni pale ulipopima sababu zilizotufanya tusijitolee ovyo. Hatukuwa dude zile walifikiria sisi tulikuwa, yaani binadamu waliogeuka kuwa nusu binadamu; sisi tulikuwa hadi-koa wananchi na ni kifo tu kingelichotuzuilia kuwa hivyo, hata viwe ni viapo vingapi tulivyoungama kwa ajili ya kuteswa.

Baada ya kujadiliana na wafungwa wapya, waliendelea kuelimishwa katika kambi za Mwea ambako wahojaji walikuwa chini ya District Assistant Mkikuyu. Walikuwa wanajifunza mambo mapya kama vile kubeba ndoo zilizojazwa mawe kwa vichwa vyao, huko wakikimbia au kutembea kwa magoti juu ya njia iliyomwagwa mawe madogo madogo. Mtu mmoja aliyeitwa Akulino alijitupa ndani ya mto Thiba ili kuepukana na taabu hiyo. Aliokolewa lakini baadaye alijinyonga katika chumba chake.

Kazi iliyokuwako katika kambi ya kazi ya Othaya ilikuwa ngumu. Tuliamka asubuhi sana, na mara baada ya kuhesabiwa, tulibeba tarimbo na vijiko vya mchanga; wakati mmoja tulichimba mitaro na wakati mwingine tulichimba mitaro mipya katika ukusanyaji wa ardhi, na wakati mwingine tulisafiri mwendo wa maili sita kwa miguu, yaani safari ya wakati mwingine na mbili kila siku. Hata ikiwa ni kazi gani, tuliifanya mpaka saa kumi za mchana, bila chakula cha mchana. Hakuna shaka kuwa wafungiwa katika

kambi hii walisukumwa zaidi ya pengine pote nilipojua na hii ilionyeshwa wazi na vile miili yao ilikuwa minyonge.

Ukusanyaji wa ardhi ulikuwa jambo bora lakini uliendeshwa kwa njia mbaya. Kulingana na desturi yetu ya wenyewe wa ardhi, watu wengi walikuwa na mashamba madogo mahali pengi katika nchi. Kazi ya Serikali ilikuwa kusanya mashamba haya, kukata sehemu fulani kwa mahitaji ya watu wote kama skuli, hospitali, vilabu vya vijana, vileleo vya chai au viwanda vya kahawa, na kuweka sehemu iliyobaki katika mahali pamoja juu ya ramani. Mipaka ilitolewa kutoka ramani na kuchimbwa chini katika ardhi. Mwenye ardhi kama hiyo aliulizwa kuweka sahihi kuwa anakubali ardhi hiyo mpya na wakati huo alilipa shilingi kama kumi kwa kila ekari kwa ajili ya kazi hiyo, alipewa Hati ya Ardhi ambayo ilimwezesha kukopa pesa. Ingawa ni mpango uliopendeza, haukuungwa mkono na wananchi. Komiti zake zilikuwa za wale waliokuwa "waaminifu", makarani walipendelea kuhongwa, na wafungiwa hawakuulizwa juu ya ardhi yao bali wakaambiwa ati jamaa wao watawaakilisha. Tena, palikuwako na mapendeleo juu ya mahali mtu atakapopewa ardhi—mahali pabaya au pazuri. Serikali ilifikiria kuwa Hali ya Hatari ilileta hali ambayo iliwezesha ukusanyaji kulazimishwa; ukusanyaji ungeleta maendeleo ya uchumi na ungewezesha wakulima kupata hati ambazo zingewawezesha kukopa pesa kutoka kwa banki. Bila shaka wafungiwa wengi walipoteza ardhi zao wakati huo na kulazimishwa huko kumeleta uchungu mwingi baina ya wengine. Vitakuwa vigumu kwa watetezi wetu kubadilisha mpango huo wakiingia katika Serikali isipokuwa iwapatie watu wengine ardhi ya bure mahali pengine.

Siku ya tatu katika Othaya, niliwaambia wafungiwa wengine ambao walikuwa chini ya uongozi wangu tukiwa Manyani, South Yatta na Athi River, wasimjulishe ye yote, hata askari, kuwa mimi nilikuwa mwenye elimu. Nilikusudia kujifanya pumbavu ili niweze kujua yale yaliyokuwa yakitendeka. D.O. wa huko aliitwa Salisbury, na tulimbatiza "Karuahu" kwa vile alikuwa mnyonge na mkatili na nilikuwa nimeanza kusikia hadithi juu ya vitendo vyake. Nilijifanya mjinga kabisa. Niliwaita askari wa daraja ya chini kama "koplo", makoplo niliwaita "sajini" na masajini niliwaita "sajini-meja" au "kapiteni" au jina lingine lo lote kubwa lililonijia kichwani. Baada ya kujiingiza katika kundi lililokuwa likifagia afisi ya D.O. nilianza kutafuta mambo. Ilionekana kama alikuwa akiuza seng'enge iliyoletwa na Serikali lakini hakupeleka pesa hizo kwa Serikali, bali alizitumia kwa mambo mengine. Tena nilikisia vibaya juu ya pesa zilizohusiana na hospitali ya Othaya na pesa za wafungiwa. Ilionekana ni vizuri kuandika barua nyingine na rafiki wangu kutoka Manyani, Domenico Kihoro aliwahi kunipatia karatasi kutoka stoo. Jumapili yake, niliandika barua

nikijificha kwenye kona moja ndani ya hema ya mablanketi nikilindwa na wafungiwa niliowaamini. Nguvu za barua, na zaidi ilipowafikia wanasiasa huko Uingereza, zilinistaajabisha kila mara, na hiyo ilifyatua mambo.

Komiti ilifika kutoka Nairobi ili kupeleleza hali ya kambi. Askari wa C.I.D. walitumia miezi kadhaa katika Othaya wakiandika misemo ya watu, na ingawa tulisikia kuwa ulikuwako ushahidi wa kuwezesha kesi ipelekwe kortini, Serikali ilipinga mambo hayo yasifike kortini. Hii ni hadithi nyingine ya Kenya ambayo iliambiwa wale waliojua kwa nini Colonel Young aliwacha kazi kama Mkuu wa Polisi mwaka wa 1955. (Sababu za kuacha kazi kwa Col. Young hazijaelezwa lakini kulileta makisio mengi). Au ni kwa sababu hiyo au nyingine ndipo Salisbury akabadilishwa mpaka North Tetu, Divishoni nyingine ya Nyeri. Lakini hakufika huko—alipelekwa katika kambi za "kuokoa" huko Mwea. Afisa mwingine ambaye alikuwa Mwea alikataa kufanya kazi baada ya kuona yaliyotendewa watu humo, na kwa hivyo ndiye aliyepelekwa North Tetu badala ya Salisbury. Salisbury alikuwa mfupi, mwepesi lakini alionekana kama asiyependa kujadiliana kwa maana. Kama maafisa wengine, alionekana mwenye nguvu tele na motomoto na alifurahia nguvu alizopewa na sheria za Hali ya Hatari kama maafisa wale wengine. Lakini hakuwa na huruma, hakuweza kufikiri sana na hakuweza kufahamu kuwa aliowatawala hawakufurahia maongozi yake kama alivyojifurahia mwenyewe.

Siku chache kabla ya kuondoka, aliingia katika kambi na kutukusanya sote hata askari, akatoa hotuba ya kututukana wakati alipokuwa akisema juu ya barua ile niliyoandika. Aliniita mbele ya wote akasema: "Mwangalieni huyu—yeye ni hatari kwa Serikali. Nyote rudini vyumbani vyenu; mtaona kesho." Bila shaka tuliona mambo kesho yake; tulipelekwa kuchimba barabara yenye mwinamo mkali katika Nduyi huko Mahiga, na hakuna aliyepumzika kamwe siku hiyo; tulichimba mpaka jasho likatutoka na kuchanganyika na ardhi iliyopitia kwenye majembe. Askari walikuwa wakali na walimpiga ye yote aliyeonyesha uvivu. Hawakunipiga kwani walionekana kama walioshindwa na uwezo wangu kwa vile ingawa nilikuwa pumbavu, niliwahi kuandika barua kama hiyo. Ukweli ni kuwa si wote waliokubaliana na vitendo vya Salisbury na hawakujali kama nilimtia mashakani, kwani nilisema kweli. Tulichimba barabara hiyo kwa wiki moja mpaka niliporudishwa nyuma kwa "mfereji" hadi kambi ya Aguthi. Nilipoondolewa, kazi ya barabara iliachiliwa. Kusudi la Salisbury lilikuwa kunifanya nidharauliwe kama ilivyowezekana, na wenzangu walikuwa "wameokolewa" kama vile alivyofikiria, angefaulu. Lakini walinipenda hata zaidi na wakaniuliza niendelee kuandika barua.

Othaya ilikuwa kambi mbaya. Kama mtu alipatikana na tumbaku alipigwa bila huruma. Askari waliokuwa huko ni wale wengi wao wali-

kuwa humungati hapo mbeleni, na ingawa walitupiga vibaya vile, hatukuwauliza tulipofunguliwa. Tulisema kuwa ilitupasa tuwasamehe kwani hawakujua vile walivyokuwa wakifanya. Hakuna moyo wa kulipiza kisasi ambao ungeiharibu Kenya. Kila Jumamosi tulikwenda kuoga na kusafisha nguo katika mto wa Thuti. Huo ulikuwa mto ulioanzia milimani, maji safi yakitiririkia kwenye mawe kama yenye imani, mto wa nchi yangu, kilio cha mbali kulingana na uchafu wa mto Tuckwell uliotoweka mchangani au bahari kubwa ya Saiyusi. Kote kuzungukia kulikuwa na mashamba yaliyolimwa na Wakikuyu, na ilikuwa vizuri kuona miwa, mahindi na mimea mingineyo kama ndizi kwa mara nyingine. Kila mahali vileleni vilionekana vijiji ambavyo vilijengwa wakati wa hatari hapo mbeleni. Sisi hatukupendelea kuishi namna hiyo, kusongamanishwa pamoja bila uhuru na maisha ya jamaa yakiachiliwa ovyo machoni mwa dunia. Nilipokuwa nimeketi chini nikijifunika kwa blanketi iliyonichoma nikingojea nguo zangu zikauke, nilifikiri juu ya mambo hayo na mageuko yatakayokuwako baada ya muda mfupi.

Siku za Jumapili tulikubaliwa kwenda nje ya mlango mkubwa kwenye mahali palipopanuka, huko tukizungukwa na askari, tulikubaliwa kusema na jamaa wa nyumbani bila kupingwa. Hiyo Jumapili ya kwanza, jamaa zangu walifika wengi. Shangazi wangu Wangui, ambaye niliishi naye huko Bafuni nilipotoka Uganda; msichana wake Nyakinya; dada yangu Njoki ambaye alikuwa ameolewa na John Kimondo; dada yangu Wangui aliyeolewa na Gatiyu Wambura tuliyefungiwa naye South Yatta; jamaa wengine—Simon Gachiengu na Godfrey Mugweru, na msichana wangu kwa desturi aliyeitwa Wangari ambaye ameolewa na mtu wa Nairobi—yeye ni msichana wangu kwa desturi ya Kikuyu kwa vile yeye ni msichana wa Nyakinyua, msichana wa shangazi yangu Wangui. Wote walilia sana waliponiona lakini mimi nilikuwa nimepotewa na machozi kwa hivyo nikawasihi wasilie kwani kufungiwa ni kitu ambacho wale wote wanaopigania uhuru lazima wapitie ndani yake. Walikuwa wameniletea ndizi, *njahi*, maziwa na tulikula na kunywa sote pamoja hapo nje.

Sikumwona mama wakati huo na nikamwuliza Wangui kama alikuwa mgonjwa. Ndipo Wangui akanieleza pole pole kuwa Mary Wanjiku, mama wangu, alifariki Januari, 1958 wakati nilipokuwa Athi River. Niliduwaa kwa muda na nikamwuliza arudie vile alivyosema. Alirudia maneno hayo. Nilikaa kimya kwa muda wa dakika tano na mara nilijisikia kama nitalia moyo wangu nje, lakini sikuweza kufanya hivyo mbele ya watu zaidi ya mia saba. Mate yangu yalionja uchungu, kichwa changu kiliuma na sikuweza kuona barabara. Baada ya muda fulani nilijisikia mwenyewe tena, nikajaribu kucheka na wajamaa hawa nikawaambia:

"Msisumbuke, hili ni deni ambalo sisi sote tutalipa. Mama amelipa lake na sisi tutalipa letu wakati wetu ukifika na kila siku inaukaribisha wakati huo." Tuliendelea kula chakula chetu lakini tulikuwa na huzuni mpya.

Kwa desturi ya Kikuyu hakuna anayependelewa sana kuliko mama wa mtu. Kwa miezi tisa anambeba mtoto tumboni mwake mpaka wakati wa uchungu wa kuzaa. Halafu mama humtunza mpaka anakuwa mtu. Mama wangu alikuwa amejaribu sana kunipatia elimu wakati nilipokuwa kijana. Miaka minane ilikuwa imepita tangu siku ya mwisho nilipomwona na sasa hakuweza kuona mazao ya jitihadi zake. Sikuwa na kitu cha kunikumbusha yeye—hata picha—ya kunikumbusha uso wake mzuri na mkarimu na wenye busara. Wakati mmoja aliniambia kuwa kitu alichotaka kuona sana ni msichana ambaye nitaoa na sasa haya hayakuwezekana. Hii ndiyo sadaka kubwa ambayo nilitoa katika kupigania uhuru. Ni vigumu kueleza thamani ya maoni yangu juu ya Wazungu. Tunaonelea kuwa uhusiano baina ya mwanaume na mwanamke ni ushirika wa kuheshimiana na kupendana, kusudi lake likiwa ni kuzaa na kulea watoto. Ushirika huo huendelea ukawa ni kama ushirika wa roho mbili ingawa si kila mara hufanyika hivyo na pengine ni kwa muda tu. Tunayo methali isemayo kuwa "*Mama wa mtu ni kama Mungu wa pili*," na kunao uhusiano baina ya mama na mtoto wake ambao hupita mambo mengine ya kibinadamu. Hakuna uhalifu ukemewao zaidi kuliko kumtukana au kumpiga mama na aibu ifuatayo kitendo kama hicho haiwezi kulinganishwa na inayofuata kama kitendo hicho kimefanyiwa bibi wa mtu. Habari ya kifo chake ziliniumiza zaidi ya mateso yote niliyofanyiwa katika kambi zote.

Nilijua baadaye kuwa wengine wao walipendelea nisiambiwe vile alivyokufa kwani walifikiria ningeweza kujitendea vibaya. Baadaye waliniambia kuwa alipatikana na ugonjwa wakati ule wa kafiu ya masaa ishirini na matatu iliyowekwa wakati Hali ya Hatari ilipochacha. Baada ya kutibiwa na wamisheni wa Katholiki, alipona lakini akaugua tena, mwili wake ukavimba na hata macho yake hayakufunguka. Miezi ya maumivu makubwa ilimalizika kwa kifo chake.

Wakati filimbi ilipolia ya kumaliza kuonana kwetu na jamaa, nilirudi ndani ya kambi, na usiku huo na nyingine zilizofuata, blanketi yangu haikukauka machozi na nilisali kwa ajili ya roho ya mama.

Mnamo Juni 24, 1958, nilifika Aguthi (Nyeri) kambi ya kazi wakati nilipotoka Othaya, na hiyo ndiyo ilikuwa kambi ya kumi na moja ambayo nilifungiwa. Ilikuwa imegawanywa katika visehemu vinane na kila kimoja kilikaliwa na wafungwa mia moja na ishirini. Ilizungukwa na seng'enge ya stima, na aliyeumia ni mmoja tu ambaye alikuwa ni mpenzi wa askari ambaye alisahau kumweleza juu ya hatari hiyo walipokuwa wakifanya mipango ya kukutana. Kambi hiyo ilikusudiwa kukaliwa na watu

wa Nyeri ambao waliletwa kutoka Mwea, Manyani na Athi River. Baada ya kukaa Aguthi kwa muda, watu walipelekwa katika sehemu zao ambako walifunguliwa na kurudi kwao nyumbani. Mwisho wa 1958, Gavana alikata shauri kwamba wengi wa wale waliofungwa mbele ya korti kwa makosa madogo ya ki-Mau Mau wapunguziwe kifungo chao, akaweka sahihi nyingine iliyowafanya wafungiwa wa kawaida kama sisi waweze kuachiliwa kwa njia ya "mifereji". Wengi wa hao walikuwa wamehukumiwa kufungwa miaka kumi na miwili hadi kumi na minne. Katika jela walifanya kikundi chao ambacho hakikuhusiana na mahabusu ambao walikuwa wahalifu wa kawaida, yaani wevi na kadhalika, ambao walijulikana kama "Mahuru Kanga." "Mahuru" ni jina la mwewe kwa Kikuyu na walipewa jina hilo kwa sababu waliibiana na kutukanana, kupigana na kulalana: hawakujiheshimu na walikuwa kama wanyama wasio na aibu na walikula takataka na nyama ya vitu vilivyokufa. Mahabusu wa 'Mau Mau' walikuwa na umoja kamili, na tabia zao zilikuwa za juu. Wale waliokuwa katika jela ya Nyeri walipelekwa Aguthi wakiwa vikundi vya watu thelathini kila wiki. Vile vitendo vilivyotendewa wafungiwa wapya katika Mwea vilifika Aguthi. Wakati mahabusu walipofika huko, walionyeshwa ubao wa kuwekea ilani wa kambi ambako paliandikwa kwa herufi kubwa: "MWITEITHIA NIATEITHAGIO" ambayo ni kusema "ANAYEJISAIDIA HUSAIDIWA." Waliambiwa kuwa walipewa dakika kumi na tano ili wafikiri kama walitaka kujisaidia au sivyo. Wale waliokubali walipelekwa ndani ya kambi mara moja, lakini wale wengine ambao walikuwa wengi walipelekwa kwenye mashimo ya adhabu. Mashimo hayo hayakuwa na kazi isipokuwa yalitumiwa kuwafanya watu kuungama bila kufanya alama juu ya mtu. Mashimo haya ambayo yalichimbwa kwenye mchanga mwekundu yalikuwa futi sita upana, futi kumi na mbili urefu, na futi kumi chini. Mtu aliambiwa kuingia ndani ya shimo, achimbe udongo kidogo, halafu apande juu kwa upande wa shimo huko akibeba ndoo yenye udongo aliochimba kwa kichwa chake. Hicho kitendo cha kupanda kilifanya mikono ya mwenyewe iwe na kazi ya kupanda (badala ya kushikilia ndoo) na ninakumbuka niliona kwa macho yangu vile mahabusu mmoja alianguka nyuma ndani ya shimo na ile ndoo ikamwangukia kifuani. Aliumia sana. Walipotoka ndani ya shimo walionekana kama panya wekundu, kwani nywele na miili yao ilijazwa na vumbi la udongo mwekundu.

Ikiwa walikuwako zaidi ya kiasi kilichoweza kuingia mashimoni, wengine walifanywa kukimbia kiwanjani wakibeba ndoo zilizojazwa pembe za mawe. Wakati nilipofika huko, Mwafrika ambaye alikuwa mkuu wa kambi aliitwa Micah, aliyebatizwa "Speaker." Micah alikuwa shujaa na niliheshimu vipawa hivyo vyake. Yeye hakuogopa cho chote

wala mtu. Mbele ya Hali ya Hatari, alikuwa mfanyi biashara, na vitendo vyake vya zamani havikuonyesha kuwa alipendelea Serikali. Kama alipigania upande wa wananchi, angalikuwa jemedari mkuu, lakini kwa sababu ambazo mimi sijaweza kufahamu, alienda upande wa Serikali. Akiwa mwenye umri wa miaka kama arobaini wakati huo, aliendelea kuendesha shughuli za biashara zake huko Fort Hall. Alizoea kutuogofya kwa kutuambia kuwa yeye mwenyewe alikuwa amewaua magaidi mia mbili na haikuwa shida kusadiki aliyoyasema. Alikuwa mmojawao walioanzisha magaidi wa kuiga, vile vikundi "waaminifu" na magaidi waliorudi msituni wakajifanya kama magaidi. Micah sasa ameacha kazi ya Serikali ambayo alipata daraja la District Assistant, na anaendesha kazi yake ya abiria za motakaa. Wakati mmoja, watu waligomea bas yake: walisema: "Usiingie ndani yake au utakufa."

Siku moja, mahabusu wapya walifika Aguthi kutoka jela ya Nyeri, na nilishuhudia kutoka nilipokuwa vile walivyotendewa. Walipigwa vibaya sana na zaidi wawili wao—Kabugi Njuma na Gachii Karanja. Micah mwenyewe ndiye aliyetayarisha waliyotendewa na Kabugi alikufa baadaye siku hiyo hiyo. Gachii alilala ndani ya hospitali ya kambi kwa siku kadhaa bila kuweza kutembea wala kusema na hata sasa yeye ni kiwete. Siku iliyofuata nilikwenda Nyeri kusaidia kujenga Provincial Red Cross Training Centre na nilipokuwa huko nilipanga juu ya kupatiwa karatasi ya kuandika, na Jumapili iliyofuata nilijifungia ndani ya choo nikaandika kila kitu kilichotendeka. Wafungiwa wengine walichunga nisije nikakutwa na afisa. Hali ya mambo katika kambi ilijikaza na maafisa walikuwa na wasiwasi mwingi juu ya yale yangaliotokea kwa ajili ya kifo hicho. Nilimpa Irungu barua hiyo, naye alikuwa mmoja wa madereva ambaye alifungiwa nami huko Manyani na aliyejua kuwa singemwendea kinyume hata wanifanye nini. Barua hiyo ilitumwa kwa marafiki wangu wa kawaida wa Uingereza na Kenya.

Baada ya upelelezi kufuatia barua yangu, Micah alihukumiwa kufungwa jela miaka miwili. Bi. Barbara Castle, M.P., alipeleka habari hiyo mbele ya House of Commons huko Uingereza. Wakati wa kusamehewa mahabusu kwa Desemba 1959, Micah alisamehewa na Gavana. Wengi wetu walifikiri kuwa ingawa alifungwa, maafisa wengine walimlinda. Kama yale yaliyotendeka Hola, tukio hilo lilifuatana na mpango uliokuwa waoza kwa kila njia. Ilionekana kama Serikali ya Kikoloni ya Kenya ilikuwa imepotewa na moyo na haikuweza tena kujua tofauti baina ya wema na ubaya.

Mnamo Oktoba 1958, nilipelekwa katika kambi ya kazi ya Showground karibu na mji wa Nyeri. Ingawa kambi hiyo haikuwa imejengwa vizuri, hapakuwa na mapigano na tuliweza kuvuta hewa kwenye moshi wa nyumba zetu, moshi ambao ulitoka baina ya mawe matatu na ulionuka mbuzi

na nguo, ambao ulipitia kwenye maezeko ya nyumba na kukaa hewani kwa rangi ya buluu—huko juu ya vijiji vya wananchi. Baada ya muda mfupi nilipofika huko, afisa mpya wa Othaya aliyeitwa John Stein aliingia ndani ya kambi akatuambia kuwa yeye hakupendelea kuona watu wa Sehemu yake wakiwa ndani ya seng'enge na kuwa tungeachiliwa. Mnamo tarehe Desemba 9, 1958, tulipelekwa katika kituo cha polisi Othaya ambako askari wa polisi aliyeitwa Kariithi alituambia: "Sasa ninyi mmepata uhuru kurudi kwenu nyumbani. Kila mmoja wenu lazima kwanza kwenda katika afisi ya Chifu wenu na kumwarifu kwamba mmefika. Halafu mwende kwa Hedimeni wa kijiji chenu na kumwarifu kuwa mmefika. Ni lazima muwe mkiripoti kwa chifu kila Jumatano. Mtakuwa mkifanya kazi ya wote, 'gitati', kila wakati mkiamriwa na Hedimeni wenu. Kama amri ya kafiu ikiwekwa, ni lazima muitii kwa sababu hiyo ni sheria. Hayo ndiyo tu niliyoulizwa niwaambie."

Nilitembea nje ya mlango wa stesheni ya polisi nikiwa mtu huru kwa mara ya kwanza. Nilikuwa huru, huru, huru kukimbia, kucheza dansi, kupiga kelele na kuimba. Lakini hewa haikuonja tofauti, vilima vilionekana kama vilivyokuwa zamani na nyuso za watu hazikuwa zimegeuka. Nilijaribu kukimbia kidogo na kuimba na hakuna aliyenipinga. Hizo amri na kupigiwa kelele na kupigwa hazikuwako tena. Nilitembea pole pole kuelekea nyumbani kwetu, huko nikimwamkua ye yote niliyemkuta kwa furaha, rafiki wangu, kila mmoja duniani alikuwa rafiki wangu siku hiyo. Tulikuwa kikundi tulipofika kijiji cha Kariko katika nyumba ya Wangui. Ilikuwa miaka kumi tangu nilipokuwa humo.

Tulipokuwa kifungioni, tulikuwa tukizungumza juu ya siku hiyo ya kwanza ya uhuru. Tungechinja beberu na kuila pamoja na wajamaa jioni ya kwanza. "Usiwakubali wakuchinjie kuku, Mwangi, si kubwa kutosha na hivyo ni kusema utarudishwa kifungoni tena. Mbuzi, beberu kamili, hakuna zaidi au chini yake." Wakati Wangui alipokutana nasi jioni hiyo, alisema kuwa tutafanya sherehe. Kabla ya mama wangu kufa, Wangui alisema, alionyesha jogoo ambaye ningechinjiwa iwe nyama ya kwanza niliyokula baada ya kufunguliwa na kurudi nyumbani. Furaha yangu ilipoa kidogo. Ni lazima tule jogoo kwa sababu hilo ndilo lilikuwa pendekezo la mama. Zaidi ya hayo, hakuna angaliyeweza kunitia ndani tena na huyo beberu tungemla wakati mwingine. Kitu kilichokuwa kikubwa ni kusherehekea uhuru wangu siku hiyo na kujitayarisha kupigania uhuru wa nchi yetu kesho yake.

9 Chama kipya cha siasa chabuniwa

USINGIZI WANGU wa kwanza nikiwa huru ulisumbuliwa asubuhi na mlio uliosikika kama ni wa simba. Nilipomwuliza Wangui ni wa nini mlio huo, aliniambia kuwa ni sauti ya binadamu, ikitolewa kwa chombo cha kupasa sauti, ikiwaita watu waende wakafanye kazi ya lazima. Baada ya kunywa kikombe cha chai, nilichukua jembe na kijiko nikamfuata Wangui hadi kwenye kambi ya Humungati kileleni cha kijiji. Hapo, watu wazima, waume kwa wake, walikusanyika vikundi vikundi na nikaambiwa nijiunge na kikundi kimoja ambacho kilitumwa kuchimba mitaro katika shamba la mmoja mwenye bahati. Kunayo nafasi ya kazi ya wote katika nchi zilizo nyuma kama vile kujenga skuli, hospitali na barabara ambazo hazi-wezekani kwa njia nyingine. Lakini ni lazima watu wenyewe wakubaliane na komiti zao zipange ni mambo gani yatafanywa kwanza. Kuwatumia watu kufanya kazi bila wao kukubali na zaidi katika kutengeneza mashamba ya wengine si haki.

Ingawa ilionekana jambo geni kuwa baada ya miaka mitano ya kufungiwa sikuruhusiwa asubuhi moja nyumbani, nilitaka kwenda kujua kazi hiyo ya "gitati" ni ya aina gani. Kila mtu alipewa sehemu ya kuchimba na bibi wa kuondoa mchanga. Nilifanya kazi na Kamuyu, bibi wa mmoja wetu, na kwa vile nilikuwa nimezoea kazi ngumu katika kifungoni, sikuona shida kama wengine. Mambo yalikuwa kama hivyo siku ya kwanza na siku ya pili. Wakati huo, niliona kuwa hedimeni aliwachagua wanawake fulani kwenda kumtekea maji na kumletea kuni. Kwa vile yeye alikuwa na bibi na zaidi alikuwa analipwa mshahara, sikuona haki yake kuwatendea wanawake wengine namna hiyo. Baada ya siku nne katika "gitati" nilionelea kuwa nimepata ya kutosha. Au nilikuwa huru au nilikuwa ningali mfungiwa: wakati huo, nilikuwa kama punda aliyefungwa kwa kamba ndefu badala ya kamba fupi. Nchi yote ilionekana kama imefungiwa, vijiji vikiwa kama kambi za kazi. Hatukuwa huru. Kwa hivyo nilimwambia Hedimeni kuwa mguu wangu wa kulia ulikuwa waniuma sana na kwa hivyo sikuweza kuendelea. Alinipa ruhusa ya wiki moja lakini hakuonekana kuwa mwenye furaha kunipa ruhusa.

Wengi wa wafungiwa waliofunguliwa mbele yangu walinitembelea siku hizo za kwanza za uhuru wangu na walifurahi sana kuniona ningali uhai kwani walikuwa wameambiwa kuwa nilifarikia Athi River. Wakati mwingine nilitembelewa na watu thelathini na jioni moja tuliimba pamoja ndani ya chumba kimoja—tuliimba Wimbo wa Afrika na Wimbo wa Kenyatta katika Kapenguria:

WIMBO WA KENYATTA KATIKA KAPENGURIA

1. Wananchi wafundishwe siasa na uwezo wa Kenyatta
   Wale wenye moyo mgumu walivumilia kufungwa
   Wale wenye roho nyonge wakawa *tutimu* (humungati).
   Kiitikio
   Hahii! Hivyo ndivyo kutakuwa na furaha
   Kwa wale watakaoshinda
   Ufalme wa Kenyatta
   Nchi ni ya Waafrika.

(Kesi ya Jomo Kenyatta ilifanyiwa Kapenguria na hakimu R. S. Thacker, Q.C.; wakili D. N. Pritt, Q.C., aliongoza waliomtetea Kenyatta. Baada ya Kenyatta na wengine watano kuhukumiwa, rufani ilifanywa katika Korti Kuu ya Nairobi, korti ya masettla, na ikakataliwa. Barua ya kufanya rufani kwa Privy Council huko London pia ilikataliwa).

2. Mrehemisha wa mataifa yote ni Jomo
   Naye alipata taabu nchini Kapenguria
   Alipotaka kutoa maisha yake yawe sadaka
   Mungu akampa uwezo mwingi tukafurahi mno.

3. Walikuwako mashahidi arobaini katika Kapenguria
   Walipofika kortini walishindwa na kesi
   Pritt aliwauliza maswali wakaaibika sana
   Thacker akawaambia "twende zetu"
   Nchi ni ya Waafrika.

4. Kesi ilipotoka Kapenguria ilipelekwa Kitale
   Pritt aliisimamisha akasema alitaka kwenda kwanza
   Alipofika Ulaya alirudi na wenzake watatu
   Ambao wangepeleleza ukweli bila ubaguzi.

5. Waliposikiliza kesi walisema Jomo awachiliwe
   Lakini wenye ubaguzi walikataa
   Wakasema "utakwenda Nairobi mbele ya korti ya masetla."

6. Ilipofika mbele ya korti ya masetla Nairobi
Attorney alihukumu kama Kapenguria
Pritt akasema itakwenda Ulaya kwa korti ya Mfalme
Ikaangaliwe kwa haki bila ubaguzi.

7. Ilipofika kortini ya Mfalme huko Ulaya
Attorney aliangusha faili akaanza kutoroka
Pritt akawaambia hakimu kuwa nimekuwa nikiwaambia
Kuwa ufalme ni wa Kenyatta
Nchi ni ya Waafrika.

Asubuhi yake, Hedimeni aliniripoti kwa Chifu wa Lokesheni ya Chinga, aliyeitwa Gachichio Wamiti, ambaye alikuwa mzee mgumu ambaye hapo mbeleni alikuwa sajenti-meja wa askari kanga (aliwacha kazi 1961). Gachichio aliniamuru niwe nikimwarifu Hedimeni jina la mtu ye yote aliyenitembelea na vile alikuja kufanya kwangu. Ingawa amri hiyo ilionekana isiyo ya kawaida, nasadiki kiko kifungu katika Sheria ya Utawala wa Wananchi (Native Authority Ordinance) za Kenya ambacho kinaweza kutumiwa kwa njia hiyo ingawa nina shaka kama Korti Kuu ingekubaliana nacho.

Jioni moja, kwa mara ya kwanza, sikuwa na wageni, na tuliketi kuzunguka moto na hapo nikamwuliza Wangui anieleze vile mama wangu alivyofariki. Roho yangu ilikuwa kama ya ngozi na nilifikiri ningeweza kuvumilia kujua ukweli. Nilisikiliza juu ya taabu zilizowapata watu wakati wa kafiu mwaka wa 1955 na 1956.

Wakati kengele ililia kijijini, wengine lakini si wote, walikubaliwa kukusanya chakula kwa muda wa saa moja wakiwa wamechungwa. Kulima na kupanda kulikuwa karibu hakuwezekani kulingana na hali hiyo na mahindi mengi yaliharibiwa kwa vile ilifikiriwa kuwa magaidi wangejificha humo. Sehemu yenye upana wa maili moja ukingoni wa msitu ilifungiwa watu na ye yote akionekana huko alipigwa risasi. Kwa ajili ya kufungiwa kwenda namna hiyo, watu hawangeweza kutorokea mahali pengine au waweze kuletewa chakula na jirani waliokuwa na bahati ya kuwa na chakula. Njaa na vifo vilitawala nchi, vikawatwaa wengi wa wanawake na watoto wetu. Ni wakati huo ambao mama wangu, Wanjiku, aliugua, na mama mdogo Gathoni na dada yake Nyakio walikufa, na maelfu ya watoto, wakisindikizwa na njaa, walitorokea mijini kama Nairobi na kutafuta riziki ndani ya mapipa, huko jamii zikavunjika na hali hii ingali yatusumbua hata leo.

Kwa muda mfupi nilioishi nyumbani, nilipanda chai na "pyrethrum" katika shamba nililogawiwa wakati wa ukusanyaji wa ardhi. Niliona kuwa shamba hilo lilikuwa kama ekari tano kasoro ya eneo lake la hapo

mbeleni. Mavuno ya shamba hilo ni ya thamani sana kwa jamaa wangu. Shangazi yangu na wanawake wengine walinishawishi nioe kwa vile sasa nilikuwa mtoto asiye na wazazi. Lakini maisha yangu ya usoni yalikuwa ya wasiwasi kwani nilifikiria ningekamatwa tena na kwa hivyo nikawaambia kuwa huo haukuwa wakati wa kufikiria mambo kama hayo.

Baada ya kuzungumza na marafiki wengi kutoka wilaya yote nilikata shauri kuwa tulihitaji chama cha siasa na kuwa ilinilazimu nianzishe kimoja. Ikiwa hatukufanya kitu ule uchungu uliokuwako baina ya "waaminifu" na wafungiwa ungeenea sana na tungepotewa na nafasi ya kufanya umoja, hali ambayo ingechelewesha uhuru wetu. Kutokana na mazungumzo yangu na D.O. na Chifu, ilionekana wazi kitu cha mwisho kile Serikali ingependelea ni kufanya chama cha siasa katika wilaya ya Nyeri. Katao lao lilionyesha udogo wa ubongo wao na ilikuwa wazi kuwa walihitaji kuelimishwa kugeuza fikira zao za wakati wa Hali ya Hatari. Nilijisikia mwenye maana nilipofahamu kuwa vitendo vyangu vilikuwa vyapelelezwa na Serikali. Walianza kunifuata baada ya barua niliyoandika Nairobi nikalalamika juu ya wanawake kufanyizwa kazi ngumu ya lazima. Tangu wakati huo nilikuwa na kazi ya kumwandikia Mkuu wa Jela barua za kumwuliza pesa za wafungiwa wengine zirudishiwe wenyewe pamoja na vitu vyao vingine. Nilikuwa nimefaulu kiasi katika hatua zangu na nilimsaidia James Thuku Mangothi kwa njia hiyo baina ya wengine.

Nilisikia kuwa Serikali ilikusudia kunifungia tena kwa hivyo haraka ilikuwa muhimu. Niliwatembelea wafungiwa wengine katika yale madivishoni mengine kwa haraka—yaani South Tetu, North Tetu na Mathira. Niliungwa mkono kote nilikokwenda na nikakata shauri kuendelea mara moja. Asubuhi moja, mtu mmoja kutoka North Tetu aliyeitwa Kigango alinitembelea kijijini cha Kariko akaniambia kuwa Mutahi Chiuki, aliyeendesha mkahawa mjini Nyeri, angependa nimtembelee kijijini cha Gatitu. Tulizungumza kwa muda mrefu halafu akanipeleka kumwona Wanjohi Mungau, aliyeandika gazeti lililoitwa "Habari za Kenya", ambalo lilionekana mara kwa mara pesa zilipopatikana, na ambalo lilipinga Serikali kwa nguvu. Wanjohi alionekana kuwa mwanasiasa mwenye uwezo na alikubaliana mara moja na wazo letu la kuanzisha chama kipya cha siasa katika wilaya. Wakati huo tulikuwa kikundi cha watu kumi na tulizungumza ndani ya chumba kidogo kilichokombolewa katika Majengo ya Nyeri na kilichokuwa kama afisi ya gazeti hilo. Tulikusanya shilingi mia tatu baina yetu na Wanjohi na mimi tulipewa madaraka ya kutengeneza katiba ya chama, tuipeleke Nairobi ili kuonana na watu wengine ambao wangetushauri na kutusaidia.

Wakati huo ilikuwako sheria kuwa ye yote aliyetaka kwenda Nairobi lazima apate pasi kutoka kwa D.O. Hakuna afisa angenipa pasi kama

hiyo na kwa hivyo tulifikiria kwenda Nairobi wakati wa matembezi ya Mama wa Malkia huko Nyeri mwezi wa Februari, 1959, wakati kila polisi angekuwa amefanya laini kwenye barabara na hangekuwa na nafasi ya kuuliza pasi. Tulipofika Nairobi, tulienda mara moja afisini ya Henry Clement Wariithi, wakili Mkikuyu ambaye baba yake tulifungiwa naye katika kambi ya kazi ya Aguthi, na tulimkuta wakiwa na mwingine aliyetoka South Tetu aliyeitwa Kaburu aliyekuwa karani katika Royal Technical College. Wariithi baadaye alikuwa wakili wa Jomo Kenyatta. Walitukaribisha ajabu na mara tulikubaliana juu ya mawazo ya siasa.

Siku iliyofuata tulikutana na maafisa wawili wa chama cha Nairobi Peoples Convention Party, Elijah Omolo Agar, aliyekuwa Katibu mwendeshaji na Joseph P. Mathenge, aliyekuwa katibu mkuu wa chama hicho. Mathenge ambaye alikuwa mvulana wa mzee wa korti ya kienyeji katika Othaya na ambaye alikuwa amefukuzwa kutoka Makerere College, alifurahia sana kuniona na akaniambia kuwa wafungiwa wengi walikuwa wamemwambia juu ya taabu zangu na uongozi wangu katika kambi nilizofungiwa. Omolo Agar alihamishwa baadaye akapelekwa Lamu kwani alikisiwa kuwa aliendesha mambo ya Kikomunisiti na hakufunguliwa mpaka mwisho wa 1961. Siku ya tatu tulimkuta Tom Mboya aliyesema kuwa alipokea barua zote nilizompelekea kutoka kifungioni na kuwa alikuwa akijaribu awezavyo kufanyiza uchunguzi juu ya malalamiko yangu na yaliyo maovu yaondolewe. Tulimweleza vile tulivyokusudia kuanzisha chama cha siasa na alituongeza nguvu tuendelee na mpango wetu. Tulizungumza juu ya hatari ya kueneza ukabila kwa kuwa na vyama kadhaa vya kila wilaya badala ya kuwa na chama kimoja cha nchi yote, lakini tulikubaliana kuwa kwa vile ilikuwako sheria iliyopinga kuwako kwa chama cha wananchi wote, hatukuwa na lingine isipokuwa tuanzishe cha wilaya. Tom Mboya mwenyewe alitaka kupanua N.P.C.P. katika wilaya zote, lakini hatukuona njia ya kufanya hivyo bila kuvunja sheria. Alitualika kukaa kwake bure huko Ziwani Nairobi kwa muda tuliokuwa Nairobi.

Siku ya nne, N.P.C.P. ilikuwa na michezo ya kienyeji katika lokesheni ya Kaloleni, Nairobi, na tulialikwa kuhudhuria. Waimbaji waliimba vizuri sana zile nyimbo za siasa, lakini wimbo ninaoukumbuka sana ni ule ulioimbwa kwa Kiswahili na mtungaji wake mwenyewe, Mhindi aliyeitwa H. Ambu Patel. Maneno yake yaliwakilisha mapendekezo ya wananchi na yalimtaja Jomo Kenyatta na viongozi wengine mara nyingi. Nilikutana na John Stonehouse, Mjumbe wa Bunge wa Leba wa Uingereza sehemu ya Wednesbury na alipendezwa sana na hadithi yangu ya maisha ya kuhamishwa na zaidi alitaka kujua zaidi juu ya alama iliyoonekana gotini langu la kulia baada ya tukio la Athi River. Ameeleza juu ya mkutano wetu katika kitabu chake kinachoitwa "Prohibited Immigrant" (Mgeni Marufuku).

Pia tulimwona Dr. Kiano, aliyewakilisha Kiambu na Fort Hall na alituambia kuwa alikusudia kuanzisha vyama vya siasa katika wilaya hizo mbili. Alicheka alipotuambia kwa Kikikuyu: "*Mundu ndatigaga gwake gukihia agathii guthara kwene*" yaani "mtu hawachi kwake kukichomeka akaenda kupoza moto kwa jirani." Tulicheka aliposema hivyo na hakutupa shauri lingine ingawa aliahidi kuonana nasi tena ili tuzungumze juu ya kupanua *Habari za Kenya* liwe gazeti la kitaifa. Usiku wa mwisho tulikaa na Henry Wariithi tukizungumza juu ya katiba ya chama chetu kipya, ambacho tulikipa jina la Nyeri Democratic Party—N.D.P.

Ilipendeza kuiona Nairobi tena baada ya miaka mingi hivyo. Umbo lake lilikuwa limegeuka kabisa kwani kila mahali palikuwa na nyumba mpya ndefu isipokuwa katika malokesheni ya Waafrika ambayo yalikuwa yapasuka kwa ajili ya wingi wa watu. Niliona mabadiliko mengi katika watu. Wengi wa wasichana Wakikuyu walivaa mavazi ya kuvutia na wanaume walionekana kama wote walivaa masuti. Katika mambo ya siasa, Nairobi ilikuwa yaendelea kasi kwa ajili ya mpango mzuri wa N.P.C.P. na kile kingine kilichoitwa Nairobi African District Congress, na nilifikiri kuwa si vizuri wilaya za risavu ziachwe nyuma. Ikiwa hatukuweza kuanzisha matawi ya chama kimoja cha nchi yote, ilitubidi tuanzishe vyama vya wilaya na kwa haraka pia.

Tuliporudi Nyeri, tulitengeneza katiba yetu tukitumia nyumba ya mmoja aliyefungiwa, Kimunya Kamana wa huko kijiji cha Gatitu. (Kimunya sasa anafanya kazi ya kukusanya kodi ya nyumba kwa Nakuru Municipal Council). Katiba hiyo ilichapwa na Daniel Motoku, kijana wa yule mzee Kirori Motoku, tuliyefunganishwa pingu katika ndege tulipohamishwa kutoka Kisumu hadi Lodwar. Hawakuwako Vijana wengi wenye elimu ambao walikuwa na ushujaa wa kufanya mambo kama hayo katika Jimbo la Kati la Kenya. Jioni ya Februari 20, 1959, katiba ilikuwa tayari na lililobakia ni kuituma kwa Mwandishi wa Vyama (Registrar of Societies) ili chama chetu kiandikishwe tuweze kuanza mambo.

Nililazimishwa kuvunja sheria kwa kwenda Nairobi bila pasi. Pia nilivunja masharti mengine ambayo chini yake tulipaswa kukaa katika lokesheni pasipo kutoka nje yake bila ruhusa ya Chifu. Serikali ilijua vile nilivyokuwa nikifanya kutokana na wapelelezi wake, na polisi walikuwa wananiwinda. Niliambiwa hivyo na wapelelezi wangu na nilingojea kukamatwa saa yo yote. Lakini hiyo haikuwa kitu kama niliwahi kukamilisha katiba mbele ya kushikwa. Ilikuwa wazi wakati huo kuwa wazo la kuwa na chama kipya cha siasa liliungwa mkono na wote katika wilaya, chama ambacho kingetuwezesha kusema wazi yale tuliyotaka kwa Serikali kwa njia ya kidemokrasi kufuatia katiba yetu.

Mnamo saa sita za usiku wa Februari 20, 1959, nilikuwa natayarisha matangazo ya *Habari za Kenya* wakati Wazungu wawili waliingia chumba changu wakaniuliza kama mimi ndiye Josiah Mwangi. Niliwajibu kuwa mimi ndiye na hapo wakaniambia twende nao katika stesheni ya polisi ya Nyeri. Nililala ndani ya "cell" usiku huo bila blanketi na kulikuwa baridi sana kwa sababu stesheni hiyo ilijengwa zamani sana wakati ambao starehe za wafungiwa hazikufikiriwa. "Habari za Kenya" zilitangazwa siku iliyofuata na ndani yake yalikuwa maneno yangu juu ya mawazo na maongozi ya N.D.P.

Nilipelekwa stesheni ya polisi ya Othaya ambako niliulizwa maswali na D.O. mpya aliyeitwa Henley. Huo ulikuwa wakati wangu wa kwanza kukutana naye na hatukusikilizana. Aliniambia kuwa tangu nilipofunguliwa, nilikuwa nimetenda mengi ambayo yalishangaza Serikali. Nilikuwa nimejifanya D.C. mdogo katika wilaya na atajaribu kunifungisha tena. (Ole wangu—kwa nini sikusisitiza kuwa beberu achinjwe pamoja na kuku wa mama?) Kama hayo hayakuwezekana alisema ataona kuwa nimeondolewa kutoka divishoni yake: wakubwa wawili hawawezi kukaa pamoja. Nilimjibu kuwa kama nikifungiwa tena, haitakuwa ni sababu nilifanya makosa bali ni kwa sababu nilisema ukweli. Wakikuyu husema kwamba "maji ya mwenyewe hayamwachi". Ikiwa yangali yalikuwako maji ambayo nilikuwa bado kunywa nilipokuwa kifungoni, basi ningerudi na kuyamaliza. Hiyo ilikuwa ni kama hali iliyotarajiwa na umbile na hata yeye hangeweza kuipinga. Henley hakupendezwa na majibu yangu na kesho yake alimwita D.C. Burton aliyefika kuniona ndani ya "cell" yangu. Burton alikuwa mtu wa kuaminiwa na mkarimu, askari wa kawaida ambaye mambo ya siasa na wanasiasa walimsumbua roho. Aliniuliza kwa nini nilianzisha chama cha siasa na kwa nini nilikwenda Nairobi bila pasi. Nilimjibu kama nilivyomjibu D.O. na hapo waliniacha wakifanya mazungumzo kwa makini.

Niliondolewa kutoka stesheni ya polisi nikapelekwa katika kambi inayofungiwa wahalifu wadogo. Nilipokuwa humo, mamia ya watu walifika kuniona, kuzungumza nami huko wakanitia nguvu niendelee kufanya kama nilivyokuwa nikifanya. Wanjohi Mungau alifika kuniona kutoka Nyeri na tulisema naye akiwa nje ya seng'enge. Nilimwambia kuwa ile katiba ya chama chetu ni lazima itumwe mara moja bila kuchelewa kwa Mwandishi wa Vyama. Watu wetu hutengeneza mzinga kutokana na mti ulio na shimo katikati. Tunafunga pande zote mbili na kuuweka kwenye tawi la mti mwingine. Tukitaka kutoa asali kutoka ndani yake, tunafungua upande mmoja na kutia moto wenye moshi ndani yake, na ikiwa moto huo umo ndani yake, tunatoa asali kwa amani. Kwa hivyo nilimwambia Wanjohi kwa Kikuyu: "*Ndukanarute gicinga mwatu*"

—maana yake usiondoe moto ndani ya mzinga, na kwa hivyo alifahamu kuwa ilitulazimu kuendelea kuwa na moto na kuituma katika na kufanya lingine lo lote lililohitajikana kabla ya kuandikishwa kwa chama.

Wageni wangu walikuwa wengi hivi ati Henley alinirudisha katika chumba cha polisi ambamo watu hawangenifikia na nilikaa humo mpaka Februari 27, 1959, wakati nilipohamishwa na kupelekwa kambi ya kazi ya Kandongu, ambayo ilikuwa mojawapo ya kambi za taabu nyingi katika sehemu ya Mwea ndani ya wilaya ya Embu. Nilikuwa mfungiwa tena —mapumziko yangu yalikuwa yamekwisha.

Hapo Kandongu, nguo zangu za kawaida zilitwaliwa pamoja na vitu vyangu vingine na nilipewa tena suruali na shati nyeupe za mfungiwa na nikaingizwa ndani ya chumba ndogo: Kenya hiyo! Lakini chumba hicho hakikuwa kama zile za Manyani. Tulikubaliwa kuondoka na kuoga kama tulivyopenda. Katika Kikuyu tunasema: "Ugonjwa wa kurudi ndio humwua mtu" na kwa hivyo nilisikia woga kidogo kwa vile nilivyotendewa hapo mbeleni. Katika Kandongu, walikuwako wafungiwa wengine ambao walikuwa Aguthi ambako walikataa kufanya kazi au kuungama. D.C. wa huko alikuwa ameamuru kuwa wapigwe kwa ajili ya kuvunja masharti na walikuwa wamepigwa kwa kiboko cha ngozi ya kiboko, tendo ambalo lilikuwa kinyume cha sheria. Palikuwa na uchunguzi juu ya jambo hilo. D.C. huyo alifanywa hakimu katika Kenya baadaye.

Baina ya marafiki wangu walikuwa Kiongo Kiburu, Marungo Ngumi, Q.C. (aliyepewa daraja hiyo kwa kuwa hakimu bora kabisa), Wahome Kihara na K. Nguru, tuliyemjua kama "Kapila" kwa sababu yeye angejifanya wakili katika korti za wafungiwa, na A.R. Kapila alikuwa wakili Mhindi aliyemsaidia Pritt katika kesi ya Kenyatta ya Kapenguria. Tulisema mengi juu ya kambi tulizofungiwa. Waliniambia juu ya "Mashambuliano ya Langata", ambayo yalikuwa ni mapigano baina ya askari wa polisi, na wa jela wakati "grenedi" zilitumiwa kuwashambulia wafungiwa ambao hawakuweza kujilinda. Walipigana kama mashujaa siku hiyo na walinyamazishwa na ile dawa ya machozi na kutupiwa maji baridi kutoka mifereji ya mipira ya wazima moto.

Pia waliniambia juu ya Embakasi. Wakati Serikali ilipokosa ushahidi wa kutosha kutushitaki kortini ya kawaida, tulifungiwa. Lakini hapakuwa na haja ya ushahidi mwingi wa kuwahimiza hakimu ambao pia walikuwa wenye kutawala, na siku zile za kwanza za Hali ya Hatari, maelfu walihukumiwa kufungwa jela kwa kula kiapo. Wakati tulipokuwa hatua kupingana na Serikali, wale waliofungwa jela walikuwa wanafanya vile vile katika jela za Kenya. Baina ya hawa ni wale waliofanyizwa kazi katika kujenga kiwanja kipya cha ndege cha Embakasi, Nairobi. Mahabusu waliopelekwa huko walichukia kusaidia Serikali kama vile

sisi tulivyokuwa na Serikali ilichukua hatua kali kuwalazimisha kufanya kazi. Kiongo na Matungo waliniambia vile maisha yalivyokuwa magumu huko, na wengine walijikata vidole ili wasipelekwe kufanya kazi kiwanjani: wengine walijichoma ndani ya vinywa vyao ili waweze kutema damu ili wapelekwe hospitali kwa kukisiwa kuwa na ugonjwa wa kifua. Tusije tukasahau kamwe kwamba kiwanja cha ndege cha Embakasi, Nairobi, kinachofaharisha hali ya wasafiri katika Afrika, kilijengwa kwa jasho na damu ya watu wetu wakipigania uhuru na kitabaki kama ukumbusho wa kudumu wa wale waliokufa wakiwa jela wakati wa miaka kilipojengwa.

Baada ya siku sita katika kambi, nilisoma ndani ya gazeti juu ya yaliyotendeka Hola ambako wafungiwa kumi na mmoja walikufa. Gazeti hilo lilitupiwa marafiki wangu na askari Mkikuyu aliyeitwa Mwai ambaye alikuwa mwenye huruma. Ripoti ilisema kuwa walikufa kwa ajili ya kunywa maji yenye sumu. Nilijua mengi kukubaliana na hadithi hiyo, na zaidi kwa sababu haikuonekana kama askari wenyewe walikuwa na kiu, kama vile askari hawakupatikana na ugonjwa wa kuhara Manyani. Nilikata shauri kumwandikia Stonehouse barua. Mwai aliniletea karatasi na stempu kutoka kantini ya kambi na niliandika barua ndefu, ndefu kabisa, nikamweleza yote yaliyotukia tangu tulipoonana katika dansi ya Kaloleni, na nilimaliza kwa kumwuliza aulize kuwe na uchunguzi juu ya vifo hivyo vya Hola kwa vile sikusadiki sababu zilizotolewa na Serikali. Nilimwuliza meneja wa kantini, Mhindi aliyeitwa Verji, aipeleke barua hiyo posta na alifanya hivyo. Stonehouse alimwona Waziri wa Makoloni juu ya mimi kufungiwa tena, Waziri ambaye alijibu kuwa nilifungiwa kwa ajili ya "usalama" wa nchi.

Tukio hilo la Hola lilionyesha ulimwengu vile wafungiwa walivyokuwa wakitendewa na Serikali ilichagua Komiti chini ya Fairn ili kuchungua yale yaliyokuwa yakitendeka na kusifu hatua ambazo zingechukuliwa juu ya hali ya usoni ya kambi hizo. Walipofika Kandongu, nilikuwa nimefunguliwa kutoka ile "cell" ndogo na Mkuu wa Kambi aliyeitwa Louis. Alikuwa afisa wa hekima, mwenye heshima na ambaye hangefikiria kumdhuru ye yote. Tulimpa jina la *Baba* kwa vile alikuwa akituita Baba akisema nasi. Alikuwa mtu mwema wa moyo mnyenyekevu na aliyefanya kazi kwa bidii, na alitutendea kama binadamu waliokuwa taabuni na waliohitaji msaada. Tumekuwa marafiki tangu wakati huo na wakati mwingine Louis hunitembelea kwangu nyumbani.

Wakati Fairn alipofika, nilimwambia mengi kama nilivyoweza kukumbuka juu ya yale yaliyokuwa yakitendeka katika kambi nilizofungiwa na vile wafungiwa wengine walivyoniambia juu ya kambi nyinginezo. Alionyesha kuwa mwenye kufahamikiwa na wa maana na alisikiliza yote niliyotaka kumwambia.

Muda mfupi baada ya kufika Kandongu, D.O. aliyekuwa Othaya hapo mbeleni, Salisbury, alifika kuniona. Alionekana kama alifurahia kuniona nyuma ya seng'enge tena na akasema kuwa alitumaini kuwa huo ndio wakati wa mwisho ningejihadhari namna hiyo. Alisema kuwa nilimshitaki kwa Serikali kwa kufanya makosa huko Othaya hali yeye alifanya alivyoweza kuwasaidia watu wa huko. Sasa nilikuwa nimefungiwa tena kwa sababu ya kuandika barua za mateta kwa Serikali. Nilikuwa sikuweza kunyamaza hata kwa mwezi mmoja? Kama niliendelea kuandika na kama sikujihadhari, huo ndio ungekuwa mwisho wangu. Nilimjibu: "Tunashindana nawe. Unaweza kunishinda au nitakushinde. Unawapigania watu wako na mimi ninawapigania watu wangu. Tutaishi kama maadui daima."

Baada ya wiki chache hapo, wafungiwa wengine ambao walishindwa kupitia ndani ya "mfereji" waliletwa kutoka kambi ya kazi ya Mariira katika wilaya ya Fort Hall. Baina yao alikuwa Taddeo Mwaura Ichahuria, ambaye alikuwa mzee lakini aliyestaajabisha kwa ujuzi wake wa Kiingereza. Alikuwa mwananchi halisi tangu alipozaliwa ilionekana, na alikuwa mwalimu wa juu. Ndugu wake, Goddard Mburu alielimishwa Fort Hare College katika South Africa, na sasa yeye ni District Assistant katika utawala wa majimbo. Taddeo, ambaye nilimpenda na kumwamini kama baba wangu, alinisaidia kutoa mateta yetu mbele ya komiti ya Fairn. Sasa yeye ndiye mwenye kiti wa tawi la K.A.N.U. la Fort Hall. Wengine walikuwa Ngugi Mwaganu, ndugu wa Bildad Kaggia aliyeshitakiwa pamoja na Jomo Kenyatta katika Kapenguria; Kinuthia ambaye sasa ni katibu wa Kenya Domestic and Hotel Workers Union; Mwangi "Cowboy" mmoja wa mashujaa zaidi aliyepigana msituni. Wengine waliletwa kutoka Nyeri na mmojawao alikuwa Jeremiah Kirumwa Keiru, ambaye baadaye alikuwa mshiriki wangu katika kazi ya National Secretarial Service; na John Michael Mungai, rafiki sana wa Fred Kubai ambaye pia alishitakiwa Kapenguria na mpigania uhuru mkuu.

Walinichagua niwe kiongozi wao na tulijiunga kidemokrasi kama tulivyofanya hapo mbeleni ndani ya kambi nyingine. Kakuna aliyetupiga na kama tuliandika barua kwa Serikali, Louis mwenyewe alizipitisha kwa wakuu wake bila kutushurutisha au kututukana. Tulimpenda na tuliheshimu masharti ya kambi.

Katika sehemu nyingineyo ya kambi, lakini ambayo iliwekwa kando makusudi, walikuwamo watu wengine waliofungiwa kwa kuwa wanachama wa chama kipya cha siri kilichoitwa "Kiama Kia Muingi" (K.K.M.) yaani *chama cha wananchi*. Kilisemekana kuwa kilikuwa na jina lingine la "Kiama kia Rubia" yaani *chama cha rupee* (shilingi mbili). Nimetaja juu ya kutotosheka kwa watu wa kawaida juu ya Ukusanyaji wa Ardhi

ulioanzishwa na Serikali ya kikoloni. Hali hiyo ilikuwa zaidi katika wilaya ya Fort Hall na Kiambu na inasemekana kuwa watu wengine walianzisha chama ambacho kililazimishwa kuwa siri wakati wa Hali ya Hatari ambacho kusudi lake lilikuwa kukusanya shilingi mbili kutoka kwa kila mwana-chama ili kuandika wakili ambaye angepeleka kesi nyinginezo mbele ya Korti Kuu na kuandika barua za malalamiko kwa Afisi ya Makoloni.

Serikali ilisema kuwa chama hicho kilihusiana na Mau Mau, na kwa hivyo walionyesha kutofahamikiwa na hali ya mambo na vile vyama viwili vilivyokuwa. Wakikuyu walijaribu tena kwa njia ya kufuatia katiba kupinga mabadiliko ya haraka juu ya wenye ardhi wakati nchi ilikuwa katika Hali ya Hatari. Wakati Serikali ilipokata shauri kuendesha mpango huo wa kuunganisha mashamba kwa nguvu bila kupenda kwa watu, watu walilazimika kufanya vyama vya siri. Vile Serikali ilikubali hivi majuzi kuwa kulifanyika makosa katika wilaya ya Fort Hall wakati wa kuunganisha mashamba kunaonyesha vile kusimama kwao kulikuwa haja. Wanachama wa K.K.M. hawakukubaliwa kuchanganyikana na sisi isipokuwa wakati walipokuwa wakituletea chakula. Walifanyizwa kazi kwa nguvu na walilipwa shilingi nane kila mwezi. Hatua nyinginezo zilizotumiwa katika kambi zao na zaidi katika kambi za Mwea zilizokuwa karibu nasi zilileta kuungama kwa uwongo na wengi waliofungiwa waki-kisiwa kuwa wanachama wa K.K.M. hawakuhusiana kamwe na chama hicho. Kwa maoni ya wengi wetu, ilionekana kama Serikali ilikusudia kutia chumvi ya chuki ili kuwahimizia watu wa Kenya na Uingereza kuwa ilikuwa haja kuendelea kuwa na sheria za wakati wa Hali ya Hatari. Wafanyi kazi wengi wa Serikali walitamani kama ingewezekana hali ya mambo ya wakati wa Hali ya Hatari ingeendelea daima au iwe kitu cha kawaida.

Kadongu ilijulikana hapo mbeleni kuwa kambi iliyokuwa mbaya zaidi katika Kenya, lakini wakati huu ilikuwa imepoa kwa vile tulielekea mwisho wa "kuokolewa." Sisi hatukufanya kazi hata kuondoa ndoo za vyoo vyetu. Nilipendelea kujifunza kuandika kwa ufupi (short-hand) na Rufus Kinuthia, ambaye alikuwa mwandishi kwa ufupi na mpigaji chapa alinifundisha kila siku. Baada ya miezi miwili aliniwezesha kuandika kwa ufupi na niliweza kuandika maneno mia moja kwa kila dakika. Hiyo ndiyo faida niliyopata wakati wa kufungiwa kwangu kwa pili. Singekuwa na nafasi ya kujifunza hayo baada ya kuachiliwa kwa vile ilikuwa vigumu kuweka hatua na siasa za Kiafrika, kutafuta mali ya kula na kujifunza kitu wakati huo huo. Ile International Red Cross ilipeleka Komiti nyingine ya kuchungulia hali ya mambo, na nilifurahia kuwa na nafasi nyingine ya kusema na Philippe Junod, "Muthuri wa Itathi", ambaye kwanza tulikutana naye huko Lodwar. Walikuwa na Dr. Rubli aliyetoka Zurich katika nchi ya Switzerland.

Baada ya kuwaambia juu ya taabu zetu niliwatembeza kambini ili wakutane na wafungiwa wengine ambao walishangazwa na unyenyekevu na wema wa wageni hao kama vile mimi nilivyokuwa nimeshangaa. Kabla ya kuondoka walinipa kitabu kilichoonyesha vile mahabusu wa siasa au wa vita wanavyotendewa. Nilikithamini sana kitabu hicho na ningali nakiweka ingawa ninafikiria hakutakuwa na haja kukitumia katika Kenya tena. Tumekuwa tukiandikiana na Dr. Rubli tangu wakati huo na wakati nilipopitia Zurich tarehe Julai 10, 1961, nilijaribu kujua nyumbani kwake, lakini kwa ajili ya kutojua lugha na ukosefu wa muda wa kutosha, sikuweza kumpata.

Baada ya miezi michache, D.C. wa Hola, wakiwa na mmoja wa kikundi cha "Atiriri" wa huko Athi River, walifika kutuchagua na kutupa daraja. Wenzangu wengine, pamoja na Taddeo, walitiwa ndani ya lori iliyokuwa na chumba cha seng'enge nyuma yake wakapelekwa Galole. Wakati huo Serikali ilikuwa imegeuza jina la Hola na kulifanya Galole. Walifahamu kwamba jina "Hola" litaendelea kuwaaibisha daima. Nilikaa huko Kandongu kwa muda na nilimkosa Taddeo sana; alikuwa rafiki mwenye heshima na mwenzangu niliyempenda. Siku moja Mzungu mmoja aliyeitwa R. G. Wilson alifika kutuona wakiwa na Rochester. Wilson alikuwa mtu mrefu, aliyejengwa uzuri na mwenye sauti ya upole na ukarimu. Alituambia kuwa alichaguliwa kuwa Special Commissioner wa Kambi za kufungiwa na kuwa ikiwa tabia zetu zilimtosha, atahakikisha kuwa tutaachiliwa upesi kama ilivyowezekana. Rochester alinisalimia kwa ufupi bila kusema lo lote juu ya mambo ya zamani na wote wawili wali-wacha kambi. Muda mfupi baada ya hivyo, Rochester aliletwa kambi ya Karaba, huko huko Mwea, na kama maili kumi na nne kutoka Kandongu. Siku chache zilipita halafu John Michael akapelekwa huko na baada ya siku tatu nilimfuata huko.

Karaba ilikuwa kambi yangu ya kufungiwa kwa mara ya kumi na nne na ndiyo ilikuwa ya mwisho. Haikuwa kambi ya kufungiwa kama zile nyingine kwa sababu sikuwekwa ndani ya kambi bali niliambiwa kuwa nilifungiwa kwenda zaidi ya maili tatu nje ya kambi. Karaba ni yenye joto karibu kama Kowop na ilikuwa kwenye nchi isiyovutia. Nilipewa kazi ya kuwafundisha watoto wa askari katika skuli ya kambi na nilipende-lea hivyo sana. Watoto hao watakua katika Kenya mpya iliyo tofauti na hiyo ya zamani. Wakati wa jioni niliwasomesha askari waliokuwa na elimu wakiwa pamoja na wafanyi kazi wa "uokozi", nikawafundisha Kiingereza, historia na kuandika kwa ufupi. Mwanafunzi mmoja wangu alikuwa Joseph Gaturuku Mathu (ambaye mbeleni alikuwa mfungiwa aliyefanya kazi ya ukarani ambaye sasa anakamilisha masomo yake ya Cambridge School Certificate kwa kusoma na barua na ambaye sasa ndiye

mwandishi wa gazeti letu la Nyeri linaloitwa *Uiguano Witu* (Usikizano wetu). Tulikaa katika nyumba moja huko Karaba. Mwingine alikuwa James ambaye alikuwa mmojawao wa wale waliotuchagua huko Lodwar. Nilipoanza kuwafundisha siasa, huyo James (mwanafunzi wangu), akiwa mwenye wasiwasi akiangalia kwenye mlango, alimwambia mwalimu wake, aliyekuwa mimi, kuwa kufundisha siasa hakukufaa.

Kutokana na ripoti ya Komiti ya Fairn, kambi za kufungiwa watu zilitolewa mikononi ya wakuu wa jela zikawa chini ya utawala wa majimbo. R. G. Wilson, ambaye alikuwa D.C. katika Nyanza, alimfanya Rochester mkuu wa kambi zote tatu huko Mwea. Katika utawala mpya wa kambi, hakukuwa na kupigwa. Badala yake tuliwekwa katika vyumba vidogo na wale wahojaji walitutembelea na kusema na sisi. Haikuwa rahisi kwa wao kusema na watu ambao walikuwa kama bubu kutoka saa mbili hadi saa saba za mchana. Walionekana kama waliopendelea kutoroka baada ya kusema machache. Ye yote aliyewajibu kamwe alifikiriwa kuwa alikuwa "ameokolewa" na mara moja alirudishwa kwao na kuachiliwa. Wakati huo ulionekana kama ndio Serikali ilifahamu kuwa mpango wao wa kuunga-misha na "kuokoa" ulikuwa bure. Sifa yote ambayo ilitolewa na Afisi ya Makoloni juu ya "uokozi" wa wafungiwa 80,000 yafaa ifikiriwe kufuatana na kutofaulu kwa mpango huo.

Yaweza kuwashangaza wengine kuwa wakati huu tulikuwa marafiki na Rochester ambaye alinitendea ukatili kupindukia huko Athi River. Tunasema kuwa "Wanaume wakipigana hawaendelei kukasirikiana wala kuchukiana." Alikuwa anatii amri za mwingine huko Athi River, na sasa alikuwa akifuata amri tofauti, ambazo zilikuwa zenye maana kulingana na hali ya mambo wakati huo. Niliweza kutii amri zake wakati huo. Inastaajabisha vile inavyowezekana kusahau ya zamani ikiwa mtu anageuza tabia zake na mara niliona kuwa sikumchukia tena hata kidogo.

Siku moja niliitwa mbele ya Komiti ya Rufani ambayo ilichungulia juu ya sababu zilizotufungisha. Nilieleza kuwa vitendo vyangu havikusta-hilisha kushikwa kwangu na kufungiwa tena na kuwa haukuwako ushahidi juu yangu ambao ungenifungisha katika korti ya sheria. Mwishoni wa 1959, tulitembelewa na Ian Macleod, Waziri wa Makoloni, ambaye alisema maneno mafupi na akaonyeshwa kuzunguka kambi. Alijaribu kusema na wafungiwa wengine ambao walikaa peke yao lakini hakuna aliyemjibu.

Wakati huo, wanawake waliofungiwa jela ya Kamiti karibu Nairobi wakati wote wa Hali ya Hatari waliletwa Karaba, na baina yao alikuwa msichana wa Senior Chief Koinange na wasichana wawili kutoka Nyeri, Margery kutoka Gathaithi na Miriam Muthoni aliyetoka Mumbuini karibu na nyumbani kwangu. Miriam alikuwa amehukumiwa kufa kwa hatia ya kubeba bastola lakini hukumu yake iligeuzwa na sasa alikuwa

mfungiwa kama wengine. Tulitumia muda mrefu tukizungumza juu ya vile wanawake walivyotendewa huko Kamiti na sikuwa na shaka juu ya sababu zilizomfanya Eileen Fletcher kuacha kazi yake huko Kamiti. Zilikuwako hadithi za wasichana wachanga waliofungwa maisha, mateso kutokana na wahojaji na hali ya usaliti ambako wanawake ambao walikuwa wanyonge walifanywa kuarifu juu ya wengine. Ninatumaini mmojawao ataandika hadithi juu ya maisha katika jela ya wanawake ya Kamiti.

Wakati wa Krismasi ya 1959, nilitoa mchezo wa Kuzaliwa kwa Kristo ambao ulionyeshwa katika kambi na katika kijiji kilichokuwa karibu. Mchezo huo uliwapendeza wote waliokuwako. Nilimfundisha mtoto wa kiume wa Rochester kuiga malaika na kusema kwa Kikuyu yale maneno yaliyosemwa na malaika kwa wachungaji usiku ule Yesu aliozaliwa. Aliiga vizuri sana. Naupendelea mchezo huo wa Kuzaliwa kwa Kristo.

Tarehe 8 Februari 1960, nilipokea barua kutoka kwa Attorney-General iliyoniarifu kuwa aliamriwa na Waziri wa Makoloni kunifungulia tarehe 12 Februari nirudi nyumbani kwetu. Nilimshukuru kwa ile taabu aliyochukua juu yangu. Askari na wafanyi kazi wa "kuokoa" walinifanyia karamu ya chai ya kuniaga kwa vile nilikuwa mwalimu wao kwa muda huo na asubuhi ya tarehe 12 Februari niliacha Karaba nikielekea kwetu Nyeri ndani ya motakaa ya aina ya Mercedes iliyostarehesha, ya Rochester. Ubongo wangu ulikuwa juu ya jambo moja tu. Sasa angekuwa beberu kamili: hakuna nafasi ya kuku tena!

10 Utisa uliyojaa ("Kenda Muiyuru")

SERIKALI iliniwekea "mkeka mwekundu" wakati niliporudi nyumbani. Burton alikuwa aendelea kuwa D.C. na alinibeba kwa motakaa yake hadi Othaya, huko akanieleza vile mambo ya uchumi yalivyokuwa yameendelea katika wilaya tangu nilipofungiwa, akanionyesha nyumba za kupendeza zilizoonekana kila mahali katika mashamba yaliyokusanyika na laini za mashimo yaliyokuwa tayari kupandwa kahawa na michai. Tulipofika Othaya, mimi na Burton tulifanya mazungumzo mafupi na D.O. wa huko na nilimweleza juu ya methali ya Kikuyu isemayo "Adui haanguki anapotupwa." Alionekana kama alishindwa na alinipa Land-Rover ya Serikali ya kunipeleka nyumbani kwangu ambao ulikuwa mwendo wa maili sita huko kijiji cha Kariko. Sikuamriwa kufanya ripoti kwa Chifu au Hedimeni na wakati wa usiku huo nilipiga hodi kwa Wangui na nilikuwa nyumbani tena. Kulikuwa usiku sana na kwa hivyo hatungeweza kufanya sherehe usiku huo na kwa hivyo baada ya kuzungumza mpaka kuni za moto zikaisha, tulikwenda kulala.

Asubuhi yake, hatukufanya shaka lo lote na shangazi wangu alimchagua mbuzi mnono aliyekuwa naye, aliyekuwa wa rangi moja nyeusi, na tukamchinja na kusherehekea pamoja na wajamaa wote na hakuna ambaye hakutosheka. Kwa mara ya kwanza nilijifikiria kuwa nilikuwa huru daima. Kwa vile nilinusa hali ya mageuko ya mambo, nilinusa geuko katika mawazo ya D.C. na D.O. Siasa hazikuwa mchezo mchafu, na labda hazikuweza kuzuilika na zingesaidia "vijana kutoa kiasi cha pumzi." Labda huo ndio ulikuwa mwisho wa kuwa ndani ya seng'enge na mwanzo wa kupigania "Uhuru sasa." Kazi iliyobaki ni ya kuongoza hiyo "pumzi" katika kufanya chama ambacho kingeweza kutawala nchi yetu na kuongoza maisha yetu.

Nilikuwa nimepewa karatasi nyekundu kabla ya kuondoka Karaba ambayo ilisema kuwa kwa vile nilikubaliana na maongozi ya "kuokolewa", ningefungiwa kwangu nyumbani kwa muda usiojulikana ili kujaribiwa kama "kuokolewa" kwangu kulifaa katika lokesheni yangu. Hivyo ilikuwa ni kama kumwuliza mwanaelimu wa sayansi ahutubu juu ya maisha ya

samaki katika ardhi kavu. Hawakunihoji wakati wa pili wa kufungiwa na hawangeweza kamwe "kumwokoa" mwananchi, kwa hivyo kama siasa zilikuwa uhalifu, haingewezekana kunipindua na hakuna jaribio au jela ingaliyofanya tofauti.

Nilikaa siku chache nyumbani nikijifahamisha mambo ya wajamaa na nikiangalia maendeleo katika shamba langu. Halafu nilikwenda kujua yaliyokuwa yakitendeka juu ya chama chetu cha Nyeri Democratic Party. Nilikuta kuwa Wanjohi Mungau na mwenzake Mugo Muringa, walikuwa wamefungiwa nyumbani kwao mara baada ya kushikwa kwangu na hakuna mwingine aliyeweza kufanya cho chote. Wengine wa wale ambao hawakuwa na elimu walijaribu kufanya kitu lakini mambo ya kufanya mipango yaliwashinda ingawa walijaribu wawezavyo. Ilinihuzunisha kusikia kuwa Kiambu na Fort Hall walikuwa na vyama vyao vya siasa hali Nyeri, ambayo ndiyo ilitangulia, sasa ilikuwa ya nyuma na ilionekana kama haikuwa katika mashindano.

Mara nilipoachiliwa, hata Wanjohi alifunguliwa na siku hiyo hiyo, wakiwa na mwenzangu, Ndegwa Mundia, alinitembelea kwangu Kariko. Tulizungumza hali ya mambo na tukakata shauri kuanzisha mipango yetu mara moja. Ingawa nilikuwa nimefungiwa nyumbani kwangu, nilijaribu kuvuta kushikwa kwa kutembea hadi mjini Nyeri ambako tungeweza kufanya mipango ya chama kwa njia bora.

Mnamo mwezi wa Machi, Jeremiah Nyagah, Mjumbe wa Lejiko wa Nyeri na Embu na Dr. Kiano walifanya mkutano huko Othaya. Mikutano ya aina hiyo ilikuwa ikifanywa na wajumbe kila mahali nchini ili kueleza matokeo ya mkutano wa katiba uliofanywa ndani ya nyumba ya Lancaster huko London ambako walikuwa wametoka. Katika ujuzi wangu, huo ndio ulikuwa mkutano wa wote wa siasa wa kwanza ambao ulifanywa Othaya.

Ulihudhuriwa na watu kama elfu saba. Kutoka mahali pasipojulikana, walitokea kikundi cha watu ambao walivaa alama za kijani kibichi juu ya mifuko ya kifuani na makoti yao na baina ya wao niliwatambua wengine wa wenzangu tuliofungiwa nao. Siwezi kusema ni nani aliyewatayarisha hata leo lakini wengine wao walikuwa ni wale walioanzisha chama cha Nyeri Democratic Party. Kufuatia amri zao, mkutano uliendelea vizuri na hii ilinionyesha haja ya nguvu zinginezo za viama vya siasa. Baada ya mkutano huo, nilisafiri pamoja na Dr. Kiano na ndipo tulizungumza juu ya kufanya chama, siyo cha Nyeri tu, lakini cha nchi yote. Kabla ya kuachana aliniuliza niendelee kufanyiza chama cha wilaya yangu.

Sikufahamu vizuri vile maneno "sehemu ya nyumbani" katika amri ya kunifungia humo: kwa upande mwingine, Kenya ilikuwa "nyumbani" kwangu. Kwa hivyo nilitaka kujaribu maana yake kwa kujifanya huru

kwenda nilipotaka na nilikwenda Nyeri makusudi bila kujificha na kila mtu aliweza kuniona. Nilishikwa siku hiyo hiyo na nikarudishwa Othaya ambako Henley, yule D.O. alinishitaki kwa kuvunja sheria ya kufungiwa kwangu nyumbani, na kwa hivyo nikarudishwa Nyeri na nikatiwa ndani ya jela ya Nyeri. Baada ya wiki moja, nilipelekwa mbele ya hakimu wa Nyeri, Carthew, ambako sikukiri makosa: nilimwambia kuwa nilishtakiwa kwa kifungu cha sheria ambacho hakikuhusu kesi hiyo. Hakimu huyo aligeuza kurasa kadhaa za Sheria halafu akasema kuwa mimi nilisema kweli na hapo akawaambia polisi warudi wakasahihishe kazi yao. Alfajiri yake, walifika kortini wakinishtaki kwa kifungu kingine ambacho kilifaa, na wakati huo nilimwambia hakimu kuwa hali yangu ilikuwa vile wilaya ya Nyeri, Jimbo la Kati na Kenya yote hata Afrika yote zilikuwa "nyumbani kwangu" na kama mimi nilifungiwa katika sehemu hizo sikufahamu makosa yangu. Baada ya kufanya upelelezi katika vitabu vya sheria bila kusema cho chote, huyo "Bwana Kali"—kama alivyoitwa hakimu huyo—niliachiliwa. Nilipotoka nje ya korti, rafiki zangu waliotoka mjini walinibeba juu-juu barabarani ingawa mvua ilikuwa yanyesha na askari wa polisi waliokasirika walitazama bila kuweza kufanya lo lote.

Hali ya siasa katika wilaya ilikuwa ya hatari wakati huo. Hakuna chama cha siasa cho chote ambacho kilikuwa kimekubaliwa na Mwandishi wa Vyama ingawa maombi kadhaa yalikuwa yamepelekwa, mengi ambayo yalikuwa yamekataliwa, ingawa mengine yao yalicheleweshwa makusudi ikitumainiwa kuwa yatakufa kifo cha kawaida. Wakati huo huo kulikuwako na mwito wa siasa ambao haukuwa na njia ya kueleza mawazo yake na ambao ulifanyiza vyama vingi vya siasa ambavyo havikuwa na mipango, na mojawapo ambao ungeendesha kitendo ambacho kingewezesha Serikali kufunga vyama vinginevyo vya siasa na kutia kafiu katika wilaya. Vikundi hivyo vilijiita "Peoples Convention Party" (P.C.P.), "Congress Independent Party", "Democratic Party", "Karanja's Group" na "Ex-K.A.U. Committee"—vyote ambavyo vilitokana na ukatazaji wa Serikali kukubali kuwa kulikuwa na haja ya wanasiasa na vyama vya siasa. Wanjohi Mungau, Tom Gichohi na mimi tuliitisha mkutano tarehe 20 Mei, 1960 wa viongozi wote wa vyama hivyo hapo Karatina. Wakati huo, chama cha Kenya African National Union (K.A.N.U.) kilikuwa chatayarishwa Nairobi na kwa hivyo niliwaambia kuwa wakati ulikuwa umefika wa kusahau tofauti zilizokuwako baina yao na kuwa ingelifaa kama waliondoa vyama hivyo vyote. Ilitulazimisha kufanya komiti ya viongozi ya K.A.N.U. katika Nyeri ambayo ingekuwa tawi la chama cha taifa (K.A.N.U.) wakati wa kuandikishwa utakapokubaliwa. Viongozi wa vyama fulani walisimama na kukubaliana na mawazo yangu ya kumaliza vyama vyao na hivyo tuliweza kuanzisha tawi la K.A.N.U. ambalo nilichaguliwa kama mwenye-kiti wake,

Wanjohi akawa naibu wangu, Thomas Gichohi akawa katibu, Wambugu Kamuiru akawa mweka hazina na maafisa wengine watano. Komiti hiyo ilifanya mambo vizuri kwa muda wa miezi kadhaa.

Nikiwa kama mwenye kiti, nilihudhuria mikutano katika Kiambu na Nairobi wakati wa kufanya K.A.N.U. Kuandikishwa kwa K.A.N.U. kulicheleweshwa kwa vile Serikali ilikataa kukubali kuwa Jomo Kenyatta awe Rais wake. Kama vile ilivyotendeka wakati wa K.A.U., James Gichuru alichukua hatua ya kuitosha Serikali na akakubali kuwa rais ili kuweka kiti moto kungojea Mzee Kenyatta. Watu wengi wanashangaa kwa vile wanasiasa wa Kenya walishindwa kufanya umoja baina yao wenyewe na vile sasa tunavyo vyama viwili vya siasa, yaani K.A.N.U. na K.A.D.U. badala ya kuwa na kimoja. Kama nilivyoona vile hali ya mambo ilivyoenda wakati huo, zilikuwako sababu ambazo zilileta hali hiyo. Sababu ya kwanza na ambayo ilikuwa muhimu, ni ile hofu ya makabila mengine madogo kuwa watatawaliwa na Wakikuyu na Waluo. Hiyo ilikuwa hofu ambayo ilitokana na ukabila lakini ambayo ilizidishwa na vile hakuna wanasiasa ambao walikuwa wameondoa picha ya ukabila: nguvu za uanasiasa za wengi zilitegemea vile walivyoungwa mkono na kabila lao. Serikali ya Kenya, ambayo ilihimiza juu ya vyama vya siasa vya mawilaya na ambayo iliwakataza wajumbe kusema pengine isipokuwa katika wilaya zao ilifanya mengi ya kuzuilia maendeleo ya maongozi, uaminifu na hali ambayo ingeleta masikilizano baina ya makabila mbali mbali.

Sababu ya pili ilikuwa hofu ya wanasiasa fulani juu ya mawazo ya wanasiasa wengine. Zilikuwako chuki nyingi lakini viongozi wengine walikuwa wanawaogopa mmoja au wawili wa wengineo na walikuwa tayari kuhakikisha kuwa hawakuwa katika chama kimoja na wao. Serikali ya Kenya ilizidisha chumvi katika farakano hizo za ukabila kwa njia ya kukataa kuwa Jomo Kenyatta ndiye tu aliyekuwa kiongozi aliyetambuliwa na wote, na kama si yeye hakuna mwengine angefikiria kuwa amechukua mahali pake mpaka yeye aseme kuwa hakutaka nafasi ya kuwa kiongozi wa Mwafrika. Kwa hivyo walicheleweshe, hata ikawa karibu walichelewa, kutambulisha nguvu za uongozi wa wanasiasa fulani na sasa waligawanya nchi ikawa kama sehemu mbili wakati ambao umoja unahitajiwa zaidi ya mengine ili kupambana na shida zinazotuelekea. Vile yale maongozi ya wabeberu ya "gawanya na utawale" yalivyoendeshwa kwa kumwagwa kwa pesa kutokana na pande za Katanga na Rhodesia haijulikani lakini kuanzishwa kwa K.A.D.U. iliyopendelea majimbo ni wazi kuwa kulihusikana na Katanga na matumaini ya masettla Wazungu fulani katika Kenya.

Sababu ya tatu ni vile wanasiasa wengine walijipendea makuu kama kawaida. Hilo si jambo la Kenya pekee—hutendeka pote duniani. Pakiwa na chama kimoja tu, kutakuwako na mwenye-kiti mmoja, mwenye-kiti

mdogo mmoja, katibu mkuu, mweka hazina, na kadhalika. Vikiwako vyama viwili, iliwezekana kuzidisha utukufu na nguvu za viongozi mara mbili. (Hakuna katika Afrika kwa sababu nchi chache sana za Afrika zinazoweza kuwa na starehe ya vyama vingi hivyo). Lakini watu wengine hufikiri kuwa kunayo haja ya kuwa na vyama kadhaa na ingawa hili si jambo muhimu, mara zile sababu za kwanza zikiwashika watu, basi sababu ya tatu huongezwa nguvu. Kwa hivyo vyama viwili vilitungwa, K.A.N.U. ambacho zaidi kiliungwa mkono na Wakikuyu, Wajaluo na Wakamba lakini kilichokuwa na wanachama wengine kutoka makabila madogo, na K.A.D.U. kilichokuwa na kabila la Kalenjini na makabila mengine madogo katika Kenya. Kabila la Abaluhya ambalo lina watu wengi liligawanyika baina ya vyama hivyo viwili. Tulikuwa tungali tunangojea kuandikishwa kwa tawi letu la K.A.N.U. wakati hali ya mambo ilizidi kuwa mbaya sana katika Nyeri, mnamo mwezi wa Mei, 1960.

Mwanzoni wa mwezi huo, Hedimeni wa kijiji aliyeitwa Wambugu, ambaye alionekana mtu asiye na dhara, aliuawa katika kijiji cha Gichiche huko Othaya mwendo wa maili nne kutoka nyumbani kwangu, na mwili wake ulitupwa ndani ya shimo la choo ambako ulionekana baada ya siku tatu. Serikali ilisema kuwa mauaji hayo yalihusiana na hali ya siasa na kwa hivyo askari wa Special Branch walisema kuwa walikuwa na ushahidi wa kulishana viapo na mikutano na kwa hivyo afisa aliyekuwa akifanya kazi kama Provincial Commissioner, Burton, ambaye alikuwa D.C. katika Nyeri, aliweka vijiji kadhaa chini ya kafiu za usiku. Serikali iliwakataza watu kuondoka au kuingia humo. Yule D.O. Henley alichukua hatua kali na maisha yakageuka kuwa yasiowapendeza watu. Serikali ilikuwa imevumbua kuwa watu wengi walikuwa wametoa pesa na kupewa risiti zilizokuwa na alama "G.M.K." Watu wengine walisema kuwa herufi hizo zilisimama badala ya "Gikumbo Mount Kenya" lililokuwa jina la skuli ya K.I.S.A. ya Karatina ambayo ilikuwa imefungwa na wengine walizitafsiri kwa njia nyingine. Hakuna shaka kuwa watu wengi walitoa pesa hizo wakisadiki kuwa zitatumiwa kwa skuli ambayo ingefunguliwa na kuongezwa na Wanjohi Mungau. Mimi nilimwunga mkono katika jitihada yake ya kuongeza nafasi ya elimu kwa wananchi.

Serikali iliogopa yale yaliyokuwa yakitendeka na ikasema kuwa ulikuwako ushahidi wa kulishwa viapo visivyo halali katika jimbo la Rift Valley na Fort Hall. Kwa hivyo ilifanyiza "kifagio" kilichojulikana kama "Operation Milltown" ambacho kiliwashikisha watu sitini wakafungiwa katika kisiwa cha Lamu pande za pwani. Baina ya wale walioshikwa walikuwa Wanjohi Mungau, Mugo Muringa na Ndegwa Mundia. Askari mmoja wa polisi aliniambia kuwa jina langu lilikuwamo baina ya hao wengine hapo mwanzoni lakini liliondolewa kufuatia amri ya P.C. Ilise-

mekana kuwa labda kungekuwako na msukosuko huko Uingereza kama nilirudishwa kifungoni.

Bibi wa Hedimeni aliyeuawa baadaye alishtakiwa kwa mauaji ya bwana yake na akahukumiwa, na hata hivyo Serikali iliendelea kuzidisha uvumi kuwa ugaidi ulikuwa umeanza tena nchini. Wakati huo, D.C. wa Nyeri alikwenda Nairobi kuonana na viongozi wapya wa K.A.N.U., na Josef Mathenge, aliyekuwa mmoja wa walioongoza Nairobi Peoples Convention Party. Aliwauliza watembelee Nyeri wafanye mikutano na kukanusha viapo vya siri. Aliahidi kuiuliza Serikali ikubali kuwe na tawi la K.A.N.U. katika Nyeri ili viongozi wa siasa wawe na nafasi ya kutawala vitendo vya wafuasi wao. Mnamo mwezi wa Juni, mkutano mkubwa ulifanywa hapo Ruringu kama maili moja kutoka mjini Nyeri ambao ulihudhuriwa na watu kama 15,000. James Gichuru, Josef Mathenge, Arthur Ochwada (kiongozi wa vyama vya wafanyi kazi kutoka Nyanza), Mwai Kibaki (ambaye alikuwa mwalimu wa uchumi katika Chuo Kikuu cha Makerere na aliyechaguliwa kuwa Executive Officer wa K.A.N.U.), Henry Wariithi (wakili ambaye alichunga mambo ya Mzee Kenyatta) na mimi, wote tuliuhutubia mkutano, tukahimiza juu ya umoja na tukakemea vyama vya siri na vitendo vingine kama hivyo kama visivyokuwa na haja wakati huo kwa vile hali ya siasa ilikuwa imegeuka. Mimi mwenyewe niliwauliza wale waliotoka kifungoni kusahau yaliyotendeka na nikawauliza waliokuwa upande wa Serikali kujiunga na sisi. Baada ya siku chache, D.C. aliruhusu mkutano mwingine wakati viongozi wa tawi la Kanu walichaguliwa. Watu walitaja jina langu niwe mwenye-kiti lakini tulikuwa tumeagana na Josef Mathenge kuwa ingelifaa kama yeye angekuwa mwenye-kiti wakati huo, na kwa hivyo nilisimama juu ya meza nikawaambia kuwa sikutaka kuwa mwenye-kiti. Maafisa waliochaguliwa siku hiyo walikuwa Josef Mathenge kama mwenye-kiti, Muriithi Wagochi (aliyefungiwa) akawa mwenye-kiti mdogo, Wambugu Kamuiru (aliyefungiwa) akawa mweka-hazina. Watu hawakupendezwa nilipokataa kuwa mwenye-kiti na kwa hivyo uchaguzi wa maafisa wengine uliahirishwa na watu wakarudi kwao.Alvan Karanga aliyekuwa D.O. Mwafrika wa North Tetu alitualika sote katika nyumba yake bàada ya mkutano na yule D.C. wa kusimamia alikuwako. Ilionekana kama kwamba kwa mara ya kwanza Serikali ilifahamu kuwa tulikuwa tunajaribu kujenga badala ya kuvunja nchi yetu.

Ilifikiriwa katika nchi kuwa kuwachagua maafisa kwenye mikutano ya faragani haikuwa njia iliyo bora. Kwa hivyo ilifikiriwa kuwa ingefaa kuanza uchaguzi kutoka kila lokesheni ndogo ambako komiti zingechaguliwa mbele ya wote, halafu wanachama wengine wachaguliwe kutoka kila lokesheni wakichaguliwa na wanakomiti wa lokesheni ndogo, na pia

kuwe na uchaguzi wa kidivishoni ambako wanachama wa kila lokesheni wangefanya uchaguzi. Kile chama ambacho kingechaguliwa kwa wilaya yote kingekuwa "Governing Council" ambacho kingekuwa na wanachama kumi na wawili kutoka kila divishoni na maafisa wa kila wilaya, ambao walichaguliwa na "Governing Council" ingawa haikuwa haja kwao kuwa wanachama wake. Nilichaguliwa kuwa katibu wa kutayarisha mambo tukiwa na rafiki wangu wa zamani, Eustance Mimamo, ambaye alikuwa kiongozi wa sehemu huko Manyani na aliyekuwa hadi-koa shupavu. Tom Gichohi, ambaye aliacha kazi ya ukarani katika Reli (ambako pia alikuwa afisa wa tawi la chama cha wafanyi kazi wa reli) alifanywa kuwa katibu. Gachuru Ngorano ambaye alikuwa mmojawapo wa wafungiwa waliohusikana na msiba wa Hola alifanywa kuwa mweka-hazina mdogo. Mambo mengineyo katika uchaguzi huo hayakuwa ya kutosha lakini sasa tulikuwa na mwanzo wa chama.

Iliyobaki ni kuwafanya wote wawe wanachama. Tulipata vitabu vya risiti na kadi za wanachama kutoka afisi ya katikati huko Nairobi na hapo tukaanza propaganda ya kuwaandikisha wanachama. Baada ya mwezi mmoja, tulikuwa na wanachama 35,000 katika wilaya na tulikuwa mbele ya wengine wote katika nchi. Maafisa wa matawi ya chama walichaguliwa kwa kila divishoni, na ilistaajabisha kuona vile wazee, waume kwa wanawake, walivyofanya misitari kwa mamia, hata hali ya hewa iwe vipi na yale mahitaji ya kulima mashamba yao. Binadamu hawezi kuishi kwa mkate peke yake. Walipofika afisini, afisa wa divishoni aliwaeleza juu ya mawazo ya K.A.N.U. na ahadi walizokuwa wakifanya na walilipa zaidi ya shilingi tano na wakaweka sahihi ya kidole au ya kalamu juu ya kadi ya uwanachama.

Kenneth King'ori, mtu aliyekuwa na elimu ambaye alikuwa amefanya kazi kama mwandishi wa Korti la Kiafrika la Nakuru, na ambaye baba wake alikuwa dereva wa D.C. alikuwa amefunguliwa kutoka jela siku ile ile mimi niliofunguliwa. Alichaguliwa katibu wa propaganda na tulikata shauri kuitafsiri katiba ya K.A.N.U. kwa Kikuyu ambayo tungeitawanya kote katika wilaya. Pia tulitawanya gazeti lingine lililotoa maoni juu ya maongozi na habari za K.A.N.U. Ikifika Septemba, tulikuwa na gari mpya la K.A.N.U., lililokuwa na rangi nyekundu, nyeusi na ya kibichi kufuatia marangi ya bendera ya K.A.U. na ambayo iliandikwa kuwa "Kutumikia nchi yako ni kumtumikia Mungu," na "Jomo Kenyatta ndiye kiongozi wetu," na ile alama ya ngao yenye simi zilizokatana ambayo ilitumiwa na K.A.U. kabla ya kupigwa marufuku. Kwa wakati huu tulikuwa tumeanza kuwafundisha wananchi juu ya kuimba nyimbo za kitaifa na pia timu za wacheza dansi ili kurudisha utukufu wa maisha yale ya kizamani. Ilifanywa karamu ya chai ya kusisimua ya K.A.N.U. hapo uwanjani wa Nyeri ambayo ilihudhuriwa na zaidi ya watu 15,000 ili kuwaaga

wanafunzi sitini ambao walichangiwa pesa ili waweze kusafiri kwa ndege hadi Amerika ambako wangepata nafasi ya kujifunza ili waweze kutwaa kazi za madaraka katika taifa letu jipya.

Sasa tulikuwa na chama cha siasa lakini nchi haikuwa po pote bila utulivu wa hali ya uchumi. Watu wengine katika Nyeri mjini walikuwa wamejaribu kufanyiza chama kilichojulikana kama Nyeri African Traders Society ili kiandikishwe. Serikali ilikataa kuandikishwa kwa chama hicho ati kwa sababu hawakuwa na imani na maafisa wengine wake na hata hivyo ilionekana kama yalikuwako maongozi tofauti yaliyoongoza komiti iliyoongoza. Kwa hivyo nilimwona D.C. ambaye alikubali kuwa kama hiyo farakano ya ndani ingeondolewa, angeunga kuandikishwa kwa chama mkono. Mwishoni wa Julai 1960, nilichaguliwa kuwa mwenye-kiti faraghani, mjini Nyeri. Joseph King'ori, ambaye alifanya kazi ya kuuza kuni na mwenye biashara katika soko la Kamakwa, alifanywa mwenye-kiti mdogo. John King'ori aliyehitimu mtihani wa K.A.P.E. na ambaye alikomboa duka la ushonaji wa nguo mjini Nyeri alichaguliwa kuwa katibu wa kudumu aliyepewa mshahara, na Nahashon Gakuo, tajiri aliyekuwa mwenye duka mbili za kuokea mikate, mtu wa hekima na wa kuaminiwa sana, na ambaye aliweza kusema Kiingereza na alikuwa msaidizi katika hospitali hapo mbeleni, alifanywa mweka hazina. Thomas Elijah Gikonyo, ambaye alichaguliwa kuwa mwandishi mdogo, alikuwa kijana wa tatu wa Philip Nganatha, ambaye alikuwa mfuasi wa misheni ya Protestanti wa nguvu katika eneo hilo na aliyejengesha kanisa la mawe la Wandumbi kabla ya kuangushwa na kuuawa na mwendeshaji wa baisikeli mwanzoni wa 1960. Ndugu wake mmoja Thomas alikuwa anasomea Addis Ababa katika Ethiopia na wote walikuwa wa dini ya Katoliki. Ninakumbuka vile Thomas alivyoniambia juu ya maziko ya babake yaliyohudhuriwa na maelfu, karibu matata yalitokea kwa sababu wa-Katoliki walidai kuwa kwa vile Philip alikuwa Mkatoliki tangu alipokuwa mtoto, ingefaa azikwe kufuatia mila za Kikatoliki. Wa-Protestanti walipinga wazo hilo kwani walisema kuwa hata yawe ni yapi aliyofanya hapo zamani, sasa yeye alikuwa ni kiongozi wao. Usiku uliotangulia mazishi yake, mwili wake ulichungwa na Wa-Protestanti kutoka Wandumbi na ukasimamiwa hadi kaburini kwa motakaa nyingi. Sehemu iliyozunguka kaburi lake ilisimamiwa zaidi na Wa-Protestanti na Wa-Katoliki waliwachiliwa nje kwenye barabara. Yako maoni magumu juu ya farakano za misheni katika nchi yangu na jadiliano juu ya mtu aliyekufa wakati huo lilionekana jambo lisilopendeza na lisilofahamika kwa wengi wetu. Farakano hizo zilitokana na mawazo ya Wazungu wamisheni wengine ambao walifikiria kufaulu kwa wingi wa wanachama wao na ambao walitumia maiti hiyo kama mfano wa kuonyesha vile walivyokosea Ukristiano wakijaribu kujipatia mapendeleo na makuu.

Thomas Elijah alifanya mengi katika kuanzisha chama cha wafanyi biashara katika Nyeri na alikuwa mwananchi wa kweli na mwenye bidii. Hapo mbeleni alikuwa amefanya kazi kwa Nyeri Marketing Board. Mweka-hazina mdogo alikuwa bibi aliyetoka South Tetu aliyeitwa Wanjiku James, ambaye alifanya biashara ya vyakula katika mji wa Nyeri. Wadhamini wa chama hicho walikuwa Josef Mathenge, M.L.C., na Paul Waithaka ambaye alifungua duka la vyombo vya nyumbani. Katika mkutano wa mwaka uliofanywa Februari 1961, maafisa hao wote walichaguliwa tena isipokuwa katibu na katibu mdogo. John King'ori alishindwa na Charles Mwaniki Kamara ambaye alikuwa akifanya kazi kwa Central Province Marketing Board kama karani na mwendesha baisikeli wa kuchekesha. Thomas Elijah alikuwa amefungwa kwa kujionyesha sana juu ya mambo ya siasa, na mahali pake palichukuliwa na Wachira Kinguru, mfanyi biashara aliyetoka Karatina.

Chama chetu kilienea kote katika wilaya ya Nyeri na tuliweza kuiambia Serikali juu ya mambo mengineyo yaliyohusiana na maendeleo ya Waafrika kama vile kutokuwako na leseni za kutosha za biashara, njia iliyofaa ya kujaza fomu za maombi ya motakaa za abiria, maombi ya kukopeshwa pesa na ubaguzi katika biashara ya wanyama. Ni mimi tu baina ya maafisa wa chama ambaye alikuwa kifungioni. Chama kilikuwa na afisi ndogo mjini Nyeri ambayo ilijaa kila siku na watu waliokusudia kuwa wafanyi biashara walikuwa wakitafuta msaada. Sisi Wakikuyu tunayo bidii kuu juu ya biashara na kwa vile kulikuwa na ukosefu wa kazi ya mshahara, watu wengi walijaribu kujipatia pesa kwa kufanya biashara ya aina hii au ile.

Mnamo Septemba, 1960, matata yalitokea mkahawani mmoja mjini Karatina, ambayo mwishoni yaliwahusu viongozi wa chama chetu katika wilaya juu ya hali ya siasa. Afisa Mzungu wa polisi alifika mkahawani huo kumshika mtu lakini alipigwa. Aliondoka halafu akarudi na kundi la askari wengine na wakajaribu kuwashika watu wengi waliokuwamo, pamoja na Josef Mathenge na maafisa wengine wetu. Kikundi cha watu kilichofika mara moja hapo hakikupendezwa na vitendo vya polisi na mambo yalichafuka wakati umati huo ulifika katika kituo cha polisi kuwaokoa viongozi wao. Kwa bahati njema, umati ulipoa lakini ilikuwa wazi kuwa tukio kama hilo halingefanyika mahali pa kwanza. Kufuatia vile hali ya siasa ilivyokuwa moto moto, kutotumia nguvu kwa mwanapolisi kungesaidia zaidi kuliko kuwafanyia watu ukatili au kuwatukana. Katika korti iliyofuatana na tukio hilo, D.C. wa hapo mbeleni ambaye alikuwa aupanda mlima Kilimanjaro, alikubali kutoa ushahidi kwa upande wa washtakiwa, akaeleza juu ya tabia bora zaidi za viongozi wa chama na vile walivyoweza kutawala mikutano ambayo ilifanywa baada ya "Operation

Milltown." Tulimtuma Eustance Kimano na gari la K.A.N.U. aende akamlete kutoka Kilimanjaro na walirudi Nyeri usiku. Aliambia korti kuwa hakujua sheria yo yote iliyokataza watu kusema "Uhuru" au kufanya alama ya "V". Mathenge na wenzake walitozwa faini lakini hawakufungwa ingawa Thomas Elijah alihukumiwa na akafungwa baadaye kwa hatia nyinginezo zilizotokana na tukio hilo.

Wakati tulipokuwa tukimla beberu baada ya kuachiliwa mara ya pili, Wangui alinikumbusha kuwa wakati ulifika nifanye ndoa. Kwa muda wa miaka kadhaa, kazi yangu ya siasa ilinizuilia kufikiria sana jambo hilo lakini nilikubali kuwa yeye alisema haki. Nilikuwa wa umri wa miaka 31, na dada zangu wote walikuwa wameolewa. Nilipokuwa nikifanya kazi Nyeri, wakati mwingine nilitembelea afisi ya Kenya Distributive and Commercial Workers Union. Kazi yangu hapo ilihangaishwa na uzuri wa msichana mjana aliyekuwa akifanya kazi ya karani katika afisi hiyo; aliyekuwa akipiga chapa na kufaili barua, ambaye jina lake ni Doris Nyambura. Alikuwa msichana mzuri zaidi ya wote niliowaona tangu hapo. Pamoja na uzuri wake, alikuwa mwenye bidii tena kijana, kwani alikuwa wa umri wa miaka 18. Katika Kikuyu, hatuhukumii msichana kufuatana na uzuri wake peke yake, bali pia kwa tabia zake, uaminifu wake na nafsi yake. Ni lazima awe mpenda watu anayewalaki wageni kwa moyo safi. Doris alikuwa na hayo yote. Alizaliwa baina ya jamii kubwa na alikuwa msichana wa tano wa mzee Gordon Njee na mama Sephora Mumbi waliokuwa wa kijiji cha Riamukurwe katika lokesheni ya Aguthi. Gordon alikuwa mfanyi biashara na miaka mingi iliyopita alikuwa Mkikuyu wa kwanza kuendesha *tekisi-ring'i*. Harun Muturi, ndugu wake mkubwa Doris, alikuwa akifanya kazi ya karani wa hesabu katika kampuni ya chapa ya Mhindi huko Nairobi. Dadake mkubwa, Miriam, aliolewa na makanika aliyefanya kazi Nanyuki na walikuwa na watoto sita. Dadake wa pili, Esther Muthoni, ameolewa na Peter Njoka wa wilaya ya Embu, ambaye ni karani mkubwa katika Relwe na wana watoto wawili. Joyce, dadake wa tatu ameolewa na dereva anayeitwa Kibara na wana mtoto msichana. Ndugu wa tatu wa Doris, Matuto, Mbogo na Kariuki, na dadake yule mchanga kabisa, Mukami, wangali wako skuli katika Riamujirwe Intermediate School, chini ya mkuu wa skuli, Charles Mukora. Charles, ambaye ni rafiki wangu, ni hodari kwa michezo—yeye huwakilisha Kenya katika kuruka urefu (long-jump) na pia hucheza senta-hafu katika timu ya mpira ya Jimbo la Kati na pengine ya Kenya. Watu hao wote walikuwa na uhusiano mpya wa pekee baada ya kuoa na ninawaita "Athoni".

Ilinichukua muda wa wiki mbili kumfanya anikubalie nimwoe, lakini sikujali kwani nilijua alikuwa akifanya uchunguzi kama ilivyo kawaida na

hata mimi nilikuwa nafanya uchunguzi. Si jambo rahisi kwa msichana kukubali mara moja hata ingawa yeye anakupenda kufa na kupona. Ukimwuliza, hukujibu: "Sikubali na sikatai," halafu baadaye atakuambia: "Sasa ni sawa, unaweza kwenda ukamwone baba yangu." Mambo hayako tofauti sana katika dunia. Kwa hivyo tulikwenda pamoja kwa baba yake ambaye alikubali na sasa tukaanza kutayarisha mambo ya ndoa. Ilikuwako hitilafu kidogo kwa sababu mama yake Doris, Sephora Mumbi, alishikwa wakati wa "kifagio" cha "Operation Milltown" kwa vile alisemekana kuwa alihusiana na chama cha G.M.K. Alihukumiwa kufungwa miezi miwili na akatozwa faini ya shilingi mia moja na hamsini pia. Kama alishindwa kulipa hizo shilingi, kifungo chake kingeongezwa miezi mingine miwili. Doris aliniambia hawezi kuolewa wakati mama yake alikuwa jela na mimi nilikubaliana naye, lakini ilinilazimu nioe na sikupendelea kuahirisha sherehe ya harusi kwa miezi kadhaa. Baada ya kutumia usiku mzima bila kulala nikifikiria hatua ningelizochukua, asubuhi yake nilimwendea D.C. nikamweleza shida zangu. "Ninataka kuoa na mama wa mpenzi wangu yuko jela na mpenzi anasema hawezi kuolewa wakati mama wake yuko jela." Ingawa D.C. alikuwa bado kuoa, alionyesha huruma na baada ya kujikuna kichwa, alicheka na akaniambia: "O.K., nitafanya kitu. Peleka karatasi hii mbele ya korti, lipa faini na atafunguliwa." Ndipo akaandika barua kwa wazee wa korti, akavuta hukumu ya kufungwa. Nilikimbilia kortini, nikalipa shilingi mia na hamsini, nikapewa risiti na waranti ya kuachiliwa, nikafanya haraka kwenye kilima ambako iko jela ya Nyeri, ambapo baada ya dakika chache, mama wake Doris alitoka nje ya mlango mkubwa wa jela, akaniamkua kwa upole, machozi yakimjaa machoni kwa furaha aliyokuwa nayo.

Kunayo mambo fulani ambayo hufanywa katika nchi yetu ambayo ni ya kudumisha urafiki baina ya jamii hizo mbili katika kuoa. Watu ambao hawafahamu husema juu ya "bei-ya-bibi" (mahari) au "kununua" bibi; maneno hayo huleta kutofahamikiwa juu ya yale yanayokusudiwa na yale yanayotendwa, ambayo ni kuhamisha ng'ombe na vitu vinginevyo kutoka kwa jamaa ya mwanamume anayeoa na kuwapeleka kwa baba wa msichana. Ikiwa msichana na mwanamme watashindwa kusikilizana si rahisi kwa wao kufanya talaka bila sababu ya kutosha. Baba ya msichana ataona vigumu kukubali kurudisha mali kutokana na mateta yasiyo na maana. Wajamaa wa msichana humshawishi sana aendelee kuwa bibi isipokuwa haiwezekani kamwe. Ilikuwa haja nipeleke zaidi ya ng'ombe tisa kwa baba wa Doris. Ng'ombe mmoja wa kike huhesabiwa kama mbuzi kumi, mbuzi mmoja ni wa thamani ya shilingi ishirini. Nilikuwa na ng'ombe wengi kwa sababu wakati dada zangu walipoolewa, tuliletewa ng'ombe wengi na jamii za mabwana zao.

Hapo zamani, ilikuwa kawaida kwa mwanaume mwenye kuoa kufanyizwa mambo kadhaa mbele ya wanawake wa upande wa mpenzi wake. Alifanywa kubeba mzigo wa kuni, au ndizi au chungu cha maji. Ilimpasa afaulu kwani hili lilikuwa jaribio la kuonyesha vile alivyojitolea kwa mpenzi wake. Wanawake wangemngojea ndani ya chumba kimoja na kuona jitihadi yake, halafu walitoa maoni yao yaliyomfaa na mara nyingi yalikuwa ya kumsifu. Mambo kama hayo hayafanywi kwa wingi siku hizi katika sehemu yangu na wanawake wa upande wa Doris walisema kuwa kufungiwa kwangu kulitosha.

Pia iko sherehe nyingine ambayo inaendelea kufanywa mahali pengi inayojulikana kama "Ngoima". Kondoo sita wanono ("ngurario") huchinjwa na wazee kutoka pande zote mbili hukusanyika na kula nyama hizo pamoja. Hiyo ni hatua nyingine ya kuongeza nguvu za urafiki baina ya jamii hizo mbili. Desturi nyinginezo za hizi zinaendelea kufifia siku hizi. Nilisamehewa kufanya sherehe hii ya "ngurario." Lakini sikusahemewa kufanya "pombe ya mtoto" (ya mtoto atakayepotea). Kwa vile kwetu kulikuwa maili ishirini kutoka kwa Doris, nilimpa Gordon Njee pesa ili atayarishe kupikwa kwa pombe hiyo kwa niaba yangu. Ilimlazimu Gordon kupata barua kutoka kwa Chifu ili aruhusiwe kupika pombe. Taabu yangu ni kuwa mimi sikutumia pombe: mashauri ya mama juu ya unywaji wa tembo yaliongezeka nguvu wala hayakupunguka kwa ajili ya kifo chake. Lakini wazee walisema ilinilazimu nionje pombe langu, na kwa hivyo nilitwaa pombe ndogo kutoka kibuyuni nikaionja kwa ulimi na nikawashawishi wasinilazimishe kunywa yo yote na walikubali.

Tena ilikuwa desturi kwa mwanaume kutoa zawadi kadhaa kwa baba na mama wa msichana kurudisha mahali pa zile baba wa msichana alizotoa kwa wazazi wa mama wa msichana wakati wa ndoa yao. Zawadi hizo huwa tofauti kwa kila jamii lakini kwa kawaida baina yazo ni ukanda wa ngozi (wa kufunga kuni na mizigo mingineyo), kikapu (cha kamba), na nguo ya mama iliyofanywa maridadi na shanga, simi, mkuki wa pekee na nguo ya ngozi ya baba wa msichana. Wakati mwingine, wazazi wa msichana hupendelea zawadi nyingine badala ya hizo. Ikiwa hivyo, maagano hufanywa na zawadi hizo hutolewa kufuatia vizazi. Kwa mfano, mimi nilimpa baba wa Doris kabuti na ninatumainiwa kupewa kabuti na yule atakayemwoa msichana wangu. Wazazi wa mpenzi wangu walishauri kuwa zawadi nyinginezo zifanywe kwa pesa na tukakubaliana niwape shilingi elfu moja. Walikubali nilipe hizo kwa vifungu kwa vile nilipeleka ng'ombe mara moja, na hata sasa ningali ninalipa sehemu iliyobaki.

Kwa wale wetu wenye elimu, mambo ya ndoa huwa ya gharama kubwa kwa vile tunafuata desturi za zamani na za siku hizi. Lakini kwa

bahati njema, nilikuwa na akiba ya pesa zilizokuwa nami wakati nilipohamishiwa kwenye Vilima Vitatu Vikavu. Baada ya kufanya kazi nyingi hivyo ya siasa, sasa zitatumiwa kwa kunisaidia kwa mambo ya starehe. Jamaa wangu na wa ukoo wangu na marafiki wengineo katika siasa walitoa gharama iliyobaki. Pesa zilihitajikana ili kuwanunulia wasimamizi wangu watatu suti tatu mpya na pia kuwanunulia wasimamizi wa Doris watatu nguo mpya, tena ilikuwako karamu nyumbani kwa Doris na kwetu pia, tulifanya dansi katika Ruringu Social Club, tulipigwa picha, gharama ya motakaa na hasara ya kanisa. Sherehe hizo zote zilinigharimu shilingi elfu tatu. Ingawa imani yangu ilikuwa ikipunguka wakati mwingine, ningali nilikuwa bado Mkristo, na vile vile Doris, na tulipendelea kufanya ndoa yetu katika kanisa la Presbyterian hapo Nyeri. Kasisi aliyetufunganisha aliitwa Reverend John Kagai, mzee aliyetoka pande za South Tetu, ambaye alizoea kutembelea wafungiwa katika kambi zao ingawa hakutembelea kambi moja nikiwa ndani yake. Nguo ya ndoa ya Doris ilikuwa nyeupe yenye urembo wa dhahabu na ilinipendeza sana. Wasimamizi wangu walikuwa Josef Mathenge, M.L.C., John Baptista Wambugu, mwalimu mkubwa katika Nyeri Secondary School na kiongozi wa Kenya National Union of Teachers, ambao wote wawili walikuwa Wakatoliki, na Harrison Thuku mwandishi na msemaji wa habari katika Mount Kenya Broadcasting Station. Msimamizi mkubwa wa Doris alikuwa Anna Njoki, msichana wa mzee Kirori Motoku tuliyefunganishwa naye tuliposafiri kwa ndege kwenda Lodwar. Wengine walikuwa Florence Mumbi na Gladys Gathiri ambaye sasa anafanya kazi ya ukarani katika afisi ya K.A.N.U. ya tawi la Thomson's Falls na dadake mdogo Doris, Mukami.

Tarehe 10 Septemba, 1960, niliamka asubuhi na mapema kabla ya kuwika kwa jogoo, nikiwa na mawazo mengi kwa yale yaliyokaribia kutendeka. Wakati jua lilipochanuka, Wangui aliniita na mara marafiki wangu watatu walifika kunibeba huko wakitoa vicheko vya kunichangamsha. Kwenye amani ya kanisa, nilimpeleka Doris hadi mahali pa sadaka tukasimama mbele ya mzee kasisi pamoja, hapo tukamjibu yale maswali ya kawaida. Halafu nilimvika Doris ile pete juu ya kidole chake na nikamwambia kuwa sasa tuliumba mtu mpya, yaani Bibi Josiah Mwangi.

Karamu ya kwanza ya upande wa Doris iliandaliwa katika skuli ya Riamukurwe, na ilitayarishwa zaidi na mkuu wa skuli. Wanafunzi walikuwa wakijitayarisha kwa wakati huo kwa siku kadhaa na ilikuwako ilani kubwa kwenye mlango iliyosema "KARIBU" ambayo ilizungushiwa maua yaliyotolewa katika shamba la skuli. Ni desturi kwa wanawake wa upande wa msichana kuigiza kuwa wanamkataa kutoka kwao:

huzuni wao kwa ajili ya kupotewa naye hutulizwa na "honga" kubwa. Hivyo tulipokaribia skuli, walikuwako mamia ya wanawake waliofunga njia, huko wakicheza "mikondi". Walibeba kikapu ("gitaruru") kikubwa ambacho kwa kawaida hutumiwa kwa kupakulia chakula. Pia kikapu hicho hutumiwa kwa kupeperusha ghasia kutoka mbegu kama mahindi. Mpaka kikapu kilipojaa pesa, hawakunikubali niingie. Wasaidizi wangu walikuwa wamekisia tukio hilo na katika motakaa yetu tulikuwa na ndoo iliyojazwa senti kumi na senti tano za thamani ya shillingi mia moja, ambazo tulimwaga ndani ya kikapu. Wanawake hao walitufungulia njia lakini baada ya kutembea kidogo, walitujia tena. Wakati huo tulimwaga thumuni na shilingi zenye thamani ya shilingi mia moja na tulienda kuelekea mlangoni ambako tulilipa kodi ya mwisho ya noti mbili za shilingi mia. Wanawake wetu ni wakali wakati kama huo. Mara nyingi, pesa hizo hurudishiwa mama wa mwanamume, lakini wakati huu zilikwenda kwa wazazi wa Doris.

Tulikuwa na keki maalum ya ghorofa mbili iliyotengenezwa na Bi. Diment, bibiye Community Development Officer wa Nyeri, na marafiki wengi wa makabila yote walihudhuria kuila pamoja nasi, hata yule D.C. aliyemfungulisha mama wa Doris. Huu ulikuwa wakati wanafunzi walikuwa wakienda Amerika kwa ndege na Josef Mathenge alichukua sehemu ya keki hiyo ili wakale pamoja huko Nairobi wakingojea aeropleni. Ilikuwako karamu nyingine kwetu nyumbani kijijini cha Kariko ambayo ilihudhuriwa na wote wa kijijini na iliyofuatwa na dansi katika Ruringu Social Club. Siku iliyofuata tulikwenda Mombasa kustarehekea ndoa yetu na Doris. Tulikuwa tumewaalika wengi katika harusi yetu, na wageni wengine walikuwa wakitutembelea hata mwezini wa Aprili, 1961, miezi saba baadaye.

Niliporudi Nyeri, Joseph Kirira, Jeremiah Kirumwa na mimi tulipendelea kuanzisha biashara mjini Nyeri ambayo tuliita "National Secretarial Service." Hiyo ilikuwa ndoto yetu wakati tulipokuwa kifungioni. Joseph Kirira tulimchagua kuwa katibu wake, Jeremiah Kirumwa akawa mwangalizi wa kazi na mimi nikawa meneja mkuu. Biashara hiyo ilikuwa na pande nyingi. Tuliandika barua za wale ambao hawakujua kuandika na ambao waliona shida kuu wakijadiliana na Serikali katika kesi zao mbele ya korti. Tuliandika na kuchapisha vijitabu viwili ambavyo tulimaliza mwaka wa 1961, cha kwanza kilikuwa juu ya "Desturi za Kikikuyu na mafundisho mbele ya kuoa" na cha pili kilikuwa "Demokrasi katika Afrika." Pia tuliendesha mafunzo ya wanafunzi wa kupiga tepuraita—waume kwa wake—na pia ilikuwako idara ya mambo mengine ya ubiashara. Hata tuliwahi kuchaguliwa wakilishi wa kampuni nyinginezo za uundaji wa vitu. Wenzangu hao wawili walifanya kazi kwa bidii

na unyenyekevu na tulijenga sifa ya biashara yetu kwa haraka. Kwa bahati mbaya tulijiona kuwa wakati mwingi wetu ulitumiwa na mambo ya siasa na mwishoni wa 1961, tulifunga biashara yetu ili tuweze kuwa na nafasi kubwa ya kupigania uhuru.

Mara nilipokuwa na nafasi, nilianza kuandika barua kwa mpendwa Mzee Jomo Kenyatta aliyekuwa Lodwar wakati huo. Vilikuwako vitu vinginevyo alivyotaka vya kumsaidia kuendelea kuwa na afya njema huko Lodwar, na ingawa sikuwa tajiri, nilitimiza yote aliyoniuliza kwa uwezo wangu wote. Wakati Robinson Mwangi na David Oluoch Okello walipofunguliwa, tulijiunga pamoja nyumbani kwangu Nyeri na tulifurahi sana kuwa pamoja tena. Tulipendelea kwenda pamoja hadi Lodwar kumwona Kenyatta ambaye wakati huo alikuwa amehamishwa hadi Maralal kwa vile zaidi alitaka kuonana nasi. Lakini ilitulazimu kwanza tupate "pasi" na Kenyatta na mimi tulipigania kutoka pande zote mpaka Uwaziri wa Ulinzi mwishoni akaturuhusu kwenda.

Tarehe Juni 26, 1961, tulikomboa motokaa kutoka Nyeri na usiku huo tulilala Thomson's Falls. Hatukulala vyema kwa yale tuliyokisia kwa furaha. Tulianza safari yetu tena asubuhi sana, tukasafiri katika giza juu ya ile barabara ya zamani iliyoelekea Kowop. Tulipofika Maralal saa mbili na nusu asubuhi, tulipelekwa na afisa wa polisi aliyechunga wageni wa Kenyatta kwa nyumba ya Mzee.

Hapo, akingojea mlangoni, alikuwa Mzee. Alituamkua kwa njia ya ajabu na aliponikumbatia nilijisikia kama kifaranga chini ya mabawa ya mama wake; taabu zangu na masumbuko yangu sasa yalikuwa yake. Hicho kilikuwa kimzigo kidogo kwa mtu ambaye alibeba mateso ya watu wetu wote peke yake. Kunao watu wengine wanaosema kuwa Waafrika wengi katika Kenya walimsahau Kenyatta wakati wa Hali ya Hatari na kuwa kama si Odinga na wanasiasa wengine, jina lake lingesahauliwa. Hakuna uwongo kama huo. Hakuna Mwafrika aliyependa nchi yake ambaye angemsahau mtu huyo ambaye alionyesha njia ya uhuru na ambaye aliteswa hivyo kwa ajili yetu. Kunao Waafrika wengine wanaopendelea vitu vingine zaidi ya nchi yao; Mungu, amani, utajiri, pombe au wanawake. Hawa wachache wanaweza kusema hawampendi Mzee; wengine wanaweza kusema hivyo kwa ajili ya woga. Lakini wanaoishi, wachangamvu na wanaopanuka, wenye kucheka na kulia baina ya wananchi ni wale wanaompenda zaidi ya kingine cho chote wanachokijua. Ndiye kiongozi wetu aliyechaguliwa na ni yeye tu ataweza kutuongoza kutoka hali ya zamani, kutoka ndani ya kumbukumbu za giza zilizopita na kutuletea mwanga wa maisha mema ya hapo usoni. Kenyatta hategemei K.A.D.U. wala K.A.N.U., India Congress au India Freedom Party, New Kenya Party au Coalition; yeye ni zaidi ya chama cho chote cha siasa. Yeye hasemi kuwa

watu wake ni wale waliofungiwa, "waaminifu", magaidi, humungati, Mau Mau, Wakatoliki, Waprotestanti, Waislamu, Waasia au Wazungu. Kenyatta ni mkuu kuliko Kikuyu ye yote, ni mkuu kuliko Mjaluo ye yote au Mnandi, Masai au Mgiriama—yeye ni mkuu kuliko raia mwengine katika Kenya—yeye ndiye Mwafrika mkuu zaidi ya wote. Hatambui kabila, wala taifa na hana chuki ya kisasi kwa yale yaliyotendeka; yeye ni binadamu lakini mwenye hekima kuliko binadamu mwingine ambaye nimemwona. Wote ni watu wake, madaraka yake na ni watoto wake: huwapenda wote, huwatukuza na kuwasahihisha wakikosa na huwasifu wakifanya vyema.

Tulizungumza mengi pamoja bila kupingwa na mtu. Ingawa alitaka kusikia vile tulivyotendewa katika kuhamishwa kwetu, yeye hakuishi katika mambo ya zamani. Alikuwa atazamia mambo ya usoni na akatueleza juu ya mipango yake mingi ya kupambana na mahitaji ya wananchi. Tulimpa zawadi kadhaa pamoja na chungu cha kupoza maji kilichoumbwa na wanawake wa Fort Hall chenye mfano wa pekee. Tulikuwa tumesikia kuwa alikuwa na shida ya kuweka maji baridi huko kwenye joto. Bibi wangu, Nyambura, pia alimtumia vyungu viwili. Alituonyesha ile kofia tuliyomtengenezea tukiwa Lodwar na nyingine aliyotengenezewa na bibi wake Ngina, ambaye alikuwa amefungiwa Kamiti. Ngina alitupiga picha sote pamoja. Halafu tuliketi kula chakula. Nilipomaliza sahani yangu, Mzee aliniuliza kama ningetaka nyongeza. Nilimjibu kwa nilikuwa nimekula kutosha. Ndipo akaniangalia akaniambia kwa msemo wa baba: "Sasa huko kifungioni. Wewe na mimi ni lazima tule chakula hiki mpaka kimalizike." Nilikubali kwa vile huo haukuwa wakati wa kuanza kutotii amri zake. Nilikuwa karibu kupasuka mara mbili—kilikuwako chakula kingi. Wakati huo, tulikutana na wasichana wake wawili wa kupendeza ambao walikuwa wakisomea hapo Maralal. Alfajiri yake tuliendelea na mazungumzo yetu juu ya siasa, uchumi na mambo ya starehe ya usoni ya Kenya, na pia tulizungumza juu ya safari yangu, ya Uingereza. Alinipa barua za salamu kwa wanafunzi na marafiki wengine waliokuwa London. Nilikuwa nikipitia Ghana na nilipewa salamu za pekee kutoka kwa Kenyatta nimpelekee Dr. Nkrumah na wananchi wote wa nchi ya Ghana. Mzee aliniambia mambo mengi ya hekima ambayo sitayasahau. Wakati jioni ilipofika na wakati wa kuagana, ilionekana kama tulikuwa pamoja kwa muda wa saa moja tangu tulipofika. Tulimwacha tukiwa na huzuni lakini roho zetu zilikuwa zimeridhika sana kwa vile tuliheshimiwa kuonana na kuzungumza naye.

Ni jambo la kuchekesha lakini la kweli kuwa Serikali ya Kenya ilikuwa inasema juu ya "kumwokoa" mtu mtukufu aina hiyo. Mnamo mwezi

wa Aprili, 1960, iliwatuma waandishi wa magazeti na wa televishoni ili kumhoji kama vile yeye alikuwa mnyama wa pekee katika chumba cha wanyama waliowekwa kwa maonyesho. Hakuna "mfereji" ungekuwa mkubwa kutosha kupitiwa na Kenyatta na haikuwezekana kufuta ukubwa kutoka ndani ya mtu wa aina hiyo. Serikali ilijionyesha vile haikufahamu mambo kwa kujaribu kumfanya kitu bure na kujaribu kuwajenga wanasiasa wengine badala yake. Lilikuwa jambo geni kuwa hata mnamo mwezi wa Agosti, 1961, Gavana wa Kenya alikuwa bado kutafuta wakati wa kuonana na mtu ambaye angeongoza nchi yetu ya kupendeza kwa njia ya umoja.

Niliporudi kutoka Maralal, nilizungumza juu ya matembezi yangu na Oginga Odinga, M.L.C., ambaye alinipa pesa za safari yangu ya kwenda Uingereza.

Nilipokuwa Uingereza, nilikutana na wengi wa marafiki wa zamani wa Kenyatta na nikawapa ujumbe wake. Pia nilimpa Karuga Koinange barua kutoka kwa Mzee, wakati alipokuwa mwenye-kiti wa Kenya Students Scholarship Fund, na katika barua hiyo, Kenyatta alikubali kuwa mdhamini wa K.S.S.F. Chama hicho kilianzishwa na wanafunzi wa Kenya ili kujaribu kuwapatia msaada wanafunzi wengine ambao walikwamia huko kwa ajili ya ukosefu wa pesa za kuwawezesha kuendelea na masomo yao. Niliuhutubia mkutano wa wanafunzi wa Kenya. Siku moja nilifurahiwa kualikwa kwenye chuo cha Oxford ambako niliona furaha kuu kukutana na Bi. Margery Perham. Baada, ya mazungumzo marefu, alinishauri nikamilishe kuandika kitabu hiki ambacho, nilikuwa nimeanza kuandika nilipokuwa Kenya juu ya niliyoyaona wakati wa Hatari hapa Kenya. Alisema kuwa watu wengi katika Uingereza hawakufahamu yaliyokuwa yakitendeka hapa. Kwa vile Dr. Nkrumah alikuwa akitembelea Ulaya ya Mashariki—Russia na China—nilikubali kufanya vile nilivyoweza kwa muda wa wiki chache uliobaki na Bi. Perham alinitendea vizuri sana kwa kunipatia chumba cha kufanyia kazi yangu. Nilipokuwa karibu kumaliza kazi yangu, nilifurahiwa sana kusikia habari mnamo tarehe 14 Agosti kuwa sasa Jomo Kenyatta alikuwa nyumbani pamoja na watu wake huko Kiambu.

Vita vya uhuru katika Kenya vilichukua muda mrefu na vilikuwa vyenye uchungu kuliko vingine po pote. Ilikuwa muhimu kujenga hali ya uwananchi yenye nguvu ya kutosha kuwawezesha wananchi kuvunja hali ya nguvu za Wazungu ambayo walikuwa wameijenga kwa miaka mingi, hali sisi tulikuwa watoto katika ujuzi na mazoea ya siasa za siku hizi. Hali kama hiyo hailetwi na maneno matamu ya ukarimu na mapenzi. Kwa vile tulikuwa tumekosa njia na wanyonge, tuliunda umoja wetu kwa njia kali. Tulilazimishwa kudumisha umbo la umoja kwa muda mrefu

kulivyo tulivyokusudia kwa sababu Serikali ya Kikoloni haikuona mbali au ilifikiria sana juu ya siasa za utawala wao zaidi ya vile walifikiria hali ya maisha yetu, na kufunguliwa kwa kiongozi wetu kulicheleweshwa kihalifu. Lakini hivi karibuni tutaitupilia mbali: ziko hatari kubwa katika majaribio ya kujenga na kutia chumvi kuwako kwa upinzani baina ya watu ambao hivi karibuni watakuwa huru.

Viongozi wetu ni lazima wafahamu kuwa tumewaweka pale walipo siyo kukamilisha makuu yao binafsi wala siyo wawe wakitembea huku na huko wakivaa nguo gali na motakaa kama mabalozi na mawaziri, bali wajenge Kenya mpya ambamo kila mtu atakuwa na nafasi ya kujielimisha kamili kulingana na uwezo wake, ndani ya nchi ambayo hakuna atakayeumia au afariki kwa ajili ya ukosefu wa utabibu mwema, na ambamo kila mtu ataweza kufanya kazi ya kumtosha kujilisha na kuwalisha jamaa zake. Hatua hiyo inahitaji uongozi wenye madaraka, bidii, umoja, uaminifu na ukweli wa kupenda nchi yetu katika roho zetu sote. Wale wajipendao wanaojitafutia nguvu watakwenda. Tunayo hadithi katika nchi yetu inayosema kuwa bwana mmoja na bibi wake walikuwa wanaketi kwenye moto na bwana akamwambia bibi wake: "Mpenzi wangu, nitamnunua ng'ombe ambaye nitamleta nyumbani na atamzaa mtoto na tutapata maziwa mengi." "Ah, ndiyo," akamjibu bibi, "ahsante mpenzi bwana wangu, na mimi nitamkama huyo ng'ombe." Hapo bwana alikasirika akamjibu bibiye: "Ah, la hutafanya hivyo usije ukamwua mtoto wake kwa kumnyang'anya maziwa," na kwa vile alivyokuwa amekasirika alimtupa bibiye ndani ya moto na bibi akachomeka vibaya kichwani. Bwana huyo alikuwa pumbavu na alimaliza bila ng'ombe, maziwa na bibi aliyechomeka vibaya ambaye alitumia wakati mwingi akimpeleka hospitali. Wanasiasa wetu ni lazima waache kushambuliana baina yao wenyewe na waponyane huu ugonjwa wa kujipendea makuu au si hivyo, tutapotewa na yote.

Sisi wa K.A.N.U., tukiwa chini ya uongozi mkuu wa Jomo Kenyatta hatufikirii juu ya Kenya peke yake. Tunakusudia kuendelea kufanyiza Shirikisho la Afrika Mashariki, tukielekea kufanya Umoja wa Afrika Mashariki na ya Kati mpaka tufikie ile hali kuu ya "Uafrika" (Pan-Africanism). Hakuna wetu atakayenyamaza kimya wakati wananchi wengine, au wawe ndani ya Angola, Mozambique, South Afrika au Rhodesia, wangali wako chini ya wabeberu. Labda itakuwa haja kutoa sadaka nyingine mpaka wawe huru na tuko tayari kutoa sadaka yetu. Farakano iliyoko baina ya mataifa iliyowagawanya wawe vikundi vya Casablanca na Monrovia lililetwa na uadui uliomo baina ya wabeberu wa Magharibi na Wakomunisiti wa Mashariki. Ni jambo la kustaajabisha vile viongozi wengine Waafrika walivyonasika kwa urahisi katika mtego

huo. Itakuwa juhudi ya chama chetu na taifa letu kuleta umoja katika Afrika kama ule tulio nao katika Kenya.

Basi huo ndio mwisho wa hadithi moja na mwanzo wa nyingine. Nikiangalia nyuma kwa muda wa miaka iliyopita kama nilivyoeleza ndani ya kitabu hiki, kunayo mengi ya kujifunza. Iliwezekanaje watu wengi namna hiyo wakawa wajinga namna hiyo na kuitia Kenya katika moto wa Hali ya Hatari? Kwa nini hata sasa Waingereza wangali waendelea kuleta hali ya aina hiyo katika Rhodesia? Hayo ndiyo maswali makubwa, maswali ambayo ni wale tu ambao wanafahamu mchezo wa siasa wanaoweza kujibu. Lakini yako maswali madogo. Ni kitu gani kinachokigeuza kiumbe kinyonge kikiwa ndani ya seng'enge na kuwa kama mnyama asiye na akili? Ni kitu kilichowafanya waliokuwa upande wa Serikali—majeshi ya ulinzi na wengineo—kuwa wakati wote Mungu na Haki zilikuwa upande wao hata uwe ni ukatili gani au uhalifu gani waliowatendea binadamu? Ni dude gani lililowasindikiza maafisa wengine ambao hata sasa waonekana kuwa watu wenye maana kufuata maongozi ya kinyama na ukatili na mateso kama yale yaliyoleta vifo vya Hola? Serikali ya Kenya ilifikiriaje kuwa ingeweza kuwahamisha wananchi 12,000 daima?

Waandishi wa historia wa siku hizi waweza kuona shida kufahamikiwa na upande wetu wa hadithi hii. Maandishi mengi ambayo yangewasaidia yatakuwa yamechomwa kabla ya uhuru wetu. Lakini yale niliyoeleza juu ya maisha yetu katika mahamishoni yanaweza kuwasaidia kuona dalili za ukweli na haki juu ya umoja, na anaweza kufahamu kwa nini hatuwafikirii askari wetu wa misitu kama hadi-koa, magaidi au wauaji, lakini kama mashujaa watukufu waliopigania uhuru wetu. Kitabu hiki na taifa letu jipya, ziwe ukumbusho mdogo wa yale yaliyotendeka. Kuteswa kwao na maumivu waliyopatwa nayo yalikuwa ndio msingi wa taifa.

Nyongeza — Kuunganishwa kwa Mashamba

KUUNGANISHWA kwa Mashamba (Land Consolidation) ni jina ambalo linatumiwa kueleza mpango mkubwa wa kugeuza uwenyewe umiliki wa ardhi ambao ulianzishwa na Serikali ya Wakoloni katika sehemu nyingine za makabila mengi katika Kenya na ambao ulianzishwa hapo kwanza katika nchi ya Wakikuyu. Hatua za kuunganisha Mashamba zilianza kwa kupima na kuhesabu ekari za vishamba vya kila mtu ambavyo vilikuwa vimetawanyika kote (pengine wengine walikuwa na vishamba thelathini vilivyotawanyika pote nchini). Baada ya kuondoa sehemu tano kwa mia za jumla ya ekari za kila mmoja, sehemu ambayo ilitumiwa kwa haja za wote kama barabara, skuli, vijiji dispensari na mengineyo, sehemu iliyobaki iliwekwa pamoja. Kama alikubali, sehemu hiyo yake mpya iliwekewa mipaka na mwenyewe alipewa Hati ya Ardhi (Freehold Title).

Serikali ilianzisha mpango huo wakati wa Hali ya Hatari na sababu yake ni kuwa ilifikiria kuwa ilikuwa na nguvu za kutosha kuwatawala Wakikuyu wakati huo, nguvu ambazo zingeliiwezesha kuushindikiza mpango huo mgumu kwa haraka na bila shida, na pia ilifikiriwa kuwa ungeleta nafasi ya ukulima mwema ambao ungeeneza nguvu za Wakikuyu na kuleta maendeleo ya wenye mali wa daraja la kati, na ulifikiriwa kuwa shina lingalilowezesha kuwapatia wenyeji pesa za maendeleo ya starehe kama afya na elimu.

Hapo kwanza, viongozi wengine Waafrika waliupinga. Walishuku hatua zo zote zilizowalazimisha Wakikuyu kufuata jambo kama hilo hali kabila hilo lilikuwa taabuni kuu na ni wakati huo hakukuwako na njia ya kufanya upinzani. Pia walishuku kuwa mageuko makubwa ya aina hiyo ya ardhi hayakulingana na desturi au dini juu ya ardhi ambayo walirithi kwa wazazi wao. Waombaji ("ahoi") walisumbuka sana kwa vile wangepotewa na haki zao kufuatana na kutolewa kwa Hati za Ardhi kwa wenyewe halisi. Pia ilifikiriwa kuwa kwa vile wananchi 80,000 walikuwa nje ya nchi (wakifungiwa au kufungwa) huo haukuwa wakati uliofaa kuanzisha mpango huo. Wengine walifikiria mpango huo haungeendeshwa kwa njia ya haki na wakoloni. Hofu nyingi za aina hiyo zilithi-

bitishwa. Uhongaji kwa njia kubwa uligunduliwa katika wilaya ya Fort Hall mwaka wa 1960 wakati wafungiwa wengi walirudi nyumbani na kukuta kwamba hawakuwa na ardhi na hata leo hali na haki za waombaji si wazi. Lakini katika wilaya ambako uunganishaji umekamilika, yako maendeleo ya ukulima yaliyo wazi na upinzani juu yake umepunguka. Labda upungufu huo uliletwa na kufunguliwa kwa ardhi ya Nyanda za Juu zilizokuwa za Wazungu hapo mbeleni zikapewa masettla Waafrika.

Yale maongozi ya kuwakusanya Wakikuyu na kuwaweka katika vijiji kama hatua ya usalama mwaka wa 1953 na 1954 yalionekana kama yali-youfaa mpango wa uunganishaji wa ardhi, na ilikusudiwa kumlazimisha ye yote aliyekuwa na chini ya ekari tatu za ardhi kuendelea kuishi katika kijiji baada ya Hali ya Hatari. Kwa vile hakuna nyingi za Halmashauri za Sheria katika ulimwengu ambazo zingepitisha sheria ya aina hiyo, hakuna aliyekubali kutii amri zilizotolewa na maafisa wa kawaida bila kuungwa mkono na Sheria ya Halmashauri juu ya jambo muhimu namna hiyo, na kwa hivyo kusudi hilo halikufaulu na limeondolewa kabisa.